

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Tano – Tarehe 3 Februari, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nane, Kikao cha leo ni cha Tano, Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu kwa mwaka 2018/2019 (*The BoT Annual Report for the year 2018/2019*).

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019/2020.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019/2020.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Siku ya leo tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na swali linaulizwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa PAC Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki. Sasa unaweza kuuliza swali lako Mheshimiwa.

Na. 51

Hitaji la Mwekezaji kwenye JASI

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Kata za Bendera na Makanya zina jasi nyingi na jasi inaweza kutoa malighafi kutengeneza gypsum boards, mabomba ya maji machafu, saruji, POP na mbolea:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kupatikana kwa mwekezaji ili aanzishe viwanda hivyo katika maeneo hayo ya Wilayani Same?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo, namwona Mheshimiwa Waziri Angella Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa kati unaoongozwa na sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2025. Aidha, viwanda vinavyotumia rasilimali zinazopatikana nchini na kuzalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi vimepewa kipaumbele. Kutokana na utekelezaji wa azma hiyo, nchi yetu sasa imeweza kuzalisha baadhi ya bidhaa zinazotosheleza soko la ndani na ziada kuuza nje ya nchi ikiwemo bidhaa zinazotokana na malighafi ya jasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua lengo la Serikali ni kuongeza uzalishaji wa ndani na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje katika maeneo yote yenye rasilimali zinazoipa Tanzania faida ya ushindani (*competitive advantage*), Serikali itaendelea kuvutia uwekezaji katika maeneo yote yenye rasilimali ikiwemo jasi inayopatikana katika Kata za Bendera na Makanya Wilayani Same.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutumia fursa hii kuupongeza uongozi wa Mkao wa Kilimanjaro na Wilaya ya Same kwa kutenga eneo katika Kata ya Makanya kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha saruji na kuingizwa katika Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkao wa Kilimanjaro na hatua za kutafuta wawekezaji zinaendelea. Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zingine kama vile Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Mamlaka ya EPZ, Tume ya Madini na wadau wengine tutaendelea kushirikiana kuzitangaza fursa za uwekezaji za Wilaya ya Same ili kuvutia na kutekeleza uwekezaji katika jasi iliyoko wilayani Same.

Aidha, napenda kuzikumbusha Wizara, taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia mikakati ya kuboresha mazingira ya uwekezaji katika maeneo yao ikiwemo kuainisha na kuyapembua kiyakinifu maeneo yote yenye rasilimali, kuyatenga na kuyarasimisha kwa ajili ya uwekezaji ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima na wawekezaji ili kufikia dhamira ya Serikali kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Kaboyoka, nimekuona swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza ni kwamba kutokana na utafiti uliofanyika kuangalia uwepo wa jasi katika Kata ya Bendera na Makanya umechukua muda mrefu, je, Serikali haioni umuhimu kusaidiana na Wizara ya Madini ili watume wataalamu wakafanye utafiti wa kina kujua kuna-deposit kiasi gani ili hata TIC wakiwa na nyaraka hizo iwe rahisi kwa mwekezaji kujua kwamba kuna potential ya kuwekeza katika eneo hili? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Mheshimiwa Kairuki, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, awali yote kwanza nichukue nafasi hii kupongeza sana uongozi wa Wilaya ya Same kama nilivyoeleza awali kwa kuweza kutenga eneo hili la uwekezaji zaidi ya ekari 4000

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niweze kujibu swali dogo nyongeza la Mheshimiwa Kaboyoka, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ukiangalia kwa takwimu za uzalishaji za hivi sasa kwa Makanya peke yake uzalishaji ni zaidi ya takriban tani 145,000 na kwa upande wa Bendera ni takriban tani 25,200. Vilevile ukiangalia kwa takwimu tulizonazo kwa TIC nchi nzima tumeweza kusajili zaidi ya miradi 78 ambayo inahusika na uzalishaji wa cement na uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na jasi. Kwa hiyo, ukiangalia inathibitisha kabisa kwamba kweli Wilaya ya Same inahitaji mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hitaji la kufanya utafiti, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Madini kuweza kuona ni kwa namna gani tunaweza kuharakisha kufanya utafiti ili kuweza kujua rasilimali iliyoko pale kwa kujua tani ni ngapi ili kuweza kuwa na uhakika hata mwekezaji anapokuja basi ijulikane atawenza kuzalisha kiasi gani lakini vilevile uhai wa migodi ile pia ni kwa miaka mingapi. Nishukuru sana kwa kufuutilia na nishukuru kwa namna ambavyo mmekuwa mkishirikiana pia na Mheshimiwa Kilango na uongozi mzima wa Wilaya ya Same.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu nilikuona.

MHE. DKT. MARY M NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali hili muhimu. Ukija Wilaya ya Hanang katika ukuta wa Bonde la Ufa malighafi zote za kutengeneza cement zimejaa na naambiwa kwamba hakuna mahali ambapo malighafi zote zimekuwepo isipokuwa kwenye eneo lile. Je, Mheshimiwa Waziri atatuletea wawekezaji ili na Wilaya yetu ya Hanang iwe na kiwanda kikubwa cha cement?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Angellah Kairuki, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ukiangalia kwa Tanzania katika maeneo ambayo imethibitika kuwa na jasi ni pamoja na Pwani, Dodoma, Kilimanjaro, Mtwara, Lindi, Singida na Manyara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kufuutilia na kuona ni kwa namna

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunaweza pia na kwa upande wa Manyara kuona wanaweza kupata mwekezaji. Kwa sasa kiko kiwanda kikubwa kabisa cha China cha Huashan ambapo wameonesha nia ya kuja kuwekeza. Tunachokifanya sasa ni kuwapeleka katika maeneo mbalimbali ili watakapoona deposit ile kama inawaridhisha basi iwe ni rahisi kuweza kufanya uwekezaji. Vilevile wajenzi wa Stigler's Gorge na wenyewe wameonesha nia ya kuwekeza katika kiwanda kikubwa kabisa cha kuzalisha cement hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo limekuwa likileta changamoto, wengi wamekuwa wakitaka wapewe eneo ambako kunakuwa kuna chokaa au *limestone* ambayo inakuwa ni rahisi zaidi na ni rasilimali muhimu au malighafi muhimu katika uzalishaji wa cement.

Kwa hiyo, bado tunaendelea kushawishi na naamini watakapokuja katika maeneo pia ya Manyara watakapoona kiasi kinathibitika na endapo wataridhika basi naamini inaweza ikawa ni rahisi wao kuwekeza.

SPIKA: Tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, swali linaulizwa na Mbunge wa Lushoto Mheshimiwa Shaabani Shekilindi. Mheshimiwa Shekilindi uliza swali lako tafadhali.

Na. 52

Kumalizia Ujenzi Wa Maabara – Lushoto

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Lushoto wamejitalidi kujenga maboma mengi ya maabara lakini mpaka sasa Serikali haijawaunga mkono:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga mkono juhudhi hizo za wananchi kwa kumalizia maboma haya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi imekamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara 13 katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kati ya maabara 159 zinazohitajika.

Aidha, maabara 138 zinaendelea kujengwa kuitia mapato ya ndani ya Halmashauri na nguvu za wananchi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Halmashauri inaendelea na hatua za mwisho za ukamilishaji wa maabara katika Shule za sekondari za Mlongwema, Kwemalamba, Lukozi, Ngwelo na Shume zilizopatiwa shilingi milioni 5 kuitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R).

SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Hata hivyo, kabla ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, naomba nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Wilaya ya Lushoto kwa mvua zinazoendelea kunyeshaa takriban sasa ni miezi minne bila kujua zitaisha lini. Niwatoe hofu kwamba taarifa za mvua

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zimefika sehemu husika, ni imani yangu kubwa sasa kwamba baada ya mvua kupungua miundombinu ile itarejeshwa na wananchi watapata huduma kama ilivyokuwa awali. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize maswali mwili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze kwa majibu mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kusema kuwa ametupatia fedha za maabara, ni kweli. Hata hivyo, kuna shule nyingi sana katika Wilaya ya Lushoto zaidi ya 50 lakini zenyе maabara hazifiki sita. Kwa nini sasa Serikali isitumie mfumo kama ule wa mwaka jana wa kutoa fedha za kukarabati maboma ya madarasa ili kukarabati maabara kuepusha usumbu kwa wanafunzi wetu hasa wasichana ambapo tutaepusha mimba za utotonii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Jimbo la Lushoto lina sekondari nyingi sana zaidi ya 28 lakini zenyе hosteli naamini hata tatu hazifiki. Je, kwa nini sasa Serikali isitupe hata fedha kwa mwaka huu ili kukarabati maboma ya hosteli ambayo yameshajengwa kwa nguvu za wananchi mfano Mlongwema...

SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi nafikiri umeeleweka, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza umeona Mheshimiwa Mbunge amehemewa, mimi nimeenda Lushoto pamoja na kwa Mheshimiwa Shangazi ni kweli wana shule nyingi na wanajenga kwa nguvu za wananchi. Nawapongeza sana Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Shangazi kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika kupeleka elimu katika maeneo yale. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimetembelea baadhi ya maboma ya maabara ambayo kwa kweli hayajakamilika. Maombi ya Mheshimiwa Mbunge tumeyapokea, Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapata maabara katika kila shule ya sekondari kwa sababu ni lazima tuwe na masomo ya sayansi ambayo yanafundishwa kwa vitendo na siyo nadharia.

Mheshimiwa Spika, kwa bajeti ya mwaka huu na bajeti ambayo tunaendelea nayo, nimhakikishie kwamba katika maombi ambayo ameshayaleta pale ofisini tutayafanyia kazi, hawesi kukosa baadhi ya maabara ambazo zitakamilika. Hatujengi maabara tu, tunajenga maabara lakini pia kupeleka vifaa ili wanafunzi waweze kufanya mazoezi kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote mwaka huu ambao tunaendelea nao tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maabara na majengo mbalimbali lakini na mwaka huu ambao tunaanza mchakato wa bajeti tutatenga fedha. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge Halmashauri huko wanaendelea kutengeneza bajeti ni muhimu kwenye bajeti hii ambayo tunaenda nayo 2020/2021 tutenje fedha kuanzia vyanzo vya Halmashauri na sisi Serikali Kuu tutatafuta fedha tuwekeze pale ili tuweze kuboresha maabara, majengo ya hosteli, kumbi za mikutano na nyumba za walimu. Ahsante sana.

SPIKA: Pamoja na majibu hayo Mheshimiwa Naibu Waziri bado kuna swali linalofuata la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoaa Mjini akiulizia ujenzi wa maabara za sekondari. Mheshimiwa Edwin uliza swali lako sasa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 53

Maboma ya Maabara katika Shule za Kata Nchini

MHE. EDWIN M. SANNDA aliuliza:-

Maboma mengi ya maabara kwenye Shule za Sekondari za Kata nchini hayajakamilika na hata pale yanapokamilika hakuna vifaa vya maabara na tunahitaji sana wanasayansi kuelekea uchumi wa viwanda:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha maabara hizo na lini zitakamilika?

(b) Je, ni lini vifaa vitapelekwa katika maabara zilizokamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu tafadhalii, swali hili ni la Wabunge wote kwa kweli la maabara katika shule za sekondari.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi na Washirika wa Maendeleo imekamilisha ujenzi wa maabara 5,801 kati ya maabara 11,369 zinazohitajiki. Hivyo, upungufu uliopo ni maabara 5,568. Serikali inaendelea na ukamilishaji wa vyumba vya maabara kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na mapato ya ndani kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Kondoa Mji, imeidhinishiwa jumla ya Sh. 8,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara katika Shule ya Sekondari Bicha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya maabara vyenye thamani ya shilingi billioni 19.13 katika shule 2,948 za sekondari zilizokamilisha ujenzi wa maabara. Serikali kwa kushirikisha wananchi na wadau wa maendeleo itaendelea kuboresha maabara za masomo ya sayansi ili ufundishaji wa masomo hayo ufanyike kwa vitendo na siyo nadharia.

SPIKA: Mheshimiwa Edwin Sannda, uliza swali lako la nyongeza.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Labda tu kabla ya kuuliza maswali yangu ya nyongeza, nikuombe tu univumilie kidogo kwa sababu haya majibu ya Serikali sioni matumaini kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunazungumzia uchumi wa viwanda na tegemeo kubwa lazima tuweze kuzalisha wanasayansi wa kutosha kabisa. Sasa mimi natoa mfano tu wa Mkoaa wetu wa Dodoma tulikuwa kwenye vikao vya ALAT hata kwako Mheshimiwa Spika tuko chini ya 20% ya ukamilishaji wa maboma ya maabara. Sasa huu uchumi wa viwanda unakwenda kulishwa na watu kutoka wapi kama tunawapeleka watu wa masomo mengine na siyo wanasayansi?

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia shilingi milioni 8 ambazo Halmashauri ya Mji Kondoa tumeidhinisha hizi ni zile fedha ambazo nimezitoa mimi kupitia Mfuko wa Jimbo mwaka jana na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tulikwishazitoa. Boma moja la darasa linajengwa kwa shilingi 25 sisi tunazungumzia shilingi milioni nane. Hebu Serikali ione ni namna gani tunakuja na mkakati wa dharura sasa kama ambavyo tumefanya kwenye maboma ya madarasa na kwenye nyumba za walimu ili tuweze kukamilisha hizi maabara nchi nzima. Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, walau mimi nina maabara moja tu kati ya sekondari nane (8) ambayo imekamilika na yenyewe haina vifaa. Ni lini tutapata angalau hivyo vifaa vya maabara kwenye hata hiyo moja ambayo mpaka sasa imeshakamilika? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali tafadhali.

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wakati Serikali ikiangaika kupata fedha kwa ajili ya elimu baadhi ya wabunge wanaandika barua huko kwa kutumia nembo za Bunge kuzuia fedha zisije. Ndiyo maana tukiwa wakali muwe mnatuelewa tu, nia njema, tazama matatizo yalivyo makubwa. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameuliza maswali mawili, moja anauliza mkakati wa Serikali wa kumalizia maabara ambazo wananchi wameweka nguvu zao lakini jambo la pili anataka kujua ni lini tutapeleka vifaa katika shule yake.

Mheshimiwa Spika, tulisambaza vifaa vya maabara kwenye shule na maabara mbalimbali. Nafikiri baada ya kutoka hapa mbele tuwasiliane tuone ni kwa nini maabara yako moja ambayo imekamilika haikupata vifaa ili tuweze kupeleka vifaa katika shule yako hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini nikupongeze sana kwa swali muhimu, ni kweli kwamba tunahitaji uchumi wa viwanda na tunahitaji zaidi wanafunzi wetu wasome masomo ya sayansi na huwezi kusoma sayansi kama hauna maabara zenye vifaa na wale wataalam wa maabara ili waweze kufanya mazoezi kwa vitendo. Tunampongeza Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine ambao kwa kuititia Mfuko wa Jimbo wamepeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maabara. Najua wengine wamejenga madarasa, wengine wamenunua madawati na wengine wamejenga nyumba katika maeneo ya jirani ili walimu wetu waweze kupanga kwa bei nafuu sana.

Mheshimiwa Spika, nilichosema hapa ni kwamba Serikali ina mpango, kwenye bajeti hii Waheshimiwa Wabunge wote tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maabara. Tulishatoa taarifa kwenye Halmashauri walete taarifa ya maabara ambazo zimekamilika, vifaa vinanunuliwa na vinasambazwa katika maeneo yale. Tunaendelea kutoa wito tupate hizo taarifa ili tuendele kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, umesema vizuri hapa kwamba hapa tunazungumzia maabara katika shule za sekondari na katika mpango wetu ule wa kupata fedha zile ambazo zina kizungumkuti huko na wenzetu wameshiriki, katika mpango ule nilisema juzi hapa tunajenga shule mpya za watoto wa kike maalumu 26, tunajenga madarasa na mabweni kwa maana ya mabwalo zaidi ya 300 na tunakamilisha maabara zaidi ya 400. Kwa hiyo, huenda hii fedha ingekuja kwa wakati na ndiyo ulikuwa mpango wa Serikali hii kazi ya kulalamikia maabara hata kama isingeisha ingepungua sana. Tutoe wito Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema juzi hii kazi Serikali ni yetu sote tulishirikiane fedha zikitafutwa tunapeleka fedha Halmashauri, tunapeleka fedha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoka Mfuko Mkoo lakini pia tunatumia wadau mbalimbali ili tuweze kupata fedha tuweze kukamilisha miundombinu mbalimbali ya elimu.

Mheshimiwa Spika, tushirikiane katika jambo hili na kama ambavyo umeshazungumza katika Bunge hili. Pia sisi kama Wizara tunakwazwa sana na mambo haya kwa sababu tunaweka mipango na Wabunge wameleta maombi mbalimbali pale Wizarani, fedha zimeiva halafu kuna watu wanaweka kitumbua mchanga. Ahsante sana.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa James Mbatia, uliza swali la nyongeza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ukiangalia malengo endelevu ya dunia yanaenda kwa vipaumbele. Kipaumbele cha Nne ni elimu bora, sawa Jumuishi/Shirikishi kwa wote. Kipaumbele cha Tisa ni viwanda, ubunifu na miundombinu. Serikali imekuwa ikiwekeza kwa kasi kubwa kwenye miundombinu lakini ili uweze kutekeleza na kusimamia vizuri miundombinu yafaa kuwekeza zaidi ya mara mbili kwenye elimu kabla ya miundombinu. Serikali haioni umuhimu wa kuja na mpango mkakati bila kupepesa macho ili wawekeze kwenye elimu na hasa sayansi ili maabara zetu zikiwa kwenye hali nzuri ikiweko ya Rasesa ambayo Mbunge naijenga kule Vunjo waweze kuwekeza na watoto wetu wawe wabunifu waweze kuendesha karne ya sanyansi na teknolojia na hasa viwanda?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maoni na mawazo yake mazuri na ya kisayansi. Nimhakikishie kwamba mpango wa Serikali upo mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba tunaondoa changamoto hii. Tunaweka mpango mzuri wa kumalizia maabara zetu, kupata mabweni ya kutosha kwa watoto wa kike lakini kupata walimu wa sayansi hasa masomo ya hesabu, fizikia, kemia na biologija ili masomo hayo yaweze kufundishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati tunatekeleza mkakati wa muda mrefu tunao mpango wa muda mfupi. Kama nilivyosema kwenye bajeti hii tunazo fedha na vyanzo viro katika maeneo mbalimbali. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kabla ya mwezi wa pili au wa tatu tutakuwa tumepeleka fedha katika majimbo yetu ili kukamilisha miundombinu ya elimu. Mpango wa mwaka huu tumeelekeza Wakurugenzi na nyie Waheshimiwa Wabunge hakikisheni kwenye mpango mnaoanzisha pale kuwe na kipengele hicho cha kuwekeza katika walimu na madarasa lakini pia maabara katika halmshauri zile.

Kwa hiyo, tukishirikiana na Halmashauri zetu sisi Wabunge na wadau mbalimbali wa maendeleo na Serikali Kuu jambo hili linawezekana. Hatuwezi kuwa na viwanda halafu wageni ndio waje kufanya kazi hapa kwetu lazima tuwe na viwanda na vijana walioandaliwa vizuri wafanye kazi katika viwanda hivyo ili tuweze kuwekeza katika uchumi wa viwanda na uchumi wa kati.

SPIKA: Ahsante. Tunaama TAMISEMI, tunaelekea Wizara ya Kilimo, swali sasa linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 54

Dawa za Kuulia Wadudu Wanaoharibu Pamba

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali inahamasisha kilimo cha pamba kwa wananchi huku ikiwa haina uwezo wa kupeleka dawa za kuulia wadudu na zinapopatikana huwa ni chache?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussen Bashe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza si sahihi kusema kuwa Serikali inahamasisha kilimo cha pamba ikiwa haina uwezo wa kupeleka sumu za kuulia wadudu na hata zinapopatikana huwa ni chache. Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha mazao yote ikiwemo zao la pamba ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya utekelezaji wa hamasa za kilimo cha pamba, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 eneo la ekari 1,488,406 lilitimwa na kuzalisha kiasi cha tani 132,961. Chupa milioni 4.6 za viuadudu zenye thamani ya shillingi bilioni 16.8 na vinyunyizi 15,300 vyenye thamani ya shillingi milioni 462 vilinunuliwa na kusambazwa mwaka huo. Aidha, katika msimu wa 2018/2019 eneo la ekari 1,865,000 lilitimwa na kuzalisha kiasi cha tani 222,725 ambapo chupa milioni 6 za viuadudu vyenye thamani ya shillingi bilioni 29 na vinyunyizi 23,000 vyenye thamani ya shillingi bilioni 1.8 vilinunuliwa. Vilevile, katika msimu wa 2019/2020 eneo la ekari 1,786,890 lilitimwa na kuzalisha kiasi cha tani 350,473 ambapo chupa milioni 8.2 zenye thamani ya shillingi bilioni 41 na vinyunyizi 20,000 vyenye thamani ya shillingi bilioni 1.6 vilinunuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2017/2018 jumla ya ekapaki 965,300 na vinyunyizi 3,302 vilisambazwa katika Mkoa wa Geita. Aidha, jumla ya ekapaki 736,345 na vinyunyizi 3,020 vilisambazwa katika mkoa huo katika msimu wa 2018/2019. Kwa msimu wa 2019/2020, Mkoa wa Geita umekwisha kusambaziwa kiasi cha ekapaki 8,748 na usambazaji bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, uchache wa viuadudu vya zao la pamba umechangiwa na baadhi ya wakulima kutumia viuadudu katika kupulizia mazao mengine kama vile mahindi na viazi vitamu ili kudhibiti viwavijeshi. Vilevile, kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya viongozi wa vijiji katika baadhi ya maeneo ukiwemo Mkoa wa Geita ambapo viuadudu havikupelekwa kwa wakulima na badala yake kuuzwa katika maduka ya pembejeo kinyume na taratibu za usambazaji wa viuadudu vya zao la pamba. Watu zaidi ya 12 walikamatwa na kati yao 9 walifunguliwa mashtaka ambapo watu nane (8) walihukumiwa kifungo cha miezi sita jela kila mmoja. Serikali itaendelea kufuatilia upatikanaji wa viuadudu vya zao la pamba na kuhakikisha vinawafikia wakulima kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali, Mheshimiwa Musukuma nimekuona.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Sina sababu ya kumjibu rafiki yangu Mheshimiwa Bashe kwa sababu alikuwa mwenzetu huku alikuwa anazijua vizuri takwimu.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema ni sahihi. Swali langu la kwanza hivi viuadudu tunapokuwa tumelima pamba vinakuja wakati ambapo siyo sahihi na vinapokuja vingine vime-expire. Hizi takwimu anazosizoma Mheshimiwa Bashe ni takwimu za makaratasi. Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari tutakapomaliza Bunge hili twende kwa wananchi wangu wa Kijiji cha Rubanga, Isirwabutondwe, ukajionee madhara waliyoyapata kipindi kilichopita?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika msimu wa pamba 2018/2019 kumeingia mdudu anaitwa ushirika na Waziri anaufahamu kabisa. Tumekuwa na matatizo makubwa sana kati ya mkulima na wanunuzi wa pamba uliosababishwa na ushirika. Yote haya yamesababishwa na Serikali kutokutusikiliza sisi wakulima. Ushirika ni chombo ambacho kimetuvuruga sana wakulima wa pamba pamoja na kwake Mheshimiwa Bashe miaka ya nyuma lakini Serikali ilichukua uamuzi wa kusema sasa ushirika lazima ununue pamba kwa bei inayotaka ushirika. Sasa Mheshimiwa Waziri nilikuwa nauliza kwa sababu Serikali inautambua ushirika na una asset zake ambazo zinaweza kukopeshwa benki, mko tayari sasa kutoa kauli kwamba wakope hela bank ili waingie kwenye ushindani na makampuni mengine ili msimu ujao kusitokee vurugu iliyotokea mwaka huu?

SPIKA: Majibu ya swali hayo muhimu. Mheshimiwa anasema dawa zilizo expire badala ya kuuwa wadudu wa pamba wanatenepa. Majibu, tafadhalii. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba ni ukweli usiofichika kwamba wakulima wa pamba kwa muda mrefu wamekuwa wakikibiliwa na changamoto ya kupewa baadhi ya viuadudu vikiwa chini ya kiwango. Sisi kama Wizara ya Kilimo tumeamua kwamba katika msimu wa mwaka huu ambaa sasa hivi wakulima wamelima viuadudu vyote vitakavyosambazwa msambazaji atasaini mkataba wa *quality assurance* ili pale ambapo atapeleka kiuadudu ama dawa itakuwa na tatizo la ubora atakuwa *heard responsible* na kushtakiwa kwa uhujumu uchumi kwa sababu kile ni kitendo cha kuhujumu uchumi wa mkulima na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini mbali na hapo, tumewataka wasambazaji wote ambaa wataingia makubaliano ya kusambaza dawa hizi wahakikisha wana-provide extension services. Kwa sababu si sahihi kwenda ku-damp dawa katika go-down bila kushiriki katika zoezi la kutoa elimu ya usambazaji na upulizaji wa dawa. Kwa hiyo, usambazaji katika msimu huu utaendana pamoja na makubaliano juu ya suala la ubora na yeypole atakayesambaza dawa ambayo itakuwa chini ya ubora atachukuliwa hatua za kisheria na business as usual katika suala la dawa halitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushirika, kwanza kuhakikisha ushirika unajengwa ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi na Serikali iliyoko madarakani inasimamia utekelezaji wa ilani wa chama kilichopo madarakani. Ni sahihi kwamba kumekuwepo na viongozi wa ushirika ambaa siyo waaminifu. Tatizo hili si tu linasababishwa na ushirika lakini vilevile wako baadhi ya wanunuzi wa pamba na Mheshimiwa Musukuma anawajua na sisi wote tunajua kwamba wanafanya mchakato wa kuvuruga mfumo ili waweze ku-benefit.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tumeamua safari hii kwanza ushirika haununui pamba anayenunua pamba ni mfanyakishara binafsi. Tunachokifanya ni kwamba tunatumia Ushirika na Vyama vya Msingi ili wakulima waweze kukusanya pamba yao sehemu moja na kupitia ushirika kudhibiti suala la ubora ambalo linaathiri zao la pamba katika soko la dunia.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Msimu huu haujasababishiwa matatizo yake na ushirika msimu huu bei ya pamba imekumbwa na tatizo katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, msimu ujao kutakuwa hakuna malipo ya cash, wakulima wote watatakiwa wawe bank account, Vyama vyote vya Msingi vitakuwa na bank account na wafanyakishara wote watalipa fedha za wakulima kuititia bank account. Hivi tunavyoongea bank ya CRDB na NMB wanazunguka vijijini kuwafungulia wakulima wa pamba akaunti bila gharama. Akaunti zao zitakuwa bure ili msimu ujao tusikumbane na matatizo yaliyotokea katika msimu huu.

Mheshimiwa Spika, lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge na ninyi mshiriki katika suala la kuhakikisha katika ngazi za AMCOS viongozi wanaopatikana ni waaminifu ili waweze kusimamia vyama vya ushirika na kuweza kufikia lengo la Serikali kujenga ushirika uliokuwa imara.

SPIKA: Ngoja tuangalie hapo wanaolima pamba, Mheshimiwa Ndassa nilikuona, uliza swali la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Nimemkiliza vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali langu ni dogo sana, kwa sababu sasa wakulima wa pamba tayari wameshalima pamba yao lakini tatizo lililopo hivi sasa hakuna viuadudu ambavyo vimeshapelekwa. Bwana Waziri wewe, najua wewe ni champion wa pamba, ni lini dawa za kuua wadudu zitapekwa kwa wakulima wetu wa zao la pamba?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi, ni lini? Mheshimiwa Hussien Bashe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Spika, nataka nimjibu Mheshimiwa Senata Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunavyoongea usambazaji wa viuadudu umeanza katika maeneo ambayo wakulima walianza kulima mapema mwezi Oktoba, katika baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Geita. Mpaka sasa tumeshasambaza chupa laki tisa na zoezi la usambazaji linaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na kalenda tutahakikisha viuadudu vinafika kwa wakati. Kwa mujibu wa kalenda wakulima wanatakiwa kupulizia mara ya pili kuanzia tarehe 15 Februari, tunahakikisha kwamba wakulima wote watapata dawa kwa wakati. Ndani ya Serikali na Bodi ya Pamba mchakato unaendelea na taasisi za fedha zimeshajitokeza kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge hili kuomba, kilimo cha pamba kwa miaka yote kimeendelea kutegemea mgogo wa Serikali. Pamba ni zao ambalo limelimwa kwa muda mrefu likitegemea kubebwa na Serikali. Niombe na nitumie nafasi hii umewadia wakati wa zao la pamba kusimama lenyewe, dawa ziuzwe katika maduka kama wakulima wengine wanavyopata, mbegu zipatikane na sisi kama Serikali tunajenga huo mfumo ili bidhaa hizi zisiwe tena mpaka zitengemee intervention ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana hakuna dawa wala mbegu ya bure. Nitumie Bunge hili kulisema hili wazi, vikao vya wadau tumekaa tumekubaliana wakulima wanakopeshwa mbegu na wameshakopeshwa wamelima, safari hii watakopeshwa viuatilifu na mwisho wa msimu kila mkulima atakatwa Sh.150 ili kulipia mbegu walizokopeshwa safari hii jumla ya tani 24,000 na viuadudu na viuatilifu watakavyokuwa wamekopeshwa katika kipindi hiki cha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kupulizia dawa. Kwa hiyo, nimtoe hofu kuanzia tarehe 15 wakulima watakuwa katika nafasi nzuri ya kupata dawa husika.

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale nilikuona, swali fupi sana kwa Wizara ya Kilimo.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Awali ya yote nitoe pole kwa wananchi wa nchi nzima hii ambao wamepata adha ya mafuriko hasa wa Wilaya yangu ya Liwale na Mkoa wa Lindi. Nawapa pole sana Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nafuu wakati huu wanahangaika na makazi yao.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo hakuna mtu ambaye hajui kwamba nchi yetu asilimia 75 ni wakulima lakini naona Serikali usimamizi wa kilimo wameachia Vyama vya Ushirika ambavyo havina uwezo wa kulismamia. Mfano kwa suala la kuagiza vifaa au pembejeo wameachiwa Vyama vya Ushirika ambapo wao ndiyo wanaoingia mikataba na suppliers wa pembejeo hata kwenye mauzo. Kama Serikali mtaamua kuviachia Vyama vya Ushirika kusimamia kilimo basi tutendelea kusuasua kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri mwaka huu kwenye zao la korosho tumechelewa msimu tumekuja kuanza msimu mwezi wa kumi na moja wakati korosho wakulima wameshaanza kuzivuna tangu mwezi wa nane. Jambo hili mliliachia kwenye Vyama vya Ushirika matokeo yake tumechelewa kuanza msimu toka mwezi wa Novemba mpaka leo wakulima bado wana korosho.

SPIKA: Sasa swali.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Je, Serikali ipo tayari kusimamia mazao haya badala ya kuviachia Vyama vya Ushirika?

SPIKA: Mheshimiwa wa Waziri mwenyewe wa Kilimo, majibu ya swali hilo, Serikali mpo tayari?

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza si kweli kwamba tumeachia Vyama vya Ushirika kusimamia mazao. Mazao mengi hasa ya kimkakati yanasmamia na Bodi za Mazao ikiwemo Bodi ya Korosho na Vyama Ushirika vimekuwa vinakusanya hayo mazao na kuyapeleka sokoni kwa ajili ya kuuza kwa niaba ya wanachama si kwamba vinasimamia uzalishaji na hili tutaendelea kulifanya kazi na tutaendelea kulismamia.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka kusema tu kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tunataka mazao yote, pembejeo zote, kuanzia mbegu, mbolea viuadudu, hivi vyote vitakuwa vinasambazwa na sekta binafsi katika maeneo yote. Tunataka Watanzania watumie fursa hii kuona kwamba sasa ni wakati mwafaka kuna fursa ya kupeleka viuadudu vya korosho, pamba, kahawa na katika mazao yote tunataka sekta binafsi isambaze vitu vyote hivyo badala ya kutegemea Serikali. Serikali sisi tutasimamia kuratibu maendeleo ya zao na namna ya kutafuta masoko lakini siyo kusambaza pembejeo ni fursa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe tu Mheshimiwa Kuchauka na Watanzania wote wanaotaka kusambaza sulphur huko kwenye zao la korosho, wanaotaka kupeleka viuadudu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

huko kwenye pamba, wanaotaka kupeleka kwenye kahawa, kwenye tumbaku sio Vyama vya Ushirika ni sekta binafsi. Sisi tutasimamia ubora wa usambazaji wa vitu hivyo ili viwafikie wakulima.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na niwaombe Watanzania watumie nafasi hiyo.

SPIKA: Ahsante sana, ni fursa muhimu hiyo. Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, swali liwe fupi sana.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inahimiza sana kilimo.

Je, Serikali inasemaje kutokana na zoezi linalowavunja moyo wakulima wa Urambo la wakulima kunyaing'anywa mali zao, nyumba zao na wengine mpaka wamekimbia miji yao kutokana na madai kwamba waliuza isivyotakiwa kwa mauzo ya tumbaku ya mwaka 2016/2017. Serikali inatoa kauli gani kuhusu hili zoezi linalowavunja moyo wakulima wa Urambo? (Makofii)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu ya swali hilo muhimu la watu wa Urambo.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto mbalimbali katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo eneo la Urambo kwa baadhi ya viongozi wa Vyama vya Ushirika waliingia kwenye matatizo kwa sababu waliuza tumbaku ya wananchi bila kufata taratibu na wali-collude na wafanyabiashara na hivyo kuathiri bei ile ambayo ingetokana na soko.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, tulikabidhi taarifa kamili ya ukaguzi TAKUKURU ili wawafuutilie viongozi mbalimbali wale ambao walikiuka maadili ya viongozi na ambao hawakusimamia mazao sawasawa wakasababisha hasara kwa wananchi na kwenye Vyama vya Ushirika. Hilo zoezi linaendelea nchi nzima wale viongozi wote wanakamatwa na TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa amesema wananchi wanakamatwa, TAKUKURU sidhani kama wanakamata wananchi ambao hawakuvunja hizi taratibu, ila kama kuna tatizo kama hilo, sisi tutafuutilia sasa hivi, tutaongea na viongozi wa TAKUKURU ili watuambie ni kitu gani kinachoendelea kwa wananchi wa Urambo ili tuweze kuhakikisha kwamba tunashirikiana na TAKUKURU na kuchukua hatua kwa wale ambao ni wabadhirifu badala ya wananchi wa kawaida wale ambao ni wakulima, ahsante.

SPIKA: Bado tuko Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

Na. 55

Ucheleweshwaji wa Pembejeo kwa Wakulima

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Je, Serikali inasema nini juu ya ucheleweshwaji wa pembejeo za kilimo hasa mbegu na mbolea ambazo huwasababishia wakulima hasara?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kllimo, Mheshimiwa Omary Mgumba tafadhali

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Jimbo la Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upungufu wa mbolea nchini umechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kuchelewa kupatikana kwa mahitaji kutoka kwa makampuni ya mbolea hapa nchini; kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutokana na bei nzuri ya mazao kwa msimu wa 2018/2019; kuongezeka kwa kilimo cha kibashara baada ya Serikali kuwashakikisha wakulima kuwa haitafunga mipaka na kuingilia upangaji wa bei za mazao ya kilimo; na kuwepo kwa mvua nydingi ambazo zimesababisha kuongezeka kwa viwango vya matumizi ya mbolea kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2019/2020 upatikanaji wa pembejeo zikiwemo mbegu bora hadi kufikia Desemba, 2019 ni tani 71,155.13. Kati ya hizo, tani 58,509.9 zimezalishwa nchini, tani 5,175.79 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 7,469.44 ni bakaa ya msimu 2018/2019. Aidha, upatikanaji wa mbolea hadi kufikia tarehe 30 Januari, 2020 ni tani 410,499 zikijumuisha tani 92,328 za UREA na tani 84,311 za DAP. Kati ya hizo, tani 225,417 zimeingizwa kutoka nje ya nchi, tani 16,685 zimezalishwa ndani ya nchi na tani 168,397 ni bakaa ya msimu wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa upungufu wa pembejeo nchini, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya ndani ya nchi. Hatua hizo ni pamoja na kutoa vibali kwa wasambazaji wakubwa wa mbolea kuagiza nje ya mfumo wa BPS kutokana na mahitaji ya wakulima na soko ambapo tani 200,000 zimeagizwa na hadi kufikia tarehe 30 Januari, 2020; kutoa kibali cha kuagiza tani 45,000 kwa Umoja wa wasambazaji na wauzaji wa pembejeo za kilimo; na kuagiza mbolea tani 43,000 kwa kutumia mfumo wa BPS ambapo mbolea hiyo imeanza kuingia nchini na kusambazwa nchini tangu tarehe 28 Januari, 2020. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuboresha mifumo ya uzalishaji, uthibiti na usambazaji wa pembejeo nchini ambapo sekta ya umma na binafsi zitashirikisha na kuhamasishwa kuzalisha pembejeo nchini ili kukidhi mahitaji.

SPIKA: Mheshimiwa Kikwembe

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini nzuri za Serikali kutaka kuhakikisha wananchi wanapata mazao yao pindi wanapokuwa wamelima vizuri lakini napenda kujua, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inafanya utafiti wa kutosha kuhusiana na aina ya mbegu na aina ya mbolea pamoja na aina ya udongo wa sehemu husika ili wananchi waweze kulima vizuri na wasiweze kupata hasara? Katika Mkoa wangu wa Katavi, Jimbo la Kavuu mahindi yameenda vizuri na mvua hizi lakini bado kuna mdudu ambaye amekuwa akishambulia mahindi na hivyo kusababisha hasara.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Mkoa wa Katavi na Mikoa mingi ya Kusini Magharibi imekuwa ikitajwa kama ni mikoa ya uzalishaji wa mazao ya chakula yakiwemo mahindi, mpunga na maharagwe.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mkakati gani hususan katika Mkoa wa Katavi kuhakikisha kwamba inafanya utafiti na ku-introduce zao la biashara kwa wakulima wa Mkoa wa Katavi ili waweze nao kutoka kwenye masuala ya mazao ya chakula waende sasa kufanya biashara katika mkoa huo? Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba watu wao wanapata mazao ya kibiashara?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhali

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali kwanza tuna Kituo chetu cha Utafiti cha Mlingano Tanga ambacho tumekipa jukumu mahsus kwa ajili ya utafiti wa udongo kuangalia afya ya udongo na tabaka la udongo ili kufahamu kwamba udongo wa sehemu husika unakubali mazao gani, una upungufu wa virutubisho vya ardhi vya mbolea kiasi gani ili sasa kumwelekeza mkulima kulima kulingana na ikolojia ya eneo lake na mazao yanayokubali kutokana na ardhi ile.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo ya awali tumeshamaliza kwenye mikoa zaidi ya 16 na sasa hizi pia tumetambulisha maabara yetu kama pale SUA na Chuo cha Kibaha (TARI) kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, niwahamasishe wakulima wote kuchukua nafasi hasa kwenye kilimo cha biashara ni vizuri kufanya utafiti wa udongo kabla ya kulima kwa sababu ardhi imeshachakaa sana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mkakati wa Serikali tuliokuwa nao kwa ajili ya kutambulisha mazao ya biashara katika mikoa ya Nyanda za Juu hususan katika Mkoa huu wa Katavi. Kwanza hili ni swali zuri sana na ni mkakati wa Serikali sasa hivi kuwatengenezea wakulima kuwa na kiiunua mgongo wakati wanapofikisha miaka zaidi ya 60 kwa sababu kuendelea kulima mazao muda mfupi mahindi na mpunga maana yake ni kuwalazimisha wakulima kulima mpaka kufa. Katika mipango hii ya Serikali katika Mkoa wake wa Katavi, mwaka huu tumeshaanza kuzalisha miche zaidi ya 600,000 ya korosho na tumeshagawa sasa hivi katika Wilaya ya Tanganyika miche zaidi ya 250,000 na tarehe 8 mwezi huu tunakwenda kugawa miche iliyobaki ya korosho zaidi ya 350,000 katika Wilaya zote za Mkoa wa Katavi ili sasa kutambulisha na kuhamasisha wakulima hawa wakalima mazao muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, vilevile mwaka huu temegawa zaidi ya miche 800,000 ya kahawa katika Mkoa huo huo wa Katavi na mwaka huu unaokuja katika bajeti tumeponga kuzalisha miche 1,000,000 ya kahawa, miche 1,000,000 ya korosho na miche 1,000,000 ya maparachichi ili kwenda kuipanda katika Mkoa huo wa Katavi. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napata tabu sana na hili swali la Mheshimiwa Muhammed, Muhammed. Swali lake jinsi lilivyo hata Waheshimiwa Wabunge mkilitazama mtaona lilivyokakaa, nalifuta swali hili.

(Swali Na. 56 limefutwa kwa Maelekezo ya Kiti)

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali la Mheshimiwa Joseph Haule, Mbunge wa Mikumi.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 57

Kufuta Umiliki wa Mashamba Pori – Jimbo la Mikumi

MHE. JOSEPH L. HAULE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafuta umiliki wa mashamba pori ya muda mrefu ya Mauzi Estate, Miyombo Estate, Sumagro Estate Kisanga Estate (Lyori Estate) yaliyopo kwenye kata za Tindiga, Masanze, Kilangali na Kisanga na kuyagawa kwa wananchi wanyonge ili waweze kupata maeneo hayo wanayoyahitaji sana ili kufanya shughuli zao mbalimbali za kujiletea maendeleo?

SPIKA: Mheshimiwa Lukuvi, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuchukua hatua dhidi ya wamiliki wote wa ardhi nchini ambao wameendelea kukiuka masharti ya kumiliki ardhi ikiwemo kutoendeza ardhi kwa mujibu wa sheria na taratibu; kuendeleza ardhi kinyume na masharti ya umiliki; na kutolipa kodi ya pango la ardhi.

Kwa upande wa mashamba, katika kipindi cha kuanzia Disemba, 2015 mpaka sasa, jumla ya milki za mashamba 45 zimebatilishwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa Mkao wa Morogoro, jumla ya mashamba 15 yamebatilishwa ambapo mashamba 10 kati ya hayo yapo katika Wilaya ya Kilosa anapotoka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliunda timu ya kupitia mashamba yote yaliyobatilishwa katika Mkao wa Morogoro pamoja na kukagua mashamba yenyе sifa za kubatilishwa. Mashamba ya Mauzi Estates, Sumagro Estates, Kisanga Estates na Miyombo ni mionganoni mwa mashamba ambayo timu yangu iliweza kuyakagua na hatua za ubatilisho wa milki zinaendelea. Jumla ya mashamba yaliyokaguliwa na kupendekezwa kubatilishwa ndani ya Mkao wa Morogoro ni 23 na yote yapo katika Wilaya ya Kilosa. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imeelekezwa kufanya taratibu za ubatilisho kwa mashamba hayo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ambazo zimebaini kuwepo kwa mashamba yasiyoendelezwu katika maeneo yao, kuwasilisha Wizarani mapendekewe ya kubatilisha milki za mashamba husika ili taratibu za kuyabatilisha zikamilishwe kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (Sura113).

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Haule, Mbunge wa Mikumi.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nisema kwa masikitiko makubwa sana Wilaya ya Kilosa ni moja kati ya Wilaya zinazoongoza kwa migogoro mikubwa sana ya mashamba na migogoro mikubwa sana kati ya wakulima na wafugaji kutohana na upungufu wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika Kata ya Tindiga kumekuwa na mgogoro mkubwa sana kati ya Kijiji cha Tindiga na NARCO ambao wamemega eneo la Tindiga na kuwapa wafugaji lakini kulikuwa na kesi tangu mwaka 2013 mpaka 2019 wananchi wa Kijiji cha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tindiga wameshinda lakini mpaka leo wanazuwa kulima na ndiyo tunaowategemea kwa kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumetokea maafa makubwa sana akina mama wamebakwa na wakulima wamepigwa vibaya sana na kulazwa hospitali kwa sababu ya kuzuiwa kwenda kulima. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Tindiga ambao wameshinda kwenye Mahakama ya Ardhi ili warudishiwe ardhi yao? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali ilitoa mashamba kwa wawekezaji katika Kata ya Kisanga, Kata ya Masanze pia Sumargo pale Kilangale. Hata hivyo, hawa wawekezaji wameshindwa kutumia mashamba haya ipasavyo na kupoteza ajira kwa wananchi na Serikali inakosa mapato mengi kwa sababu yale mashamba ni pori na hayatumiki. Imeleta migogoro mikubwa sana pale Masanze mtu alipgwa risasi akafariki, pale Kisanga mwananchi alipgwa risasi akafariki, pale Sumargo, Kilangali migogoro ni mikubwa watu wanaumia sana. Wizara ya Ardhi mnatoa kauli gani kwa Wilaya ya Kilosa ili wananchi waweze kurudishiwa mamshamba haya na kuyaendeleza kwa kilimo ili kusaidia Taifa letu la Tanzania? (Makofii)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Haule, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza juu ya wananchi wa Tindiga, wiki iliyopita niliongea na wananchi hawa waliletwa na Mheshimiwa Mbunge, nimekubaliana naye aniletee mimi barua na vielelezo hivyo vya kesi, maana mimi siwezi kujua yanayoendelea na kesi na mimi nina wanasheria, walete hizo hukumu za kesi kama kweli wameshinda mimi nitawasaidia ili wapate haki yao. Tulishaelewana na nafikiri alitaka hapa sasa wananchi wengi zaidi wasikie. Serikali lazima itekeleze uamuzi wa Mahakama na Serikali haiwezi kumwonea mtu. Kwa hiyo, fanyeni yale niliyowaelekeza leteni barua na vielelezo vile ili tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, la pili, swali hili ni swali la msingi ambalo umeuliza. Katika mashamba ambayo yameshafutwa Mkoa wa Morogoro 15 yanatoka Wilaya ya Kilosa. Niliunda timu ya wizara, ilipokwenda kukagua mashamba yote ya Kilosa tukagundua kuna mashamba mengine mapya 23 ambayo yana sifa ya kufutwa pamoja na haya uliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu wa kufuta hauanzii Wizarani unaanzia Wilaya ya Kilosa. Tulikuwa na timu ya hovyo pale wilayani Maafisa Ardhi waliokuwa wanafanya kazi ile pale wao sio Maafisa Ardhi walikuwa wamejivisha tu Uafisa Ardhi lakini hatukuwa na Afisa Ardhi. Kwa hiyo, tumefanya utaratibu tumeleta Maafisa Ardhi, kuna Afisa Ardhi mzuri sana tumemtoa kutoka Mkoa wa Mbeya tumempeleka pale sasa ndio wanaanza kazi ya utaratibu wa awali wa kisheria wa kusababisha haya mashamba yafutwe.

Mheshimiwa Spika, lazima notice ya wale wenye mashamba itolewe na Afisa Ardhi Mteule wa Wilaya ya Kilosa hamkuwa naye. Kwa hiyo, nimeelekeza huyo Afisa Ardhi aanze na mashamba haya. Hivi sasa ameshatoa notice ya siku 90 kwa wenye mashamba wajieleze kwanza hatua itapanda itafika kwangu tukiridhika na maelezo yao kwamba wanazo sifa za kufutiwa tutampalekea Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Nishati, swali la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 58

Utekelezaji wa Miradi ya REA III Mkoa wa Mtwara

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA aliuliza:-

Mkoa wa Mtwara una jumla ya Vijiji 869 na Vitongoji 1,826 na jumla ya Vijiji 372 vimethibitishwa kupatiwa umeme ikijumuishwa kufanya Vijiji vitakavyosalia kuwa 497 na hii ni sawa na wastani wa 23.6% ya utekelezaji wa huduma kwa kila Wilaya ndani ya Mkoa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza miradi ya REA katika mkoa huu?

(b) Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Mji wa Masasi ilitengewa Vijiji saba tu kati ya Vijiji 31, je, ni lini vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Engineer Stella Manyanya, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini katika vijiji vyote vya Tanzania Bara. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2021. Mradi wa REA III Mzunguko wa Kwanza unaoendelea unapeleka umeme katika vijiji 167 vya Mkoa wa Mtwara.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Mji wa Masasi mradi wa REA III Mzunguko wa Kwanza unatekelezwa katika vijiji saba ambapo hadi kufika Januari, 2020 vijiji vitatu vya Mumbaka, Mlundelunde na Chanikanguo vimewashiwa umeme. Aidha, mkandarasi anaendelea na kazi za mradi katika Vijiji vya Mayula, Minazini, Mtakuja na Nangose A na B. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi zitakamilika mwezi Aprili, 2020. Gharama za kupeleka umeme katika Wilaya ya Masasi ni shilingi milioni 658.

Mheshimiwa Spika, vijiji 20 vilivyobaki katika Wilaya ya Masasi vinatarajia kupelekewa umeme kuitia mradi wa REA III Mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza mwezi Februari, 2020. Mradi huu utakamilika mwezi Juni, 2021.

SPIKA: Mheshimiwa Chuachua.

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza kwa kuwa mpango ulikuwa ni kupeleka umeme katika vijiji saba na mkandarasi kwa sasa hayoko site isipokuwa kwenye kijiji kimoja ambacho amepeleka umeme kwenye kaya saba peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haioni haja ya kumfukuza mkandarasi huyu ambaye hafanyi kazi kwa kasi inayohitajika kwa kuwa site hayupo na kwa sababu ni vijiji vichache sana ambavyo vimewekewa umeme na pia alipewa vijiji vichache?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tumeambiwa Mji wa Masasi umeungwa na Grid ya Taifa kutokea Mkoa wa Ruvuma lakini hali ya kukatikakatika kwa umeme ni mbaya zaidi kuliko hata kabla haijaungwa. Ni juhudhi gani sasa zinatakiwa zifanywe na Serikali kuhakikisha kwamba inawaondoa wananchi wa Masasi katika adha hii kubwa nay a muda mrefu ya kukatikakatika kwa umeme? Ahsante sana. (Makofii)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, baadhi ya wakandarasi hata hapa Dodoma utendaji wao ni mdogo sana. Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chuachua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mkandarasi ambaye yuko site, kwanza tunataka atimize wajibu wake kwa mujibu wa mkataba aliousaini. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala hilo litafuatiliwa ili kujuu tatizo lake ni uwezo au ni jambo gani ili aweze kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya pili, niseme tu kwamba kwa ufahamu nilionao ni kwamba kwa sasa bado Masasi haijaungwa kutoka kwenye Gridi ya Taifa kutoka Mkoa wa Ruvuma kwa sababu hata hiyo *line* haijajengwa isipokuwa kuna mpango wa kufanya hivyo. Naamini endapo utekelezaji huo utafanyika, hali ya Mji wa Masasi itakuwa ni bora zaidi ikizingatiwa kwamba umeme ambaa umekuja mpaka Songea Mjini Ruvuma ni wa KV 220 na capacity ya megawatt 60 ni mwingi na unatosheleza kupeleka mpaka maeneo hayo.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami napenda kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri yangu ya Mtwara Vijiji ninazo kata mbili za Moma na Muungano ambazo mpaka sasa hivi mkandarasi hajaweka umeme hata kijiji kimoja. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba anawapelekea wananchi hao umeme kwa haraka?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Engineer Stellah Manyanya tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Ghasia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya kuweka umeme kuna hatua. Hatua ya kwanza ni mipango kama kawaida na ku-plan network kama itakavyokuwa. Hatua ya pili ni ya kujenga kwa mfano kujenga *line* kubwa au *line* ndogondogo na baada ya hapo kuweka transforma na kuwasha. Katika misingi hiyo niseme tu kwamba nalichukua kama ambavyo umeeleza kumfuatilia huyo mkandarasi tuone kwamba hajafanya kitu kabisa au yuko kwenye hatua ambazo zimebakiza kuweka transforma tu na kuwasha.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wakandarasi wote nchini kwamba suala la umeme katika vijiji kama ambavyo Serikali inategemea kusambaza umeme katika vijiji vyote Tanzania ni la muhimu hasa ikizingatiwa katika kipindi hiki ambacho Watanzania wanahitaji kuwekeza katika viwanda na shughuli mbalimbali za kibashara na maisha yao.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, niwaombe wakandarasi, Serikali imewapa heshima, hasa wakandarasi wa ndani kuwapa nafasi ya kufanya kazi hizo badala ya kuwategemea wakandarasi wakubwa kutoka nje, watumie wakati huo mzuri na watumie nafasi hiyo kuhakikisha kwamba hawaiudhi Serikali na kusababisha kuwanyang'anya kazi na kuwapa kazi wakandarasi kutoka nje jambo ambalo walikuwa wakiliilalamikia siku zote.

SPIKA: Bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Nishati, swali litaulizwa na Mheshimiwa Halima Zitto Kabwe, samahani, Halima Abdallah Bulembo. (Kicheko)

Na. 59

Mabadiliko ya Rangi za Nyaya za Umeme

MHE. HALIMA A. BULEMBO aliuliza:-

Katika viwango vya kidunia vya umeme vile ambavyo tunavyofuata, kuna mabadiliko ya rangi za nyaya za umeme yaliyotokea tangu mwaka 2004 kwa nchi yetu ya Tanzania:-

Je, mabadiliko hayo yanafahamika kila mahali?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya rangi za nyaya za umeme ni jambo la kawaida katika taaluma ya uhandisi wa umeme, hivyo mitaala yote ya mafunzo ya uhandisi wa umeme yanazingatia mabadiliko haya. Mabadiliko ya rangi za nyaya za umeme yalitokea mwaka 2004 na hivi sasa yanafundishwa nchini kuititia Vyuo vya Ufundis Stadi (VETA), Vyuo vya Ufundis Mchundo na Vyuo Vikuu. Aidha, somo la rangi za nyaya za umeme linafundishwa katika somo la Fizikia katika shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa umeme mkubwa kimazoea (*high voltage*) unakuwa na rangi tatu ambazo ni nyekundu, njano na bluu. Nyaya za rangi hizo huwa ni moto. Vilevile kwa umeme mdogo (*low voltage*) unaotumia njia tatu (*three phase*) unakuwa na rangi nne ambazo ni nyekundu, njano, bluu na nyeusi. Kwa upande wa umeme wa njia moja (*single phase*) unakuwa na rangi mbili nyekundu na nyeusi.

Mheshimiwa Spika, kutohana na mabadiliko hayo yaliyoanza mwaka 2004 na kukamilishwa mwaka 2006 ya BS 7671 (*British Standard*) iliyowianishwa rangi mpya kwa umeme mkubwa (*High Voltage*) ni kahawia, nyeusi na kijivu kwa umeme mdogo (*low voltage*) *three phase*, rangi mpya ni kijani yenye mchanganyiko na njano, bluu kwa nyaya za moto ni kahawia nyeusi na kijivu. Kwa upande wa njia moja (*single phase*) unakuwa na rangi mbili za kahawia na bluu. Serikali itaendelea kutoa elimu kwa watu wote wanaohusika na matumizi ya rangi hizi ikiwemo wakandarasi, wafanyabiashara, wenye viwanda na wananchi kwa ujumla.

SPIKA: Mheshimiwa Halima, swali la nyongeza nimekuona.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa niishukuru Wizara kwa majibu yao mazuri lakini kiukweli mabadiliko hayajaanza kufundishwa vyoni wala shuleni na TANESCO wamekuwa wakitumia nyaya za zamani. Kwa hiyo basi, kuna mkanganyiko mkubwa zaidi na ukizingatia sasa hivi tuko katika uchumi wa viwanda. Hivyo basi, naomba Serikali yangu itafute namna sahihi ya kutatua mkanganyiko huu ili kuепusha athari zinazoweza kujitokeza katika kuchanganya nyaya za umeme. Nakushukuru. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Si swali as such, ni ushauri. Kwa hiyo, naomba tu muupokee.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI): Mheshimiwa Spika, pamoja na kupokea ushauri kwa sababu jambo hili ni la muhimu, naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi hizi rangi hazina athari kwa ujumla wake isipokuwa chimbuko la mabadiliko haya ya rangi ilikuwa ni kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi kwa upande wa wenzetu ambao tumekuwa tukichukua standard zao (Commonwealth) walipokuwa wameungana na hawa nchi za Ulaya. Kwa hiyo, unakuta watu wa AU walikuwa na standard zao na watu wa British walikuwa na standard zao ilibidi wawianishe na ndiyo zikatokea hizi rangi nyiningine ambazo zimejitokeza.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mazoea, watu wetu walikuwa wamezoea mtindo huu wa red yellow, blue. Sasa kinachofanyika ni kwamba kupitia TBS, kuanzia mwaka 2010 tulianza kufanya huo uwianisho na tayari tumeshafikia hatua nzuri. Vilevile ili kuondoa hizi changamoto ambazo zinaweza kusababisha madhara kutokana na watu kuchanganya hizo rangi japo pia tunasisitiza na sheria inasema kwamba mtu anayefanya wiring installation iwe kwenye high voltage au low voltage lazima awe na uwezo wa kutosha na awe amethibitishwa au kama akifanya mtu mwingine asiyethibitishwa lazima apeleke kwa aliyethibitishwa.

Kwa hiyo, tunategemea kwamba TBS itakuja na huo mwongozo maalum unaoelekeza hizi standards ili sasa ziweze kutumika kwa mkazo zaidi. Hata hivyo, suala la mpito hilo hata kwenye nchi nyiningine lilifanyika.

Mheshimiwa Spika, pia nawaomba wakandarasi wanapokuwa wamefanya kazi inayochanganya mfumo wa zamani na mfumo wa sasa, waweke maelekezo pale kwenye main switch ili mtu yejote anayefika aweze kujua kwamba mfumo huu umechanganya.

SPIKA: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali litaulizwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Mheshimiwa Nyina Mtemi.

Na. 60

Vifo Vitokanavyo na Uzazi

MHE. ANNE K. MALECEL aliuliza:-

Vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga bado ni tatizo nchini:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani kupunguza na ikiwezekana kuondosha kabisa vifo hivyo?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo kutoka kwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhalii.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeboresha Vituo vya Afya zaidi ya 352 na vingine kujengwa upya ili vitoe huduma zote za afya ya uzazi kabla na wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua ikiwemo kumtoa mtoto tumboni kwa njia ya operesheni na kuzijengea uwezo wa kutoa huduma ya damu salama kwa watakaohitaji. Aidha, Hospitali 67 za Halmashauri zinajengwa ili huduma ziwatifikie wananchi wote wa vijijini na mijini kwa usawa na urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba upatikanaji wa dawa na vifaa tiba vinakuwepo muda wote, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 270 mwaka 2018/2019. Juhudi hizi zimewezesha wajawazito kuendelea kupata huduma za afya ya uzazi na mtoto ikiwemo kinga tiba dhidi ya Malaria (SP), Fefol ambayo ni madini ya chuma na folic acid ambayo ni kinga tiba dhidi ya upungufu wa damu, vipimo vya shinikizo la damu, kaswende, wingi wa damu, sukari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwezi Agosti 2019, Wizara ilizindua na kusambaza nchi nzima mwongozo wa kitaifa wa matibabu ya watoto wachanga na uanzishwaji wa vyumba maalum vya matibabu ya watoto wachanga "National Guideline for Neonatal Care and Establishment of Neonatal Care Units" mwongozo huu unalenga kuwajengea uwezo watoa hudumu juu ya huduma muhimu kwa watoto wachanga. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na wadau wa UNICEF wameanza kusambaza vifaa mbalimbali kwa ajili ya vyumba hivyo maalum vya watoto wachanga kwa baadhi za hospitali za mikoa na Halmashauri.

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi ambavyo inajitahidi kuboresha afya ya Watanzania lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamoja na jitihada za Serikali lakini kuna tatizo kubwa ambalo liko vijijini na mijini, wanawake wengi bado wakiwa wajawazito hawana ile elimu ya kuona kwamba ni muhimu waende *clinic*. Sasa Serikali mnajitahidi kiasi gani kuhakikisha wanawake wakiwa wajawazito vijijini pamoja na mijini wanakwenda *clinic?* (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tafiti zilizofanywa katika nchi yetu ya Tanzania, bado watoto ambao wana chini ya umri wa mwezi mmoja baada ya kuzaliwa wanakufa kwa wingi na ukweli tafiti zimeonesha kwamba hawajapungua kabisa, wanaendelea kufa. Serikali mnaniambia nini katika hili? (*Makofî*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpa pongezi sana amekuwa ni champion mkubwa sana katika masuala ya afya ya uzazi wa akina mama na mtoto. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudhi zake hizo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika maswali mawili mawili ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaauliza. La kwanza ni kuhusiana na akina mama kwenda kliniki. Ni kweli, Serikali imewekeza juhudhi kubwa sana katika kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya. Mwaka 2015 idadi ya akina mama ambao walikuwa wanakwenda *clinic* ilikuwa ni asilimia 38 kwa mara zote nne katika kipindi cha ujauzito lakini Serikali imeendelea kuweka juhudhi, mikakati mbalimbali pamoja na kutoa elimu kwa akina mama, hivi tunavyoongea hadi kufikia Desemba 2019, asilimia 80 ya akina mama wanakwenda kiliniki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii nayo ni hatua kubwa sana katika kuhakikisha akina mama wanapata elimu, ushauri katika kipindi chao cha ujauzito na hii inaweza kusababisha hata kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Nitoe rai kwa akina mama wote na akina baba kwa sababu masuala haya ya ulezi wa ujauzito ni jukumu la wazazi wote wawili kuhakikisha kwamba kila mama mijamzito anafika kliniki kwa ajili ya kuweza kupata ushauri nasaha na jinsi gani ya kuweza kutunza ujauzito ule.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili vifo vya watoto chini ya mwezi mmoja, ni kweli katika takwimu ambazo hazishuki ni pamoja na hii. Katika mwaka 2015, tulikuwa na watoto wachanga chini ya mwezi mmoja wakifariki 26 kwa vizazi hai 100,000. Sasa hivi tunapoongelea Desemba mwaka jana imeshuka kwa *unit* moja tu mpaka 25 kwa vizazi hai 100,000.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi kama Serikali tunajaribu kuweka hatua, kwanza kuhamasisha akina mama kwenda kliniki; pili kuhakikisha kwamba chanjo zote za msingi za watoto chini ya miaka mitano zinapatikana; kutoa elimu kwa watoa huduma wa afya pamoja na akina mama ikiwa ni pamoja na jinsi ya kutunza watoto njiti. Visababishi vikubwa vya watoto chini ya mwezi mmoja ni zile *complication* ambazo wanazipata wakati wa kupumua wakati wa kujifungua, maambukizi ya magonjwa ambayo wanayapata wakati wa kujifungua ikiwa ni pamoja na uzito wa chini.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo mikakati ambayo tumejaribu kuifanua kwa kupanua huduma za afya kuhakikisha kwamba akina mama wajawazito ambao wana pingamizi wanapata huduma kwa haraka. Tumepunguza sana maambukizi ya watoto hawa na kuhakikisha wale watoto njiti wanatunza kwa njia ya *kangaroo motherhood* ambapo kwa kiasi kikubwa tunaamini sasa tutapata matokeo makubwa sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, bado tupo Wizara hii hii.

Na. 61

Ugonjwa wa Mguu Kifundo

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA aliuliza:-

Ugonjwa wa Mguu Kifundo unatibika katika Hospitali ya Rufaa Kitete – Mkoani Tabora ambapo hupokea zaidi ya Watoto 40 wenye tatizo hilo kila mwezi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa vya kutosha kama vile POP, bandeji, pamba, kiatu na gongo-pinde ili kusaidia watoto hao?

(b) Kutokana na ukubwa wa tatizo hilo kwa watoto Mkoani Tabora na familia nyingi hazina uwezo wa kufika Hospitali kupata huduma; je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ili watoto wengi zaidi waweze kupata huduma hiyo?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Majibu ya swali hilo kutoka kwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utoaji wa huduma hizi, vifaa tiba vya huduma za utengemao vimeingizwa katika mfumo wa ununuzi wa Bohari ya Dawa (MSD) kuanzia mwaka 2018/2019 na hivyo kufanya upatikanaji wa POP bandeji, pamba na viatu na gongo-pinde kupatikana kwa uhakika. Aidha, Wizara imeagiza waganga Wafawidhi na Wafamasia katika vituo vya kutolea huduma za afya kupeleka mahitaji yao mapema Bohari ya Dawa ili pasiwepo na upungufu wa aina yoyote wa vifaa tiba ikiwa ni pamoja na vifaa hivyo vinavyotumika katika kutoa huduma za utengamao.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa tatizo hilo hapa nchini, Wizara yangu imeandaa Mpango Mkakati wa muda wa Kati (*Medium Term Strategy: 2017-2021*) unaolenga kufikisha huduma za utengemao hadi ngazi ya Wilaya ifikapo Juni 2021, ambapo kwa sasa huduma hii hupatikana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali zote Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa.

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWEIFUNGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Waziri amesema kwamba ugonjwa huu ni tatizo kubwa nchini lakini katika Mkoa wa Tabora hasa Wilaya za Sikunge, Kaliua pamoja na Uyui umekuwa ni mkubwa zaidi hadi kusababisha kila siku watoto 40 kufika katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete. Watoto hawa ni wengi sana na ndiyo hawa ambao wamejitokeza kuja hospitalini, hatujui hawa ambao hawajaja hospitalini. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wazazi kuhusu ugonjwa huu wa mguu kifundo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Daktari aliyeo katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete yupo tayari kufanya kliniki kwenye Wilaya hizi ili angalau kuwafuata wazazi ambao hawana uwezo wa kuwapeleka watoto wao Kitete?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti kidogo ili Daktari huyu aweze kufika kwenye Wilaya hizi na kuweza kutibu watoto wetu? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hili, inaelekea Wanyamwezi wana mguu kifundo sana, watoto 40 kila mwezi? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge kutoka Mkoa wa Tabora, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba mguu kifundo kwa lugha ya kitaalam tunaita Talipes ni ugonjwa ambao hutokea kwa baadhi ya watoto; mmoja kati ya watoto 1,000. Niseme

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tu kwamba mtoto akibainika mapema anaweza akapata matibabu na zaidi ya asilimia 80 ya hawa watoto miguu hurejea kuwa katika hali ya kawaida. Nitumie fursa hii kuongea na jamii ya Watanzania kusema kwamba wazazi wote ambao wana watoto ambao wana tatizo hili la mguu kifundo wawafikishe katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya ili waweze kupata huduma za utengamao. Kama nilivyosema hapo awali, ugonjwa huu unaweza ukatibika kwa kutumia utaratibu wa hizi huduma za utengamao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, sisi kama Wizara hatuna shida kama tuna mtaalam pale katika hospitali yetu ya Kitete kumpa usaidizi ili kuweza kufanya kliniki katika Wilaya zote. Hili Mheshimiwa Mbunge tunaweza tukakaa tukaangalia utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba hii huduma inaweza ikapatikana katika Wilaya nyingine ambapo si rahisi kufika katika hospitali yetu ya Kitete pale Tabora.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maji na swali la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 62

Ubore shaji wa Huduma ya Maji – Halmashauri ya Mbeya Vijijini

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Halmashauri ya Mbeya ina upungufu mkubwa wa maji karibu kwenye Vijiji zaidi ya 153 na hasa katika Kata ya Mjele. Je, Serikali ina mpango gani wakupeleka maji kwenye Vijiji hivyo na hasa Vijiji vya Mjele, Chang'ombe na Ipwizi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo toka kwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njenza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la maji lililopo katika Halmashauri ya Mbeya Vijijini, katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Serikali imepanga kutekeleza miradi tisa ya maji ambayo ni Idimi - Haporoto, Iwindi, Mshewe, Ipwizi, Mjele - Chang'ombe, Galijembe, Nsenga - Wimba, Iyawaya na Isangala group. Kiasi cha shilingi bilioni 6.4 kimetengwa katika bajeti ya 2019/20 kwa ajili ya kazi hiyo. Hadi kufikia mwezi Disemba 2019, jumla ya miradi 2 ya Idimi - Haporoto na Iwindi imekamilika na kiasi cha fedha shilingi bilioni 1.5 kimetumika katika ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kukamilisha miradi yote iliyopo kwenye bajeti ya 2019/2020, jumla ya vijiji 21 vitapata huduma ya maji vikiwemo vijiji vya Mjele, Chang'ombe na Ipwizi ambapo jumla ya wakazi wapatao 44,364 watanufaika.

SPIKA: Mheshimiwa Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza nianze kuipongeza Serikali na kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa usimamizi mzuri wa utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Mbeya.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa bajeti ya ziada ya shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya mradi wa maji uliotolewa kwa ajili ya Mji wa Mbalizi pamoja na Kata za Bonde la Songwe na Ilota. Pamoja na pongezi hizo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni lini miradi ya maji itapelekwa kwenye Vijiji vya Illembu, Santilia, Inyala pamoja na Irukwa ambapo kunajengwa vituo vya kisasa vya afya na pia kuna Hospitali ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini sasa Mradi wa Mbalizi utakamilika kuhakikisha wananchi wa Bonde la Songwe, Ilota na Mji Mdogo wa Mbalizi wanapata huduma ya maji ya uhakika? Nashukuru sana. (Makofii)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayofanya katika Jimbo lake. Sisi kama viongozi wa Wizara, mimi pamoja na Waziri wangu tulishafika kule kuhakikisha Mradi wa Mbalizi wa kiasi cha shilingi bilioni 3 tunausimamia ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sasa hivi baadhi ya kazi zinafanywa na wataalam wetu wa ndani wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya. Ndani ya mwezi Machi, mradi ule utakamilika na wananchi wa Mbalizi watapata huduma ya maji. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi katika Vijiji vya Santilia pamoja na Illembu na Irukwa tulipata fedha zaidi ya shilingi bilioni 25 za Lipa kwa Matokeo na wafadhili wa DFID na Kijiji hiki cha Santilia kipo. Sasa tupo katika hatua ya manunuzi kuhakikisha tunaukarabati mradi ule na wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu ya maji.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kumhakikishia kwa Vijiji vya Illembu na Irukwa katika awamu hii inayokuja ya fedha za Lipa kwa Matokeo tutaviweka katika kuhakikisha nao wanapata huduma hii muhimu sana ya maji. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki. Mheshimiwa Kiula, tafadhalii.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa ruhusa yako naomba nitoe shukrani zangu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufulsi, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, wewe mwenyewe, Wizara ya Afya na TAMISEMI kwa kutoa shilingi milioni 700 kukarabati Kituo cha Afya Kinyambuli.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba tarehe 30 upasauji wa kwanza wa kihistoria umefanyika Mkalama na tumepata mtoto wa kike. Ahsanteni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba sasa swali namba 64 liweze kupatiwa majibu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 63

Ujenzi wa Barabara ya Iguguno – Meatu Kwa Kiwango cha Lami

MHE. ALLAN J. KIULA aliuliza:-

Barabara itokayo Iguguno –Nduguti –Sibiti hadi Meatu ni kiungo muhimu cha Mikoa ya Singida na Simiyu:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo hasa ikizingatiwa kuwa kazi kubwa ya ujenzi wa Daraja la Sibiti imekamilika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo na tunaishukuru Serikali kwamba daraja la Sibiti limekamilika sasa. Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Bariadi – Kisera – Mwandoya – Ngoboko – Mwanhuizi – Sibiti – Mkalama hadi Iguguno Shamba yenye urefu wa kilometra 289 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Sehemu kubwa ya barabara hii ni ya changarawe na inapitika wakati wote wa mwaka.

Aidha, ujenzi wa Daraja la Sibiti na barabara unganishi kwa kiwango cha changarawe zenyne urefu wa kilometra 25 umekamilika. Hata hivyo, taratibu za manunuzi ziko katika hatua ya mwisho kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara hizo unganishi zenyne jumla ya urefu wa kilometra 25.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini nilizotaja, mkakati wa Serikali kwa sasa ni kukamilisha kuunganisha makao makuu ya mikoa kwa barabara za lami na kujenga barabara kuu zote zinazounganisha Tanzania na nchi jirani kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa kwenye Shoroba za Maendeleo (*Development Corridors*). Baada ya hapo, barabara nyingine ikiwembo ya Iguguno – Mkalama – Sibiti – Mwanhuizi – Ngoboko – Bariadi zitafuata kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Kiula, nimekuona.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, naishukuru tena Wizara kwa kazi kubwa inayofanyika hasa kwa kukamilisha Daraja la Sibiti. Napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Wizara ipo tayari kujenga kilometra 40 kutoka Iguguno mpaka Nduguti kabla ya barabara yoyote ile kukamilika kwa sababu shughuli nyingi zinafanyika sasa pale makao makuu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu barabara hiyo sasa ni barabara ya kiuchumi na magari mengi yanapita huko. Je, Naibu Waziri yuko tayari kufuatana na mimi baada ya Bunge hili ili akaone umuhimu wa uwekihi wa lami katika barabara hiyo? (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba juhudi kubwa zinafanyika kuunganisha mikoa. Hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Kiula tumefanya juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba barabara hii aliyoitaja kutoka Iguguno – Nduguti - Igumanga kwenda mpaka Sibiti imekuwa bora na hata kufanya ujenzi wa madaraja makubwa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Kiula kwa sababu tumejenga daraja kubwa pale Mnolo ni kwa sababu ya juhudi zake pia na ushirikiano anaoutoa. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo kuhakikisha maeneo mengi yamekuwa bora na yanapitika halafu kidogokidogo mbele ya safari tutakuwa na harakati ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuambatana na Mheshimiwa Kiula, Mheshimiwa Kiula anafahamu ipo miradi mingi inayofanyika katika eneo lake ikiwepo kwenye Daraja la Msingi kuna ujenzi mkubwa unaendelea vizuri na miradi mingine mingi ipo na ipo sababu pia ya kutembelea Mkalama. Nitatembelea huko ili tuweze kuona pia miradi mingine inakamilishwa kwa ubora mkubwa. Ahsante sana.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mwanne Nchemba, swali fupi sana.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi wa barabara za lami, Mkoa wa Tabora sasa hivi tuna matatizo makubwa ya mafuriko. Mafuriko ni makubwa, naomba Serikali itambue kwamba Tabora nayo ni mionganoni mwa mikoa yenyé mafuriko.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Tabora Manispaa, Kata ya Ipuli ambayo tunaitwa Freemason au Chuo cha Utalii pamoja na Malolo wananchi mpaka sasa wako nje, wanateseka kutokana na kutokuwa na miundombinu ya mifereji inayopitisha maji mengi. Mifereji iliyopo ni midogo mno, nimeomba univumilie kwa sababu hali tuliyonayo sasa wananchi wote wa Mkoa wa Tabora hususan Manispaa wana matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, nimuombe sasa Mheshimiwa Naibu Waziri aende Tabora akutane na Wahandisi wa TANROADS pamoja na TARURA ili watafute njia gani mbadala ya kuwasaidia wakazi wa maeneo hayo. (Makofii)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza, Naibu Waziri majibu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanne Mcchemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge maeneo mengi tumpata adha ya hizi mvua kubwa ambazo zinaendelea kunyesha. Nitumie nafasi hii nimpe pole Mheshimiwa Mbunge lakini pia niwape pole wananchi wa Tabora Mjini. Natambua maeneo haya uliyoyazungumza ya Ipuli na Malolo kuna shida na nakubaliana na ushauri wako.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunaendelea kufanya uratibu wa maeneo yote nchini kuhakikisha kwamba tunafanya maboresho.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kama nilivyozungumza hivi karibuni wakati nikijibu swal la Korogwe Mjini tuwe na ushirikiano kama Mbunge unavyosema wenzetu wa TARURA na TANROADS na upande wa Mipango Miji tushirikiane ili miji yetu hii inayokua kwa kasi lazima tuje na mipango mizuri ya kudhibiti maji ya mvua hususan tunapopata mvua nydingi namna hiyo. Kwa hiyo, nakubaliana na ushauri wako nitakwenda Tabora kufanya hivyo kama ulivyoshauri.

SPIKA: Napata malalamiko mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba joto limezidi sana humu ndani. Kwa hiyo, nataka niwaambie vijana wangu huko waongeze baridi.

WABUNGE FULANI: Hapana.

SPIKA: Baridi imezidi sana humu ndani, wataalam punguzeni hii baridi. (Kicheko)

Mbunge wa Kasulu Vijijini, Mheshimiwa Augustine Vuma uliza swal lako tafadhali.

Na. 64

Barabara ya Kasulu Mjini hadi Kibondo

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Kasulu Mjini hadi Kibondo utaanza?

SPIKA: Majibu ya swal hilo, bado tuko Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kasulu Mjini - Kibondo kilometra 149 ni sehemu ya barabara ya Nyakanazi - Kasulu kilometra 236 kuelekea hadi Kigoma na pia kutokea Kasulu kuelekea Manyovu/mpakani mwa Tanzania na Burundi kilometra 68.25.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imechukua hatua kadhaa za kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami ambapo kwa kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zimepatikana fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu ya Kabingo – Kasulu – Manyovu kilometra 260.6.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa maandalizi ya kusaini mikataba ya ujenzi yanaendelea na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2020.

SPIKA: Mheshimiwa Vuma, swal la nyongeza.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wa Kata za Kalela, Kwaga, Lusesa, Kasangezi, Muzi pamoja na Bugaga kwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kweli barabara ya kutoka Kidahwe - Kasulu sasa ni lami. Wananchi hawa tangu uhuru sasa wamepata barabara ya lami na wana furaha kubwa sana wanaishukuru Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, nini kauli ya Serikali kuhusu barabara ya kutoka Kasulu - Uvinza ukizingatia wananchi wa Kata za Lungwe Mpya na Asante Nyerere na maeneo mengine wanapata tabu sana? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, nini mipango ya Serikali kuhusu barabara ya kutoka Kitanga - Kibondo ukizingatia wananchi wa Kata za Kitanga, Kigabye na maeneo ya jirani wanapata tabu sana wanapoenda Kibondo? Nashukuru. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Vuma swalii lako la msingi ni Kasulu – Kibondo, maswali ya nyongeza barabara nyingine kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri lakini wewe ni mtu wa barabara, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Vuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Vuma kwa umahiri wake, najua anawapigania sana wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maswali yake niseme kwamba tunazitazama hizi barabara alizozitaja lakini kwa sababu tumekuwa na changamoto ya ujenzi wa barabara za lami hususan kuunganisha Mkao wa Kigoma, naomba wananchi hawa watuvumilie. Hata hivyo, niseme tu hii barabara ya kutoka Kasulu kwenda Uvinza kwa maana inaanzia pale Kanyani kwenda Kibaoni kilometra 53 tunajitahidi kuiweka barabara hiyo katika hali nzuri. Niwahakikishie wananchi wa maeneo haya ikiwemo wananchi wa Nguruka wataweza kupita vizuri.

Mheshimiwa Spika, tukikamilisha ujenzi wa barabara hii kubwa ambayo nimeitaja kwenye jibu la msingi, tutatazama namna nzuri ya kufanya ili tuone tunafanya maboresho makubwa kwenye barabara hii. Hii ni pamoja na kuiangalia kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara yake ya pili hii aliyoitaja kutoka Kitanga kwenda Kibondo ni barabara ambayo inasimamiwa na TANROADS, Mkao wa Kigoma na ipo katika hali nzuri. Niseme tu kuna changamoto katika Daraja hili la Mto Malagarasi, eneo hili ndiyo wananchi wanapata shida kuvuka kwenda Kibondo. Nimhakikishie Mheshimiwa Vuma na wananchi wa maeneo haya kwamba mara baada ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, lipo daraja la chuma katika Mto Malagarasi, tutaangalia uwezekano wa daraja hili kulihamishia kwenye maeneo haya ili wananchi wa Kitanga waweze kupita kwenda Kibondo bila matatizo yoyote. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Swalii la mwisho kwa siku ya leo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, litaulizwa na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo. Mheshimiwa Taska Mbogo, tafadhalii.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 65

Mpango wa Kuwatambua Watanzania Walio Nje

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Watanzania wengi wanaoishi nje ya nchi wamejikuta ni raia wa nchi wanazoishi kwa sababu mbalimbali ikiwemo kazi lakini si kwamba hawaipendi Tanzania:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatambua Watanzania waliochukua uraia wa nchi nyingine ili waweze kukuza uchumi wa nchi na kusaidia ndugu zao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia masuala yanayohusu Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*diaspora*) pasipo kubagua wale waliochukua uraia wa nchi nyingine kwa lengo la kuhakikisha kuwa mahitaji yao ya kikonseli yanashughulikiwa na pia kuongeza ushiriki wao katika kuchangia maendeleo ya nchi na ndugu zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ya kuwatambua *diaspora* katika kukuza uchumi. Mikakati yao ni pamoja na kuhimiza *diaspora* kujisajili kwenye Balozi zetu na maeneo ya uwakilishi; kuratibu makongamano ya *diaspora* ndani na nje ya nchi; kuratibu mikutano ya *diaspora* na viongozi wa Serikali wanapofanya ziara za kikazi nje ya nchi; kuhamasisha *diaspora* kuunda na kusajili jumuia zao na kuwashimiza kuwa washawishi wazuri wa uwekezaji kutoka mataifa mengine kuja kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, idadi ya *diaspora* wa Kitanzania nje ya nchi inakadirwa kuwa ni zaidi ya milioni moja, ambapo idadi ya *diaspora* waliojisajili kwa hiari kwenye Balozi zetu na maeneo ya uwakilishi ni takribani laki moja. Aidha, *diaspora* hao wamekuwa wakimiliki akaunti kwenye taasisi mbalimbali za kifedha kama vile Benki za Azania, CRDB, NMB, Stanbic na pia kuwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF, ikiwa ni pamoja na kumiliki nyumba 166 zilizouzwa na Shirika la Nyumba la Taifa zenye thamani ya shilingi bilioni 5.5 hadi kufikia Februari, 2019. Pia *diaspora* wameleta mafanikio makubwa kwa ndugu zao na taifa kwa ujumla kwa kuchangia sekta mbalimbali kama vile afya ambapo tumekuwa tukipokea wataalam wa afya na magonjwa yenyе kuambukiza na yale yasiyoambukiza kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, tunao mfano mzuri katika sekta ya afya ambapo Novemba, 2019 tulipokea msaada wa sanamu ya vitendo (*simulative manikin*) kutoka kwa Jumuiya ya Watanzania Wanaoishi Uingereza yenyе thamani ya shilingi milioni 100; vitabu vy'a afya vyenye thamani ya shilingi milioni 30 viliviyogawiwa katika Maktaba Kuu ya Shirika la Elimu Kibaha, Taasisi ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Namanyere iliyopo Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, Mbeya pamoja na Pemba.

SPIKA: Mheshimiwa Taska ameridhika. (*Kicheko*)

MHE. TASKA R. MBOGO: Hapana, nina maswali Mheshimiwa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Swali la nyongeza fupi.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba wapo Watanzania zaidi ya milioni moja wanaishi nje ya Tanzania kama diaspora. Sheria ya Citizenship ya Tanzania inakataza uraia pacha. Je, ni lini Serikali ya Tanzania itabadiilisha sheria hiyo na kuruhusu uraia pacha? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mwaka 2014 Serikali ya Tanzania iliota uraia kwa wageni waliokuwa wanaishi kama wakimbizi 150,000 nchini Tanzania. Je, Serikali haioni kwamba kutoruhusu uraia pacha tunawanyima haki Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuja kushiriki na kujenga nchi yao na kukaa na ndugu zao?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo kwa swali lake zuri la msingi lakini na maswali yake mazuri mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu kubadilisha sheria ili kuruhusu uraia pacha. Suala la uraia pacha ni la Kikatiba, kwa hiyo kabla hatujaongelea sheria tunapaswa kwanza tukaongelee Katiba. Mchakato wa kubadilisha Katiba bado unaendelea, pale Katiba itakapobadilika na kuruhusu uraia pacha ndipo tutakwenda kurekebisha Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995 ili kuongeza kipengele cha kuruhusu uraia pacha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anasema kwamba hatuoni kwamba kuzuia uraia pacha tunanyima haki. Watanzania hawa ambao wako nje tunaowaita diaspora, bado wanaendelea kufurahia haki nyingine ambazo zimetolewa hapa Tanzania ikiwemo haki ya kuwekeza kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 na haki nyingine ambazo wangeweza kuzipata.

Kwa hiyo, tunashauri kwamba Watanzania hawa kwa hivi sasa na ambao wamefanya kazi nzuri sana kama ambavyo nimeeleza, ikiwemo kuleta misaada mingi sana katika huduma za afya na baadhi ya Majimbo kama Chakechake, Kondoa, Makunduchi, Kivungwe pamoja na Namanyere yamefaidika, bado tunaendelea kushirikiana nao na wanaendelea kufurahia haki zao kama diaspora.

SPIKA: Ahsante sana. Mtakubaliana nami kwamba muda wa maswali umepita kabisa, sasa niende kwenye matangazo ya wageni.

Jukwaa la Spika tuna wageni 41 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambao ni Mabalozi wastaafu wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Faraji Mnyepe. Aidha, mionganii mwao yupo Dkt. Marten Lumbanga, Katibu Mkuu Mstaafu. Karibuni sana Bungeni. (Makofii)

Pia, hapa naomba msikilize kwa makini, yupo Mbunge Mstaafu ambaye alikuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Getrude Mongella. Karibu sana mama yetu. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sifa zake ni nyingi lakini ndiye aliyeongoza ule Mkutano wa Beijing na mabadiliko ya Beijing. Baadhi ya kina mama mpo humu ndani kama matokeo ya mambo ya Beijing. Kwa hiyo, tunakupongeza sana mama, ahsante sana. (Makof)

Waheshimiwa Mabalozi wote, naomba tusimame sasa pale tulipo. Karibuni sana hapa Bungeni. Hawa ni Mabalozi Wastaafu, waliokuwa Mabalozi wetu katika nchi mbalimbali huko nje, wametuwalisha kwa uaminifu mkubwa na leo wametenga muda kutembelea Bunge letu. Karibuni sana Waheshimiwa. Ahsanteni sana. (Makof)

Tuna wageni wanne ambao ni maofisa kutoka Bunge la Uganda waliokuja kwa ajili ya kubadilishana uzoefu. Yupo Ndugu Opata Cossian; Dkt. Tumukwasibwe Robert; Ndugu Lubowa William na Ndugu Alice Nyamwenge. Karibuni sana, mtakaporudi basi muende mkamsalimie Spika wa Uganda, Mama Rebecca Kadaga. (Makof)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, ambao ni wanafunzi wa Taaluma ya Tiba ya Mazoezi ya Viungo kutoka Chuo Kikuu cha KCMC kilichopo Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Joshua Lameck. Wale wa kutoka KCMC; karibuni sana, wanasomea orthopedics.

Mgeni mwengine wa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ni Ndugu Nick Reynolds a.k.a Bongo Zozo, Balozi wa Kutangaza Utalii Tanzania. (Makof)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Mbona maneno yamekuwa mengi sana, kuna nini?

WABUNGE FULANI: Hatujamuona.

SPIKA: Bongo Zozo hawajakuona Bwana. (Makof/Vigelegele)

MBUNGE FULANI: Fujo isiyoumiza.

SPIKA: Ahsante sana. (Makof)

Wengine ni mgeni wa Mheshimiwa Janet Mbene ambaye ni mtoto wa rafiki yake kutoka Jijini Mbeya, Ndugu Humphrey Mwakatundu. Karibu Humphrey. (Makof)

Wageni 46 wa Mheshimiwa Anne Kilango ambao ni Wanakwaya wa Kwaya ya KKKT Wilayani Same, Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Mchungaji John Kinkoro. KKKT Same, oh karibuni sana, mnapendeza kwelikweli. (Makof)

Wageni 86 wa Mheshimiwa Devotha Ninja ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Sunday School ya Kanisa la Anglicana Morogoro wakiongozwa na Mchungaji Kiongozi Peter Mkengi. Ooh, karibuni sana. Watoto wanapendeza hao, safi sana. (Makof)

Pia yuko Mchungaji Vedasto Vahaye; karibu sana Baba Mchungaji. Vilevile yupo Mwalimu Martha Mabeka; ahsante mwalimu. (Makof)

Kipekee, Mheshimiwa Devotha Ninja, katika kundi hilo yuko mwanae, binti yake Tamari; yuko wapi Tamari? Huyo hapo, hongera sana. Tamari umemuona mama alipokaa, hujamuona? Hakuoni hapa chini. Ahsante sana. (Makof)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni 54 wa Mheshimiwa Amina Mollel ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Viwandani Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Malick Masoud. Wale wa Viwandani, karibuni sana. (Makofii)

Mgeni wa Mheshimiwa James Millya ambaye ni rafiki yake, Ndugu Angela Nchalla. Karibu sana Angela. (Makofii)

Mgeni wa Mheshimiwa Amina Makilagi ambaye ni kaka yake kutoka Serengeti, Ndugu Cosmas Manyaki. Karibu sana Cosmas. (Makofii)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosoma masomo ya Sayansi ya Siasa, Utawala na Historia UDSM; ooh, karibuni sana, hawa wanasoma Political Science; karibuni sana. (Makofii)

Wageni 10 kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni Waandishi wa Habari za Utawala Bora Tanzania wakiongozwa na Ndugu Elias Msuya. Karibuni sana Waandishi wa Habari, karibuni popote pale mlipo. (Makofii)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Haya, ngoja niwapate.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Mbatia akae, Mheshimiwa Lubeleje akae, Mheshimiwa Musukuma akae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Naam.

SPIKA: Tuanze na wewe Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwongozo wangu ni jambo lililoteka Bungeni hivi leo ambapo Kiti kilifuta swali namba 56 ambalo ilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Muhammed Amour, jambo ambalo nahisi kwamba tumeinyima Serikali fursa ya kueleza juu ya madai ya vitendo ambavyo vinafanywa na wanajeshi wetu ambavyo vinatia doa Jeshi letu. Ilikuwa ni fursa nzuri kwa Serikali kuelezea juu ya matukio hayo ya madai ili kuweka sawa.

Vilevile ilikuwa ni fursa nzuri kwa Serikali kueleza wana mpango gani kusogeza kambi mbali na wananchi ili matatizo hayo yasitokee.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba Bunge tulikuwa na haki ya kusikiliza Serikali wanasema nini kwa sababu hilo swali lilipelekwa na jawabu limekuja hapa. Pengine Kiti kilikuwa kione busara kulirudisha swali hilo ili jawabu hilo litoke ili tulisafishe Jeshi letu na Serikali.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante. Hili nilijibu moja kwa moja; swali linasema hivi, wote tuna maswali kwenye tablets, swali linasema: 'Askari wa JWTZ wamekuwa wakiwapiga na kuwanyang'anya wavuvi mali zao". Hii ni just too broad, huwezi ukasema askari wa JWTZ, lazima useme askari labda wa kambi fulani au wa mahali fulani au eneo fulani, lakini huwezi ku-claim Jeshi zima kwamba kazi yake ni kupiga wavuvi na kadhalika. Kwa hiyo, ndiyo sababu ya kulifuta. Kwa hiyo, wakati mwininge swali lilenge mahali ambapo Serikali wanaweza kujibu. (Makofii)

Kama Mheshimiwa Ally Saleh anavyosema sijui makambi yahame, kwa hiyo makambi yote nchi hii yahame? Maana swali halijielekezi kambi gani linalohusika na kadhalika. Ndiyo maana swali hili tukalifuta.

Waheshimiwa Wabunge, mnapotunga maswali yatungeni katika namna ambayo Serikali inaweza ikapata nafasi ya kulijibu swali lako specifically ikalenga katika kile ambacho unahitaji kijibiwe. Maana wavuvi wako kila mahali; wako Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, wako Visiwani, sasa hapa Jeshi zima hili, hili ni swali ambalo halina mbele wala nyuma. (Makofii)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Aliyekuwa anaongea naomba arudie tena. Natoa nafasi huyo aliyekuwa anaongea badala ya kuongea kimyakimya aseme tu.

Haya, tunaendelea, Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mpwapwa kuna Mto mkubwa unaoitwa Kijasongwe na una madaraja makubwa matatu; Daraja la Chimaligo, Daraja la Gulo na Daraja la Godegode. Mwaka juzi Daraja la Godegode limevunjika, wananchi kule kata saba hawana mahali pa kupita, maji yamejaa, daraja halijajengwa. Jana Daraja la Nyasungwi Chimaligo nalo limevunjika. Madaraja haya ni kiungo kikubwa katika ya Mpwapwa pamoja na Jimbo la Chilonwa. Ombi langu kwa Wizara ya Ujenzi; tunahitaji bailey bridge haraka sana ili kurudisha mawasiliano katika Wilaya ya Mpwapwa.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Ujumbe huo naamini kabisa umefika Serikalini. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, una neno fupi?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge Lubeleje kuhusiana na madhara makubwa ambayo yamesababisha madaraja kwenye jimbo lake yaondoke na kukatika.

Mheshimiwa Spika, janga hili ni la nchi nzima na nitalitolea taarifa wiki hii hapa Bungeni. Tunaendelea kufanya tathmini hadi tarehe 30 kiwango cha fedha kinachohitajika ili kurudisha miundombinu ya barabara kwenye hali yake tayari tumeshakipata. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wiki hii nitaomba nafasi niweze kutoa taarifa rasmi kwa nchi nzima. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge Lubeleje atapata taarifa hiyo.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Na mimi nasimama kwa Kanuni ya 47(1), naisoma na kifungu cha 3.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa pole kwa ndugu zetu waliopoteza ndugu zao kule Kilimanjaro tarehe 1 Februari, siku ya Jumamosi. Yaliyotokea nadhani Wabunge wote tunafahamu mpaka kupelekea ndugu zetu 20 kupoteza uhai.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa sababu suala hili ni zito, ili tuweze kuona namna ya kulijadili na kulitolea uamuzi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maneno tofauti tofauti, tunaona mitandaoni Wabunge wenzetu wanaongea mitandaoni, wanatoa kauli za kulaumu Serikali wakati sheria za usimamizi wa vikundi hivi tumezitunga sisi wenyewe Bungeni. Kwa hiyo, ndiyo maana naona kama kuna umuhimu wa kuweza kukaa kama Bunge tukajadili tukaona namna ya kuliweka hili suala likae vizuri kwa sababu wenzetu wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, lakini sidhani kama kuna umuhimu sana wa kulaumu Wachungaji kwa sababu haya mambo yapo na ni masuala ya kiimani. Kwa hiyo, naomba tujadili kwa sababu humu kila mtu ana imani yake, sasa hatuwezi kuzuia tu kwamba labda kulikuwa na makosa, kama kulikuwa na makosa basi kwa idhini yako kama utaruhusu tuweze kujadili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Hoja yako haijaungwa mkono. Kwenye orodha yangu bado Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kutumia Kanuni ya 47 pamoja na ile ya 48 na sitaisoma na ni kuhusu jambo la dharura.

Kwanza, ni suala lilitotokea kule Mkoani Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi juzi ambapo watu zaidi 20 wamepoteza maisha kwenye mkusanyiko wa madhehebu ya dini na nitoe pole sana kwa wale waliopoteza maisha na wale ambao wapo hospitalini waweze kupata uhueni na pia nitoe pole kwa Watanzania wengine waliopoteza maisha wiki iliyopita zaidi 40 kwa ujumla pamoja na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, hili la mkusanyiko ambalo limesababisha vifo vya watu 20 kule Kilimanjaro, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 19(3) inasema: "Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umaja wa kitaifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nimerejea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu haya majanga ambayo yanatokea pamoja na matakwa ya kisheria ambayo yanatakiwa na Katiba na sheria zilizowekwa ambayo yamesababisha vifo vya wenzetu zaidi 20; na ukizingatia majanga haya ambayo asilimia 96 yanababishwa na sisi binadamu; na kwa kuwa madhehebu ya dini hapa nchini sasa uratibu wake katika kuhudumia au kutoa huduma zake, najua suala la kiimani ni very sensitive, lakini ni vyema sisi kama taifa na Wabunge tukaweza kuisimamia Serikali vizuri, tuienze Serikali vizuri na tuweze tukaazimia utaratibu mzuri wa kuleta umaja kwa sababu mauaji ya namna hii yanaweza kutokea kama yalivyotokea ya Kibwetere kule Uganda.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ili wenzangu waweze kuniunga mkono.

SPIKA: Samahani Mheshimiwa James, nimekusikiliza sana lakini hoja yako kwa kweli exactly ndiyo ambayo alikuwa anaitoa Mheshimiwa Musukuma na hoja hiyo haikuungwa mkono. Kwa jinsi hiyo kuirudia tena wewe itakuwa ni jambo ambalo si sawasawa kwa sababu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

haikuungwa mkono kwa kweli na sisi wote tumekuwa mashahidi kwamba hoja hiyo kwamba ijadiliwe hivi sasa jambo hilo Wabunge hawakulinga mkono. Basi imekuwa bahati mbaya tena, ni hoja ya msingi lakin haikuungwa mkono.

Katika matangazo yangu ya wageni wa leo nilisahamu wageni wa Mheshimiwa Medrad Kigola amba ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Mufindi Kusini, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ndugu Greyson Kadovela. Wale wa Mufindi, ahsanteni sana na karibuni sana. (Makofij)

Tunaendelea, Katibu.

NDG.ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

TAARIFA YA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA ITALII KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019

NA

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019

SPIKA: Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kemilembe Lwota, Mwenyekiti mwenyewe karibu. (Makofij)

MHE. KEMILEMBE J .LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kamailiviyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ina sehemu kuu nne ambapo Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inaelezea kwa kifupi muundo na majukumu ya Kamati. Sehemu ya Pili inaelezea Uchambuzi Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati na Maoni na Ushauri wa Kamati. Sehemu ya Tatu inabainisha Mapendekezo ya Kamati katika masuala mbalimbali. Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya awali, sasa naomba kutoa taarifa ya matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala mbalimbali. Uchambuzi huu umeainisha maeneo mahsusini ya shughuli zilizotekelizwa kwa kufafanua masuala muhimu ambayo Kamati ilibainisha na kuyatolea maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Kamati ilikutana na viongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yao kama ifuatavyo: -

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa Kuhusu Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilibainisha kuwa Tume imojiwekeea malengo mbalimbali ikiwemo kuimarisha utaratibu na ushirikiano wa wadau katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na uundaji wa mipango ya matumizi ya ardhi za Wilaya 25 na Vijiji na Vijiji 7,500 kufikia mwaka 2020. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, malengo hayo hayawezi kufikiwa kwa wakati, kwa sababu Tume hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi za kirasilimali na za kimuundo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, Kamati ina maoni kwamba, Serikali inapaswa kuipa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi fedha za kutosha ili iweze kuratibu kazi ya upangaji wa matumizi ya ardhi kote nchini. Hatua hii italiwezesha Taifa kuondokana na matatizo ya migogoro ya ardhi inayoendelea kuongezeka kwa sababu maeneo mengi hayana mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuongeza kasi ya uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi na kudhibiti utekelezaji na usimamizi wake, kuna umuhimu wa Tume hiyo kuongezewa mamlaka ya kiudhibiti kwa kubadili muundo wake ili uwe Mamlaka ya Upangaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Nchini. Hatua hii itawaongeza nguvu za kiutendaji na kuendelea kutekeleza majukumu ya kimkakati katika mipango ya matumizi ya Ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Taarifa Kuhusu Mkakati wa Taifa wa Upimaji na Upangaji wa Ardhi. Moja kati ya eneo ambalo Kamati hii imedhamiria kuhakikisha inaisimamia kikamilifu na kuhakikisha inatekelezwa na Serikali, ni kuwepo kwa Mkakati Madhubuti wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Wizara iliyasilisha taarifa kuhusu Mpango wa Taifa wa Upangaji, Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi ambayo ilianisha mwelekeo wa Serikali katika kupanga, kupima, kumilikisha na kusajili kila kipande cha ardhi nchini.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Wizara imebuni miradi miwili (2) mikubwa itakayotekeliza na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni miradi itakayochangia kupima, kupanga na kumiliksha kila kipande cha ardhi nchini kwetu. Hatua hii itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Hata hivyo, ili kupata muendelezo wa zoezi hili hata baada ya fedha za wafadhili kuisha Kamati inaona ni vyema Wizara ikahakikisha inatenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya kuendeleza miradi husika na miradi mingine inayofafana na huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Programu ya Urasilimisha Makazi Holela Nchini. Kamati ilipewa taarifa kwamba, hadi kufikia Disemba 2019, Wizara ilifanikiwa kuendesha zoezi la urasimishaji makazi holela mijini, ambapo jumla ya vipande 126,691 katika Halmashauri 29 vilirasimishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ambazo zinazorotesha programu hii. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa wataalam wa sekta ya ardhi katika baadhi ya Halmashauri mbalimbali, uhaba wa vitendeza kazi, gharama za urasimishaji ambapo wananchi, hususan wa kipato cha chini, bado wanashindwa kumudu kuchangia gharama za urasimishaji.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini pamoja na kwamba zoezi la urasimishaji wa makazi holela ni muhimu kwa kuwatambua na kuwapatia wananchi walengwa wa mradi huo kuwapatia hati ambazo hatimaye zitasaidia Serikali kukusanya mapato, watekelezaji wa zoezi hili wanapaswa kuhakikisha linakamilika kwa haraka ili kuweza kukabiliana na kasi ya wananchi wanaoendelea kujenga makazi holela. Aidha, iwapo zoezi hili la Upimaji, Upangaji na Umlilikishaji wa Ardhi, pamoja na Mipango Madhubuti ya Matumizi Ardhi vitawekewa Mkakati unaotekelzeza kwa haraka, ujenzi wa makazi holela utapungua na hatimaye kuisha kabisa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inapaswa kuhuisha jitihada za programu zote kwa lengo moja la kitaifa ambalo ni kuwa na nchi ambayo ina mipango thabiti ya matumizi ya ardhi yake, ardhi ambayo imepimwa, kupangwa na kumilikishwa. Huu utakuwa ni muarobaini wa kudumu kwa kutatua changamoto zote za ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utendaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Kifungu cha 22 cha Sheria ya Mahakama za Utatuvi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216 kinampa mamlaka Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzisha Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika eneo la kijigrafia la Wilaya, Mkoa au Kanda. Kamati imebaini kwamba tangu sheria hiyo ianze kufanya kazi tarehe 1 Oktoba, 2003 Wizara imefanikiwa kuunda na kuwezesha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 55 tu, kufikia Disemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kamati, idadi ya Mabaraza hayo ni ndogo, ikizingatiwa kuwa, wananchi walioko katika Wilaya ambazo hazina Mabaraza hayo, hulazimika kupeleka mashauri yao katika Wilaya za jirani zilizo na Mabaraza. Aidha, kwa uchache huu, Mabaraza yaliyopo huwa na idadi kubwa ya mashauri yanayosubiri uamuzi na hivyo kujenga mazingira yanayoweza kushawishi vitendo vya rushwa katika utoaji wa haki. Hivyo basi, ni vema Serikali ikawa na mkakati wa kudumu wa kuanzisha na kuyawezesha Mabaraza mapya ya Ardhi katika kila Wilaya nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) tarehe 17 Januari, 2020. Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Shirika la Nyumba, kwa mfano kukamilisha miradi midogo ya ujenzi wa nyumba za makazi ambapo jumla ya nyumba 456 zimekamilika katika miradi 8.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wa miradi mikubwa minne (4) iliyopo katika Jiji la Dar es Salaam ambayo kwa sasa imesimama. Miradi hiyo ni Morocco Square, Seven Eleven - Kawe, Golden Premier Residence - Kawe na Plot 300 Regent Estate Mikocheni. Miradi hii ilibuniwa na kuanza utekelezaji miaka ya 2012 na 2013 na ilitarajiwa kukamilika mwaka 2015 na 2016. Aidha, miradi hii ilikadiriwa kuwa na gharama za ujenzi za takribani shilingi bilioni 338.1 na tayari imekwishatumia shilingi bilioni 154.6 za miradi hiyo na deni la shilingi bilioni 10.6 zilizoidhinishwa lakini bado hazijalipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba miradi hii inahitaji jumla ya shilingi bilioni 183.5 ili iweze kukamilika lakini kwa sasa imesimama kutokana na ukosefu wa fedha. Moja kati ya sababu za ukosefu wa fedha, ni Shirika kutopata kibali kutoka Hazina cha kuweza kukopa kiwango stahiki kumalizia miradi hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini kwamba, kuna madai mengine ambayo yameletwa na wakandarasi wa miradi hii yanayotokana na madai ya ziada kwa sababu ya mabadiliko ya ukubwa na usanifu wa mradi, gharama ya kusimama kwa miradi, riba ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuchelewesha malipo, pamoja na sababu nyingine kama hasara kwa sababu ya kushuka kwa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa miradi husika, sasa ni miaka nane (8) na tayari kiasi cha fedha shilingi bilioni 154.6 zimekwishatumi katika miradi hiyo. Kusimama kwa miradi hiyo, siyo tu kunashusha thamani yake kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia na kiusanifu, lakini kunawaweka wateja ambao tayari wametoa fedha zao au kukopa benki ili kununua baadhi ya nyumba katika miradi hiyo katika hali ya sintofahamu. Kwa upande wa Serikali na hususan Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), riba ya deni la mkopo inayoongezeka inaifanya Serikali ipoteze fedha ambazo zingetumika katika uendelezaji wa miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kama msimamizi wa kisera wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa, imekuwa ikiishauri Wizara kuhusu namna bora ya kuinusuru miradi hii. Eneo mojawapo ambalo Kamati imekuwa ikitoa ushauri wake, ni kwa Wizara kuwa na mkakati endelevu ambao utalisaidia Shirika kupunguza ghamra za miradi na hatimaye kupunguza, kama siyo kuondoa kabisa hasara ambayo tayari shirika limepata.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanapaswa kuzingatiwa na Shirika na kwa usimamizi wa Wizara katika mpango huo ni pamoja na kuongeza urefu wa kulipa mikopo, kupunguza viwango vya riba vya mikopo, kubadilisha malipo ya mikopo yote kwa kila mwezi na pia kubadilisha sarafu ya mikopo hiyo kutoka mikopo ya dola za kimarekani kuwa mikopo ya shilingi za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kupanga ni moja na hatua ya kutekeleza mipango hiyo ni jambo lingine. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikaharakisha utekelezaji wa mipango hiyo ili kuokoa miradi husika na pia kuokoa fedha za umma. Kamati ina maoni kwamba, Shirika litumie fursa ya vyanzo vya mapato vilivyopo ili kukusanya fedha zitakazosaidia kuendeleza miradi inayohusika na yote iliyosimama. Aidha, kwa kuzingatia kuwa Shirika lina miradi mingi kwa sasa, ni vyema rasilimali zilizopo ndani ya shirika, kwa maana ya watumishi na vitendea kazi, zikatumika kukamilisha kwanza miradi iliyopo kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhuisha Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na kufanya tathmini kuhusu tija ilipo katika mfumo wa matumizi Mseto ya Ardhi (*Multiple Land Use System*). Kamati ilifahamishwa kwamba Wizara imeunda Kamati ya Wataalam, inayofanya tathmini ya Mfumo wa Matumizi Mseto ya Ardhi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na uwezekano wa kuhuisha Sheria ilioanzisha mamlaka hiyo ili iendane na hali halisi ya sasa. Taarifa iliyopo ni kwamba Kamati imekamilisha kukusanya taarifa muhimu na kwamba sasa inakusanya maoni ya wadau, ikiwa ni pamoja na wananchi wanoishi ndani na nje ya hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tangu Kamati ianze kushauri kuhusu jambo hili sasa ni zaidi ya miaka mitatu (3). Hata hivyo, zoezi la tathmini, utafiti na kukusanya maoni unachelewa kwa hivyo kusababisha maamuzi kuhusu jambo hilo kutofanyika kwa wakati kwa mustakabali wa Taifa na Hifadhi na wanaoishi ndani ya Hifadhi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Kamati ilipokea taarifa mbalimbali kuhusu utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Mnamo tarehe 22 Oktoba, ya 2019, Kamati ilipokea taarifa kuhusu hali ya uhifadhi wa Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Maeneo ya Ardhi Oevu nchini.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa kwamba, tangu ianze kutekeleza majukumu yake mwaka 2016, TAWA imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kuimarika uhifadhi kunakotokana na kupungua kwa ujangili, kuthibitiwa kwa vitendo vya uingizaji na ulishaji wa mifugo katika Mapori ya Akiba na kuanzishwa na kufanya mabadiliko ya kimfumo kwa usimamizi wa uhifadhi kutoka wa kiraia kwenda Jeshi Usu. Aidha, TAWA imesaidia kuimarisha utalii kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vinavyosimamiwa na Mamlaka kutoka watalii 35,475 mwaka 2015/2016 hadi watalii 126,428 kwa mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 234.7.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), ina changamoto mbalimbali. Pamoja na kwamba mapato ya Mamlaka hiyo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 38.8 mwaka 2015/2016 hadi kufikia shilingi bilioni 48.8 mwaka 2017/18, lakini bado kuna ongezeko linaloweza lisikidhi mahitaji halisi ya utekelezaji wa shughuli za Mamlaka hiyo ambayo yanakadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 150 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyngine inayokabili Mamlaka hii ni ukosefu wa sheria mahsusini inayosimamia utaratibu wa utekelezaji wa majukumu yake. Kwa sasa, Mamlaka bado inatekeleza majukumu yake kutokana na Kifungu cha 8 cha Sheria cha Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 pamoja na Amri ya Serikali iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 135 la tarehe 9 Mei, 2014 (pamoja na marekebisho yake). Kukosekana kwa sheria mahsusini, kumesababisha Mamlaka hii, ambayo inasimamia maeneo makubwa zaidi ya kiuhifadhi, kusuasua kiutendaji na hivyo kupunguza ufanisi katika utekelezaji wake wa majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa Kuhusu Hali ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuleta mabadiliko ya sheria ambayo yanaongeza muda wa umiliki wa vitalu vya uwindaji kutoka miaka mitano na kuwa miaka kumi hadi kumi na mitano. Aidha, inapongeza hatua ya Serikali kupunguza madaraja ya vitalu, kutoka madaraja matano hadi madaraja matatu. Vilevile, Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali, kuongezea muda kwa wamiliki wa vitalu vya sasa wakati ikiendelea kufanya maboresho ya uendeshaji wa uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi wa Kamati, zoezi la kugawa vitalu kwa njia ya mnada, limeonekana kuwa na tija zaidi kimapato ikilinganishwa na utaratibu uliokuwepo hapo awali. Katika mnada wa vitalu uliofanyika Juni 2019, kampuni mbili kati ya nane zilizoshiriki mnada wa vitalu zilishinda jumla ya vitalu saba kati ya vitalu 26 vilivyotangazwa.

Mheshimiwa Spika, vitalu saba vilivyotangazwa kwa njia ya mnada thamani yake ilifikia dola za kimarekani 831,000 ikilinganishwa na dola za kimarekani 288,000 iwapo vitalu 26 vyote vingegawanywa kwa utaratibu wa awali. Hivyo, ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada wa kielektroniki umewezesha nguvu ya soko kuamua ada ya kitalii cha uwindaji wa kitalii na pia umeongeza uwazi na utawala bora katika zoezi la ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba pamoja na ongezeko hilo la mapato, Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye tathmini ya kina ili kujua ni kwa sababu gani, iwe za kiushindani, za kimasoko, za kiubora wa vitalu vyetu, au sababu nyngine yoyote iliyoababisha vitalu 19 kati ya vitalu 26 kutopata mnunuzi. Ni kweli, mapato yameongezeka lakini kama vitalu vyote vingepata wanunuzi katika mnada uliofanyika, ingechangia kuendeleza uhifadhi na kuongeza pato la Taifa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu utendaji wa hotel na lodge za Serikali zilizobinafishwa. Kamati ilitaka kupata taarifa hiyo kutoka Serikalini kwa lengo la kufahamu kwa kina kuhusu utekelezaji wa mikataba na makubaliano, faida inayotokana na uwekezaji pamoja na tija inayotokana na uwekezaji uliofanyika katika kutatua changamoto za upungufu za vyumba vya kulala wageni. Kamati ilikutana na Wizara kwa nyakati tofauti tarehe 28 Agosti, 2019, tarehe 28 Oktoba, 2019 na tarehe 21 Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado haijaridhishwa na mwenendo wa Serikali katika kutoa taarifa kuhusu suala hili kwa sababu Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha na Mipango bado hazijawa na taarifa ya pamoja kulieleza Bunge ya kile ambacho Kamati imekuwa ikitaka maelezo. Baada ya makubaliano ndani ya Serikali, Kamati ilikubaliana na ombi lao kwamba taarifa hiyo itawasilishwa katika vikao vya Kamati vijavyo kuelekea Mkutano wa Bajeti kama jambo mahsus.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa Kuhusu Kuanzishwa kwa Jeshi Usu. Katika jitihada za kukabiliana na ujangili na uvunaji holela wa rasilimali za wanyamapor na misitu hapa nchini na ili kuboresha nidhamu na utendaji kazi, Wizara ya Maliasili imeanzisha Jeshi Usu (*paramilitary*) ambalo lilizinduliwa rasmi mwezi Novemba 2018. Jeshi Usu linaundwa na Hifadhi za Taifa za TANAPA, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania (TAWA) na Wakala wa Misitu (TFS) kwa mamlaka itakanayo na Kifungu cha 10 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapor Na. 5 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ambayo iliwasilishwa kwa Kamati, Wajumbe walitaarifiwa kwamba, hadi kufikia Desemba 2019 takriban watumishi 2,460 wamepatiwa mafunzo ya utayari (*transformation course*) ya kuijunga na Jeshi Usu. Tunaipongeza Wizara kwa hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, katika kipindi hiki cha mpito cha kubadilisha mfumo wa utumishi kutoka uliopo sasa kwenda katika mfumo wa Jeshi Usu utaratibu mzuri uandaliwe ikiwemo kutungwa kwa sheria mahsusitakayoratibu mfumo huo ili watumishi waliopo wapewe vyeo stahiki, maslahi stahiki na mazingira bora ya utendaji wa kazi zao. Hii itasaidia kupunguza malalamiko yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilifanya ziara mbalimbali za ukaguzi wa miradi inayotekelzwa na Serikali ili kujiona hatua za utekelezaji wake. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, hususan baada ya Wabunge kupokea Mapendekezo ya Mpango na Kiwango cha Ukomo wa Bajeti ya mwaka 2019/2020, Kamati ilikagua miradi iliyotengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari naomba nilitaarifu Bunge lako kuwa, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo ni kutotolewa kwa fedha za maendeleo kwa wakati na miradi kutegemea fedha za wafadhili. Hivyo basi, Kamati inaushauri Serikali kwamba katika miradi yote inayopokea fedha za wafadhili ni vyema zikatengwa fedha za kutosha za ndani ili kuwa na uendelevu wa miradi au programu husika baada ya ufadhili kuisha. Aidha, Serikali itoe fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati. Taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi inapatikana katika ukurasa wa 26-31 wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Kwa kuwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii, Kamati imebaini masuala mbalimbali na kuyatolea maoni na ushauri mahsus, ni matumaini ya Kamati hii kwamba maoni na ushauri huo utazingatiwa kikamilifu na Wizara husika.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati. Kwa kuzingatia kuwa baadhi ya masuala yaliyobainika yanahitaji kuwekewa msisitizo wa ziada katika kuwezesha utekelezaji wake, Kamati inawasilisha kwa Bunge lako Tukufu ili Wabunge wapokee, kuyakubali na kuazimia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, bado kumekuwepo na changamoto ya utekelezaji wa bajeti za Wizara, ambapo fedha inayotengwa haifiki kwa wakati. Na kwa kuwa, ucheleweshaji huu mara nyingi hukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha. Kwa hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako kuitaka Serikali iwe na mkakati endelevu wa kutenga fedha na kuidhinisha kwa wakati ili utekelezaji wa bajeti za Wizara uwe halisi kuwaletaa wananchi maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kutungwa kwa sheria na uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA). Kwa kuwa, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ilianzishwa kwa Amri ya Kisheria (*Establishment Order*) ili kusimamia Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu. Na kwa kuwa, Mamlaka hii inasimamiwa na Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji na hivyo kukosa nguvu ya kisheria kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako kuitaka Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori utakayoipa nguvu ya kisheria kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Nchini. Kwa kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za misitu ambazo zimekuwa zikisimamiwa na mamlaka tofauti nchini. Na kwa kuwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu kwa Serikali peke yake. Na kwa kuwa bado kuna changamoto ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali hali ambayo pamoja na kuleta mgongano kwenye matumizi ya rasilimali hizo, kunachangia kuleta uharibifu na kutishia uendelevu wa misitu yetu. Kwa hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge, kuitaka Serikali kwa mara nyingine tena, iharakishe mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitumia Mfumo wa Matumizi Mseto ya Ardhi (*Multiple Land Use System*) katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa sheria. Na kwa kuwa mfumo huo umeleta changamoto nyingi, ikiwemo ongezeko la watu na mifugo na shughuli nyingine za binadamu katika Hifadhi, hali inayosababisha kuongezeka kwa gharama za kuwashudumia wananchi, pamoja na kuwepo wa uharibifu wa mazingira, hali inayotishia kupoteza hadhi ya Hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuharakisha mchakato wa kufanya tathmini ya kina kuhusu mfumo wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo ili kusaidia kuhuisha sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendana na hali halisi iliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna Kulijengea Uwezo Zaidi Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Kwa kuwa, idadi ya Hifadhi za Taifa imeongezeka kutoka hifadhi 16 hadi 22. Na kwa kuwa hata kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya 6, ni hifadhi 5 katika ya 16 zilizokuwa zina uwezo wa kuijendesha zenyewe na kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesha Hifadhi za Taifa nyingine 11. Na kwa kuwa, Shirika linalipa kodi zote stahiki ikiwa ni pamoja na gawio kwa Serikali na ili kuliwezesha Shirika hili kuzilea na kuziendeleza Hifadhi za Taifa mpya sita zilizoanzishwa. Kwa hiyo basi, Bunge linalishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia au kuliondolea baadhi ya tozo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ili kulipa nguvu ya kuweza kuzihudumia Hifadhi zote za Taifa. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mustakabali wa Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa ya Morocco Square, Seven Eleven-Kawe, Golden Premier Residence-Kawe na Plot 300 Regent Estate Mikocheni ilipo Dar es Salaam. Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa, miradi iliyotajwa japo juu imesimama, tangu ujenzi wake ulipoanza mwaka 2012 na 2013 kwa fedha za mkopo na ilitarajiwa miradi hiyo ingekamilika mwaka 2015 na 2016. Na kwa kuwa, kutokamilika kwa miradi hiyo kumeongeza gharama za ujenzi, ongezeko la riba na Serikali kupata hasara kubwa ambayo inasababisha kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha iliyowekezwa. Kwa hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua stahiki na kwa wakati kuiwezesha NHC kukamilisha miradi hiyo ili tija ya uwekezaji huo ioneckane.

Mheshimiwa Spika, mkakati endelevu wa upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi nchini. Kwa kuwa, Programu ya Upimaji, Upangaji na Umilikishaji wa Ardhi iliyokuwa inatekelezwa kwa majoribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga na kwa kutumia zaidi fedha za wafadhili imekamilika kwa mafaniko makubwa na ilitarajiwa isambazwe katika Wilaya nyingine za Mkoa wa Morogoro na nchi nzima kwa kutumia bajeti za ndani. Na kwa kuwa Serikali haijatenga fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya kuendeleza programu hiyo na hivyo kuwa chachu ya kuendelea kwa migogoro ya ardhi nchini. Kwa hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kuendeleza programu hii na nyingine ambazo zimeonyesha mafanikio makubwa katika kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2019 hadi Januari, 2020 yametokana na juhudhi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipoweka wazi kwamba, ufanisi wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam na kiushauri wakati wote. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

Vilevile nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, akisaidiwa na Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndugu Gerald Magili bila kumsahau Katibu wa Kamati hii, Ndugu Yona Kirumbi na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John kwa uratibu wa shughuli za kila siku za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya shughuli zilizotekeliza na Kamati, uchambuzi wa matokeo uliotekeliza hoja hizi na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. DKT. JASMINE TISEKWA BUNGA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 MAELEZO YA AWALI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati hiyo kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ina sehemu kuu nne ambapo Sehemu ya **Kwanza** ni Utangulizi ambayo inaelezea kwa kifupi muundo na majukumu ya Kamati. Sehemu ya **Pili** inaelezea Uchambuzi Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati na Sehemu ya **Tatu** inabainisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika masuala mbalimbali. Sehemu ya **Nne** ni Hitimisho.

1.2 MUUNDO WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imeundwa kwa mujibu wa **Kanuni ya 116** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 118** ya Kanuni za Kudumu za Bunge¹. Hadi wakati taaarifa hii inawasilishwa, Kamati ina Wajumbe wafuatao: -

1. Mhe. Kemirembe Rose J. Lwota (Mb)
2. Mhe. Shabani Omary Shekiliindi (Mb)
3. Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb)
4. Mhe. Boniface Mwita Getere (Mb)
5. Mhe. Grace Sindato Kiwelu (Mb)
6. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya (Mb)
7. Mhe. Halima Abdallah Bulembo (Mb)
8. Mhe. Khalifa Salum Suleiman (Mb)
9. Mhe. Lucy Fidelis Owenya (Mb)
10. Mhe. Hussein Nassor Amar (Mb)
11. Mhe. Neema William Mgaya (Mb)
12. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa (Mb)
13. Mhe. Flatei Gregory Massay (Mb)
14. Mhe. Risala Saidi Kabongo (Mb)
15. Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb)
16. Mhe. Yussuf Haji Khamis (Mb)
17. Mhe. Dkt. Jasmine Tiiseekwa Bunga (Mb)
18. Mhe. Yussuf Salim Hussein (Mb)
19. Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi (Mb)
20. Mhe. Mbarouk Salim Ali (Mb)
21. Mhe. Lucy Thomas Mayenga (Mb)
22. Mhe. Timotheo Paul Mnzava (Mb)
23. Mhe. Pauline Philip Gekul (Mb)

¹ Toleo la Januari, 2016

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

24. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo (Mb)
25. Mhe. Agnes Mathew Marwa (Mb)

1.3 MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ni moja kati ya Kamati za Kisekta ambazo zimeainishwa katika **Kifungu cha 6 (6)** cha **Nyongeza ya Nane** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ina wajibu wa kufanya masuala yafuatayo kwa mujibu wa **Kifungu cha 7 (1)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge: -

- a) Kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo;na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

1.4 NJIA ZILIZOTUMIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kiasi kikubwa umezingatia **Kanuni ya 117** hususan **fasili ya (3)** na ya **fasili ya (5)** ambazo kwa pamoja zinaweka masharti kwamba, Kamati itatekeleza majukumu yake kwa idhini ya Spika na kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika. Hivyo basi, njia kuu zilizotumika na Kamati kutekeleza majukumu yake ni zifuatazo:-

- a) Kufanya vikao na Wizara inazozisimamia kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo na taasisi zake;
- b) Kufanya ziara kwa lengo la kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelzwa na Wizara na taasisi zake pamoja na kukagua miradi ya mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi iliyotengewa fedha katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- c) Kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali, ikiwemo Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- d) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hiii.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 MAELEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na Shughuli zilizotekelzwa, sasa naomba kutoa taarifa ya matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala mbalimbali. Uchambuzi huu umeainisha maeneo mahsus ya shughuli zilizotekelzwa kwa kufafanua masuala muhimu ambayo Kamati ilibaini na kuyatolea maoni.

2.2 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MBALIMBALI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii imefanya vikao mbalimbali na Wizara inazosimamia pamoja na baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo kuu la vikao vilivyoofanyika ni kupokea maelezo ya Serikali ili kupata uelewa kuhusu masuala yanayohusu Sera, utekelezaji wa majukumu yao pamoja na changamoto zinazowakabili.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Kamati ilikutana na viongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ili kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yao kama ifuatavyo: -

2.2.1 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuitaka Serikali kuandaa Mipango Kabambe ya Kuendeleza Miji na Majiji

Mheshimiwa Spika, kufuatia azimio la Bunge liloitaka Serikali kuandaa Mipango Kabambe ya Kuendeleza Miji na Majiji, Kamati yangu ilifuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Bunge kwa kutaka kupata taarifa ya hatua iliyofikiwa. Mnamo tarehe 21 Agosti, 2019 Waziri mwenye dhamana, aliwasilisha taarifa husika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hiyo, Wizara iliifahamisha Kamati kwamba, Serikali iko katika mchakato wa kuandaa mpango kabambe (*master plan*) kwa ajili ya Majiji, Miji na Miji Midogo. Aidha, Kamati ilielezwa kwamba mipango miji ya miji mitano imekamilika ambayo ni Mwanza, Arusha, Mbeya, Dar es Saalam na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kupon gezwa kwa hatua hiyo, hata hivyo kasi ya mchakato huo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji yaliyopo. Kwa kuharakisha zoezi hili, itasaidia kupunguza kasi ya ujenzi holela katika Miji na Miji Midogo ambayo inakuwa kwa kasi.

2.2.2 Taarifa Kuhusu Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa nyakati tofauti ilikutana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kupokea na kujadili mikakati ya Serikali kuhusu mipango ya matumizi bora ya ardhi. Katika kikao kilichofanyika tarehe 18 Januari, 2020 Kamati iliifahamishwa kwamba majukumu ya Tume ni pamoja na kuratibu, kushauri, kuandaa, kukagua na kusambaza programu za mipango ya matumizi ya ardhi ya Kanda, Wilaya na Vijiji kwa uwiano baina ya sekta mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Upangaji Matumizi ya Ardhi, Sura 116.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake, Tume iliitaarifu Kamati kwamba imejiwekea malengo mbalimbali ikiwemo kuimarisha uratibu na ushirikiano wa wadau katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya 25 na Vijiji 7500 kufikia mwaka 2020. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, malengo hayo hayawezikufikiwa kwa wakati, kwa sababu Tume hiyo inakabiliwa na changamoto nydingi za kirasilimali na za kimuundo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, Kamati ina maoni kwamba, Serikali inapaswa kuipa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi fedha za kutosha ili iweze kuratibu kazi ya upangaji wa matumizi ya ardhi kote nchini. Hatua hii italiwezesha Taifa kuondokana na matatizo ya migogoro ya ardhi inayoendelea kuongezeka kwa sababu maeneo mengi hayana mipango

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya matumizi ya ardhi. Aidha, Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi (*Land Use Planning Project*) unaotekelozwa na Tume ukipewa fedha stahiki na kwa wakati, kutaharakisha zoezi la kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali hasa kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuongeza kasi ya uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, na kudhibiti Utekelezaji na Usimamizi wake, kuna umuhimu wa Tume hiyo kuongezewa mamlaka ya kiudhibiti kwa kubadili muundo wake ili kuwa Mamlaka ya Upangaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Nchini. Hatua hii itaiongezea nguvu za kiutendaji, kuendelea kutekeleza majukumu ya kimkakati katika Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini.

2.2.3 Taarifa Kuhusu Mkakati wa Taifa wa Upimaji na Upangaji wa Ardhi

Mheshimiwa Spika, moja kati ya eneo ambalo Kamati hii imedhamiria kuhakikisha inalisimamia kikamilifu kuhakikisha linatekelezwa na Serikali, ni kuwepo kwa Mkakati Madhubuti wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi yote ya nchi yetu. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilifanya vikao viwili (2) na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tarehe 26 Agosti, 2019 na terehe 18 Januari, 2020 katika muendelezo wa kuhakisha azma ya Kamati inatakelezwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwasilisha taarifa kuhusu **Mpango wa Taifa wa Upangaji, Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi** ambayo iliainisha mwelekeo wa Serikali katika kupanga, kupima, kumilikisha na kusajili kila kipande cha ardhi. Wizara imebuni miradi miwili (2) itakayotekelozwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza, unaofadhiliwa kwa mkopo wa Benki ya dunia, unakadirwa kugharimu dola za kimarekani milioni 150 na utekelezaji wake utakuwa ni miaka mitano (5) kuanzia 2020/21 hadi 2025/26. Mradi huu una lengo la kuboresha umiliki wa ardhi (*Land Tenure Improvement Project*), kuimarisha na kusambaza Mfumo Uunganishi wa Kutunza Kumbukumbu za Ardhi (ILMIS) katika mikoa 26 ya Tanzania Bara, kujenga uwezo kwa watendaji na kuimarisha uratibu wa usimamizi wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili, unaofadhiliwa na Serikali ya Watu wa Korea, unalenga kuandaa ramani za msingi (*base maps*), kujenga vituo vya upimaji (*continuously operated reference stations*) nchini, kujenga kanzidata ya taarifa za kijigrafia na kujengea uwezo wataalam kutekeleza mradi huo. Kwa maelezo ya Wizara, mradi huu utaharakisha huduma za ardhi za uthamini, upangaji na upimaji kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni miradi itakayochangia kupima, kupanga na kumilikisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu. Hatua hii itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Hata hivyo, ili kupata mwendelezo wa zoezi hili, hata baada ya fedha za wafadhili kuisha, Kamati inaona ni vyema Wizara ikahakikisha inatenga fedha nyingi zaidi za ndani kwa ajili ya kuendeleza mradi husika na miradi mingine inayofanana na huu.

2.2.4 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Urasimishaji Makazi Holela Nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa kwamba, hadi kufikia Disemba 2019 Wizara ilifanikiwa kuendesha zoezi la urasimishaji makazi holela mijini, ambapo jumla ya vipande 121,691 katika Halmashauri 29 vilirasimishwa. Pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ambazo zinazorotesha progamu hii. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa wataalam wa sekta ya ardhi katika baadhi ya halmashauri mbalimbali, uhaba wa vitendea kazi, gharama za urasimishaji ambapo wananchi, hususan wa kipato cha chini, bado

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanashindwa kumudu kuchangia gharama za urasimishaji. Changamoto nyiningine, ni uelewa mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa kurasimisha maeneo yao na kuwa na hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, pamoja na kwamba zoezi la urasimishaji wa makazi holela ni muhimu kwa kuwatambua, na kuwapatia wananchi walengwa wa mradi huo kwa kuwapatia hati ambazo hatimaye zitasaidia Serikali kukusanya mapato, watekelezaji wa zoezi hili wanapaswa kuhakikisha linakamilika kwa haraka ili liweze kukabiliana na kasi ya wananchi wanaoendelea kujenga makazi holela. Aidha, iwapo zoezi la Upimaji, Upangaji na Umilikishaji wa Ardhi, pamoja na Mipango Madhubuti ya Matumizi Ardhi vitawekewa Mkakati unaotekelvezeka kwa haraka, ujenzi wa makazi holela utapungua na hatimaye kuisha.

Hivyo basi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inapaswa kuhusisha jitihada za programu zote kwa lengo moja la kitaifa ambalo ni kuwa na nchi ambayo ina Mipango Thabiti ya Matumizi ya Ardhi yake, ardhi ambayo imepimwa, kupangwa na kumilikishwa. Huu utakuwa ni muarobaini wa kudumu wa kutatua changamoto zote za ardhi nchini.

2.2.5 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Chuo cha Ardhi, Morogoro (ARIMO)

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 29 Oktoba, 2019 Kamati ilipokea taarifa kuhusu utendaji wa Chuo cha Ardhi, Morogoro. Moja katika masuala ambayo taarifa iliyaweka bayana, ni pamoja na changamoto ya wahitimu wa chuo hiki kupata ajira. Kamati inashauri, kwa kuwa halmashauri nydingi hazina wataalam wa sekta ya ardhi, kuwatumia wanafunzi wa chuo hiki wakati wa mafunzo kwa vitendo kupima maeneo yao. Aidha, waangalie uwezekano wa kuwapa ajira wanafunzi wenye sifa mionganoni mwao.

2.2.6 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika Sekta ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii iliyowasilishwa tarehe 30 Oktoba, 2019, Kamati ilielezwa hatua mbalimbali ambazo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa ikizichukua katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Hata hivyo, Wizara haikuweza kufikia malengo yake kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo suala la kuwa na bajeti ndogo.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali mojawapo ambayo haiongezeki lakini mahitaji ya matumizi yake yanaongezeka kila siku. Hivyo basi Serikali inapaswa kuweka kipaumbele katika kutenga bajeti kwa ajili ya kuendeleza sekta ya ardhi hasa ukizingatia kuwa shughuli zote za maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii zinategemea ardhi.

2.2.7 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa uwepo na utendaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya nchini, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utendaji wake tarehe 31 Oktoba, 2019 na baada ya hapo imekuwa ikifuatilia utendaji wa mabaraza hayo hadi wakati taarifa hii inaandikwa. Kifungu cha 22 cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216 kinampa mamlaka Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzisha Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika eneo la kijigrafia la Wilaya, Mkoa au Kanda. Kamati imebaini kwamba, tangu Sheria hiyo ianze kufanya kazi tarehe 1 Oktoba, 2003 Wizara imefanikiwa kuunda na kuwezesha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 55 tu, kufikia Disemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kamati, idadi ya mabaraza hayo ni ndogo, ikizingatiwa kuwa, wananchi walioko katika wilaya ambazo hazina mabaraza hayo, hulazimika kupeleka mashauri yao katika wilaya za jirani zilizo na mabaraza. Hali hii huongeza gharama kwa wananchi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kushughulikia mashauri yao. Aidha, kwa uchache huu, mabaraza yaliyopo huwa na idadi kubwa ya mashauri yanayosubiri uamuzi, na hivyo kujenga mazingira yanayoweza kushawishi vitendo vya rushwa katika utoaji wa haki. Hivyo basi, ni vema Serikali ikawa na mkakati wa kudumu wa kuanzisha na kuyawezesha mabaraza mapya ya ardhi katika kila Wilaya nchini.

2.2.8 Taarifa Kuhusu Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000

Mheshimiwa Spika, hatua ya Wizara kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 inatokana na changamoto na mapungufu yaliyojitekeza katika utekelezaji wa sera hiyo tangu mwaka 2000. Aidha, kumekuwa na mahitaji mapya yanayohitaji kuzingatiwa katika Sera kama vile Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (SFYDP II) unaohimiza ujenzi wa uchumi wa viwanda, New Urban Agenda (2016), pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ambavyo kwa pamoja, yanahitaji msukumo mpya wa kisera katika kuyatekeleza ili kufikia malengo na vipaumbele vya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 illiyohuishwa itaweka mazingira wezeshi ili kuwa na makazi ya watu yaliyo endelevu, jumuishi, na yanayowezesha ustawi wa watu wote wanaoishi mijini na vijiji.

2.2.9 Taarifa Kuhusu Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Nyumba

Mheshimiwa Spika, Bunge lako kwa muda mrefu limekuwa likiishauri Serikali kutunga Sera ya Taifa ya Nyumba. Kukosekana kwa Sera inayojitegemea kuratibu masuala ya nyumba (*national housing policy*) kumesababisha kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa Sheria mahsusizi zinazoratibu masuala ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya nyumba inazidi kujitwalia nafasi katika maendeleo na mabadiiko ya kijamii na kiuchumi nchini. Hali hii imesababishwa na Sekta ya Mali isiyohamishika (*real estate sector*) kuendelea kukua kwa kasi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta hiyo. Kamati ina maoni kwamba, Sera ya Taifa ya Nyumba inayojitegemea itasaidia kuweka mfumo dhahiri wa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika kuelekezwa kwenye masuala stahiki ya nyumba ili kuondokana na upungufu wa nyumba za kupanga zenye gharama nafuu (*affordable rental housing*) na ukosefu wa nyumba bora za jamii na hasa kwa makundi yasiyo salama (*vulnerable groups*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, Sera mpya ya Taifa ya Nyumba itaweka mazingira ya kitaasisi yanayohitajika kuendeleza ufanisi, usawa, na haki katika soko la nyumba na kuweka utaratibu wa kuwezesha usimamizi, udhibiti na ukaguzi. Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kutungwa kwa sera hiyo ili ianze kufanya kazi mara moja.

2.2.10 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi yote ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) tarehe 17 Januari, 2020. Kamati imeridhishwa na hatua zinachokuliwa na Shirika la Nyumba, kwa mfano kwa kukamilisha miradi midogo ya ujenzi wa nyumba za makazi ambapo jumla ya nyumba 456 zimekamilika katika miradi 8.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wa miradi mikubwa minne (4) iliyopo katika Jiji la Dar es Salaam ambayo kwa sasa imesimama. Miradi hiyo ni **Morocco Square, Seven Eleven - Kawe, Golden Premier Residence - Kawe** na **Plot 300 Regent Estate Mikocheni**. Miradi hii ilibuniwa na kuanza utekelezaji miaka ya 2012 na 2013 na ilitarajiwa kukamilika mwaka 2015 na 2016. Aidha, miradi hii ilikadiriwa kuwa na gharama za ujenzi za

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

takribani shilingi **bilioni 338.1** na tayari imekwishatumbi shilingi **bilioni 154.6** bilioni na miradi hiyo ina deni la shilingi **bilioni 10.6** zilizoidhinishwa lakini bado hazijalipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, miradi hii inahitaji jumla ya shilingi **bilioni 183.5** ili iweze kukamilika lakini kwa sasa imesimama kutokana na ukosefu wa fedha. Moja kati ya sababu za ukosefu wa fedha, ni Shirika kutopata kibali kutoka Hazina cha kuweza kukopa kiwango stahiki kumalizia miradi hiyo.

Aidha, Kamati imebaini kwamba, kuna madai mengine ambayo yameletwa na wakandarasi wa miradi hii yanayotokana na madai ya ziada kwa sababu ya mabadiliko ya ukubwa na/au usanifu wa mradi, gharama za kusimama kwa mradi, riba ya kuchelewesha malipo, pamoja na sababu nyingine kama hasara kwa sababu ya kushuka kwa thamani ya fedha na kuhuisha dhamana za malipo ya awali na dhamana za utendaji.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa miradi husika, sasa ni miaka nane (8) na tayari kiasi cha fedha shilingi **bilioni 154.6** zimekwisha tumika katika miradi hiyo. Kusimama kwa miradi hiyo, sio tu kunashusha thamani yake kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia na kiusanifu, lakini kunawaweka wateja ambao tayari wametoa fedha zao au kukopa benki ili kununua baadhi ya nyumba katika miradi hiyo, katika hali ya sintofahamu. Kwa upande wa Serikali na hususan kwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), riba ya deni la mkopo inayoongezeka inaifanya Serikali ipoteze fedha ambazo zingetumika katika uendelezaji wa miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kama msimamizi wa kisera wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa, imekuwa ikiishauri Wizara kuhusu namna bora ya kuinusuru miradi hii. Eneo mojawapo ambalo Kamati imekuwa ikitoa ushauri wake, ni kwa Wizara kuwa na mkakati endelevu ambao uthalisaidia Shirika kupunguza gharama za miradi, na hatimaye kupunguza, kama sio kuondoa kabisa hasara ambayo tayari shirika limepata.

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Waziri mwenye dhamana ameweke wazi mipango ya Wizara kunusuru miradi hiyo na kutoa maelekezo kwa Bodi mpya ya NHC ili kufanya maboresho, ikiwemo mapitio ya mikataba ili kuondoa vifungu visivyo na tija, pamoja na kuwa na Mpango wa Kurekebisha Mikopo (*Loans Restructuring Plan*). Sababu za kurekebisha mikopo hiyo ni pamoja na kulisaidia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kupata ahueni ya kifedha ambayo uthalisaidia kumalizia miradi mingine iliyokwama au kusimama kabisa, kufanya mtiririko wa fedha wa Shirika (*cash flow*) kuendana na mapato ya Shirika, kupandisha uwiano wa mtiririko wa fedha (*cash liquidity ratio*) ambayo ni mojawapo ya vigezo vya baadhi ya wakopeshaji pamoja na kuepuka adhabu za kulipa riba za ziada endapo Shirika litashindwa kulipa mikopo hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanapaswa kuzingatiwa na Shirika kwa usimamizi wa Wizara katika mpango huo ni pamoja na kuongeza urefu wa kulipa mikopo, kupunguza viwango vya riba vya mikopo, kubadilisha malipo ya mikopo yote kuwa ya kila mwezi na pia kubadilisha sarafu ya mikopo hiyo, kutoka mikopo kwa dola za kimarekani (USD) kuwa mikopo kwa shilingi za kitanzania (TZS).

Mheshimiwa Spika, hatua ya kupanga ni moja, na hatua ya kutekeleza mipango hiyo ni jambo lingine. Hivyo basi, ni vema Serikali ikaharakisha utekelezaji wa mipango hiyo ili kuiokoa miradi husika na pia kuokoa fedha za umma. Kamati ina maoni kwamba, Shirika litumie fursa ya vyanzo vya mapato vilivyopo ili kukusanya fedha zitakazosaidia kuendeleza miradi inayosuasua au kusimama. Aidha, kwa kuzingatia kuwa Shirika lina miradi mingi kwa sasa, ni vyema rasilimali

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilizopo ndani ya shirika, kwa maana ya watumishi na vitendea kazi, zikatumika kukamilisha kwanza miradi iliyopo kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya.

Wizara ya Maliasili na Utalii

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Kamati imekutana na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na taasisi zake ili kupokea na kujadili taarifa mbalimbali kama ifuatavyo:-

2.2.11 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Utalii kusini mwa Tanzania (REGROW)

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Agosti, 2019 Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa programu ya kuendeleza utalii kusini mwa Tanzania (REGROW). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kufikia muafaka na Benki ya Dunia kuhusu maeneo ya kutekeleza mradi huu. Kamati ilielezwa kwamba, kwa kuanzia, programu hii itatekelezwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba, Serikali imebadili sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, na kwa sababu programu hii awali ilipangwa kutekelezwa katika pori hilo, ni moni ya Kamati kwamba, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ijumuishwe katika Mpango wa REGROW. Aidha, ni vema Serikali ikaharakisha utekelezaji wa programu hii ili manufaa yake yaanze kuonekana mapema.

2.2.12 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Kuhuisha Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Kufanyika Tathmini Kuhusu Tija iliyopo katika Mfumo wa Matumizi Mseto ya Ardhi (Multiple Land Use System)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Azimio la Bunge lilitotajwa hapo juu. Kamati ilifahamishwa kwamba Wizara imeunda Kamati ya Wataalam, inayofanya tathmini ya Mfumo wa Matumizi Mseto ya Ardhi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na uwezekano wa kuhuisha Sheria iliyoanzisha mamlaka hiyo ili iendane na hali halisi ya sasa. Taarifa iliyopo ni kwamba, Kamati hiyo imekamilisha kukusanya taarifa muhimu na kwamba kwa sasa inakusanya maoni ya wadau, ikiwa ni pamoja na wananchi wanoishi ndani na nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tangu Kamati ianze kushauri kuhusu jambo hili sasa ni zaidi ya miaka mitatu (3). Hata hivyo, zoezi la tathmini, utafiti na kukusanya maoni unachelewa na hivyo kusababisha maamuzi kuhusu jambo hili kutofanyika kwa wakati kwa mustakabali wa hifadhi na wanaoishi ndani ya hifadhi.

2.2.13 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tanzania Wildlife Management Authority)

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Kamati ilipokea taarifa mbalimbali kuhusu utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Mnamo tarehe 22 Oktoba, 2019 Kamati ilipokea taarifa kuhusu hali ya uhifadhi wa Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Maeneo ya Ardhi Oevu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa kwamba, tangu ianze kutekeleza majukumu yake Mwaka 2016, TAWA imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kuimariika uhifadhi kunakotokana na kupungua kwa ujangili, kuthibitiwa kwa vitendo vya uingizaji na ulishaji wa mifugo katika Mapori ya Akiba na kuanzisha na kufanya mabadiliko ya kimfumo wa usimamizi wa uhifadhi kutoka wa kiraia kwenda Jeshi Usu. Aidha, TAWA imesaidia kuimariisha utalii kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vinavyosimamiwa na Mamlaka kutoka

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watalii 35,479 mwaka 2015/2016 hadi watalii 129,428 kwa mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 234.7.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ina changamoto mbalimbali. Pamoja na kwamba mapato ya Mamlaka hiyo yameongezeka kutoka shilingi **Bilioni 38.3** mwaka 2015/2016 hadi kufikia **Bilioni 48.8** mwaka 2017/18, lakini bado ongezeko linaweza lisikidhi mahitaji halisi ya utekelezaji wa shughuli za Mamlaka hiyo ambayo yanakadirwa kuwa ni shilingi **bilioni 150** kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayoikabili Mamlaka hii ni ukosefu wa Sheria mahsusini inayosimamia uratibu na utekelezaji wa majukumu yake. Kwa sasa, Mamlaka bado inatekeleza majukumu yake kutokana na Kifungu cha 8 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 pamoja na Amri ya Serikali (Order) iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 135 la tarehe 09 Mei, 2014 (pamoja na marekebisho yake).

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa Sheria mahsusini, kumesababisha Mamlaka hii, ambayo inasimamia maeneo makubwa zaidi ya kiuhibadhi, kusuasua kiutendaji na hivyo kupunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

2.2.14 Taarifa Kuhusu Hali ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Wizara kwa kuleta mabadiliko ya Sheria ambayo yanaongeza muda wa umiliki wa vitalu vya uwindaji kutoka miaka mitano, na kuwa miaka kumi hadi kumi na mitano. Aidha, inapongeza hatua ya Serikali kupunguza madaraja ya vitalu, kutoka madaraja matano hadi madaraja matatu. Vilevile, Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali, kuwaongeza muda wamiliki wa vitalu wa sasa, wakati ikiendelea kufanya maboresho ya uendeshaji wa uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi wa Kamati, zoezi la kugawa vitalu kwa njia ya mnada, limeonekana kuwa na tija zaidi kimapato, ikilinganishwa na utaratibu uliokuwepo hapo awali. Katika mnada wa vitalu uliofanyika Juni 2019, kampuni mbili (2) katika nane (8) zilizoshiriki mnada wa vitalu zilishinda jumla ya vitalu saba (7) katika vitalu 26 vilivyotangazwa. Vitalu saba (7) vilivyogawanywa kwa njia ya mnada thamani yake ilifikia dola za kimarekani 831,000 ikilinganishwa na dola za kimarekani 288,000 iwapo vitalu 26 vyote vingegawanywa kwa utaratibu wa awali. Hivyo, ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada wa ki-elektroniki umewevesha nguvu ya soko kuamua ada ya kitalii cha uwindaji wa kitalii na pia umeongeza uwazi na utawala bora katika zoezi la ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, pamoja na ongezeko hilo la mapato, Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye tathmini ya kina ili kujua ni kwa sababu gani, iwe za kiushindani, za kimasoko, za kiubora wa vitalu vyetu, au sababu nyingine yoyote iliyosababisha vitalu kumi na tisa (19) katika vitalu ishirini na sita (26) kutopata mnunuzi. Ni kweli, mapato yameongezeka, lakini kama vitalu vyote vingepata wanunuzi katika mnada uliofanyika, ingechangia kuendeleza uhifadhi na kuongeza pato la taifa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

2.2.15 Taarifa Kuhusu Hadhi na Hatma ya Pori la Akiba la Selous Kufuatia Uamuza wa Serikali kumega sehemu ya Pori hilo ili iwe Hifadhi ya Taifa ya Nyerere

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza uamuza wa Serikali wa kumega sehemu ya pori la akiba la selous lenye ukubwa wa kilometra za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. Hatua hii ni muendelezo wa kumuenzi Hayati Baba wa Taifa ambaye alitoa mchango mkubwa katika uhifadhi wa rasilimali za taifa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hata hivyo, katika eneo linalosimamiwa na TANAPA (Hifadhi ya Taifa ya Nyerere) na katika eneo linalosimamiwa na TAWA, mpaka wa maeneo haya mawili uko ndani ya eneo la bwawa la kufua umeme la Nyerere (Nyerere Hydro Power Dam). Kamati inashauri, menejimenti zinazohusika na eneo lote lilikuwa Pori la Akiba la Selous zikae pamoja ili kuwa na utaratibu wa kulisimamia eneo hili na kuепusha migongano ya kimenejimenti inayoweza kutokea.

2.2.16 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Hoteli na Lodges za Serikali zilizobinafsishwa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kupata taarifa hiyo kutoka Serikalini kwa lengo la kufahamu kwa kina kuhusu utekelezaji wa mikataba na makubaliano, faida itokanayo na uwekezaji pamoja na tija itokanayo na uwekezaji uliofanyika katika kutatua changamoto ya upungufu wa vyumba vya kulala wageni. Kamati ilikutana na Wizara kwa nyakati tofauti tarehe 28 Agosti, 2019, tarehe 28 Oktoba, 2019 na tarehe 21 Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado haijaridhishwa na mwenendo wa Serikali katika kutoa taarifa kuhusu suala hili kwa sababu Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha na Mipango bado hazijawa na taarifa ya pamoja kulieleza Bunge ya kile ambacho Kamati imekuwa ikitaka maelezo. Baada ya makubaliano ndani ya Serikali, Kamati ilikubaliana na ombi lao kwamba taarifa hiyo iwasilishwe katika vikao vya Kamati vijavyo kuelekea Mkutano wa Bajeti, kama jambo mahsus.

2.2.17 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor Tanzania (TAWIRI)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu utendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor Tanzania (TAWIRI). Kamati inaipongeza TAWIRI kwa kufanya tafiti mbalimbali katika sekta ya wanyamapor zinazolenga kuongeza uhifadhi na kuzuia uharibifu wa mazao, na madhara kwa binadamu. Zipo tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu tembo, mamba, mbwa mwitu, simba n.k.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba matokeo ya tafiti zilizofanyika hayatumiki ipasavyo. Mfano, katika Ziwa Rukwa, utafiti umegundua kwamba njia bora ya kujenga aina ya uazio ndani ya ziwa katika maeneo ambapo binadamu wanaweza kutumia maji ya ziwa hilo bila kushambuliwa na mamba. Hata hivyo, ni sehemu chache ambazo wananchi wameweza kutumia teknolojia hiyo. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba, wananchi na wadau mbalimbali wa sekta ya wanyapor kutumia matokeo ya tafiti za TAWIRI ili kuongeza tija na ufanisi katika uhifadhi wa wanyamapor.

2.2.18 Taarifa Kuhusu Hifadhi za Taifa: Mafanikio na changamoto

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Kamati imepokea taarifa mbalimbali kuhusu Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ambazo zimekuwa zikielezea masuala mbalimbali ya utekelezaji wa Shirika hilo na Hifadhi za Taifa ambazo linazisimamia. Kamati inaipongeza TANAPA kwa hatua mbalimbali ambazo shirika hilo linachukua katika kuendeleza uhifadhi. Aidha, tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha Hifadhi za Taifa mpya sita (6) za Mto Ugalla, Kigosi, Nyerere, Burigi – Chato, Ibanda – Kyerwa na Rumanyika – Karagwe. Hii ni hatua nzuri katika kuongeza ulinzi wa rasilimali zetu. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba, hata kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi hizo mpya, tayari TANAPA ilikuwa na mzigo mkubwa kwa vile kati ya hifadhi kumi na sita (16) ilizokuwa ikizisimamia, ni hifadhi mbili za Serengeti na Kilimanjaro zilizokuwa zinafanya vizuri kwa kuzalisha ziada ambayo ilikuwa inatumika kuzisaidia hifadhi nyingine ambazo hazijaweza kujitegemea. Hifadhi tatu (3) za Tarangire, Ziwa Manyara na Arusha, zilikuwa zinazalisha kiasi cha kutosheleza gharama zake za uendeshaji. Hifadhi kumi na moja (11) zilizobakia, zinazalisha pungufu ya gharama zake za uendeshaji na hivyo kutegemea mapato ya ziada yanayotoka katika hifadhi nyingine.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali, kuipunguzia TANAPA baadhi ya tozo kwa lengo la kujengea uwezo ili iweze kuzilea na kuziendelea hifadhi mpya zilizoanzishwa.

2.2.19 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Chuo cha Wanyamapor Pasiansi na Chuo cha Likuyu Seka Maganga

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utendaji wa vyuo vya wanyamapor via Likuyu Sekamaganga kilichopo Namtumbo, Ruvuma pamoja na Pasiansi, kilichopo Mwanza. Katika taarifa zote mbili, Kamati ilibaini kwamba, vyuo hivyo vina upungufu mkubwa wa watumishi ambao unavifanya visitekeleze malengo yake ipasavyo. Aidha, ipo changamoto ya ukosefu wa ajira kwa wahitimu wa vyuo hivi.

Mheshimiwa Spika, katika chuo Likuyu Sekamaganga, iko changamoto ya ukosefu wa umeme unaotoka katika gridi ya Taifa na badala yake wanatumia jenereta hali inayokiongezea chuo gharama za uendeshaji. Aidha, Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba chuo hicho kina mandhari nzuri inyoweza kutumika kwa shughuli za kijamii kama picnic, utalii wa picha n.k, bado chuo kimeshindwa kuzitumia vizuri kwa sababu ya upungufu wa rasilimaliwatu na bajeti ndogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, vyuo hivi pamoja na vingine ambavyo vinatoa elimu kuhusu masuala ya uhifadhi, ni muhimu kwa maendeleo ya sekta hii. Kamati inaishauri kwamba, Serikali iwe na mkakati endelevu wa kuvipatia fedha vyuo hivi ili kuongeza tija. Aidha, kwa kuzingatia ukweli kwamba, kuna upungufu mkubwa wa askari wa wanyapor katika Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na TAWA, na hivyo kusababisha uvamizi wa baadhi ya maeneo ya hifadhi, Kamati inaishauri Serikali kuajiri wahitimu wanaotoka katika vyuo hivi ili kuongeza ulinzi wa hifadhi zetu.

2.2.20 Taarifa Kuhusu Utendaji wa Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) Moshi

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyowasilishwa na chuo hiki ilibainisha changamoto mbalimbali zinazokikabili chuo hicho ikiwemo upungufu wa baadhi ya miundumbini kama vile madarasa, computer, usafiri wa basi na mashine za kukata mbao (*chainsaws*).

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi uliofanyika, hoja kuu iliyoibuliwa na Kamati ni kukosekana kwa dhamira ya dhati inayolenga kutatua changamoto za chuo hicho zikiwemo upungufu wa miundumbini muhimu ya kufundishia ikilinganishwa na mahitaji halisi ya chuo. Kwa mfano, taarifa ilibainisha kwamba chuo hicho upungufu wa madarasa manne (4), computer 50, minibus 1 na mashine za kukata mbao (*chainsaws*) 40. Wakati huo huo, katika miaka mitatu (3) iliopita, chuo hicho chenye watumishi 37 na uwezo wa kudahili wanafunzi 250, kimekuwa na mapato ya wastani wa Tshs Bilioni 1.171 kila mwaka. Fedha hizo ni kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo ada za wanafunzi, fedha kutoka Hazina, michango kutoka TFS na TaFF, miradi ya uzalishaji mali pamoja na michango ya wahisani. Hata hivyo, pamoja na kupokea fedha hizo, chuo kimeshindwa kutatua changamoto ya kukosekana kwa miundumbini iliyoainishwa na hivyo kuibua maswali ya iwapo kuna ubadhirifu wa fedha inayopokelewa.

Mheshimiwa Spika, kutohara na melezo niliyotoa hapo juu, Kamati inaishauri ufanyike ukaguzi maalum (*special audit*) ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha katika Chuo hicho.

2.2.21 Taarifa Kuhusu Kuanzishwa kwa Jeshi Usu

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukabiliana na ujangili na uvunaji holela wa rasilimali za wanyamapor na misitu hapa nchini na ili kuboresha nidhamu na utendaji kazi, Wizara ya Maliasili imeanzisha Jeshi Usu (*paramilitary*) ambalo lilizinduliwa rasmi Mwezi Novemba 2018. Jeshi Usu linaundwa na Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania (TAWA) na Wakala wa Misitu (TFS)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa mamlaka itakanayo na Kifungu cha 10 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ambayo iliwasilishwa kwa Kamati, Wajumbe walitaarifiwa kwamba, hadi kufikia Desemba 2019 takriban watumishi 2,460 wamepatiwa mafunzo ya utayari (*transformation course*) ya kuijunga na Jeshi Usu. Tunaipongeza Wizara kwa hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, katika kipindi hiki cha mpito cha kubadilisha mfumo wa utumishi kutoka uliopo sasa, kwenda katika mfumo wa Jeshi Usu, utaratibu mzuri uandaliwe, ikiwemo kutungwa kwa Sheria mahsusititakayoratibu mfumo huo ili watumishi waliopo wapewe vyeo stahiki, maslahi stahiki na mazingira bora ya utendaji wa kazi zao. Hii itasaidia kupunguza malalamiko yanayoweza kujitekeza.

2.2.22 Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Azimio la Bunge la Kuipandisha Hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS) kuwa Mamlaka

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto kubwa ya uharibifu wa misitu hasa inayomilikiwa na vijiji na Halmashauri za Wilaya, hali iliyopelekea Kamati hii kuishauri Serikali kuipandisha Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuwa Mamlaka. Lengo la uamuhi huu ni kuanzisha mamlaka moja itakayokuwa na nguvu za kisheria za kudhibiti matumizi ya rasilimali zote za misitu nchini, bila kujali umiliki. Taarifa iliyowasilishwa na Wizara, ilionyesha kwamba mchakato huo umeanza kwa kukusanya taarifa na kuandaa andiko litakalopelekwa ngazi za juu kwa maamuhi.

Mheshimiwa Spika, hadi wakati taarifa hii inaandaliwa, Kamati imepata taarifa kwamba bado Wizara inaendelea kukusanya maoni ya wadau. Kamati ina maoni kwamba, mchakato huo unapaswa kwenda kwa kasi zaidi hasa ikizingatiwa kwamba kasi ya uharibifu wa misitu ni kubwa ukilinganisha na jitihada za kuilinda rasilimali hiyo muhimu. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha zoezi la kuipandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu kuwa mamlaka ili kuinusuru misitu yetu.

2.3 UKAGUZI WA MIRADI MBALEMBALI YA MAENDELEO PAMOJA NA ILE ILIYOTENGWA FEDHA KATIKA BAJETI YA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilifanya ziara mbalimbali za ukaguzi wa miradi inayotekeliza na Serikali ili kujionea hatua za utekelezaji wake. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 98 (1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, hususan baada ya Wabunge kupokea Mapendekezo ya Mpango na Kiwango cha Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Kamati ilikagua miradi iliyotengewa fedha katika Bajeti ya Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika kaguzi zote ambazo Kamati ilifanya, Wajumbe walipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo, zikainisha bajeti iliyotengwa, chanzo cha fedha za mradi husika, kiwango cha mapokezi na matumizi ya fedha zilizopokelewa. Aidha, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, Kamati ilifanya tathmini ya thamani ya fedha ya miradi hiyo pamoja na ufanisi wake baada ya kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari naomba nilitaarifu Bunge lako kuhusu ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

2.3.1 Mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) wa Ujenzi wa Nyumba za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Machi, 2019 Kamati ilifanya ziara mkoani Tanga katika Wilaya ya Muheza ili kujionea utekelezaji wa mradi tajwa. Katika ziara hiyo, Kamati ilishuhudia ujenzi wa nyumba za makazi unaotekelizwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, eneo la Chatur. Maendeleo ya mradi ni mazuri kwa ubora ila kasi ya utekelezaji wake ilikuwa chini kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha kutoka Halmashauri hiyo.

Aidha, Kamati ilibaini kwamba nyumba hizo zina nafasi finyu (*square space*) ikilinganishwa na mazingira halisi ya sasa. Kamati ilishauri, Shirika la Nyumba kuwahusisha wadau katika hatua za usanifu wa mradi ili kukubaliana ukubwa wa nyumba zitakazojengwa. Aidha, halmashauri zinashauriwa kutenga bajeti ya kutosha kabla ya kuanza kwa miradi.

2.3.2 Fungu 48, Mradi Na. 2323 – Uimarishaji wa Mipaka ya Nchi Katika Mpaka wa Tanzania na Kenya, Eneo la Horohoro

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mpaka wa Tanzania na Kenya katika Kijiji cha Jasini na Eneo la Horohoro, Mkoani Tanga. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa ikiwemo kutobainishwa mipaka ya majini na nchi kavu katika baadhi ya maeneo, hali inayosababisha wananchi wa maeneo husika kupata misukosuko ya kukamatwa na mamlaka za ulinzi katika mipaka. Mfano ni baadhi ya wavuvi wa Tanzania waliokamatwa na askari wa Kenya wakidaiwa kuvua samaki katika eneo la Kenya.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya nyumba zilizojengwa na wanachi kwa ajili ya makazi zina changamoto ya sehemu moja ya nyumba hizo kuwa Kenya na sehemu kuwa Tanzania. Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa ukanda huru (*buffer zone*) ambao ungerahisisha kubainisha mipaka. Kamati inaishauri Serikali, kuongeza kasi katika zoezi la kuimarisha mipaka ili kuwapunguzia wananchi wanaoishi mipakani adha ya kusumbuliwa na mamlaka husika kwa kwa sababu tu mipaka kutokuwa bayana pamoja na kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu.

2.3.3 Mradi wa Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi (*Land Tenure Support Program*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika mradi huu uliokuwa unatekelezwa na Wizara kwa majaribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga. Kamati imeridhishwa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huo ambayo kwa kiasi kikubwa yamechangia kupunguza migogoro ya ardhi, kuwawezesha watu kuwa na hatimiliki za ardhi pamoja na kupima na kupanga matumizi ya ardhi. Hata hivyo, kwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha za utekelezaji wa mradi huu zilikuwa ni fedha za wafadhili, na kwa vile mradi huu umefungwa, kumejitokeza changamoto ya kukosekana kwa uendelevu wa mafanikio ya mradi huo katika wilaya nyingine za mkoa wa Morogoro na nchi kwa ujumla.

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kwamba, katika miradi yote inayopokea fedha za wafadhili, ni vyema zikatengwa fedha za kutosha za ndani ili kuwa na uendelevu wa miradi au programu husika baada ya ufadhili kuisha.

Wizara ya Maliasili na Utalii

2.3.4 Mradi wa Ujenzi wa Uzio wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapozi cha Mweka

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Machi, 2019 Kamati ilitembelea Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka. Katika ziara hiyo, Kamati ilipokea taarifa kuhusu miradi mbalimbali

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inayotekelzwa chuoni hapo ikiwemo ujenzi wa uzio. Kamati ilikagua na kuona kwamba hatua iliyofikiwa ni ya kuridhisha. Hata hivyo, Kamati ilishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha hasa katika ujenzi wa madarasa, kutohana na upungufu uliopo pamoja na kukarabati miundombinu iliyochakaa.

2.3.5 Fungu 69, Mradi Na. 4811 - Kuendeleza Hifadhi ya Misitu ya Mazingira Asilia

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 na 17 Machi, 2019 Kamati ilifanya ziara katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia ya Chome na msitu asilia wa Magamba ili kujionea utekelezaji wa mradi. Kamati ilijulishwa kwamba lengo la mradi huo ni kuimarishta ulinzi kwa kujenga vituo vya ulinzi (ranger posts). Mradi ulikuwa unaendelea vizuri na kwamba ulikuwa umekamilika kwa zaidi ya asilimia tisini na tano (95%).

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia, hasa Msitu wa Chome, ni uvamizi wa wananchi wanaokuja kuchimba madini ya dhahabu. Jambo hili linachangia, sio tu uharibifu wa misitu, bali pia uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na kemikali zinazotumika kuchenjua dhahabu.

Aidha, Kamati imebaini kwamba, pamoja na misitu hii kuwa kivutio kikubwa cha utalii, na hivyo kuwa ni mojawapo ya vyanzo vya mapato, bado uongozi wa hifadhi haujaweza kuitumia fursa hiyo kikamilifu kujongezea mapato. Hii inachangiwa na sababu za kimuundo katika utumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kutouwa na kada ya afisa utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwanza inashauri Serikali kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa hifadhi za misitu ya mazingira asilia pamoja na kuwashirikisha katika kuilinda. Aidha, Serikali ichukue hatua madhubuti kudhibiti wavamizi wanoingia katika hifadhi kwa ajili ya kuchimba madini. Vile vile, Serikali ione umuhimu wa kuongeza kada ya maafisa utalii ili kutangaza vivutio vilivyopo katika misitu hiyo na kuongeza mapato kupitia vivutio vya utalii.

2.3.6 Utekelezaji wa Mradi Kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) katika Hifadhi za Taifa za Mikumi na Ruaha

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Hifadhi za Taifa za Mikumi na Ruaha, ambazo ni moja kati ya hifadhi za taifa ambapo mradi wa REGROW utatekelezwa. Malengo ya mradi katika hifadhi hizo, ni kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege. Kiuhalisia, hali ya miundombinu iliyopo sasa ya barabara na viwanja vya ndege hairidhishi. Mfano, katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wakati wa kipindi cha mvua, baadhi ya maeneo ya hifadhi hayafikiki kirahisi kwa sababu baadhi ya madaraja yameharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Spika, katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kuna athari ya kimazingira ambapo kuna tishio la kukauka kwa Mto Ruaha Mkuu. Mto huu ni tegemeo kubwa, na chanzo cha maji kwa wanyamapori. Kamati imebaini kwamba, kwa takwimu za hivi karibuni, mto huo hukoma kutiririka kwa takriban wiki kumi na tisa (19) kwa mwaka. Hali hii ni tishio kwa ustawi wa hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inafahamu kwamba moja ya malengo ya mradi wa REGROW ni kuimarishta miundombinu ya maji. Hivyo basi, ni vema Serikali ikaharakisha utekelezaji wa programu hii ili kuwezesha miundombinu yote muhimu kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuvutia watalii wengi zaidi.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2.4 KUPOKEA NA KUCHAMBUA TAARIFA ZA WIZARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63 (3) (b) imelipa Bunge loko tukufu, mamlaka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa kuzingatia masharti hayo ya Katiba, pamoja na Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua taarifa za Wizara inazozisimamia kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 katika vikao vilivyoafanyika tarehe 22 – 29 Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtsari naomba nilitaarifu Bunge loko tukufu kuhusu masuala muhimu yaliyojiteza katika uchambuzi huo kwa kila Wizara inayosimwamiwa na Kamati hii kama ifuatavyo:-

2.1.1 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyowasilishwa na Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa katika utekelezaji wa bajeti ya 2018/2019 na pamoja na bajeti ya 2019/2020 na tayari Kamati ilitolea maoni yaliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi iliidhinishwa na Bunge jumla ya shilingi 65,989,347,638/= na kupewa ongezeko la shilingi bilioni 12,155,724,516 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa na kupelekea bajeti ya Wizara kuwa shilingi 78,145,072,154. Kati ya fedha hizo shilingi Bilioni 29.26 zilikuwa ni za matumizi ya kawaida na shilingi Bilioni 46.1 ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika Februari, 2019 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Billioni 46.1 sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Bunge loko liliidhinisha jumla ya shilingi 2,081,926,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 1, 102, 104,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 979, 822,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hatahivyo, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Tume iliidhinishwa shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2019 Tume ilipokea jumla ya shilingi 1,098,873,302 sawa na asilimi 47.2 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti ulionyesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni wa kuridhisha kwa mafungu yote mawili. Kamati ilishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kusimamia sekta ya Ardhi ipasavyo ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi (Fungu 48) ililiomba Bunge loko Tukufu liidhinisha jumla ya shilingi 57, 439, 991,387. Kati ya fedha hizo shilingi 33,155,487,000/= ziliombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 24,284,504,387/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati ilibaini kwamba, maombi hayo ya fecha yalipungua kwa shilingi 20, 705, 180,767 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo punguzo hilo ni sawa na asilimia 26%. Kamati ikuwa na maoni kwamba, punguzo hilo lingeweza kusababisha Wizara kushindwa kufikia malengo iliyojiweka .

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Aidha kwa upande wa bajeti ya maendeleo bajeti ilipungua kwa shilingi 6,253,097,613 sawa na asilimia 20.2 ikilinganishwa na shilingi 30,537,602,000 iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2018/19. Kamati pia ilikuwa na maoni kwamba, kupungua kwa bajeti hiyo kungezorotesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, (Fungu 03) katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ililiomba Bunge liidhinishe jumla ya shilingi 5,951,072,000/= ili ziweze kutumika kutekeleza mpango na bajeti ya Tume hiyo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,245,072,000/= ziliombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti ulibainisha kupungua kwa fedha inayoombwa kwa shilingi 1,830,854,000 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2018/19 ya shilingi 7,781,926,000. Upungufu huu ulitokana na kupunguzwa kwa bajeti ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 5,000,000,000 mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni 3,000,000,000. Kamati ilikuwa na maoni kwamba, hali hiyo ingezorotesha shughuli za upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vilivyo fanyika Januari, 2020 Kamati ilipokea na kujadili taarifa iliyowasilishwa na Wizara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti kwa Kipindi Cha Nusu Mwaka Julai – Disemba 2019 ili kuweza kufanya uchambuzi kuhusu mapato, matumizi na changamoto nyengine ambazo Wizara inakabiliana nazo katika kutekeleza bajeti inayoendelea. Moja kati ya changamoto ambazo Kamati ilibaini katika Wizara hii, ni mapokezi madogo ya fedha ikilinganishwa na bajeti iliyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha nusu mwaka, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 164.6 kutoka vyanzo mbalimbali nya mapato yatokanayo na sekta ya ardhi. Hadi kufikia Desemba, 2019, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 56.85 sawa na shilingi bilioni 9.5 kwa mwezi. Kamati ilitaarifiwa kwamba, kasi ndogo ya ukusanyaji imechangiwa na changamoto mbalimbali ikiwemo wataalam wa sekta ya ardhi kusimamishwa kazi katika vituo vyao kutokana na tuhuma zinazowakabili. Aidha, bado kuna mwamko mdogo wa wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Ili kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato katika kipindi kilichobaki (Januari – Juni 2020) Wizara ilijinasibu kwamba itaendeleza kutekeleza mkakati wa makusanyo ya maduhuli ikiwemo, kuwapeleka wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi kwenye vyombo nya sheria ili kulipa kodi na kuendelea kutoa elimu ya mlipakodi za pango la ardhi, ada na tozo zingine zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Matumizi ya Fedha za Kawaida (OC), katika kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Desemba 2019), Wizara ilihitaji jumla ya Shilingi bilioni 7.94 kwa ajili ya matumizi hayo. Hadi kufikia tarehe 30 Desemba, 2019 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi bilioni 7.051 sawa na asilimia 88 ya kiasi kilichopangwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, kiasi cha shilingi bilioni 3.808 kilitumika sawa na asilimia 53.9.

Mheshimiwa Spikwa, kwa upande wa Fedha za Maendeleo, hadi kufikia tarehe 30 Desemba, 2019 jumla ya shilingi 7,289,589,480 zilipokelewa sawa na asilimia 30 ya bajeti ya maendeleo ya shilingi 24,284,504,387. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 4,660,701,055 ni fedha za ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 18,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Land Tenure Support Program-LTSP na Mradi wa Kupanga Kupima na kumilikisa kila kipande cha ardhi. Aidha fedha za nje kiasi cha shilingi 2,628,888,425 zilitolewa ikilinganishwa na bajeti ya 6,284,504,387 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Land Tenure Support Program-LTSP.

2.4.2 Wizara ya Maliasili na Utalii

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyowasilishwa na Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa katika utekelezaji wa bajeti ya 2018/2019. Uchambuzi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Njia zilizotumika ni pamoja na kuangalia hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi 2019, na majadiliano yaliyofanyika yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vyta Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shillingi **63,176,454,573.75** kutokana na vyanzo mbali mbali vyta mapato yanayotokana na sekta ya Maliasili na Utalii. Hadi kufikia Februari 2019, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni **32,996,004,795** sawa na asilimia 52% ya kiwango kilichokadirwa kukusanya kwa mwaka, hii ni pungufu ya asilimia 17.4% ya makusanyo ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha uliopita. Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa makusanyo na ilishauri Wizara kuipa kipaumbele sekta ya utalii na kuboresha uwindaji wa kitalii, utalii wa picha, utalii wa fukwe, utalii wa malikale na utalii wa kitamaduni ili kukusanya zaidi na kuchangia zaidi kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kamati ulibaini kwamba, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa utolewaji wa fedha kwa wakati hususan fedha za ndani. Kwa mfano, hadi kufikia Februari, 2019 hakukuwa na fedha zozote za ndani zilizotolewa ikilinganishwa na asilimia 39.1% ya fedha za wafadhili zilizotolewa. Hali hii iliathiri utekelezaji wa miradi na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Maliasili na Utalii iliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **120,202,637,734**. Kati ya fedha hizo shilingi **71,312,649,000/=** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **48,889,989,734/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo iliongezeka kutoka shilingi **bilioni 29,978,082,000** mwaka 2018/2019 hadi shilingi **bilioni 48,889,989,734** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 66%.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha nusu mwaka kufikia Desemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh.29,129,647,570** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **81** ya **Sh.36,157,707,219** fedha zilizotengwa kwa kipindi cha nusu mwaka. Kati ya fedha zilizotolewa **Sh.22,625,700,602** ni fedha za mishahara na **Sh.6,503,946,967.52** fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, **Sh.48,889,988,734** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi minane (8). Fedha hizo zinajumuisha **Sh.1,000,000,000** fedha za ndani na **Sh.47,889,988,734** fedha za nje. Hadi kufikia Desemba 2019, Wizara ilipatiwa jumla ya **Sh.4,185,688,350** fedha za nje kwa miradi miradi minne (4) ya maendeleo zilizotolewa moja kwa moja (Direct to the Project Funds-DFunds) sawa na **asilimia kumi na saba (17%)** ya **Sh.24,454,768,000** fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi kwa kipindi cha nusu mwaka. Miradi iliyopatiwa fedha ni pamoja na;

- i. Mradi wa "Sustainable Management of Natural Resources" uliopatiwa **Sh.1,094,548,000** fedha za nje;
- ii. Mradi wa "Natural Resources Management Economic Development (NRM-LED)" uliopatiwa **Sh.1,150,665,000** fedha za nje;
- iii. Mradi wa "Forestry and Value Chain Development Program (FOVAC)" uliopatiwa **Sh.1,861,992,149** fedha za nje; na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

iv. Mradi wa "Natural Resources Management for Tourism and Growth Project (REGROW)" uliopatiwa **Sh.78,483,201** fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa mwenendo wa uwasilishwaji wa fedha za wafadhili ni mdogo, ukilinganishwa na umuhimu wa kutekeleza miradi hiyo na mingineyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati endelevu wa kubuni vyanzo vipyta vya mapato ya ndani.

2.5 USHIRIKI WA SEMINA, MAADHIMISHO NA MATAMASHA

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Wajumbe wa Kamati walishiriki semina, maadhimisho na matamasha, kwa mwaliko Wizara na taasisi ambazo Kamati inazisimamia, pamoja na wadau wengine kutoka asasi za kiraia na mashirika binafsi wanaojishughulisha na sekta zinazosimamia na Kamati hii. Kwa muhtasari, Kamati ilishiriki katika matukio hayo kama ifuatavyo:-

- Kilele cha Tamasha la Urithi, Mwanza (URITHI Festival), Mwanza
- Maadhimisho ya Miaka 60 ya TANAPA na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Fort Ikoma
- Semina Kuhusu Jeshi Usu
- Sherehe za Tuzo za Waongoza Watalii, Arusha
- Mbio za Nyika za Ngorongoro (Ngorongoro Marathon)
- Sherehe ya Uzinduzi wa Jeshi Usu, Fort Ikoma
- Sherehe za Uzinduzi wa Hifadhi za Taifa za Burigi – Chato, Ibanda – Kyerwa na Rumanyika - Karagwe
- Tukio la Kupanda Mlima Kilimanjaro kwa baadhi ya Wabunge
- Semina Kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji kwa Njia ya Mnada
- Semina Kuhusu Kuhusu Kanuni za Uanzishwaji wa Mabucha ya Nyama Pori
- Semina Kuhusu Mpango wa Matumizi ya Ardhi
- Semina Kuhusu Miradi inayotekelizwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza Wizara kwa kutushirikisha katika matukio mbalimbali ambayo yanachangia kuongeza uelewa na kutuweka katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali. Hatua hii pia inachangia kuwawezesha Wajumbe kuvifahamu na kuwa mabalozi wa kutangaza vivutio vyetu vya utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kulishirikisha Bunge lako kuhusu baadhi ya matukio ambayo Wajumbe wa Kamati walishiriki na kutoa maoni yao hususan katika mada, mjadala, semina au mafunzo yaliyotolewa kama ifuatavyo:-

2.5.1 Semina Kuhusu Mapendekezo ya Kuanzishwa kwa Kanuni za Kuanzisha Mabucha ya Kuza Nyamapori

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu limekasimu madaraka ya kutunga Sheria Ndogo mbalimbali kwa Waziri, kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Katiba ya nchi, na Sheria mbalimbali za Bunge. Kamati ilipata nafasi ya kipekee, baada ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kuwashirikisha Wajumbe, kama wadau, katika mchakato wa maandalizi ya Kanuni za Kuanzisha Mabucha ya Kuza Nyamapori.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizo zinalenga kuweka masharti ambayo yatarahisisha upatikanaji wa nyamapori kwa kuwa, kwa Sheria na Kanuni zilizopo, ni vigumu kwa mwananchi wa kawaida kupata nyama hiyo. Kwa hali ilivyo sasa, ili mwananchi apate nyamapori, kuna taratibu nyingi na mlolongo mrefu ikiwemo, ulazima wa kupata vibali, leseni za kumiliki silaha za kuwindia na usafiri. Aidha, ni lazima uwindaji huo ufanyike katika msimu husika wa uwindaji. Hali hii imesababisha baadhi ya wananchi kutumia njia haramu ili kupata nyamapori.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii ambayo inatekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye mara zote amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi yetu, zinawanufaisha watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwagine, Kamati iliishauri Wizara kuhakikisha kwamba kunakuwepo kwa utaratibu madhubuti ambaa utahakikisha kunakuwepo na usalama wa afya kwa mlaji wa nyamapori. Jambo hili linaweza kufanyika kwa kuwahuusisha madaktari wa wanyapori kupima ubora wa nyama itakayouzwa. Ushauri huu unazingatia ukweli kwamba, wanyapori pia huwa na magonjwa ambukizi kwa binadamu, na mengine huwa na athari kubwa. Aidha, kuwepo utaratibu utakaobainisha vigezo na masharti ya uvunaji wa wanyamapori ili isiwe chanzo cha ujangili.

2.5.2 Semina Kuhusu Mpango ya Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, semina hii ilitolewa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kwa lengo la kuwashirikisha Wajumbe mipango ambayo Tume hiyo inayo katika kupanga matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, mipango ya matumizi ya ardhi imeonekana kuwa ni suluhisho la migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali nchini hasa wakulima na wafugaji. Hata hivyo kasi ya upangaji matumizi ya ardhi ni ndogo kwani hadi kufikia Mwezi Disemba 2019 takriban vijiji 2,300 kati ya vijiji 12,319 vilivyopo nchini ndivyo vimepangiwa matumizi ya ardhi. Kasi hii ni ndogo kulinganisha na ongezeko la migogoro ya ardhi na mahitaji ya watumiaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya utekelezaji kazi ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati imeonekana kuwa Serikali imeweka mikakati mizuri ambayo kama ikitekelezwa ipasavyo na kwa wakati itachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Wizara na hususani kuipa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi fedha za kutosha ili iweze kuratibu kazi ya upangaji wa matumizi ya ardhi kote nchini na hatimaye kuwezesha Taifa kuondokana na matatizo ya migogoro ya ardhi inayoendelea kuongezeka kwa sababu maeneo mengi hayana mipango ya matumizi ya ardhi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 MAONI

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii, Kamati imebaini masuala mbalimbali na kuyatolea maoni na ushauri mahsus, ni matumaini ya Kamati hii kwamba, maoni na ushauri huo utazingatiwa kikamilifu na Wizara husika.

3.2 MAPENDEKEZO

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa baadhi ya masuala yaliyobainika yanahitaji kuwekewa msisitizo wa ziada katika kuwezesha utekelezaji wake, Kamati inawasilisha kwa Bunge lako Tukufu, ili Wabunge wapokee, kuyakubali na kuazimia katika maeneo yafuatayo:-

3.2.1 Utekelezaji wa Bajeti za Wizara na Miradi ya Maendeleo

Kwa kuwa, bado kumekuwepo na changamoto ya utekelezaji wa bajeti za Wizara, ambapo fedha inayotengwa haifiki kwa wakati;

Na kwa kuwa, ucheleweshaji huu mara nyingi hukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha;

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali iwe na mkakati endelevu wa kutenga fedha na kuidhinisha kwa wakati ili utekelezaji wa bajeti za Wizara uwe halisi kuwaletea Wananchi maendeleo.

3.2.2 Kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA)

Kwa kuwa, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ilianzishwa kwa amri ya kisheria (establishment order) ili kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu;

Na kwa kuwa, Mamlaka hii inasimamiwa na bodi ya ushauri badala ya bodi ya utendaji, na hivyo kukosa nguvu ya kisheria kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali, kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori utakayoipa nguvu ya kisheria kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

3.2.3 Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Nchini

Kwa kuwa, nchi yetu imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za misitu ambazo zimekuwa zikisimamiwa na mamlaka tofauti nchini;

Na kwa kuwa, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya udhibiti wa matumizi rasilimali za misitu ya Serikali peke yake;

Na kwa kuwa, bado kuna changamoto ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali hali ambayo pamoja na kuleta mgongano kwenye matumizi ya rasilimali hizo, kunachangia kuleta uharibifu na kutishia uendelevu wa misitu yetu;

Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge, kuitaka Serikali kwa mara nyingine tena, iharakishe mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini.

3.2.4 Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitumia Mfumo wa Matumizi Mseto ya Ardhi (Multiple Land Use System) katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa Sheria;

Na kwa kuwa, mfumo huo umeleta changamoto nyingi, ikiwemo ongezeko la watu na mifugo, na shughuli nyingine za binadamu katika Hifadhi, hali inayosababisha kuongezeka kwa gharama za kuwahudumia wananchi, pamoja na kuwepo wa uharibifu wa mazingira, hali inayotishia kupoteza hadhi ya Hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia;

Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge, kuitaka Serikali kuharakisha mchakato wa kufanya tathmini ya kina kuhusu mfumo wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo, ili kusaidia kuhuisha Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendana na hali halisi iliyopo sasa.

3.2.5 Kulijengea Uwezo Zaidi Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

Kwa kuwa, idadi ya Hifadhi za Taifa imeongezeka kutoka hifadhi 16 hadi 22; na kwa kuwa, hata kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya 6, ni hifadhi 5 kati ya 16 zilizokuwa zina uwezo wa kijiendesha zenyewe na kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesa Hifadhi za Taifa nyingine 11;

Na kwa kuwa, Shirika linalipa kodi zote stahiki ikiwa ni pamoja na gawio kwa Serikali, na ili kuliwezesha Shirika hili kuzilea na kuziendeleza Hifadhi za Taifa mpya 6 zilizoanzishwa;

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia, au kuliondolea baadhi ya tozo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ili kulipa nguvu ya kuweza kuzihudumia Hifadhi za Taifa zote.

3.2.6 Mustakabali wa Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa ya Morocco Square, Seven Eleven - Kawe, Golden Premier Residence - Kawe na Plot 300 Regent Estate Mikocheni ilipo Dar es Salaam

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa, miradi iliyotajwa japo juu imesimama, tangu ujenzi wake ulipoanza mwaka 2012 na 2013 kwa fedha za mkopo, na ilitarajiwa miradi hiyo ingekamilika mwaka 2015 na 2016;

Na kwa kuwa, kutokamilika kwa miradi hiyo kumeongeza gharama za ujenzi, ongezeko la riba, na Serikali kupata hasara kubwa ambao inasababisha kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha iliyowekezwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua stahiki na kwa wakati, kuiwezesha NHC kukamilisha miradi hiyo ili tija ya uwekezaji huo ionekane.

3.2.7 Mkakati Endelevu wa Upimaji, Upangaji na Umilikishaji wa Ardhi nchini

Kwa kuwa, programu ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi iliyokuwa inatekelezwa kwa majaribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga, kwa kutumia zaidi fedha za wafadhili imekamilika kwa mafaniko makubwa na ilitarajiwa isambazwe katika Wilaya nyingine za Mkoa wa Morogoro na Nchi kwa ujumla kwa kutumia bajeti ya ndani;

Na kwa kuwa, Serikali haijatenga fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya kuendeleza programu hiyo na hivyo kuwa chachu ya kuendelea kwa migogoro ya ardhi nchini;

Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kuendeleza programu hii na nyingine ambayo imeonyesha mafanikio makubwa katika kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 SHUKRANI

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2019 hadi Januari, 2020 yametokana na juhudhi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipoweka wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam, na kiushauri wakati wote.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William V. Lukuvi (Mb), na Naibu wake Mhe. Dkt. Angeline L. Mabula (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla (Mb) na Naibu wake Mhe. Constantine J. Kanyasu (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. Vilevile nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, akisaidiwa na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndg. Gerald Magili. Bila kumsahau Katibu wa Kamati hii, Ndg. Yona Kirumbi na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa uratibu wa shughuli za kila siku za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 HOJA

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Kemirembe J. Lwota, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,
MALIASILI NA UTALII
03 Februari, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante Mheshimiwa Kemilembe Lwota kwa kusoma vizuri Taarifa ya Kamati na kuiwasilisha sawasawa. (Makofii)

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na anakuja Mwenyekiti Mwenyewe, Mheshimiwa Mgimwa. Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu sana, endelea kuwasilisha hotuba yako.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Taarifa yangu iingie kwenye Hansard kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mungu kwa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Taarifa ya mwaka, kwa kipindi cha Januari 2019 hadi Januari 2020. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitaa kwao kwa kufanya kazi kwa weledi na ufanisi kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati za Kudumu za Bunge za kisekta ikiwemo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji zina wajibu wa kuwasilisha Taarifa za Mwaka za shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu, taarifa ninayoiwasilisha inazungumzia utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambayo ni kusimamia na kuishauri Serikali kuhusu shughuli zote zinazotekelizwa na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taarifa hii inahitimisha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa Bunge la Kumi na Moja, nawiwa kuelezea mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa lengo la kutunza kumbukumbu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mafanikio kutokana na shughuli zilizotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji:-

(i) Kamati imeongozwa na Wenyeviti wawili, ambapo kipindi cha awali, Kamati ilipoundwa iliongozwa na Mheshimiwa sana Mama yetu, Dkt. Nagu, Mbunge wa Hanang na kipindi cha awamu ya pili inayomalizika Juni, Kamati inaongozwa na mimi mwenyewe Mbunge wa Mufindi Kaskazini. Aidha, katika vipindi vyote viwili, Mama Daktari Christine Ishengoma amekuwa kiongozi kwa nafasi ya Makamu. Kwa dhati ya moyo wangu nawashukuru kina Mama hawa kwa malezi yao mema na uongozi uliotukuka. (Makofii)

(ii) Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imeongoza na kuchochera sekta za Kilimo, Mifugo, Uvubi na Maji kuwa sekta za kipaumbele ndani ya Bunge ambapo katika majadiliano ya Bunge hususan kwenye mijadala ya Mipango ya Maendeleo na mijadala ya Bajeti ya Serikali, michango zaidi ya Wabunge 70 huzungumzia maendeleo ya sekta hizi.

(iii) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji imewezesha kuanzishwa kwa Mfuko wa Maji ambapo, pesa nydingi za miradi ya maji pamoja na kutoka kwenye bajeti ya Serikali, wadau wa maendeleo, sehemu kubwa ya miradi ya maji inatekelezeka kutokana na fedha za Mfuko wa Maji.

(iv) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji imechochea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maji Safi na Mazingira (RUWASA) ambapo pamoja na mambo mengine majukumu na uwajibikaji wa watumishi wa sekta ya maji yamehamishiwa kutoka sekta ya TAMISEMI na sasa watumishi hawa watawajibika moja kwa moja kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya maji. Hatua hii itasaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa hudumza za maji safi na majitaka vijijini pamoja na uratibu, usimamizi na ufuatiliaji.

(v) Kamati imechochea kutungwa kwa Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019.

(vi) Kamati imechochea kuanzishwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa mbolea kwa Pamoja (Bulk Procurement) ambao umesaidia kuongeza upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei inayodhibitiwa na Serikali.

(vii) Kamati imechochea na kufanikisha kuhamishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji na kuhamia Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabiachi.

(viii) Kamati imesaidia kuchochera mchakato wa Sera na Sheria ya Kilimo ambayo itakuwa muarobani wa kuondoa changamoto na ukakasi uliopo kwenye sekta ya kilimo sekta ambayo imejiri Watanzania wengi.

(ix) Kamati imechochea kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi katika Wizara ya Mifugo ambapo changamoto zilizokuwa zinawakabili wavuvi na wafugaji kwa muda mrefu sasa zinatatuliwa kwa urahisi kupitia dawati hili.

(x) Kamati imefanikiwa kuchochera na kuondolewa kwa tozo ya mraba ya Dola 0.4 katika uvubi wa bahari kuu na kuwezesha kurudisha imani kwa wawekezaji kuendelea kufanya biashara ya uvubi katika bahari kuu hivyo kuongeza mapato kwa Serikali.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(xi) Kamati imefanikiwa kuchochaea kufufuliwa kwa Shirika la Uvuvi la TAFICO ambalo pamoja na mambo mengine litafanya kazi ya kuiwezesha nchi yetu kunufaika na mazao ya samaki katika uvuvi wa bahari kuu.

(xii) Kamati imechochea kuongezwa kwa mtaji kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 60 hadi kufikia shilingi bilioni 67 za sasa na kuwezesha utekelezaji miradi 150 ambapo wakulima zaidi ya milioni moja wamenafaika na Benki hii.

(xiii) Kamati imechochea kufanikishwa kwa Serikali kuondoa tozo na ada mbalimbali zaidi ya 105 kati ya 146 zilizowekwa kwa wakulima hivyo kuboresha na kuimarika kwa bei ya mkulima kwenye mazao yao.

(xiv) Kamati imechochea na kuwezesha Tume ya Ushirika Kusimamia uuzaji wa mazao kupitia Vyama vyta Ushirika na hivyo kurudisha imani kwa wanachama wa vyama hivyo.

(xv) Kamati imefanikiwa kuchochaea mapitio ya maboresho ya Sera, Sheria na Kanuni za uvuvi kwa lengo la kuboresha sekta ya uvuvi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, Kamati inamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kukubali na kuigawa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maji na kuwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwani kumeongeza tija kubwa sana katika utendaji wa Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakushukuru sana na kukupongeza wewe binafsi kwa ushauri na maelekezo na misaada mbalimbali ambayo imeweza kusaidia kufikiwa kwa mafanikio haya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Taarifa ya Kamati inahusu uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Uchambuzi umezingatia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ya Awamu ya Pili 2016 - 2021, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo Eendelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals - SDGs*); Programu ya Kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili (ASDP11) ya Mwaka 2016; Miongozo ya Mpango wa Bajeti; Maelekezo ya kisera ya Sekta za Kilimo na Maji pamoja na llani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015-2020.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo. Kulingana na Hati, mabadiili ya majukumu ya Wizara ya Kilimo yameelekezwa kwa kirefu kwenye taarifa ya Kamati iliyoko kwenye tablet zetu. Hivyo utekelezaji wa majukumu ulizingatia majukumu ya Wizara na kujikita katika kupima mafanikio ya Wizara kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa miundombini ya umwagiliaji. Miradi hii ipo katika hatua ya manunuzi baada ya kupata mkandarasi wa kutekeleza miradi hii. Hata hivyo, miradi hii haijaanza kutekelezwa kutokana na Wizara ya Fedha na Mipango kuchelewesha kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hii licha ya kupokea maombi ya fedha hizo kutoka Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imefanikiwa kutekeleza mradi wa kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga katika Mkoa wa Morogoro. Aidha, mradi wa kuendeleza skimu ya umwagiliaji wakulima wadogo wa Njage (Simanjiro), Mwalunili (Igunga), Kwemgiriti na Kituane Mwenzae (Lushoto), Soko (Moshi) na Katela Ntaba (Busokelo) umekamilika. Ujenzi wa skimu ya Nanganga, Kiongowele na Kinyope umefkia asilimia 95. Kamati

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inaipongeza Wizara kwa kufanikiwa na kutekeleza ujenzi wa skimu zote 10 kwa asilimia 78. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa maghala ya masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya chakula. Ujenzi wa miundombinu ya maghala ya kuhifadhi ulio chini ya Wakala wa Hifadhi ya chakula, ujenzi wa maghala, vihenge umeendelea kufikia asilimia 56. Hata hivyo, changamoto ya masoko bado ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo mseto/kilimo hifadhi. Kwa asili ya mfumo wa kilimo cha Tanzania umejikita kwenye kilimo mseto na kilimo hifadhi. Ni mfumo wa kilimo unaojumlisha kwa pamoja shughuli za upandaji wa mazao ya chakula, biashara, upandaji wa miti na ufugaji katika maeneo ya shamba.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uzalishaji kwa kukabiliana na ukosefu wa rutuba kwenye udongo pamoja na upungufu wa mbolea aridhini na kutokana na ongezeko la wadudu waharibifu na magonjwa kumepelekea kuongezeka kwa matumizi ya viuatilifu, viuadudu na kemikali. Hali hii imepelekea ongezeko kubwa la matumizi ya pembejeo za kemikali na kuthibitishwa kuwa shamba kwa kutumia pembejeo huongeza uzalishaji

Mheshimiwa Spika, pamoja na tija ya matumizi ya kemikali katika kuongeza uzalishaji matumizi ya kemikali yanaathiri sana mazingira ya afya na wadudu. Ili kuondokana na athari hizi Wanasyansi wa Kilimo wameongeza matumizi ya mfumo wa kilimo mseto na kilimo hifadhi. Kufuatia maelekezo haya bila kuathiri matumizi ya kemikali ni vyema Serikali ikasaidia kupunguza matumizi ya kemikali kwa kufanya utafiti kuhusu athari za kilimo cha madawa kwenye udongo na kwenye afya.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi majukumu ya Wizara yameainishwa kwa kirefu kwenye taarifa ya Kamati. Katika utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati imebaini kuwepo kwa mafanikio mbalimbali ambayo ni pamoja na:-

- (i) Kuongeza ukusanyaji wa maduhuli kiasi cha asilimia 50.
- (ii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo aina ya maziwa, nyama, pamoja na mayai.
- (iii) Kupunguza na kutatua migogoro baina na wakulima na wafugaji kwenye maeneo ya hifadhi.
- (iv) Kutolewa kwa hekta 12,658 kutoka kwenye mashamba ya Serikali na kuwapa wakulima na wafugaji katika vijiji 18.
- (v) Kuandaliwa kwa Kanuni ya ukamataji wa wanyama chini ya Sheria ya Ustawi wa Wanyama kwa lengo la kuzuia ukamataji holela wa nyama.
- (vi) Serikali imefanikiwa kurejesha machinjio ya kisasa ya Dodoma toka kampuni ya TMCL na kuwa chii ya usimamizi wa Serikali kwa kipindi cha mpito hadi suala litakapofanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara katika Sekta ya Mifugo. Changamoto kubwa iliyopo katika Sekta ya Mifugo ni fedha kidogo za ndani zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za maendeleo ya ndani zilizotengwa kwa mwaka fedha 2019/2020 shilingi bilioni 3 tu ambayo Kamati imebaini

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hazitoshii kutekeleza mipango ya maendeleo. Wizara kushindwa kutekeleza mipango ya maendeleo kikamilifu ni kiashiria kwamba mifugo itaendelea kuwa mifugo isiyokuwa bora hivyo kushindwa kushindana na soko la ndani na la Kimataifa, kuchangia malighafi kidogo kwa viwanda, kuchangia kupungua na kuondoa umaskini kwa mfugaji mmoja mmoja. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, tathimini iliyofanywa kwa ushirikiano wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi ya Kimataifa ya Mifugo (*International Livestock Research Institute- ILRI*) kwa kipindi cha miaka 15 (2016/17- 2031/32) imeonyesha Tanzania ni nchi ya pili Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi baada ya Ethiopia. Pamoja na idadi kubwa ya mifugo iliyopo nchini inazalisha kwa tija ndogo kutokana na sababu zifuatazo: Moja, magonjwa ya mifugo; pili, ukosefu wa malisho, vyakula, maji ya mifugo na tatu breeding.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016, Sekta ya Mifugo ilichangia asilimia 7.7 katika Pato la Taifa na sekta ilikua kwa asilimia 2.6. Aidha takribani kaya milioni 4.6 zinajihuisha na ufugaji ikiwa ni asilimia 50 ya kaya zote nchini. Takwimu hizi zinaonesha mifugo ni zao muhimu kwenye kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi. Kama wote tunavyofahamu kuwa Taznania imejaliwa kuwa na maeneo mengi ya maji ya bahari kuu na maji baridi ambapo kuna rasilimali nyingi za uvuvi. Ili kuendeleza rasilimali nyingi za uvuvi zilizopo nchini Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 inaitaka Wizara kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Spika ili kuendeleza rasilimali za uvuvi zilizopo nchini kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020 ulijielekeza katika kuhakikisha:-

- (i) Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu;
- (ii) Kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi;
- (iii) Kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi;
- (iv) Kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasilimali za uvuvi;
- (v) Kuongeza upatikanaji wa vifaranga vyta samaki; na
- (vi) Kuimarisha shughuli za utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango huo wa Maendeleo ilitarajiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ijielekeze katika kuharakisha Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa mazao ya uvuvi, kuhakikisha kuna Mkakati Maalum wa kuwezesha Ufugaji wa Samaki kwenye vizimba na Mkakati wa kutoa elimu kwa wavuvi ili waondokane na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa mazalia ya samaki katika maji ya asili na kuongezeka kwa mahitaji ya samaki duniani, ukuzaji wa viumbwe kwenye maji ndio njia pekee ya kuongeza upatikanaji wa vifaranga vyta samaki kwa kujenga na kuendesha vituo vyta ukuzaji wa viumbwe kwenye maji. Bado hakuna soko la uhakika wa kuuza mazao ya samaki kwa bei yenye tija.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji unahuisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo malengo yake makuu ni:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (i) Kuwa na huduma bora ya maji kwa watu wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025;
- (ii) Kuwa na huduma bora za maji vijiji kwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi ifikapo mwaka 2025; na
- (iii) Kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuvilinda, kuvitunza, kuviendoleza na kutafuta vyanzo vinya ya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha maendeleo ya Sekta ya Maji yanafikiwa, Wizara ya Maji imejivekeea malengo ya muda mfupi na kati ambayo yameainishwa kwa kirefu kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya tathimini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kuzingatia malengo iliojiwekea. Tathimini ya Kamati imegawanyika katika maeneo manne yafuatayo:-

- (i) Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Maji Nchini;
- (ii) Utekelezaji wa Miradi ya Maji;
- (iii) Mahitaji ya Wataalam katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi kwenye Sekta ya Maji; na
- (iv) Upotevu wa Maji.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Maoni ninayowasilisha yamegawanyika sehemu mbili, sehemu ya kwanza inahusu Sekta ya Kilimo ambayo inajumuisha Kilimo, Mifugo na Uvuuvi. Aidha, sehemu hii itazungumzia pia masuala ya Umwagiliaji na sehemu ya pili inahusu Sekta ya Maji kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo. Kwa Kuwa, kilimo ndio kila kitu kwa maendeleo ya nchi yetu kutohana na ukweli kwamba kinategemewa na asilimia 80 ya Watanzania, kinachangia asilimia 30 ya pato la Taifa, asilimia 95 ya chakula kinachotumika nchini, zaidi ya asilimia 30 ya mauzo nje na asilimia 70 ya malighafi ya viwanda. Na kwa kuwa, ni takriban miaka 60 sasa, Serikali inapanga, kutekeleza na kusimamia sera, mikakati, mipango na mbinu mbalimbali za kukwamua kilimo, hata hivyo mchango wa sekta ya kilimo kwenye uchumi bado ni mdogo kutohana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na bajeti ndogo isiyokidhi mahitaji ya kuendeleza kilimo, miundombinu duni, dhana duni za kilimo na ukosefu wa taarifa za kuaminika za utabiri wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liazimie kuwa kwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 na katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2026/2027), Sekta ya Kilimo iwe kipaumbele cha Serikali kwa kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kufungamanisha shughuli za kilimo na ukuaji wa uchumi hususan kwenye uchumi wa viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo. Kwa kuwa, Serikali imefanikiwa kutoa elimu, kupunguza migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kuhamasisha wafugaji kufuga kibiaresha. Na kwa kuwa, juhudhi hizi zimepelekeza kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo maziwa yameongezeka toka lita bilioni 1.6 mwaka 2009 hadi bilioni 2.06

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwaka 2015, uzalishaji wa nyama umeongezeka toka tani 452,230 mwaka 2009 hadi tani 597,757 mwaka 2015 na uzalishaji wa ngozi umeongezeka toka ngozi milioni 5.6 mwaka 2009 hadi ngozi milioni 6.45 mwaka 2014. Hivyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Serikali kuharakisha ujenzi wa viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kwani kwa kufanya hivyo itasaidia kuwaondoa wafugaji kwenye umaskini uliokithiri. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi. Kwa kuwa, Serikali imefanikiwa kudhibiti usafirishaji na uchakataji wa biashara ya samaki wachanga, kudhibiti zana za uvuvi haramu, kudhibiti zana za uvuvi haramu zilizokuwa madukani na kuwatambua wamiliki wa viwanda vilivyokuwa vinazalisha zana haramu za uvuvi pamoja na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na hivyo kupunguza uagizaji wa samaki nje ya nchi. Na kwa kuwa, juhudhi hizi zimesaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya uvuvi na upatikanaji wake kwenye soko la ndani na hivyo kupunguza uagizaji wa samaki kutoka nje ya nchi na kuokoa fedha za kigeni kiasi cha shilingi bilioni 27.72 pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli. Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba:-

- (i) Wizara ifanye juhudhi za makusudi za kuhakikisha wavuvi wanapata soko la uhakika la kuza mazao yatokanayo na uvuvi, kuongezeka kwa mazao ya uvuvi kuwezesha samaki wapatikane kwa bei nzuri ambayo wananchi wengi wanaimudu na kwamba ongezeko la makusanyo ya maduhuli lisitokane na faini zinazopatikana kutokana na makosa ya wavuvi ikiwa ni pamoja na kutaifishwa kwa zana za uvuvi;
- (ii) Makusanyo ya maduhuli yanayopatikana yasaidie kunufaisha wavuvi na sekta ya uvuvi kwa ujumla wake; na
- (iii) Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa Sera na Sheria ya Uvuvi ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili wavuvi na uvuvi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Umwagiliaji. Kwa kuwa, kwa muda mrefu kilimo nchini Tanzania kimekuwa kikitegemea mvua kwa kiwango kikubwa, hata hivyo mabadiliko ya tabianchi yamepelekea ukosefu wa mvua ya uhakika kumepelekea kilimo kisicho na tija. Na kwa kuwa, Serikali imeiona changamoto hii na kuhamisha Tume ya Umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji kwenda Wizara ya Kilimo kwa lengo la kufungamanisha shughuli za kilimo na Tume ya Umwagiliaji ili kuongeza tija kwenye kilimo. Hata hivyo, tangu Tume ya Umwagiliaji ihamie Wizara ya Kilimo hakuna utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyofanyika kwa kiwango cha kuridhisha kwa maelezo kwamba, Serikali inafanya tathimini ya hasara iliyopatikana wakati Tume ya Umwagiliaji ilipokuwa chini ya Wizara ya Maji. Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge, liitake Serikali ianze kutekeleza miradi ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa tija kwa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; Kwa kuwa, Serikali ina nia ya kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wa mijini kwa asilimia 95 na wananchi wa vijiji kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2020/2021. Ili kuharakisha upatikanaji wa huduma hii na kupunguza għarama za uendeshaji wa miradi ya maji, Serikali imeamua kutumia utaratibu wa Force Account ambapo Serikali imekuwa ikitumia kampuni zake kama Wakala wa Majengo, Jeshi la Kujenga Taifa na Shirika la Nyumba.

Na kwa kuwa, utaratibu wa kutumia Force Account kwenye miradi ya maji umeonyesha mafanikio makubwa kwa kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma na kuharakisha kukamilika kwa miradi ya maji iliyokuwa inatekelezwa kwa muda mrefu bila kukamilika.

Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge, liitake Serikali kutathimini upya uamuzi wake wa kutumia Force Account ili kutekeleza miradi mingi kwa għarama nafuu bila kusahau umuhimu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa kukuza uwezo wa kitaalam na kiutawala kwa kampuni za kizalendo ambazo hutoa ajira kwa vijana na kodi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, Hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa napenda kuishukuru Serikali na kutambua mchango mkubwa uliotolewa na Watendaji wa Wizara ya Kilimo wakiongozwa na Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mb), Manaibu Waziri Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Hussein Bashe; Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Luhaga Mpina na Naibu Waziri Mheshimiwa Abdallah Ulega; Waziri wa Maji Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa na Naibu Waziri Mheshimiwa Jumaa Aweso, utaalamu na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa napenda pia kuwashukuru wadau wote wa sekta za Kilimo na Maji amba kwa namna moja au nyingine walishirikiana na Kamati kwa nyakati mbalimbali Kamati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyooita wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyoorodheshwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Sekreterieti ya Kamati amba ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Asmin Kihemba na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na liadhime Serikali ikatekeleze maoni na mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofij)

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA KIPINDI CHA KUANZIA JANUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli zilizotekeliza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Maji kwa kipindi cha Mwaka mmoja kuanzia Januari 2019 hadi Januari 2020, ili iweze kujadiliwa na kutolewa maamuzi na Bunge lako.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge zimeainisha Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa ni Kusimamia na Kuishauri Serikali kuhusu shughuli zote zinazotekelawa na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji.

1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia mbinu zifuatazo: -

1.2.1 Kufanya vikao vya kupitia, kujadili na kuchambua taarifa mbalimbali kuhusu utendaji wa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji;

1.2.2 Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha thamani ya fedha (Value for Money) zilizotumika kugharamia miradi hiyo;

1.2.3 Kukutana na wadau mbalimbali na kupokea maoni yaliolenga kuboresha Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji; na

1.2.4 Kupata mafunzo na semina mbalimbali zilizoandaliwa na Wadau wa Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji.

1.3 Shughuli zilizotekelawa na Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia Januari 2019 hadi Januari 2020, Kamati imeweza kutekelza shughuli mbalimbali zifuatazo: -

1.3.1 Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

1.3.2 Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

1.3.3 Kushughulikia Taarifa za Utendeji za Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

1.3.4 Kufuatilia na kushauri kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

1.3.5 Kukagua Utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

1.3.6 Kuchambua Maazimio ya Bunge Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa FAO wa Kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari za Nchi Wanachama;

1.3.7 Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge; na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

1.3.8 Kupata mafunzo mbalimbali kuitia Mradi wa kuwajengea uwezo Wabunge na Watumishi wa Bunge Awamu ya Pili (Legistrative Support Project II) kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na wadau, Kamati nyingine za Bunge kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Taarifa ya Kamati inahusu uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Uchambuzi utakaobainishwa umezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (2016/17-2020/21); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo Eendelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals - SDGs); Programu ya Kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili (ASDP11) ya Mwaka 2016; Miongozo ya Mpango wa Bajeti; Maelekezo ya kisera ya Sekta za Kilimo na Maji pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015-2020.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taarifa hii inahitimisha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa Bunge la Kumi na Moja (11). Kamati inatoa maoni ya Jumla na ya msingi na hasa ikizingatiwa kuwa maoni mengi yameshatolewa kwenye Taarifa za Kamati zilizopita hivyo, Kamati imeona hakuna haja ya kurudia kutoa maoni yale yale kila siku kinachotakiwa tu ni kwa Serikali kufanya kazi ushauri unaotolewa na Kamati.

2.1 Wizara ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Wizara ya Kilimo yameainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri (Ministrial Instrument) ya Mwaka 2017 na mabadiliko ya Muundo wa Wizara ya Mwaka 2018 ambayo yalihusisha kurudishwa kwa shughuli za umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kuongezewa shughuli za masoko na usindikaji kwa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Hati hiyo na mabadiliko yake, majukumu ya Wizara ya Kilimo ni kama ifuatavyo: -

- i. Kuandaa na kutekeleza Sera za Kilimo. Usalama wa Chakula na Ushirika;
- ii. Kusimamia Matumizi Bora ya Ardhya ya Kilimo;
- iii. Kusimamia Usalama wa Chakula;
- iv. Kusimamia Uhifadhi wa Kimkakati wa Chakula;
- v. Kusimamia Maendeleo ya Ushirika na Vyama vya Ushirika;
- vi. Kuratibu Maendeleo ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo;
- vii. Kuendeleza Miundombinu ya Kilimo;
- viii. Kuratibu masoko na kuongeza Thamani ya Mazao ya Kilimo;
- ix. Kusimamia Maendeleo ya Zana za Kilimo na Pembejeo;
- x. Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji;

xi. Kusimamia Maendeleo ya Rasilimali Watu Wizarani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Kamati ulizingatia majukumu ya Wizara yaliyobainishwa hapo juu na kujielekeza kwenye Mpango wa maendeleo wa Wizara ambapo kipaumbele ni kuhakikisha kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara ili kuhakikisha usalama wa chakula kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la njaa, uhakika wa upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu, utendaji wa shughuli za Kamati ulijikita katika kupima mafanikio ya Wizara kwenye maeneo yafuatayo: -

2.1.1 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maendeleo ya Umwagiliaji ilipanga kukamilisha ujenzi wa miradi mitano (5) ambayo ni Mradi wa Nyamitita (Serengeti), Kirya (Mwanga), Rudewa (Kilosa), Endagaw (Hanang') na Bwawa la Kongogo (Bahi).

Mheshimiwa Spika, miradi hii ipo katika hatua ya manunuzi baada ya kupata wakandarasi wa kutekeleza miradi hii, hata hivyo miradi hii haijaanza kutekelezwa kutokana na Wizara ya Fedha na Mipango kuchelewesha kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hii licha ya kupokea maombi ya fedha hizi kutoka Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mbali na kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa miradi hiyo mitano, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imefanikiwa kutekeleza Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga katika mkoa wa Morogoro. Aidha, mradi wa kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima wadogo wa Njage(Simanjiro), Mwalunili (Ilunga), Kwemgiriti na Kituane Mwenzae(Lushoto), Soko (Moshi) na Katela Ntaba (Busokelo) umekamilika. Ujenzi wa Skimu za Nanganga, Kiongowe na Kinyope umefikia **asilimia 95** Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikiwa kutekeleza ujenzi wa skimu zote 10 kwa **asilimia 78**.

2.1.2 Ujenzi na ukarabati wa maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya maghala Kuhifadhi ulio chini ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula, ujenzi wa maghala na Vihenge unaendelea na umefikia **asilimia 56.1** ya ujenzi. Hata hivyo, changamoto ya masoko bado ni kubwa kwa bidhaa za mazao yatokanayo na ulezi, mtama, ufuta, mbaazi, alizeti na mihogo.

2.1.3 Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na kuzisambaza kwa wakulima

Mheshimiwa Spika, ili nchi ifikie malengo ya kukuza uzalishaji wenye tija katika kilimo ni lazima ijitegemee katika kuongeza uzalishaji wa mbegu. Usalama wa chakula na malighafi za viwanda vitawezekana tu endapo nchi yetu itakuwa na uwezo wa ndani wa kuzalisha mbegu mbalimbali. Kwa sasa Tanzania inaagiza mbegu kutoka nje kwa **asilimia 60** ambazo huuzwa kwa bei kubwa na nyngi ya mbegu hizo hulalamikiwa na wakulima kukosa ubora kwa kuwa hazikidhi matwaka ya hali ya udongo wa hapa nchini. Aidha, kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wakulima kuwa kuna upungufu mkubwa wa mbegu za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mbegu nchini bado si wa uhakika kutokana na ukweli kwamba uzalishaji wa mbegu hapa nchini hutegemea zaidi mvua, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ni maeneo machache tu ndio hupata mvua ya uhakika. Uzalishaji wa mbegu nchini

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

utaimarika endapo miundombinu ya umwagiliaji itaimarishwa na kuwezesha uzalishaji wa mbegu bora katika kipindi chote cha mwaka na hivyo kurahisisha upatikanaji wake tena kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine za kuongeza uzalishaji wa mbegu bora ni pamoja na kuimarisha huduma za maabara za mbegu nchini kwa kujenga, kukarabati na kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya maabara za Taasisi za Utafiti wa Kilimo (Tanzania Agriculture Research Institute - TARI) na Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agriculture Seesd Agency - ASA). Aidha, ni muhimu pia kwa Serikali kujenga na kukarabati sehemu za vyumba vya baridi vya kuhifadhi mbegu ambavyo sehemu kubwa ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Tasnia ya Mbegu inakabiliwa na changamoto nyingi, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa takwimu sahihi za mahitaji ya mbegu, maghala ya kuhifadhiwa mbegu ni chakavu na hayana ubora hivyo kufanya mbegu zinazogundiwa kuhifadhiwa kwenye mazingira ambayo si salama na kufanya mbegu kuwa na ubora zisizo na viwango stahiki na hivyo kutoa mazao hafifu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tasnia ya mbegu inakabiliwa na changamoto ya uchache wa wataalamu wa mbegu na katika uchache huo wengi wanaendelea kustaafu. Aidha, kuna changamoto pia ya uelewa mdogo wa wakulima kuhusu matumizi ya mbegu bora na umuhimu wake katika kuongeza mapato na bado wakulima wengi hawapati taarifa kuhusu matokeo ya mbegu chache zilizogundiwa na upatikanaji wake.

2.1.4 Masoko na mahitaji ya kilimo cha mazao ya mboga mboga na matunda (HOTCULTURE)

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mazao ya mbogamboga na matunda kwenye mwili wa binadamu kumekuwepo na ongezeko la mahitaji makubwa duniani ya mazao yatokanayo na sekta ndogo ya kilimo cha mboga mboga na matunda ambapo utafiti uliofanywa na (Ubalozi wa Uhulanzi, 2017) ulionyesha mazao yatokanayo na kilimo cha mboga mboga na matunda yalichangia pato la Taifa kwenye mapato yatokanayo na fedha za kigeni kwa **asilimia 38** mwaka 2015, ambazo zilipatikana kutokana na mauzo ya nje yenye thamani ya **dola 545 milioni** ikilinganishwa na **dola 64 milioni** zilizopatikana mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya mboga mboga na matunda inahusika na matunda hususan jamii ya maparachichi, mboga mboga za jamii ya maharage mabichi, maua ya aina mbalimbali na mazao ya viungo (species). Sekta hii hadi sasa imeajili wastani wa **asilimia 8** ya Watanzania ambao ni takriban watu **milioni 4.4** katika mnyororo mzima wa kuongeza thamani ya mazao hayo. Wengi wanaojishughulisha na kilimo hiki ni wakulima wadogo wadogo na hususani wanawake.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mboga mboga na matunda katika nchi za ulaya yanafikia tani kati ya **30-40 kwa wiki**, licha ya ardhii nzuri inayofaa kwa kilimo hiki, hali nzuri ya hewa na inayofaa kwa kilimo cha mboga mboga na matunda kwa eneo kubwa la Tanzania, bado nchi yetu haijaweza kukamata fursa hii ya mahitaji makubwa ya soko la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hali hii inatokana na watendaji wetu kufanya kazi kwa mazoea kuwa mazao makuu ya biashara kama Chai, Pamba, Tumbaku, Kahawa na Korosho ndio yenyewe uwezo wa kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida zinazoambatana na kilimo cha mboga mboga na matunda, sekta hii ndogo inakabiliwa na changamoto zifuatazo; -hakuna mkakati wa makusudi wa kuhakikisha ulimaji wa mazao haya unaongezeka ili kukamata soko la Ulaya, kodi na tozo

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyingi kutoka kwenye Mamlaka mbalimbali za udhibiti, kuna mwingiliano wa kodi na tozo zipatazo 45 kutoka Mamlaka na Taasisi mbalimbali za Serikali.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mazingira magumu ya kibashara yanayowakabili wafanyabashara wa sekta ndogo ya mbogamboga na matunda kutoka Mamlaka mbalimbali za Serikali

Business Environment: Multiplicity of taxes, levies and fees

FEES BY LEGULATORY BODIES (29)	LGA LEVEL & FEES (7)	TRA TAXES (9)
<ol style="list-style-type: none"> 1. Fire inspection/ certificate 2. Safety Inspection 3. Health Inspection (OSHA) 4. Water use fee 5. Certificate of confrimity 6. Plant Import Permit 7. Phytosanitary certificate 8. Radiation analysis 9. SUMATRAContainer Transportation Fee 10. Chemical importation permit 11. Immigration (CTA) 12. Holiday/ entry visa 13. Immigration work permit 14. Land rent 15. Fertilizer registration 16. Fertilizer testing 17. Pesticide testing 18. Pesticide registration 19. Pesticides registration permit 20. TMDA inspection fees 21. TMDA registration fees 22. Seed inspection 23. Variety registration 24. Cerificate of seed testing 25. Cerificate of seed import/ export 26. Pension Fund 27. On farm crop inspection 28. Plant quarantine inspection 29. NEMC 	<ol style="list-style-type: none"> 1. Produce cess 2. On Transit fees 3. Health Inspections 4. "Mazingira fees" 5. Parking fees 6. Service levy 7. Business license 	<ol style="list-style-type: none"> 1.VAT on packaging materials 2. Excesise duty 3. Vehicle Inspection fees. 4. Import levies (various) 5. PAYE 6. Fuel levy 7. RDL 8.Skills and Development Levy 9.Workers Compersation Fund

Kielelezo: www.taha

2.1.5 Kilimo Mseto/ Kilimo Hifadhi

Mheshimiwa Spika, kwa asili mfumo wa kilimo wa Tanzania umejikita kwenye Kilimo Mseto/ Hifadhi. Kilimo / hifadhi ni mfumo wa kilimo unaojumuisha kwa pamoja shughuli za upandaji wa mazao ya chakula/ biashara, upandaji miti na ufugaji katika eneo la shamba. Mfumo huu waweza kuandaliwa kwa zamu au hata kujumuishwa kwa pamoja bila kuzingatia msimu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kutohana na ongezeko la idadi ya watu wanaohamia mijini uzalishaji wa mazao ya kilimo umeendelea kupungua sehemu za vijiji ambako ndiko shughuli za kilimo ziliwa zikitekelezwa kwa kiwango cha juu. Aidha, mabadiliko ya tabia nchi yamechangia kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za kilimo kwa kuwa maeneo ya mashambani yalitegemea mvua, pamoja na kukosekana kwa rutuba kwenye ardhi kutohana na mashamba kulimwa kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uzalishaji kwa kukabiliana na ukosefu wa rutuba kwenye udogo pamoja na upungufu wa mbolea aridhini na kutohana na ongezeko la wadudu waharibifu na magonjwa kumepelekea kuongezeka kwa matumizi ya viuatilifu, viuadudu na kemikali. Hali hii imepelekea ongezeko kubwa la matumizi ya pembejeo za kemikali na kusibitishwa kuwa shamba hulimwa kwa kutumia pembejeo huongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tija ya matumizi ya Kemikali katika kuongeza uzalishaji matumizi ya kemikali yana athiri sana mazingira na afya za watu. Ili kuondokana na athari hizi wanasayansi wa kilimo wanahimiza matumizi ya mfumo wa kilimo mseto/ hifadhi kwa kuwa chafaa sana iwapo shamba ni dogo na hususan kwenye maeneo ambayo ardhi imelimwa kwa muda mrefu na kukosa rutuba.

Mheshimiwa Spika, faida za mfumo wa kilimo cha mseto/ hifadhi ni pamoja na kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuimarisha rutuba ya udongo, kutunza unyevunyevu wa udongo na hivyo kurutubisha ardhi, kusaidia kuongeza uzalishaji wa mazao kwa muda mfupi, kupunguza matumizi mengi ya pembejeo na hivyo kuwa na uzalishaji endelevu. Aidha, kilimo mseto/ hifadhi husaidia pia kuhifadhi wa mazingira yaliyoharibiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo hayo na bila kuathiri matumizi ya kemikali ni vyema Serikali ikasaidia kupunguza matumizi ya kemikali kwa kufanya utafiti kuhusu athari za kilimo cha madawa kwenye udongo na kwenye afya za binadamu huku ikiweka mikakati ya kuimarisha mfumo wa asili ambaa unahuisha mchanganyiko wa mazao kwenye shamba moja ambaa bado unatumiwa na wakulima wengi wadogo wadogo kujihakikishia usalama wa chakula na kipato.

2.2 Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini (Instrument) ya Wizara, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatakiwa kutekeleza majukumu ya msingi yafuatayo: -

- (i) Kuhakikisha Sera, Sheria na Mikakati ya Mifugo inatekelezwa;
- (ii) Kuongeza upatikanaji wa maji, malisho, vyakula vya mifugo na pembejeo nyingine;
- (iii) Kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya mifugo;
- (iv) Kuwezesha upatikanaji wa masoko endelevu ya mazao ya mifugo;
- (v) Kuwezesha uongezaji wa thamani wa mazao ya mifugo;
- (vi) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za mifugo na
- (vii) Kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mifugo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2.2.1 Sekta ya Mifugo

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati imebaini kuwepo kwa mafanikio mbalimbali yafuatayo: -

- (i) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli kiasi cha **asilimia 50** kutoka shilingi **14,154, 918, 456 mwaka 2015/2016**- Hadi tarehe 31 Desema, 2019 na kufikia kiasi cha shilingi **23,844,415,611**.
- (ii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo aina ya Maziwa, Nyama na Mayai kutoka mwaka 2015/16 hadi Mwaka 2018/ 19.
- (iii) Kupungua na kutatuliwa kwa migogoro baina ya Wakulima, maeneo ya hifadhi na Wafungaji na hivyo kuwezesha **vijiji 920 kurejeshewa maeneo ya hifadhi, misitu na maeneo tengefu**.
- (iv) Kutolewa kwa **Hekta 12,658** kutoka kwenye mashamba ya Serikali na kuwapa wakulima na wafugaji katika **vijiji 18 ili** kutatua migogoro katika mikoa ya **Pwani (He. 10,858) na Ruvuma (Ha. 1,800)**.
- (v) Kuandaliwa kwa kanuni ya ukamataji wa Wanyama chini ya Sheria ya Ustawi wa Wanyama kwa lengo la kuzuia ukamataji holela wa wanyama.
- (vi) Serikali imefanikiwa kurejesha machinjio ya Kisasa ya Dodoma toka Kampuni ya TMCL na kuwa chini ya usimamizi wa Wizara kwa kipindi cha mpito hadi itakapopata mwekezaji mpya. Kutokana na kampuni hiyo kushindwa kuuza nyama nje ya nchi na hivyo kuikosisha Serikali Mapato ya kigeni, ajira kwa wakazi wa Dodoma, na kushindwa kutoa gawio kwa Serikari kwa takriban miaka 11.
- (vii) Kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi hadi kufikia katika ngazi ya cheti ambayo itasaidia wahitimu kupunguza tatizo la Maafisa Ugani.
- (viii) Wafugaji 1,697 na maafisa ugani 17 wamepata mafunzo kuhusu ufgaji kibiashara katika Halmashauri 8.
- (ix) Mashamba darasa ya malisho bora yameongezeka kutoka 15 mwaka 2016/17 na 19 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na mashamba Darasa 57 mwaka 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 380** na **asilimia 300** katika Halmashauri 21.
- (x) Uzinduzi wa Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo nchini 2020 - 2025 umefanyika kwa lengo la kutoa muongozo wa utafiti wa mifugo unaendana na mabadiliko ya teknolojia na tabia nchi ili kukidhi mahitaji ya wadau na kutekeleza vipaumbele vya Wizara / Serikali.
- (xi) Kuanzishwa na kutekelezwa kwa Dawati la Sekta Binafsi.

2.2.2 Changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa Malengo na Majukumu ya Wizara kwa Sekta ya Mifugo

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayokabili sekta ya Mifugo ni fedha kidogo za ndani zinazotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za maendeleo za ndani zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 3 tu ambazo Kamati imebaini hazitoshi kutekeleza mipango ya maendeleo iliyokusudiwa na Wizara.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara kushindwa kutekeleza mipango ya maendeleo kikamilifu ni kiashiria kwamba mifugo yetu itaendelea kuwa mifugo isiyo na ubora na hivyo kushindwa: -

- i) Kushindana kwenye soko la ndani na la kimataifa na hivyo kutochangia ongezeko la mapato yatokanayo na mauzo ya nje na hivyo kutochangia kwenye ukuaji wa uchumi;
- ii) Kuchangia malighafi kidogo kwa viwanda na hivyo kushindwa kuchangia utekelezaji wa agenda kuu ya uchumi wa viwanda;
- iii) Kuchangia kupunguza au kuondoa umaskini kwa mfugaji mmoja mmoja na kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tathimini iliyofanywa kwa ushirikiano wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi ya Kimataifa ya Mifugo (International Livestock Research Institute- ILRI) kwa kipindi cha miaka 15 (2016/17- 2031/32) imeonyesha Tanzania ni nchi ya pili Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi baada ya Ethiopia. Takwimu zinaonyesha kuna **ng'ombe milioni 32.2, mbuzi milioni 20, kondoo milioni 5.5, kuku wa asili milioni 38.5, kuku wa kisasa milioni 40.6 na nguruwe milioni 2.**

Mheshimiwa Spika, pamoja na idadi kubwa ya mifugo iliyoko nchini, Sekta ya Mifugo bado inazalisha kwa tija ndogo kutokana na sababu kuu zifuatazo: -

- a) Magonjwa ya mifugo;
- b) Ukosefu wa Malisho, vyakula na maji ya mifugo; na
- c) Mbari (breed).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016 sekta ya mifugo ilichangia **asilimia 7.7** ya pato la Taifa, na sekta ilikuwa kwa **asilimia 2.6**. Aidha, kaya takribabi milioni 4.6 zinajihuisha na ufugaji, ikiwa ni **asilimia 50** ya kaya zote nchini. Takwimu hizi zinaonyesha mifugo ni zao muhimu kwenye kuondoa umasikini na endapo utafanyika uwekezaji wa ziada, sekta ya Mifugo itaongeza ajira, pato la Taifa na kuchangia kwenye malighafi ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, vilevile tathimini ya Sekta ya Mifugo inaonyesha ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na upungufu wa nyama hasa nyama nyekundu (ng'ombe, mbuzi na kondoo) kiasi cha **tani 1,731,000** sawa na upungufu wa **asilimia 33** ya mahitaji. Upungufu wa nyama nyekundu utachangiwa zaidi na changamoto za malisho/ maeneo ya ufugaji. Aidha, ongezeko la mahitaji litatokana na ongezeko la kipato, ongezeko la idadi ya watu pamoja na watu wengi zaidi kuhamia mijini.

Mheshimiwa Spika, tathimini hii imeonyesha kuwa endapo uwekezaji wa ziada utafanyika inakadiriwa nyama nyekundu itazalishwa kiasi cha **tani milioni 3.2** kati ya mwaka 2031/32, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 199** kutoka uwekezaji wa sasa. Uwekezaji wa ziada utaongeza pia upatikanaji wa ngozi na maziwa ambayo nayo yanaonyesha kutakuwa na upungufu wa **lita 5.4** milioni katika kipindi cha **miaka 15 ijayo**.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla matokeo ya tathimi iliyofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeonyesha zipo faida za moja kwa moja kwenye uwekezaji wa ziada kwenye Sekta ya Mifugo, hata hivyo Serikali bado haijaipa sekta ya Mifugo uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, licha ya tathimi iliyofanywa na Serikali yenewe bado hakuna uwekezaji wa ziada unaofanywa na Serikali kwani ipo changamoto kubwa ya utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mfano hadi Kamati inaanidika taarifa hii Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 zilizokuwa zimetolewa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni shilingi **154,000,000:00** tu kati ya shilingi **3,000,000,000:00** zilizoidhinishwa na Bunge na kupelekea shughuli za maendeleo kushindwa kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kutotolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kumepelekea Wizara kushindwa kuanza kutekeleza yafuatayo: -

- Kujenga uwezo wa watakwimu kukusanya na kuchambua takwimu za mifugo;
- Kufanya mapitio ya Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006 na mkakati wake ili kuboresha mazingira ya biashara;
- Kutotekeleza Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania;
- Kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba, kujenga na kukarabati baadhi ya minada;
- Kuwezesha operesheni za kudhibiti biashara ya haramu ya mifugo kwenye minada na masoko ili kuhakikisha mifugo inafikishwa machinjioni, kutambua, kugawa; na
- Kutaganza maeneo ya malisho kwenye baadhi ya mikoa na kuchimba mabwawa na kukarabati malambo katika mikoa 10.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya ziara ya kutembelea Machinjio ya Kisasa ya Dodoma (Tanzania Meat Company Limited). Kabla ya Mwaka 2008 machinjio haya yalikuwa yakimilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 hadi ilipouza **asilimia 51** ya haki zake za mali ya machinjio kwa mwekezaji binafsi anayejulikana kwa jina la NICOL ili kuleta tija katika kiwanda cha MTCL na hivyo kubakiwa na **asilimia 49** ya hisa zilizokuwa zikisimamiwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO).

Mheshimiwa Spika, kabla ya Serikali kuuza hisa zake, TMCL ilikuwa ikijiendesha kwa ufanisi hadi kupata zabuni ya kuuza nyama aina ya ng'ombe, mbuzi na Kondoo katika nchi za Uarabuni, Oman na Dubai. Hata hivyo, Kampuni ya NICOL imeshindwa kutekeleza masharti ya mkataba wa wanahisa ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mpango wa Uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuwekeza shilingi **bilioni 4.571** katika kipindi cha kuanzia 2008- 2011.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kampuni ya NICOL kushindwa kutekeleza mkataba wa makubaliano kulipelekea kiwanda cha nyama kutojengwa, kushindwa kufanya upanuzi na ukarabati wa miundombinu na mitambo. Kampuni ya NICOL imekuwa ikifanya biashara na mali za Kampuni bila ya kuwekeza na bila kutoa gawio kwa Serikali kwa kipindi chote cha miaka 11 tangu akabidhiwe kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, tangu kiwanda hicho kibinafsishwe Serikali imeendelea kupata hasara kwa kupoteza ajira, fedha za kigeni kutokana na kiwanda kufungiwa kuuza mazao ya mifugo katika nchi za Jumuiya ya Kiarabu (UAE).

Mheshimiwa Spika, kufuatia hasara iliyopatikana, mwezi Desemba, 2019 Selikali ilivunja Mkataba wa mauzo ya mali za machinjio ya Dodoma na sasa machinjio hayo yanamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Kamati inapongeza Serikali kwa uamuvi wa kurudisha machinjio ya Dodoma kwenye umiliki wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo Kamati inataka Serikali kufanya uchunguzi ili kubaini wabahirifu waliohusika kuihujumu Serikali. Aidha, Kamati inapendekeza uchunguzi huu ufanyike kwa awamu mbili yaani kipindi cha kwanza cha Bodi anzilishi (7 Novemba, 2008 – Mei

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2016) na kipindi cha pili (10 Mei, 2016- 29 Desemba, 2019.) Kamati inaamini hatua hii itadhihirisha kwa uwazi utendaji wa awamu zote mbili na uwajibikaji stahiki.

2.2.3 Sekta ya Uvuvi

Mheshimiwa Spika, kama wote tunavyofahamu kuwa Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo mengi ya maji ya bahari na maji baridi ambapo kuna rasilimali nyingi za uvuvi. Ili kuendeleza rasilimali nyingi ya uvuvi iliyopo nchini, Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 inaitaka Wizara kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, ilikuendeleza rasilimali za uvuvi zilizopo nchini kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 ulijielekeza katika kuhakikisha: -

- (i) Kusimamia na kuhamasisha Uwekezaji katika Uvuvi wa Bahari Kuu na Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Uvuvi;
- (ii) Kuimarisha Miundombinu na Kukuza Biashara ya Mazao ya Uvuvi;
- (iii) Kuboresha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi za Uvuvi;
- (iv) Kuimarisha na kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi;
- (v) Kuongeza Upatikanaji wa Vifaranga vya Samaki; na
- (vi) Kuimarisha Shughuli za Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango huo wa Maendeleo ilitarajiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ijielekeze katika kuharakisha Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa mazao ya uvuvi, kuhakikisha kuna Mkakati maalum wa kuwezesha Ufugaji wa Samaki kwenye vizimba na Mkakati wa kutoa elimu kwa wavuvi ili waondokane na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake imebaini kuwa Wizara ilipanga kukamilisha upembuzi yakinifu wa Bandari ya Uvuvi hata hivyo kazi hii bado haijakamilika kutokana na kutotolewa kwa fedha ya maendeleo kwa ajili ya kazi hii, bado kuna changamoto ya kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini wingi wa samaki kwenye ukanda wa bahari na maziwa kutokana na Serikali kutopeleka pesa za miradi ya maendeleo iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa mazalia ya samaki katika maji ya asili na kuongezeka kwa mahitaji ya samaki duniani ukuzaji wa viumbwe kwenye maji ndio njia pekee ya kuongeza upatikanaji wa vifaranga vya samaki kwa kujenga na kuendesha vituo vya ukuzaji wa viumbwe kwenye maji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2019/20 Wizara ilipanga kujenga kituo ukuzaji viumbwe kwenye maji eneo la kunduchi jijini Dar es salaam hata hivyo kazi hii ilipangwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ndani, hata hivyo kazi hii bado haijafanyika kutokana na Serikali kutopeleka pesa yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo na nyingine, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza uvuvi haramu, kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, kuongezeka na upatikanaji wa samaki na kufanikiwa kuondoa kwa muda tozo ya mrabaha wa kiasi cha dola ya 0.4 kwenye kila leseni za uvuvi wa bahari kuu na hivyo kuvutia wawekezaji kwa kuongeza mapato yatokanayo na leseni za uvuvi kwa meli za ndani na nje ambacho ndio chanzo cha kikuu cha mapato kwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo. Kamati imebaini kuwa pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa samaki, bado ongezeko hilo halijaleta nafuu kwa wanachi wa kawaida kutoka na ukweli kwamba bei ya samaki bado iko juu, na hakuna soko la uhakika wa kuuza mazao ya samaki kwa bei yenye tija.

2.3 Wizara ya Maji

Mheshimiwa Spika, Maji ni rasilimali muhimu kwa ajili ya uhai wa binadamu, wanyama, mimea, na mazingira. Aidha, maji ni injini ya shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi na nyenzo muhimu katika kutokomeza umaskini na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu huo, ni muhimu kwa Serikali kuendelea kuwekeza katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na maji ya kutosha ili kukidhi mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji umekuwa ukifanywa na Serikali na wadau mbalimbali kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002. Kimsingi uwekezaji unaofanywa na Serikali na wadau mbalimbali unalenga kuendeleza rasilimali za maji nchini na usambazaji wa maji ya kunywa na kwa matumizi mengine ya kibinadamu, kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji unahusisha program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo malengo yake makuu ni: -

- (i) Kuwa na huduma bora ya maji kwa watu wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025;
- (ii) Kuwa na huduma bora za maji vijiji kwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi ifikapo mwaka 2025; na
- (iii) Kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuvilinda, kuvitunza, kuvienda na kutafuta vyanzo vipyta vya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha maendeleo ya Sekta ya Maji yanafikiwa, Wizara ya Maji imeiwekea malengo ya muda mfupi na kati ambayo ni pamoja na: -

- a) Kuhakikisha kuwa makundi yote ya jamii yanapata huduma inayoridhisha ya majisafi na usafi wa mazingira kwa kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kufikia **asilimia 85** kwa wakazi wa vijiji na kufikia **asilimia 95** kwa maeneo ya majini ifikapo 2020/21;
- b) Kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zinatunzwa, zinasimamiwa na zinatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi na
- c) Kuboresha mazingira ya kazi na kuendeleza Watumishi wa sekta ya maji ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya tathimini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kuzingatia malengo iliyojiwekea. Tathimini ya Kamati imegawanyika katika maeneo manne yafuatayo: -

- Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Maji Nchini;
- Utekelezaji wa Miradi ya Maji;

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- Mahitaji ya Wataalam katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi kwenye Sekta ya Maji; na
- Upotevu wa Maji.

2.3.1 Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Maji Nchini

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya matokeo ya utafiti uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, yaliyotolewa mwezi Mei 2019 ambapo hadi kufikia Desemba 2018, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijiji ni mijini ni wastani wa **asilimia 64.8** na **asilimia 80**, sawia.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Serikali kujiridhisha na takwimu hizi kutokana na ukweli kwamba hali ya upatikanaji wa maji maeneo mengi ya vijiji bado si ya kuridhisha kama takwimu za Serikali zinavyosema.

2.3.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maji

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma za maji vijiji ni mijini hutekelezwa kupitia miradi ya maji ambayo kwa muda mrefu imekuwa haikamiliki kwa wakati na miradi mingine kushindwa kutekelezwa kutokana na ukweli kwamba mahitaji ya miradi ya maji ni makubwa kuliko fedha inayopatikana.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya Rasilimali Fedha kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira nchini, Serikali imeazimia na inatekeleza miradi ya maji kupitia Force Account. Utaratibu huu umewezesha kuokoa fedha nydingi kwenye miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu wa kutumia force Account Wizara ya Maji imeweza kuokoa kiasi cha shilingi **bilion 18,201,389,324.71** kati ya shilingi **bilion 56,373,089,584.68** zilizokuwa gharama za awali katika kutekeleza miradi kumi (10) katika mikoa ya Arusha (**AUWASA**), Iringa (**IRUWASA**), Kagera (**BUWASA**), Katavi (**MPANDA UWSA**), Manyara (**BAWASA**), Mara (**MUSOMA UWSA**), Mbeya (**MBEYA UWSA**), Morogoro (**MORUWASA**), Rukwa (**SUWASA**), Shinyanga (**KASHWASA**), na Tabora (**TUWASA**).

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza uamuhi huu wa Serikali wa kutumia Force Account ili kupata thamani ya pesa iliyotumika (Value for Money), hata hivyo, utafiti uliofanywa na Kamati umebaini kuwa utaratibu huu wa kutumia force Account umepelekea kudhoofisha kampuni nydingi za wakandarasi wadogo/ wazawa kwani kampuni za wakandarasi hawa ziliikuwa zinajijendesha kutokana na kupata kazi za Halmashauri mbalimbali na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, uamuhi wa Serikali kutumia utaratibu wa Force Account umepelekea zaidi ya **kampuni 1,700** kufutiwa usajili kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoweza kuendelea na biashara ya ukandarasi. Hatua hii imepekelea vijana wengi kukosa ajira na kuikoseshwa Serikali mapato yatokanayo na kodi mbalimbali zilizokuwa zikilipwa na kampuni hizi.

Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia wakandarasi Wazawa kukua, Kamati inaamini bado Serikali ingweza kufanya kazi ya ziada kwa kuhakikisha inaanda **BOQ** zenyenye uhalisia kuliko ilivyokuwa ikifanyika awali ambapo. Ni vyema sasa Serikali ikajipanga upya ili kuhakikisha miradi yote itakayoteklezwa inakuwa na uhalisia wa gharama za utekelezaji badala ya kuchukulia utaratibu wa falce Account kama suluhisho la kudhibiti wizi na upotevu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inatambua nia nzuri ya Serikali kupunguza gharama kwenye ujenzi wa miradi ya maji na kuharakisha upatikanaji wa huduma za maji ni muhimu kuzingatia

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuwa, kupungua kwa gharama kusipelekee kupungua kwa ubora wa vifaa vinavyotumika kwenye miradi inayojengwa.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia kwa Serikali kutambua kuwa miradi inayojengwa kwa utaratibu wa force account inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalam kwani wataalamu wanaotumika kwenye miradi hii, wanayo majukumu yao ya msingi na sio usimamizi wa miradi inayojengwa.

2.3.3 Mahitaji ya Wataalam katika Utekelezaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Miradi kwenye Sekta ya Maji;

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kufikia malengo iliyojiwekea inahitaji kuwa na wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kusanifu na usimamizi wa miradi iliyokusudiwa. Utafiti uliofanywa na Kamati umebackini kuwa miradi ya maji imekuwa haikamiliki kwa wakati na baadhi ya miradi imekuwa ikitekelezwa chini ya kiwango kutokana na upungufu wa wataalam.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji ina upungufu mkubwa wa wataalaam kwa ajili ya usimamizi wa miradi inayotekelezwa hivyo sehemu kubwa ya kazi kubaki chini ya Wataalam Washauri na Wakandarasi. Mahitaji halisi ya Watumishi wa Sekta ya Maji ni **10,287** ambapo Watumishi waliopo ni 6,377 hivyo kuwa na upungufu wa Watumishi wapatao **3,910** katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, udhaifu mkubwa pia umejionyesha kwenye miradi ya maji vijijini ambapo inapokamilika hukabidhiwa kwa wananchi kwa ajili ya kuiendesha kuitia Vyombo vya Watumiaji Maji (**CBWOSOs**) ambao hawana ujuzi na taaluma za maji; uwezo wa kusimamia makusanyo ya fedha kutoka kwenye huduma za maji; kugharamia uendeshaji wa miradi hiyo; na kufanya matengenezo pindi miradi inapokamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imefanya mabadiliko ya Muundo wa Wizara kwa kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vlijijini (**RUWASA**) ambao umepewa uwezo wa kuajili na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji vijijini nchini kote, hata hivyo bado **RUWASA** haijapata kibali kutoka Ofisi ya Raisi- Utumishi ili iweze kuajili na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji vijijini na kuweza kufikia lengo la upatikanaji maji kwa **asilimia 85%**.

2.3.4 Uchafuzi na Uharibifu wa Vyanzo vya Maji

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina vyanzo mbalimbali vya maji kama vile mito, maziwa, mabwawa, chemichemi, malambo, maeneo oevu na maji ya ardhii. Rasilimali za maji zilizopo hutegemea kiasi cha mvua kinachopatikana katika vipindi viwili vya masika na vuli. Utafiti uliofanywa na Wizara unaonyesha kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni toshelevu kwa kuwa ni wastani wa mita za **ujazo 2,300** ikilinganishwa na kiasi cha chini cha mahitaji kinachokubalika ni mita za **ujazo 1,700**.

Mheshimiwa Spika, ingawa kiwango hicho kiko juu ya wastani wa kimataifa na kwamba rasilimali za maji zilizopo kwa sasa zinakidhi mahitaji yaliyopo. Hata hivyo, kiasi cha maji kwa mtu kimeendelea kupungua kutoka wastani wa mita za **ujazo 7,862** mwaka 1962 wakati nchi ikiwa na idadi ya watu milioni 10,6 hadi kufikia wastani wa mita za **ujazo 2,300** mwaka 2018 nchi ikiwa na idadi ya watu wapatao **milioni 54**.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu wa Rasilimali za Maji umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana na mwenendo wa ongezeko la mahitaji linalotokana na ongezeko la watu, uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira, mabadiliko ya tabianchi na shughuli za binadamu. Hali hii isipodhibitiwa kwa kuchukua hatua madhubuti za kuzuia uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ili kuthibiti hali hii, Serikali inapaswa kuchukua hatua madhubuti za usimamizi, uendelezaji na kuhakikisha kunakuwepo na matumizi sahihi ya rasilimali za maji ili kuiepusha nchi kufikia kwenye hali ya uhaba wa maji. Kwa mfano, Kamati imebaini uendelezaji wa rasilimali ya maji chini ya ardhi unafanywa bila ya kuwa na uhakika mzuri wa wingi na ubora wa maji yaliyopo kutokana na upungufu wa takwimu mahsus za uratibu na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji ikiwemo kuwa na vifaa vya ufuatiliaji mwenendo wa hali ya maji nchini, utambuzi wa viashiria hatarishi vya usalama wa mabwawa, utambuzi wa maeneo yanayofaa kuwa vyanzo vya maji ya chini ya ardhi, maeneo ambayo yamo hatarini kuathirika dhidi Ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

2.3.5 Upotevu wa Maji

Mheshimiwa Spika, kiwango kikubwa cha upotevu wa maji ni mionganoni mwa changamoto zinazozikabili Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji mikuu ya mikoa na wilaya, miji midogo, miradi ya kitaifa pamoja na miradi ya maji vijijini. Pamoja na sababu nyingine, upotevu huo wa maji unasababishwa na miundombinu chakavu inayozidiwa nguvu na msukumo wa maji yanayotoka kwenye mitambo ya kuzalisha maji hivyo kupasuka na kusababisha upotevu mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, Hali hii inasababisha mara kwa mara wananchi kukosa huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama wakati wote na hivyo kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo na maduhuli na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za matengenezo na uendeshaji wa miradi kutokana na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hii, rai ya Kamati mara zote imekuwa ni kuitaka Serikali kufanya ukarabati wa mara kwa miundombinu chakavu ya mifumo ya maji na kuzitaka Mamlaka za Maji kuongeza kasi ya ufungaji wa mita za malipo kabla (prepaid meters) ili kuzuia malimbikizo ya madeni hivyo kuongeza mapato na kupunguza kiwango cha maji kinachotumiwa bila kulipiwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati. Maoni ninayowasilisha yamegawanyika sehemu mbili, sehemu ya kwanza inahusu Sekta ya Kilimo ambayo inajumuisha Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Aidha, sehemu hii itazungumzia pia masuala ya Umwagiliaji na sehemu ya pili inahusu Sekta ya Maji kwa ujumla wake.

3.1 Sekta ya Kilimo

3.1.1 Kilimo

Kwa Kuwa, kilimo ndio kila kitu kwa maendeleo ya nchi yetu kutokana na ukweli kwamba kinategemewa na asilimia 80 ya watanzania, kinachangia asilimia 30 ya pato la Taifa, asilimia 95 ya chakula kinachotumika nchini, zaidi ya asilimia 30 ya mauzo nje na asilimia 70 ya malighafi ya viwanda.

Na kwa kuwa, ni takriban miaka 60 sasa, Serikali inapanga, kutekeleza na kusimamia sera, mikakati, mipango na mbinu mbalimbali za kukwamua kilimo, hata hivyo mchango wa sekta ya kilimo kwenye uchumi bado ni mdogo kutokana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na bajeti ndogo isiyokidhi mahitaji ya kuendeleza kilimo, miundombinu duni, dhana duni za kilimo na ukosefu wa taarifa za kuaminika za utabiri wa hali ya hewa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liazimie kuwa kwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 na katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka 5 (2021/22- 2026/27), sekta ya Kilimo iwe kipaumbele cha Serikali kwa kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kufungamanisha shughuli za kilimo na ukuaji wa uchumi hususan kwenye uchumi wa viwanda.

3.1.2 Mifugo

Kwa kuwa, Selikali imefanikiwa kutoa elimu, kupunguza migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kuhamasisha wafugaji kufuga kibashara.

Na kwa kuwa, juhud hizi zimepelekeza kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo **maziwa** yameongezeka toka **lita bilioni 1.6** mwaka **2009** hadi **bilioni 2.06** mwaka **2015**, uzalishaji wa **nyama** umeongezeka toka **tani 452,230** mwaka **2009** hadi **tani 597,757** mwaka **2015** na uzalishaji wa ngozi umeongezeka toka **ngozi milioni 5.6** mwaka **2009** hadi ngozi **milioni 6.45** mwaka **2014**.

Hivyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Serikali kuharakisha ujenzi wa viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kwani kwa kufanya hivyo itasaidia kuwaondoa wafugaji kwenye umaskini uliokithiri.

3.1.3 Uvubi

Kwa kuwa, Serikali imefanikiwa kudhibiti usafirishaji na uchakataji wa biashara ya samaki wachanga, kudhibiti zana za uvubi haramu, kudhibiti zana za uvubi haramu zilizokuwa madukani na kuwatambua wamiliki wa viwanda vilivyokuwa vinazalisha zana haramu za uvubi pamoja na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvubi na hivyo kupunguza uagizaji wa samaki nje ya nchi.

Na kwa kuwa, juhud hizi zimesaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya uvubi na upatikanaji wake kwenye soko la ndani na hivyo kupunguza uagizaji wa samaki kutoka nje ya nchi na kuokoa fedha za kigeni kiasi cha shilingi **bilioni 27.72** pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli.

Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba: -

i)Wizara ifanye juhud za makusudi za kuhakikisha wavuvi wanapata soko la uhakika la kuuza mazao yatokanayo na uvubi, kuongezeka kwa mazao ya uvubi kuwezeshe samaki wapatikane kwa bei nzuri ambayo wananchi wengi wanaimedu na kwamba ongezeko la makusanyo ya maduhuli lisitokane na faini zinazopatikana kutokana na makosa ya wavuvi ikiwa ni pamoja na kutaifishwa kwa zana za uvubi;

ii) Makusanyo ya maduhuli yanayopatikana yasaidie kunufaisha wavuvi na sekta ya uvubi kwa ujumla wake; na

iii)Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa sera na sheria ya uvubi ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili wavuvi na uvubi kwa ujumla wake.

3.1.4 Tume ya Umwagiliaji

Kwa kuwa, kwa muda mrefu kilimo nchini Tanzania kimekuwa kikitegemea mvua kwa kiwango kikubwa, hata hivyo mabadiliko ya tabianchi yamepelekeza ukosefu wa mvua ya uhakika kumepelekeza kilimo kisicho na tija.

Na kwa kuwa, Serikali imeiona changamoto hii na kuhamisha Tume ya Umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji kwenda Wizara ya Kilimo kwa lengo la kufungamanisha shughuli za kilimo na Tume ya Umwagiliaji ili kuongeza tija kwenye kilimo. Hata hivyo, tangu Tume ya Umwagiliaji

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ihamie Wizara ya Kilimo hakuna utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyofanyika kwa kiwango cha kuridhisha kwa maelezo kwamba, Serikali inafanya tathimini ya hasara iliyopatikana wakati Tume ya Umwagiliaji ilipokuwa chini ya Wizara ya Maji.

Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge, liitake Serikali ianze kutekeleza miradi ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa tija kwa mazao ya kilimo.

3.2 Sekta ya Maji

Kwa kuwa, Serikali ina nia ya kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wa mijini kwa asilimia 95 na wananchi wa vijiji kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2020/2021. Ili kuharakisha upatikanaji wa huduma hii na kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji, Serikali imeamua kutumia utaratibu wa Force Account ambapo Serikali imekuwa ikitumia kampuni zake kama Wakala wa Majengo, Jeshi la Kujenga Taifa na Shirika la Nyumba.

Na kwa kuwa, utaratibu wa kutumia Force Account kwenye miradi ya maji umeonyesha mafanikio makubwa kwa kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma, na kuharakisha kukamilika kwa miradi ya maji iliyokuwa inatekelezwa kwa muda mrefu bila kukamilika.

Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge, liitake Serikali kutathimini upya uamuzi wake wa kutumia Force Account ili kutekeleza miradi mingi kwa gharama nafuu bila kusahau umuhimu wa kukuza uwezo wa kitaalam na kiutawala kwa kampuni za kizalendo ambazo hutoa ajira kwa vijana na kodi mbalimbali za Serikali.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu uliotukuka. Kupitia uongozi wenu na maelekezo ya mara kwa mara mnayoyatoa yamewezesha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa napenda kuishukuru Serikali na kutambua mchango mkubwa uliotolewa na Watendaji wa Wizara ya Kilimo wakiongozwa na Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Asunga (Mb), Manaibu Waziri Mhe. Ommary Mgumba (Mb) na Mhe. Hussein Bashe (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvubi Mhe. Luhaga Mpina (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Abdallah Ulega, (Mb), Waziri wa Maji Mhe. Prof. Makame Mbarawa, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Jumaa Aweso (Mb), utaalamu na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa napenda pia kuwashukuru wadau wote wa sekta za Kilimo na Maji ambao kwa namna moja au nyingine walishirikiana na Kamati kwa nyakati mbalimbali Kamati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyooitoa wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Mb Mwenyekiti

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- | | |
|--|--------------|
| 2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb | " |
| 5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb | " |
| 6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb | " |
| 7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | " |
| 8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, | " |
| 9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | " |
| 10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | " |
| 11. Mhe. Lucy Simon Magereli, | " |
| 12. Mhe. Justine Joseph Monko | " |
| 13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb | " |
| 14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | " |
| 15. Mhe. Pascal Yohana Haonga | " |
| 16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb | " |
| 17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb | " |
| 18. Mhe. Devotha Methew Ninja, Mb | " |
| 19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | " |
| 20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb | " |
| 21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb | " |
| 22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb | " |
| 23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb | " |
| 24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | " |
| 25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | " |
| 26. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb | " |

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Sekreterieti ya Kamati amba ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Asmin Kihemba na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Mwisho lakini si kwa umuhimu ninawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na liadhimiie Serikali ikatekeleze maoni na mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,
MIFUGO NA MAJI

03 FEBRUARI, 2020

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mwenyekiti kwa kuwasilisha hoja ya Kamati vizuri kabisa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sasa tunaendelea moja kwa moja na uchangiaji, tutawapata wachangiaji kama sita hivi. Tuanze na Mheshimiwa Jitu Soni atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya. Pia nipongeze taarifa za Kamati zote mbili; mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, nimpongeze Mwenyekiti wetu na Kamati nzima kwa kazi kubwa na nzuri na ushirikiano mzuri na mkubwa ambao unafanywa na Wizara ambao tunazisimamia. Pia nishukuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa taarifa nzuri na kazi kubwa ambayo wamefanya na mabadiliko yote tumeweza kuyaona. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika badhi ya maeneo. Nikianza na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii; naomba nitoe maoni machache ambayo yangeweza kuboresha shughuli, najua Kamati itaweza kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria mbalimbali ambazo tumepitia na tumeefanya semina mbalimbali pamoja na Kamati hiyo, sheria ambazo zinakinzana kwenye sekta nzima ya ardhi, maliasili na utalii; kuna sheria za maliasili, lakini pia kuna sheria za ardhi na sheria za mifugo. Ziko sheria tumezibainisha ambazo zinakinzana na hiyo ndiyo unaleta changmoto kubwa na ndiyo inasababisha migogoro mingi. Tukiweza kuwiweka vizuri sheria hizi na zisiwe zinakinzana naamini migogoro mingi itakuwa imepungua.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, napendekeza kwa upande wa National Housing, sehemu kubwa siku za nyuma walikuwa kazi zao nyangi wanazi-outsource. Ni vizuri kila jambo wangekuwa wanafanya *in house*, kwa mfano kutengeneza madirisha ya aluminum wangekuwa na kiwanda chao wenyewe, kama ni kufyatua blocks wafyatue wenyewe yaani shughuli nyangi ziwe *in house* badala ya kuwa outsource ambapo gharama inakuwa kubwa na faida ndogo. Kwa hiyo, wakifanya kazi nyangi bei za nyumba zitapungua sana na wataweza kuwauzia Watanzania nyumba ambazo zitakuwa na gharama nafuu. Kwa hiyo, hilo jambo ni muhimu kwa upande wa National Housing. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wa migogoro mbalimbali ya ardhi, tungeomba sasa Kamati itusaidie. Yale yote ambayo Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wetu kumaliza ule mgogoro basi yafanyiwe kazi sasa na vile vijiji vitangazwe rasmi ili ile hofu na wananchi kuishi bila kujua hatma yao haswa katika vijiji kwa mfano Jimbo la Babati kuna Vijiji vya Ayamango, Gedamar, Gedejabong na eneo lile ambalo lina tatizo kubwa la WMA basi ingewekwa wazi ili kila mmoja ajue ni nini kimetokea. Jambo hilo likifanyiwa kazi naamini kabisa kwamba migogoro mingi itaisha. Pia kwenye *Land Use Plan* basi tuweze kuangalia ushirikishwaji katika maeneo mengi ya sekta mbalimbali ili ziendane kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, napendekeza kamati itusaidie, matumizi ya ardhi yanabadilika kila siku na hasa leo tunaangalia Mji kama wa Dodoma, kuna mashamba yako ndani ya Mji huu wa Dodoma hasa ya zabibu na nchi nyangi duniani zinakuwa na mashamba ndani ya miji. Ni vizuri hii sheria ikawekwa la sivyo tutajikuta mashamba yetu ya zazibu ambayo ni eneo pekee Tanzania ambalo tunaweza kupanda zabibu ya uhakika na ambayo ina sifa kubwa duniani itatoweza. Kwa hiyo, jambo hilo pia lizingatiwe, *Land Use Plan* kwenye miji pia izingatie kulinda mashamba mbalimbali. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nikija pia kwenye utalii, naomba Serikali kwa kupitia Kamati ishauri, najua maoni hayo tuliwaletaa na mmeyafanya kazi, lakini kwenye hii bajeti tunayoolekea maeneo mengi, hasa katika maeneo ya hifadhi ambayo yanaingiza fedha za kutosha ambapo zinalisha hizi hifadhi nyingine hasa kwa mfano Tarangire, kuna barabara tatu zinazoingia zingetengenezwa. Tumeomba kwa muda mrefu sasa barabara ile ya Minjingu kuingia getini, ile ya Kibawa Tembo kwenda Sangaiwe na ile ya Babati Mji kwenda kule Mamire zote zingetengewa fedha ili kukuza utalii katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati iweze kusaidia kuangalia miradi mbalimbali ambayo inachangiwa na hizi hifadhi katika jamii isiwe miradi ambayo kwa mfano ya kujenga shule au ya kujenga zahanati na kadhalika lakini waangalie mahali ambapo wanaweza kuchangia miradi ambayo itanyanya uchumi wa watu ili watu wakishakuwa na uchumi mzuri wao wenyewe watajenga hizo zahanati na shule. Kwa hiyo, iwe ni miradi ambayo itanufaisha wananchi wanaokaa jirani na hizi hifadhi. Pia, nipongeze kwamba mahusiano sasa yamekuwa mazuri sana baina ya hifadhi nyingi na wananchi wanaozunguka na usimamizi umeendelea kuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, nikirudi sasa kwenye sekta ya kilimo, niipongeze Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanafanya, lakini pia Wizara ya Maji ambayo Kamati yetu inasimamia. Nishukuru kwamba wamekubali lile ombi letu la kufanya miradi mingi kwa kupitia Force Account. Tumeona Force Account imekuwa na mafanikio makubwa katika sekta ya elimu na sekta ya afya. Sasa hivyo hivyo tukitumia kwenye sekta hii ya maji, nina uhakika kwamba tutaona mafanikio makubwa zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ombi letu kwa kupitia Kamati ni Serikali wakati tunapokuja kwenye bajeti iweze kuondoa kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji, mitambo ya kuchimba mabwawa, ili badala ya Serikali kutegemea bajeti yetu ndogo basi sekta binafsi iweze kufanya kazi hiyo. Leo hii bidhaa nyingi ambazo zinatokana na sekta ya kilimo hazina VAT kwa hiyo, hawapati ule msamaha wa capital goods kwa sababu bidhaa zao hazina VAT. Wakiondoa hilo katika sekta ya kilimo watu wengi wataweza kuleta hii mitambo na kutengeneza mabwawa wenyewe na kuanzisha miradi ya umwagiliaji ambayo itakuwa ni kilimo cha uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini muhimu zaidi ni maoni ambayo pia Kamati imeiomba Serikali na nasisitiza kwamba ilete ile Sheria ya *Blue Print Regulatory Reforms* mapema kwa sababu bila hiyo sekta nzima hii ya kilimo itaendelea kuwa na changamoto. Tumeainisha kwenye ripoti yetu utaona ada, tozo, ushuru na kodi nyingi kwenye sekta moja tu ndogo ya *horticulture* hivyo hivyo iko katika karibu sekta nzima ya kilimo na mifugo, kuna utitiri wa kodi na tozo na ada mbalimbali ambazo zinafanya bidhaa zetu zinakuwa ghali kuliko bidhaa zinatoka nje. Tunaendelea kuishauri Serikali kwamba ni vizuri bidhaa ambazo tunaagiza kutoka nje kwa mfano matunda na mboga ambazo tuna uwezo wa kuzalisha nchini basi Serikali iweze kuwekeza zaidi. Sehemu kubwa tunachohitaji ni kuwa na mazingira rafiki, siyo lazima Serikali iwekeze fedha, wakiweka mazingira wezeshi basi sekta binafsi itaweza kuchukua fursa hiyo na kuifanyia kazi ili watu wengi zaidi waweze kunufaika na kuzalisha ndani ya nchi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwa upande wa mbegu tumeona asilimia 60 ya mbegu tunaagiza kutika nje ya nchi. Ni vizuri sasa Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama mbalimbali ambazo zinafanya uzalishaji wa mbegu hizo hapa nchini kuwa wa chini ili tuzalishewenyewe hapa nchini na fursa hiyo ipo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu ni kwamba sekta hii ya kilimo inakua kwa asilimia 4.5 ingawa ni sekta ambayo inaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania lakini kwenye bajeti haipewi umuhimu wake. Tunaomba tuangalie namna ya kuongeza bajeti

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

angalau ifikie asilimia 10. Ndiyo tunakubali kwamba Serikali inasema miradi yote ambayo inatekelezwa mjini iwe ya elimu, afya, maji, barabara, miundombinu, nishati, yote hiyo inachangia kwenye sekta ya kilimo lakini ukichukua *budget approved* na Bunge na *budget disbursed* kwa upande wa maendeleo huko vijiji bado haifiki asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri ile asilimia 10 ili iweze kufikiwa yote hiyo, tunakubali ni sekta ya kilimo na mifugo kwa mapana yake, ni vizuri *budget disbursed* ambayo tunapitisha hapa Bungeni, ile *approved* basi ilingane na asilimia 10 tutaona maendeleo huko kwenye sekta ya kilimo. Kwa sasa hivi bado haijafikia iko kwenye asilimia 8.2, ni vizuri tukahakikisha kwamba hiyo miradi yote tunayosema iko vijiji bajeti hizo ziende kwa sekta zote tutaweza kufanya vizuri zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa maji tungeomba Serikali iangalie namna ya kuboresha. Kuna mitambo ya kusafisha maji, water purifiers, wangeweza kuondoa kodi ili gharama za kupata maji safi na salama vijiji iwe ndogo. Pia solar water pumps zikiondolewa kodi watu wengi zaidi watapata maji safi na salama na bajeti kwa upande wa afya ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa magonjwa yanayotokana na maji itapungua na watu watakuwa na afya njema na Watanzania wengi wataendelea kupata maji. Serikali inafanya kazi kubwa na nzuri, lakini hizi reforms tunahitaji ziende kwa haraka zaidi kwa wakati mmoja ili tupone haraka. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja moja kwa moja. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Charles Mwijage, utafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Haonga na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa ajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima nikaweza kuwepo mbele ya Bunge lako. Nikushukuru wewe binafsi kwa mambo mawili; moja umefanya kazi yangu au ya Wabunge wengine iwe rafiki kwa kuleta hii Bunge Mtandao, yaani unasoma bila matatizo na mambo yana-flow yenywe. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia sekta za leo, hizi sekta mbili ndizo sekta mhimili za uchumi jumuishi. Yapo maswali, ziko hoja nydingi za kwamba uchumi unakua, watu wako vipi, ukitaka watu na uchumi ukue lazima uguse hizi sekta hizi, zinaitwa sekta za uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufikisha pongezi zangu mezani kwako, nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Luhaga Mpina. Watu wa Rutoro na vijiji vyake na watu wa Miseni wanamshukuru kwa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Tumekuwa na migogoro muda mrefu kati ya NARCO na wananchi lakini kwa kauli yake ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais migogoro ile ameimaliza. Nachoomba kwa Serikali Mheshimiwa Mpina sasa toa maelekezo wa watekelezaji wako ili washirikiane na Serikali ya Mkoa wa Kagera waweze kuonesha wananchi watakuwa wapi wakifanya shughuli zao na NARCO watakuwa wapi wakiendelea na shughuli za mifugo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nichangie mchango wangu katika taarifa hizi za Kamati. Niwapongeze Wenyeviti wote na Kamati zao zote mbili. Napenda nizungumze kidogo kuhusu suala la mifugo. Katika mchango wa Kamati, imeelezea vizuri sana Tanzania ni namba mbili kwa idadi ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumze kwa masikitiko kwamba tuna idadi ya mifugo, hawa ng'ombe tulionao huwezi kuwapeleka sokoni na Kamati imezungumza tatizo la masoko.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nyama yetu haiwezi kuuzwa kwa sababu tuna idadi ya ng'ombe kinachotakiwa katika soko la dunia ni nyama quality, kuna watu ambao wanajali afya zao. Kwa hiyo, niungane na Kamati kusema kwamba Serikali inapojenga uchumi jumuishi lazima iwekeze katika mifugo. Wizara hii lazima isaidiwe kama Kamati inavyosema, kusudi tuweze kutengeneza malisho na kuzalisha mifugo yenye tija.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo Tanzania ina fursa ya kuzalisha lita milioni nne za maziwa kwa siku lakini tunazalisha lita laki moja au laki moja na nusu. Tukizalisha lita milioni nne kwa siku maana yake tutaongeza afya ya Watanzania, tunaweza kufikia hatua hata ya kugawa maziwa bure kwa watoto wa shule. Taarifa nilizonazo ni kwamba huu ukanda wa Dodoma, Iringa na Mbeya mnawenza kuchakata zaidi ya lita milioni moja kwa siku, lakini ukanda wa Tanga kwenda mpaka Moshi kuna opportunity ya kuchakata lita milioni moja kwa siku, ukanda wa Kagera kwenda kwenye hizi hifadhi tunazogombania kuna uwezo wa kuchakata lita zaidi ya milioni moja. Ina maana lita milioni nne kwa siku wananchi wote watajumuishwa. Kwa hiyo, hakuna atakayelalamika kwamba uchumi wa vitu unapanda wa watu unadhoofu. Ni kwa sababu, watu moja kwa moja watakaokwenda kuuza maziwa wataweza kuhusishwa katika mchakato huo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Kamati ya Bajeti ambalo linahusiana na hapa, suala la mazao. Iko Tume ya Serikali wanasema ilichunguza bei ya ngozi kwamba ngozi zetu haziuzwi. Napenda nichangie katika Kamati hii na Kamati ya Bajeti, ngozi ni bidhaa ya kiglobali, *it is a global product*, huwezi kuichunguza hapa. Unapochunguza soko la ngozi lazima uangalie Pakistan anafanya nini kwenye sekta ya ngozi na wewe Tanzania unafanya nini? Huwezi kujaza kodi kwenye sekta ya ngozi Tanzania au kwenye industrial sector ya ngozi Tanzania wakati Pakistan anaiacha ngozi iende ishindane duniani ukaweza kushindana naye. Nilipaswa nilizungumze hilo tuweze kulielewa vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sekta ya uvuvi, mimi nusu ya Jimbo langu ni maji, ninavyo visiwa tunafanya shughuli ya uvuvi. Nikubaliane na Mheshimiwa Waziri na Serikali namna mlivyodhibiti uvuvi haramu, nakubaliananaloo, nawapa mapendekezo. Njia mnayotumia sasa haiwezi kuwa endelevu, ili kuleta udhibiti ulioendelevu nashauri muwashirikishe wananchi wa sehemu husika. Kabla wavuvi wengi hawajaja, hawa wanaofanya samaki wapotee, katika maeneo ya kwetu walikuwepo wavuvi, kwetu Bumbire, Goziba, Kelebe, Bakibwe wavuvi walikuwepo, sasa huwezi kuja na mapolisi kuzuia uvuvi haramu bila kumhusisha mzee wa mahalia. Huyu mzee wa mahalia pale lazima umuhusishe akuambie mwenye kokoro ni nani, aweze kutoa taarifa. Wewe katika mapato makubwa unayompa lazima urudishe kwa mtu wa pale ili aweze kuona shughuli zinazofanyika na yeye ana manufaa, nilitaka nilizungumze hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini tumezungumza katika Kamati ya Kilimo sikuona suala la soko. Tunalo tatizo la soko la mazao, ni kipaumbele na ni kikwazo kikubwa. Nipenda kuzungumzia mahindi na nafaka. Ili tuweze kutafuta soko la uhakika la mazao yetu, hasa nafaka, lazima Taifa lijikite kwenye kujenga storage capacity, hizi silos, ma-godown. Kenya yuko mtu mmoja anao uwezo wa kutunza tani laki saba. Sasa Serikali iige mfumo wa sekta ya mafuta ihamasishé sekta binafsi tuwe na uwezo mkubwa wa kuhifadhi.

Mheshimiwa Spika, jambo lililo wazi katika ukanda wetu wa Afrika haiwezi kupita miaka mitatu hatujapata shida ya chakula, Mungu atunusuru. Haya mafuriko na wale nzige tutapata shida ya chakula hata tufanyeje. Sasa kama tungkuwa na storage capacity kubwa ya kutunza tani milioni nne na Serikali katafuta mfumo mzuri wa ku-finance watu wanaleta mazao yanakuwa managed, halafu benki zinatoa mikopo. Ina maana mazao yangenunuliwa, mkulima kaondoka, halafu kile chakula kikabaki kwenye silos. Haiwezekani, lazima tutapata jirani yetu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwenye shida ya chakula na sisi kwa sababu tuna faida ya uoto tungeweza kuwa-supply hawa wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Kamati na Serikali kwamba tuwekeze kwenye silos. Kasi ya Serikali kuwekeza kwenye storage ni ndogo sana. Tuongeze kasi ya kuweza kuongeza storage capacity kusudi tutumie hizo finance modalities tuweze kuwa na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo mazingira ya biashara na nimshukuru Mheshimiwa Jitu umenikumbusha *Blue Print Regulatory Reform*. Nimesikitika tunapokwenda kwenye kuuza mbogamboga, tunapozungumzia avocado, kwenda kuuza avocado Ulaya ukiangalia tozo zinazotozwa inaonekana kama mkulima labda anapewa adhabu. Ni vilevile hata kwenye samaki, mmezungumza samaki hawana soko lakini linganisha tozo na kodi tunazotoza sisi upande wa Tanzania na wanazotoza wenzetu wa Kenya na Uganda, *landing fee* ya ndege Mwanza na *landing fee* ya Entebbe ni tofauti, lakini kontena la minofu ya samaki linapotoka kwenye kiwanda Mwanza linatozwa kiasi gani na wenzetu wa upande wa Uganda wanatoza kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa tunazungumzia bidhaa zetuna nizungumze hili, ili tuweze kujenga uchumi na shilingi iliyo imara lazima tu-export zaidi. Hatuwezi kulenga kujitosheleza hapa, tulianguka zamani kwa sababu tulilenga kujitosheleza, *we must invest in import substitution come export promotion*. Kwa hiyo, kujitosheleza-kujitosheleza hakutatusaidia, lazima uuze nje na lazima tuuze nje kwa mazao haya niliyoyasema kwamba ndio yanashikilia uchumi jumuishi. Uchumi jumuishi uko kwenye kilimo, mifugo na kwenye utalii kwa sababu wananchi wazawa wa Tanzania wataweza kuhusika moja kwa moja na kuweza kupata kipato. Kwa hiyo, uchumi wa vitu na wa wananchi utaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nawapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi mbili. Naipongeza Serikali, tuongeze nguvu, mwelekeo wetu ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage kwa mchango wako mzuri sana. Nimuite Mheshimiwa Paschal Haonga na Mchungaji ajiandae na atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Profesa.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nami nitachangia Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na nitaanza na utekelezaji wa kusuasua wa bajeti ya maendeleo ya Wizara ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa imekuwa ni kama mazoea Serikali kutekeleza bajeti ya kilimo kwa kusuasua. Hivi navyozungumza kwa taarifa ambazo ninazo kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji, kwa taarifa ambazo zilitolewa kwenye Kamati yetu ni kwamba kati ya pesa za maendeleo ambazo zilikuwa zimetengwa karibu shilingi bilioni 143.57 hadi sasa fedha ambazo zimeshapokelewa ni kidogo tu, ni kama shilingi bilioni 21.4 tu sawa na 14.9%. Kama tutaenda hivi tafsiri yake ni kwamba mpaka tunafika mwezi wa sita mwishoni kwa kweli sidhani kama tutafika asilimia 40. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hatuwezi leo kutekeleza bajeti ya maendeleo kwa kupeleka fedha tafsiri yake ni kwamba Wizara hii kuna shida na shida hii ni kubwa siyo ndogo. Kama shida hii ipo ni vizuri Serikali ituambie tatizo liko wapi? Kama Bunge tunaidhinisha fedha lakini fedha ambazo zinatolewa ni asilimia kidogo tu ambayo ni asilimia 14. Katika asilimia 14 hii fedha za

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ndani zilizotolewa ni kama shilingi bilioni 5 tu lakini fedha za nje ni bilioni 15. Yaani leo fedha za kutoka nje zinakuwa nyingi kuliko fedha za ndani. Hivi uzalendo uko wapi kati ya hao watu wan je wanaotupatia pesa nyingi na fedha zetu za ndani ambazo zinakuja kidogo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapa kuna tatizo hatuwezi tukaendelea kuendesha nchi kwa kutumia fedha za nje tu. Kama zitaendelea kutoqua fedha za nje, kwamba, kama zisingekuja Bilioni 15 maana yake tungekuwa na Bilioni 5 tu ambazo ni fedha za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka nijue, kwa sababu Serikali imekuwa ikijinasibu kwamba makusanyo yanazidi kuongezeka kila mwezi, lakini leo utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo, sekta ambayo inaa jiri Watanzania zaidi ya asilimia 70 utekelezaji wa Bajeti yake ndiyo namna kama hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni vizuri Wizara hii wajipime waone kama wanatosha, na kama hawatoshi siyo dhambi kuwapisha wale ambao wanadhani kwamba wanaweza wakafanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili jambo si la kwanza na huu mwaka si wa kwanza maana yake mwaka jana mwaka wa fedha ilikuwa hata asilimia 50 hawakufika. Mwaka uliotangulia, nyuma kidogo, ilikuwa asilimia 16, na miaka ya nyuma ilikuwa asilimia tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa tukienda kwa *trend* kama hii kwa sekta inayojiri Watanzania walio wengi tutakuwa hatuwatendei Watanzania haki. Ni vizuri tuangalie namna ya kuweza kufanya, na Serikali ione kwamba Watanzania hawatendewi haki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu pembejeo. Hivi ninavyozungumza hapa mbolea aina ya UREA kwa Mikoa inayozalisha chakula; wanaozalisha mahindi kwa wingi, Mikoa ya Songwe, Rukwa, Ruvuma, Iringa na maeneo mengine, mbolea aina ya UREA imeadimika; yaani mbolea kuipata ni shida kweli.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ituambie, kwamba kwa kutumia mfumo wa kununua mbolea kwa pamoja (*bulk procurement*) tutaweza kutatua tatizo hili la upatikanaji na bei? Leo mbolea aina ya UREA imeadimika, na kipindi hiki msimu huu, kwa maana ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ndio muda ambao wakulima wanatakiwa waweke mbolea ya kukuzia mahindi.

Mheshimiwa Spika, inawezekana msimu unaokuja kukawa na tatizo la chakula kwa sababu wananchi hawana mbolea ua kukuzia aina ya UREA. Hata hivyo hata hiyo kidogo ikipatikana bado bei elekezi haifuatwi. Kwa mfano kutoka shilingi 54,000 kwa mfuko wa UREA leo umefika shilingi elfu 68. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali hii ni Serikali ya wanyonge gani?, kama mbolea inapanda kutoka 54,000 kwenda 68,000 ni mnyonge yupi anayesaidiwa hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nadhani Wizara hii ya Kilimo kuna tatizo. Bila kujali Itikadi ya Vyama vyetu ni vizuri Wabunge wote tuangalie namna ya kuweza kuiwajibisha Serikali ya namna hii. (Makofi).

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la kulipa mawakala walio-supply pembejeo mwaka 2015. Mawakala walikopa pesa Benki wakapeleka vocha kwa maana ya ku-supply zile pembejeo kama mbolea pamoja na mbegu hawajalipwa pesa zao ninavyoongea hadi leo. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, wako Mawakala hawa waliokopa pesa Benki wameuziwa nyumba zao na wengine wamefariki kwa sababu ya pressure kwa sababu anauziwa nyumba hana mahali pa kukaa lakini hadi sasa Serikali imejificha kwa mwamvuli wa kwamba tuko kwenye uhakiki; hivi ni uhakiki gani ambao hauishi? Mbona Serikali haituambii? Hata kama wamehakikiwa watu wako watano iwalipe hao watano waliohakikiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, leo watu wanafariki kwa sababu ya pressure ya kuuziwa nyumba Serikali haijatuambia itawalipa lini watu hawa ambao wamehakikiwa, na ni watu wangapi?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atuambie wangapi wamehakikiwa hadi leo. Vilevile watuambie mpango wa kuwalipa; kwamba watawalipa lini? Kwa sababu wanaendelea kupotea hawa. Wanemosha wana watoto na wana ndugu wanaowategemea, leo hawajalipwa. Hawa ndio wanyonge ambao waliisaidia CCM hata kuipa kura. sasa hili jambo Mheshimiwa Waziri aangalie kama Serikali imeshindwa kuwalipa iwaambie kwamba tumewadhulumu, hatutawalipa; kwa sababu kama ni tangu 2015 hadi leo tafsiri yake ni kwamba Serikali haina dhamira njema ya kuweza kuwalipa Mawakala hawa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lambo lingine kuhusu suala Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kutoa gawio Serikali Kuu. Jambo la kustaajabisha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko hivi karibuni ilitoa gawio Serikali Kuu, takriban mlioni karibu milioni mia tano. Jambo la kusikitisha ni kwamba leo Wizara inazungumza hapa utekelezaji wa Bajeti wa kusuasua lakini Serikali Wizara ya Kilimo kuititia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko wanatoa gawio Serikali Kuu milioni mia tano.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui inakuwaje, yaani mgonjwa ambaye inatakiwa uongezewe damu inafika mahali nawe unataka kumtoa damu, hili ni jambo la ajabu sana. (Makofii)

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, yaani mgonjwa unatakiwa uongezewe damu na wewe unaamua ku toa damu kwa mwingine.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Haonga kuna taarifa unapewa subiri kidogo. Naomba umpe taarifa, ndiyo endelea.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa anayezungumza, kwamba kuna suala la mchanganyo wanaposema gawio watu wengi wana confuse. Nadhani Mheshimiwa Haonga hajaweza kutofautisha kati ya gawio na mchango.

Mheshimiwa Spika, tunaposema gawio ina mambo matano ndani yake. Kuna suala la dividend, kwa maana ya gawio. Kwa mashirika na Taasisi ambazo zinafanya biashara per se inaitwa dividend, ndiyo maana ya gawio. Kuna asilimia 15 ya pato ghafi ambayo ni mchango wa Taasisi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo naomba nimpe Mheshimiwa Haonga taarifa kwamba hiyo iliyotolewa si gawio ni mchango wa Taasisi kwa Mfuko Mkuu wa Serikali. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Haonga unapokea taarifa hiyo ya Mheshimia Chegeni?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, mimi naomba niendelee. Huyu bwana wananchi wake wakulima wa pamba kule wanadai Serikali takriban Bilioni 4.4, sasa nadhani angepata nafasi ya kuweza kuchangia angeweza kuzungumzia mambo ya pamba ili kule kidogo aweze kuwasaidia wakulima wa pamba. Naomba nimuache, nimempuuza tu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachozungumza hapa ni kwamba, leo kama Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko hizo fedha kama zilikuwepo nyangi kwa nini wasingepeleka kwenye angalau wangepeleka NFRA basi wakanunue hata mahindi; kwa sababu bado zinazunguka kwenye Wizara hiyo hiyo. Leo wanatoa pesa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko unapeleka Serikali Kuu halafu mwisho wa siku....

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

TAARIFA

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Haonga unapewa. Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante; naomba nimpe taarifa. Tufike wakati sasa humu tuangaliane kwamba tunafikiri kwa kiasi gani. Kama Wabunge humu ndani tunatunga sheria za mashirika kwenda kutoa dividend kwenye maeneo mbalimbali na mambo mengine ya kisheria. Tumetunga sheria humu ndani sisi wenyewe; kwamba kila wewe ukiwa Spika hapo ulipe hiki, ukiwa Shirika ulipe hiki. Sasa inakuwaje leo Mbunge aliyetunga sheria anasema hili ni la hovyo? Tunamuambia Mheshimiwa Haonga alete sheria humu Bungeni ya kuahirisha haya mambo aliyyasema yeye.

MBUNGE FULANI: hayo yakwake.

SPIKA: Mheshimiwa Haonga pokea taarifa hiyo.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, nadhani watu wengine kama hawa itabidi tuwasamehe tu kwa sababu hawafahamu vitu vingi. Atuambie ni sheria namba ngapi, lakini pia nadhani tu ni vizuri afuatilie mambo mengine. Nadhani ameamua kunipotezea muda tu, tumsamehe tu anapoteza muda wa walipa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapa ninachoshauri, ni vizuri Serikali iangalie, isiwe inakunywa uji wa mganjwa kwa sababu kufanya namna hii huku ni kunywa uji wa mganjwa; kwa sababu Wizara hii inachechemea, inatakiwa isaidiwe na si Wizara tena ianze kutoa gawio huku inafanya hivi. Sasa mambo kama haya ni mambo ambayo kwa kweli hii Wizara inatakiwa isaidiwe. Tunayazungumza haya si kwamba labda tunaichukia sana Wizara, tunapenda kuisaidia Wizara, lakini inaonekana kwamba Serikali haiko tayari, Wizara hii iweze kusaidiwa, Wizara ambayo inajiri Watanzania zaidi ya asilimia 70. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la Serikali kutoangalia vipaumbele vya wananchi; na hapa nazungumzia suala la maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipozunguka kwenye ziara mbalimbali nchini maeneo mengi wananchi wetu walizungumzia kuhusu maji. Alikuja Mbozi wananchi walizungumzia kuhusu maji, wanataka maji amekwenda Mombasa wanataka maji, amekwenda

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunduma wanataka maji, amekwenda Rukwa nai maeneo mbalimbali wananchi wanataka maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri, ni vizuri Serikali ikaangalia vipaumbele vya wananchi badala ya kwenda kwenye vipaumbele ambavyo si vya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo ukienda nchi nzima hakuna sehemu ambayo wananchi wamesema wanahitaji ndege, wanesema wanataka maji. Kwa hiyo mimi nashauri, kama Bunge lako hili Tukufu ambalo unaliongoza wewe; ninashauri kwamba ni vizuri Serikali...

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Haonga kuna taarifa sijui wapi! Kuna taarifa pale!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge. Pamoja na kazi kubwa ambayo inayofanywa na Mheshimiwa Rais lakini hata katika Jimbo lake kuna Miradi dhahiri shahiri ya maji inayotekelizwa katika kuhakikisha wananchi wa Mbozi wanapata maji. Hata hivyo kikubwa nataka nimwambie kwamba ukisoma maandiko ya dini yanasema yapaswa kushukuru kwa kila jambo ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Haonga utakataa na hilo nalo la kwamba maandiko yanasema kushukuru kwa kila jambo.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, mdogo wangu Aweso afahamu kwamba zile fedha si fedha za msaada, ni fedha za walipa kodi wa Tanzania na watu wa Mbozi pia wanalipa kodi; afahamu siyo msaada. Ndiyo maana hata maeneo mengine ambayo hakuna Madiwani bado pesa zinakwenda kwa sababu ni kodi za Watanzania; kwa hiyo afahamu hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia afahamu kwamba pamoja na kodi zetu kulipa vizuri aelewé kwamba kwenye Jimbo langu pamoja na Miradi ya maji ambayo ilitakiwa imalizike imechelewa kumalizika, kwa maana hiyo hizi kodi zetu hazitendewi haki vizuri, maana wakandarasi wame-raise certificates ili waweze kulipwa hawajalipwa, na Mradi wangu wa maji pale Itewe wa Bilioni 1.5 Wakandarasi wame-raise certificates hazijalipwa hadi sasa; Aweso anafahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata pia visima vinne ambavyo Mheshimiwa Waziri aliahidi alipokuja Mheshimiwa Rais pale Mloo bado hujakamilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapokuja hapa tunashauri ni vizuri Serikali ikaangalia vipaumbele vya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tuangalie; nina uhakika hata ukienda Jimboni kwako wewe kule wale wananchi wanahitaji maji zaidi kuliko ndege. (Makofi/Kicheko)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Haonga naona kengele ya pili imelia. Haonga anashika anapiga chini ya mkanda. (Kicheko/Makofi)

Mchungaji nimekuona ni nafasi yako sasa. (Kicheko)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu. Kwamba Wizara hizi ni Wizara nyeti kama alivyosema Mheshimiwa wa Bukoba; ni Wizara Mtambuka ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi leo sitakuwa na huruma kwa Mawaziri. Asilimia kubwa ya Mawaziri tulionao katika Serikali hii wanafanya kazi ambazo ni *ad hoc* au wanashughulika na kero wanaacha suala la msingi na majukumu ya Kiwaziri. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kiwaziri ni kushughulika na Sera, usimamizi na tathmini, lakini muda mwingi utawakuta Mawaziri hawa wako barabarani. Utamkuta Waziri huyu anachukua *ruler* anapima samaki; wanafanya kazi za *operational* ambazo inaonekana kwamba mifumo ya nchi hii imefeli. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Waziri anapoanza kufanya kazi za *operation* maana yake mifumo imefeli. Unamchukua Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naye anaenda mahali na camera kutatua mgogoro wa Kiwanja sijui cha Juma na Hadija, maana yake mifumo imefeli. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, unamkuta Waziri wa Kilimo naye anahangaika sijui nani ameuza nini wanaenda kwenye kazi za *operational* wameacha majukumu yao ya kazi na hii inamuwia Rais kazi ngumu sana, inafika mahali na yeye mpaka anaanza kusuluhisha na ndoa barabarani. (Makofii/Kicheko) **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendesha nchi kwa namna hiyo kwa sababu kazi zenu Mawaziri mmeacha kushughulika na masuala ya Sera; na mimi nataka nijikite zaidi Maliasili kwa sababu mimi ni Waziri Kivuli wa Maliasili, lakini mnashughulika zaidi na kutatua migogoro na mnapenda sana kutatua migogoro kwa sababu mnaunda Kamati, ikiisha Kamati mnaunda nyiningine, kwa sababu kuna hela huko; mmeacha majukumu yenu ya kutengeneza Sera. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kutoka kwenye maendeleo kama hamsimamii Sera zenu; kazi za migogoro kuna watu wanaofanya kazi hizo; na hatuwezi kuwaonea huruma lazima tuwaseme ndiyo kazi yenu mliyoitiwa hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Maliasili pamoja na kwamba ina vivutio vingi katika nchi yetu lakini bado haiko katika tano bora za kuwa *destination* ya watalii katika nchi hii; hilo ni tatizo kubwa kwa sababu tumeyaacha masuala ya msingi. (Makofii)

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, leo unamkuta Waziri anapiga kelele kwamba anataka kurogwa ameacha kuleta *ideas* za kutuhamisha kutoka hapa tulipo twende hapo mbele. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwenye mitandao kila wakati anasema wanataka kumroga badala ya kukaa chini.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Spika, taarifa

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, apate *ideas* namna gani ya kukuza watalii katika nchi hii. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mchungaji kuna taarifa unapewa.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Spika, nashukuru nilikuwa naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mfumo wa kiutawala nchini Mawaziri wetu ni Wabunge pia ni *Parliamentarians*; na kama ambavyo sisi Wabunge hatuna mipaka kwenye kufatilia kero za wananchi basi ni hivyo hivyo Waheshimiwa Mawaziri ambao pia ni *parliamentarians* kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawana mipaka kwenye ku-implement nafasi zao za Kibunge; ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa unapokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Mboni.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, kama Waziri ni Mbunge achague kimoja anaweza akakataa Uwaziri afanye kazi ya Kibunge. Sisi ni back benchers, hawa wanatakiwa watupe majibu na wafanye majukumu ambayo wamepewa kwa mujibu wa kazi; lakini wewe unapoteza kodi ya wananchi tena usinipotezee muda kwanza tufanye kazi ya wananchi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Maliasili ina majukumu mawili; kutunza Maliasili na kutangaza utalii. Kuna majukumu makubwa sana ya kutunza Maliasili, nalo ni jukumu kubwa sana. Wako watu wa TANAPA, Ngorongoro, kazi yao ni hiyo. Tunategemea Waziri asimamie sera. Narudia tena, operational si kazi yake, kama ni kutangaza wako watu wa TTB wanatangaza. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, leo kazi ya kuleta watalii hapa imebaki kuwa ya *travelling agents* si ya kwake tena, wao sasa wanaingia kwenye *operational* na wanaacha kazi zao; ndiyo maana kumekuwa na migongano mingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano takwimu zinaonyesha watalii wengi wanaokuja nchini kama nilivyosema wanaletwa na *travelling agents* lakini Waziri hasimamii zile sera ili kuhakikisha tu-boost huu utalii uje. Hawa wanaosema wameongezeka wengi wao ni wale ambao hata hao akina Esther na akina Heche wakipita pale Serengeti nao wanajumuishwa kwamba ni watalii, nao wanaongezwa kwenye idadi; halafu mnajaza idadi hapa kwamba watalii wameongezeka kwa sababu hatufanyi kazi ambayo tunatakiwa tufanye. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Waziri ambaye ni makini kama tunataka tukuze utalii katika nchi yetu...

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: ...Mheshimiwa Spika, China peke yake mwaka jana....

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

TAARIFA

SPIKA: Taarifa Mchungaji unapewa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kuna watalii wa ndani na kuna watalii wa nje. Sasa kama hawatambui watalii wa ndani labda ni tafsiri ya kule Iringa.

SPIKA: Taarifa unapewa Mchungaji.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nampuuza huyu, angekuwa Mbunge nampuuza, angekuwa Mbunge makini angejua utalii wa ndani unaingiza shilingi ngapi katika nchi hii. Sasa kwa sababu hujui pamoja na kwamba unatoka Serengeti tusipoteze muda. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano naishauri Wizara ya Maliasili, mwaka jana China peke yake watalii kutoka China kuja duniani kote kutembea sehemu nyingine walikuwa milioni 150, lakini waliokuja Tanzania walikuwa karibu 11,000 tu. Kwa Waziri makini, hayo ndiyo masuala ya kukaa na kujadiliana na ku-capturise katika watu milioni 150 hawa Wachina, Tanzania nifanye nini ili hawa watu milioni 150 wangapi watakuja Tanzania. Lakini badala yake unawachukua akina Steven Nyerere mnaenda Mlima Kilimanjaro sijui unamtangazia nani. Alisema Mheshimiwa Lema juzi hapa, unaenda nao kule unafanya kazi za operation, mnapiga picha sijui unamtangazia nani? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu China ilitegemewa kutoa watalii milioni 180 duniani kote, lakini huoni Wizara ikikaa kwamba hapa pana mtaji mkubwa tunataka Wachina waje, hakuna mkakati wowote. Bahati mbaya sasa hivi imekuja hili gonjwa labda watapungua, lakini hakuna mkakati wowote ambao kama Wizara inapanga, kwamba kwenye eneo hili hebu tu-capturise tunawaleta watalii wangapi, badala yake unaenda kutatua mgogoro wa Loliondo sijui na nani.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, taarifa.

T A A R I F A

SPIKA: Taarifa!

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, mwenzetu kwanza amejikita kwenye kulalamika haoneshi solution, lakini yeye ni mojawapo wa pioneer wanaopinga ununuzi wa career zetu kwa sababu ameonesha watalii wa China ni zaidi ya 50,000 lakini waliofika Tanzania ni wachache. Maana yake wenzetu ambao wana career zao ndio hao wanapeleka watalii wengi wanaishia kwenye nchi zao. Yeye anatakiwa sasa afike mahali ile pioneering yake ya kupinga Tanzania kuwa na ndege zake kwa ajili ya kuboresha utalii, aanze kuanzia leo kuunda na kutupa mawazo mengine yatakayotufanya tuende mbele. (Makofi)

SPIKA: Pokea taarifa hiyo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, Waziri makini angefanya projection kwamba Tanzania nataka nifanye iwe destination Africa watalii waje wengi wanatoka wapi? Waziri makini angefanya projection kama hivyo angweza ku-capitalize kutoka China kuna watalii wangapi. Sasa hivi wanaongoza kuja Tanzania ni watalii toka Marekani. Waziri makini asingehanganika na kina Steven Nyerere, Waziri makini angewachukua watu kama wakina Roger Federer, sijui kama unamjua wewe Roger Federer. Unawatangaza duniani kama wenzetu Rwanda wameandika visit Rwanda hapa unamchukua...

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, unamchukua wachezaji wazuri wa tennis au unamchuku huyu wa basket Reblon James unatangaza nchi yako...

SPIKA: Kuhusu utaratibu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ni marufuku Mbunge kujielekeza katika jambo ambalo halipo mezani na...

SPIKA: Tumsikilize tuge kanuni gani halafu uweze kuendelea. (Makofii)

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 28.

SPIKA: Hebu isome, naomba tusikilizane Waheshimiwa twende kwa utaratibu. (Makofii)

Naomba tusikilizane, Waheshimiwa tusikilizane kanuni 28 amesema.

WABUNGE WENGINE: Aaaah!

MBUNGE FULANI: Kwa kuheshimu muda asisome.

SPIKA: Naam!

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuokoa muda na sijafungua tablet naomba nisisome.

WABUNGE WENGINE: Aaaah!

SPIKA: Unaweza ukakaa tu Mheshimiwa, Mchungaji malizia dakika zako.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, kama tupo serious na kuongeza utalii lazima tuwe serious. Rwanda baada kusema inavyotangazwa mpira duniani kule ime-double watalii kuja kwenye nchi yao.

Kwa hiyo, unaita watu, unatangaza na watu wanajulikana kama vile akina Serena Williams. Unatangaza, unachukua watu wakina hawa wakina Steven Nyerere nani anawajuwa? Hata hapo Blataya ya Malawi hakuna anayewajua lakini Waziri ndio anaenda nao kuwatangaza nani anawajuwa? We are not serious, anapanda mlima hata hatua mbili hafiki unamtangazia nani? (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama tupo serious na biashara hii nimshauri Waziri tumieni pesa watafuteni watu ulikuwa haupo, watafute kama watu akina Roger Federer, akina Djokovic wanajulikana akipiga tennis pale wanaandika visit Tanzania dunia nzima inaona. Na usiogope kurogwa hamna atakaye kuroga tangaza nchi vizuri. (Makofii)

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa unaniacha hoji. Kuroga roga ndio kitu gani? Maana yake unaonge vitu ambavyo Spika havielewe. (Kicheko)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, vilikuwa kwenye mitando Mheshimiwa. Sera, sera ya utalii ilikuwa ni *low volume high yield* ambayo ni mwaka 1976. Lakini ukienda katika utendaji na jinsi Waziri anavyofanya sasa hivi ina-contradict. Sasa hivi wanataka *mass tourism*, lakini ukiangalia wanavyo *practice* hii ya *low volume* na *high yield* na hii ya *mass tourism* katika *implementation* yao kuna contradiction fukwe hamjaziandaa, hakuna vitanda ukingalia maeneo mengine...

SPIKA: Hiyo kengere ya pili Mchungaji.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, wamenikatisha katisha Mheshimiwa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Kengele ya pili. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nimekuona umesimama. (Makofii)

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea. Wakati Mheshimiwa Mchungaji Msigwa anajadili hoja hii alikwenda katika kugusa mipaka na madaraka ya Rais katika kutenda kazi zake kwa kujaribu kufananisha mifano aliyokuwa nayo ndani ya Bunge kama vile ndivyo kazi ambazo anazifanya ndai ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kazi za Mheshimiwa Rais zinaenda na sehemu ya kwanza, sura ya pili ya ibara ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini vilevile kanuni zetu ukienda kuzisoma viko vifungu ambavyo vimeendelea kuzingatia kuwa na heshima na kulinda kazi na shughuli zote ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akizifanya ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima yako naomba mwongozo yale yalisosemwa na Mheshimiwa Msigwa leo hapa ndani ambayo yanataka kuharalisha kazi hizo za Rais kama hizo ndizo. Kwa heshima ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu hasard imerokodi yaliyosema kwangu mimi sitakuwa na busara kama nitayarejea kama vile alivyokuwa ameyasema lakini Hansard imeyanukuru yale maneno ambayo ameyasema akielezea kazi za Mheshimiwa Rais nchini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kama jambo hili linaweza uendelea au kuna hatua yoyote ya kuyaondoa maneno kwenye Hansard ya leo.

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nilitoa mfano wa Mheshimiwa Rais ila sikuwa na maana ya kumdhalilisha Rais. Ila nilizungumza kwa namna ambavyo Mawaziri hawafanyi kazi zao ina mlazimu mpaka na Rais kwa sababu kuna wakati Rais alipita mahali kuna watu walikuwa wanalamikia masuala ya ndoa kwa hiyo Rais akifika mahali akawa anasuluuhisha. Kwa hiyo, wasimuhusishe Rais kati ya hili watimize majukumu yao Mawaziri. Sikuwa na nia yakumdhalilisha Rais. (Makofii)

SPIKA: Kwa kuwa hukuwa na nia basi nakushauri u-withdraw hiyo part.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe hiyo sehemu ya Rais.

SPIKA: Nakushukuru sana, ahsante sana. Prof. Jumanne Kishimba sasa awe muongeaji wetu wa mwisho mchana wa leo.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naungana na Wabunge wenzangu kuchangia Wizara hizi mbili za Kilimo, Uvuvi na Maliasili.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, Mawaziri na Watumishi wote wa Wizara zote hizi. Naipongeza Wizara Kilimo hasa kwa suala kuondoa bei na *indication price* kwenye mazao yote itatusidia sana hasa kwenye mazao yetu ya pamba ambayo yalikuwa yana tusumbua sana wakati wa kutao bei na mara bei zinapoanguka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala hili la soko la mazao limeendelea kuwa tatizo kubwa sana. Kwa hiyo tunaomba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara zijaribu namna yoyote kuendelea kuwabana wenye viwanda hasa vya pombe na viwanda vingine waweze kutumia mali za Tanzania kwenye pombe au bidhaa ambazo sio za nje.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni kwamba kuna bia kama za balimi, kuna bia kama za eagle ambazo watumiaji ni watanzania ambazo watumiaji ni *local*. Vizuri wenye viwanda na Wizara Kilimo na Wizara ya Biashara ijaribu kuwabana ili kuwasidia wakulima wetu kupata bei za mazao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilikuja na suala la bangi, bahati nzuri nchi zingine mbili ukiondoa Uganda, Zambia na Malawi wameruhusu. Na vizuri mwaka 2015 Bunge lako hili lilipitisha nitaisoma sheria hiyo. Kifungu cha 12 cha *Drug control and enforcement act*. Cha 2015 kinaipa DCEA mamlaka ya kuruhusu ulimaji, usafirishaji wa bangi, mirungi, micocoa OPM kwa ajili yamatumizi ya tiba.

Mheshimiwa Spika, bei ya bangi duniani imepanda mara dufu na nchi zote zinazozunguka zimekwisha ruhusu. Wakati wa majumuisho tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo... (Makofi)

SPIKA: Hii ni hoja muhimu sana naomba tuisikilize. (Makofi)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Kilimo kwa kuwa sheria hii ipo, aje atupe ufanuzi kwamba watu wanaotaka kulima wamuone nani na imetungwa na Bunge hili mwaka 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, waliopiga marufuku bangi ni wazungu miaka ya 40. Lakini wazungu wale wale wamegundua ndani ya bangi kuna dawa. Na sisi wenye tunenda kwenye viwanda vya dawa. Je sisi tuki-import dawa yenye material ya bangi tutakuwa tuna-import toka wapi? Na tunatai-declare na namna gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Kairuki taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, naiona hoja ya Mheshimiwa Kishimba, lakini nipende kusema kwamba tayari hata sisi wizarani tumeshapata wawekezaji kama wawili wambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika kilimo lakini pia kuchakata mafuta bangi kwa ajili ya matibabu. Tunaendelea kulifanya kazi kama Serikali kwa sababu hakuna bado miongozo kifungu cha 12 kimeeleza kama itakubalika au laa! Ni hatua zippi na utaratibu gani uweze kufuata.

Kwa hiyo, nimuuombe Mheshimiwa Mbunge atuachie kama serikali na mamlaka zinazohusika tuendelee kulichaka na pindi litalopokuwa tayari basi majibu yatatolewa. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Kishimba taarifa hiyo.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, taarifa yake naiunga mkono, labda chakuomba kwa kuwa bei ya masoko ni bei ya ushindani ni vizuri Serikali ifanye uamuvi huo mapema zaidi.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma taarifa.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilikuwa napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kikawa idha Bunge linapotunga sheria kinachofuata ni kanuni. Nilikuwa nafikiria Mheshimiwa Waziri angetuambia kanuni zipo tayari ili tuanze kulima maana bangi itaporomoka bei.

SPIKA: Mheshimiwa Kishimba endelea.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, sisi Tanzania kwa record kwa Afrika ni nchi tatu kwa kulima bangi ya magendo. Sasa kama wataruhusu na sheria kama ilivyo inaweza ikatusaidia sana kuongeza mapato na kuondoa magendo. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani yupo hapa kama anaweza kutoa msamaha hata kwa bangi iliyopo kwa miezi 6 kama msamaha anavyotoa wa silaha wananchi wakawasilisha bangi hizo polisi watu wakauziana polisi na TRA wakapata fedha na wanunuzi wakaja kununua hapa. Inaweza ikasaidia watu wetu wakapata pesa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wakati dunia inapobadilika lazima twende haraka sana, Uganda wamepewa hii AU zaidi ya dola ya milioni mia tano kwa ajili ya kilimo cha bangi wanatoa udongo toka Malaysia. Lakini sisi bahati nzuri wakulima wetu wana utalaamu wa kulima bangi muda mrefu. Kwa hiyo, kama serikali itapitisha na hiyo sheria kwa kuwa ipo, basi tumuombe Mheshimiwa Waziri wakati wote kama atapitisha iwe mapema kabla bei haijaporomoka. Ahsante sana nashukuru sana.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge bado dakika za Mheshimiwa Kishima zipo pale. Lakini niwahakikishie *this is not a joke anachochangia*. Nilikuwa Canada majuzi hapa kwenye Mkutano wa Maspika wa Commonwealth duniani, ni *big business in Canada, big, big business*. (Makofi)

Kwa hiyo, anazungumza kitu cha msingi sana wala sio utani. Eeeh tena linaweza likawa zao moja kubwa kabisa la biashara linaloweza kuongoza kuliko mazao mengi tu, kabisa likafanya mapinduzi makubwa sana ya kipato. Kwa hiyo, anachokizungumza Mheshimiwa Kishimba hazungumzi bangi itumike vile ambavyo tunafahamu hapa nchini. Tunazungumzia habari ya kilimo moderated, monitored na utaratibu wote halafu wanapelekewa wanaohitaji kwa ajili ya kutengeneza madawa ya wanyama na binadamu. Malizia Mheshimiwa Kishimba dakika zako.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa hiyo tulikuwa tunaomba sana Wizara ya Kilimo wajaribu kulifikilia kama ulivyosema kwamba hii bangi sasa ni tiba. Kama ni tiba na sisi tunaagiza material kutoka nje na dawa kutoka nje ambazo zina bangi.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ni vizuri sasa kutumia bangi yetu na huenda tukawa wazalishaji wazuri zaidi maana yake watu tayari wanao uzalishaji wa bangi. Na inaweza ikasaidia Wizara ya Afya kupunguza na kupunguza ghamama za pesa tunazoagiza toka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji amelisema vizuri kwamba na yeze lipo mezani, tunaomba wenzetu wa Zambia na Malawi wananchi wamelalamika kwamba baada ya kuwa imeruhusiwa, wameruhusu matajiri peke yake.

Tunaomba kama wataruhusu basi na wakulima wetu wadogo wadogo wapewe nafasi hizo ili na wao waweze kujipatia chance kwenye muda huu ambao zao hili litakuwa kwenye soko. Badala ya kuyapa makampuni makabwa peke yake ya nje ni vizuri na wakulima wadogo na watu wadogo wadogo wakaruhusiwa ili wote ku-enjoy bahati ambayo itatokea duniani. Ahsante sana. (Makofii)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Heche sawa nakusikiliza kama dakika mbili.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushuruku nimesimama kwa Kanuni 68(7) kuomba mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea. Wakati Mheshimiwa Kishimba anazungumza na baadaye Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji akasimama. Kule Tarime, Kata Kibasuka pamoja na vijiji vyake, watu wengi sana wamekamatwa na wengine wanapewa kesi hata za kusingiziwa bangi. Hata hivi tunavyozungumza ukienda utakuta polisi wana-patrol. Na kumbe sheria ipo na inaruhusu kilimo hiki, sasa ningeomba mwongozo wako kwa sababu kuna sheria pia ilitungwa hapa mwaka jana ambayo imeleta tatizo kubwa sana kwenye suala hili la bangi. Ili tuone ni jinsi gani sheria hizi zinakuwa synchronize na watu wetu wasionewe kwa sababu maelfu ya watu wapo ndani kwa sababu ya bangi naomba mwongozo wako kuhusu jambo hili na wengine wanapewa uhujumu uchumi kwa sababu ya masuala ya bangi haya. Na sisi bahati nzuri tunaunza Kenya pale soko ni zuri tu. (Makofii)

SPIKA: Kwamba kuna sheria inaruhusu kilimo cha bangi ndio mwongozo ambao mnataka tutoe? Sijui Serikali Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, katika sheria zote tulizonazo nchini hatuna sheria ambayo inaruhusu kilimo cha bangi mpaka sasa. Na tunayo sheria ambayo imeweka mamlaka yakudhibiti matumizi, uzalishaji, uuzaji na ufanyaji biashara wa dawa za kulevyta nchini bado sheria hiyo inatumika mpaka sasa. Sheria ambayo ameisema Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji haiendani na hayo anayofikiri Mheshimiwa Mbunge kwamba kumeharalishwa uzalishaji wa bangi katika nchi yetu. (Makofii)

SPIKA: Muda hautoshi, tutaendelea na uchagiaji jioni ya leo Wizara hizi ni muhimu sana kamati hizi ndizo zinawakilisha hasa zile shughuli za wananchi wetu, wapiga kura. Kwa hiyo, ninawachagiaji wa kutosha wengi na niwahakikishie kila aliyeomba kuchangia atapata nafasi, ila nikikuita ukiwa haupo humo ndani ndio imetoka hiyo. Maana yake majina niliyonayo ni mengi. Kwa hiyo, naomba wanataka kuchangia tuwahi ili tuweze kupata nafasi ya kuweza kufanya hivyo.

Basi kwa hatua hii nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni ya leo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Saa 6.58 Mchana Bunge *lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(Saa 11.00 jioni Bunge *lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na session ya jioni ya Mkutano wa Kumi na Nane, Kikao cha tano.

HOJA ZA KAMATI

TAARIFA YA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA ITALII KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019

NA

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Kama nilivyosema asubuhi, basi tunaendelea na majadiliano yetu, naomba tuanze na Mheshimiwa Khadija Aboud. Hayupo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Bobali.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia. Kwanza kabisa nawapa pongezi Wenyeviti wote wawili wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Kamati ya Ardhi. (Makofii)

Mheshimimwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri hasa kwa upande wa Kilimo, Maji pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvvi. Nawapa pongezi sana hasa kwa upande wa mifugo, kwa kweli mambo waliyoyafanya yote yanaonekana ni mazuri sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo, naomba nichangie kuwa wote tunajua kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo. Pia kilimo kinachangia kwa asilimia 30 ya pato la Taifa na asilimia 95 ya chakula kinatokana na kilimo, asilimia 30 ya mauzo ni ya nje na asilimia 70 malighafi inachangia malighafi ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, nikisema hivyo, naomba na ninashauri kuwa kilimo kipewe kipaumbele na hasa kwenye bajeti tunayokuja kutunga hapo baadaye kuwa asilimia 10 ya bajeti nzima iweze kwenda upande wa kilimo ili kuweza kutekeleza Azimio la Abuja pamoja na Malabo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaipongeza Serikali kuona Tume ya Umwagiliaji imerudishwa Wizara ya kilimo kutoka Wizara ya Maji kwa sababu tangu wameingia huko kwenye Wizara ya Kilimo, ndiyo wenyewe tunategemea sana kilimo cha umwagiliaji. Huwezi kuongea kilimo cha umwagiliaji bila ya kuongea kilimo. Kilimo cha umwagiliaji ndicho tunachotegemea sana kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Umwagiliaji tangu wamehamia Wizara ya Kilimo, nawapongeza Serikali pamoja na Benki ya Dunia kwa kuweza kukamilisha vizuri mradi wa kuongeza mpunga unaotekelawa huko Mkoani Morogoro. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, pia Tume ya Umwagiliaji imeweza pia kukamilisha miradi mingine, pamoja na skimu 10 kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo alivyoisema kwenye Kamati yetu ambayo tumeiorodhesha. Ila tatizo lililopo ni kuwa walikuwa watekeleze tena miradi mingine mitano lakini hawakuweza kuitekeleza kwa sababu ya tatizo la fedha. Ninaloshauri na tunaloshauri ni kuwa fedha za maendeleo na hasa zinazotoka kwenye nchi yetu naomba ziwe zinatengwa za kutosha na ziwe zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, wote tunaelewa kuwa mboga mboga na matunda ni muhimu sana kwa afya ya binadamu na hasa kwa upande wa lishe ya binadamu kutoka kwa mtu mzima mpaka kwa mtoto, tunahitaji kupata matunda pamoja na mboga mboga pamoja na vyakula vingine. Kwa hiyo, kilimo cha mboga mboga na matunda kinaajiri watu zaidi ya 8%.

Mheshimiwa Spika, ninachoshauri hapa ni kuwa soko lipo ila uzalishaji bado haujawekwa sawa sawa. Kwa hiyo, nilichokuwa nashauri, uzalishaji kwa wingi uweze kuangaliwa, pia na soko la uhakika liweze kuonekana vizuri sana kwa sababu kilimo cha mboga mboga na matunda unakuta ni vijana wengi na akina mama ndiyo wanaolima kilimo hiki.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililopo ni tozo na kodi ambapo Kamati imeona kuwa ni zaidi ya 45 hivi. Hii tuliongea na TAHA ambao ndiyo sana sana wanaoshughulika na mambo ya kilimo cha mboga mboga na matunda.

Mheshimiwa Spika, kilimo mseto wote tunakijua. Kilimo mseto ni kuchanganya changanya mazao mbalimbali, hasa ndiyo kilimo mseto ambapo wakulima wadogo wadogo Tanzania tumekizoea sana. Kilimo hifadhi ni ile unalima mazao yanafunika udongo, unyevunyevu unabaki, halafu unaweza ukafanya kilimo cha kubadilisha badiilisha kiasi rutuba inabaki kwenye udongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kuwa kilimo mseto pamoja na kilimo hifadhi viweze kuhimizwa kwa wananchi kwa sababu kama unatumia kilimo mseto na unatumia unachanganya kwa mfano mahindi pamoja na karanga au pamoja na maharage, zile nodules mizizi yake inatengeneza nitrogen. Kwa hiyo, kama inatengeneza nitrogen unaweza ukapunguza matumizi ya mbolea ya kemikali na ukatumia hiyo mbolea ya asili. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mimi nawapongeza sana kwa upande wa mifugo. Mmefanya vizuri, mmepunguza mambo mengi, samaki wameongezeka kwenye mifugo, lakini soko bado samaki bei iko juu. Kwa hiyo, tunaomba sana kuhusu hilo. Pia nawapongeza kwa sababu ya kutoa 0.4 mrabaha ambao inaweza ikachangia kuleta mapato mengi kwa muda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari, nilikuwa nashauri tena, najua Serikali iko kwenye mkakati wa ujenzi wa bandari, lakini mpaka sasa hivi bado hawajaamua ni wapi itajengwa hii bandari. Hapo naongelea uvuvi wa bahari kuu. Kwa hiyo, naomba ili tuweze kuongeza kipato cha nchi yetu lazima tuangalie uvuvi wa bahari kuu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kingine ni ufugaji wa viumbe kwenye maji.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na Mwenyezi Mungu akubariki zaidi na zaidi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Hamidu Bobali, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu niweze kuchangia taarifa ya Kamati hizi mbili. Nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Kilimo, Kamati ambayo nilidumu kwa takriban miaka miwili na nusu.

Mheshimiwa Spika, nianzie na suala la korosho. Msimu uliopita huu wa 2019 hakukuwa na malalamiko mengi ya wakulima wa korosho kucheleweshewa kulipwa fedha zao, ingawa bei ime-drop tofauti na msimu uliopita ule wa 2018, lakini malipo yalikwenda kwa haraka. Changamoto ni msimu wa 2018.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri yupo hapa, anajua, wako wakulima mpaka leo wanadai fedha zao. Mpaka sasa nititegemea taarifa ya Kamati *inge-include* kwamba ni kwa kiwango gani ama ni kiasi gani ambacho wakulima bado wanadai hawajapatiwa fedha zao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka taarifa ya mwaka 2019 ya Kamati hii ya Kilimo ilielezea na iliitaka Serikali kuhakikisha wanakamilisha malipo ya wakulima kwa wakati. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ihakikishe kwamba deni la msimu wa 2018 wanalimaliza. Taarifa zilizopo ni kwamba *information* ambayo Waziri anayo, ile *amount* ambayo wakulima walikuwa wanadai na Serikali ikatoa, namshukuru Mheshimiwa Rais alitoa zile fedha, lakini zile *information* inaonekana hazikuwa sahihi, kuna fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 10 ambazo hawa wakulima waliachwa, hawakuwa *included*. Kwa hiyo, hii ndiyo leo ukienda pale Mtwara unakuta wakulima wa korosho siku zote wanaenda Mtwara, wanarudi wanaambiwa tutawalipa pesa ikitapikana.

Mheshimiwa Spika, imefikia hatua wakulima waliouza korosho 2019 wamekatwa fedha zao wakiambiwa kwamba tuliwalipa shilingi 3,300/= mwaka 2019 kwahiyo tunazikata hizi fedha kwenda kuwalipa wakulima wengine ambao hawajalipwa, lakini mpaka sasa malipo hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, kwa kuwa Waziri yupo, Naibu Waziri yupo, wajitahidi kuhakikisha wanakamilisha kulipa deni la mwaka 2018. Kuna wakulima wengi ninaowafahamu, wapo wanadai na kila siku wamekuwa wakisumbuka kwenda Mtwara kufuutilia fedha zao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lipo zao la nazi, nimekuwa nikisema sana hapa zaidi ya mara mbili mara tatu. Zao hili liko hatarini kupotea na ni zao ambalo kwa mikoa ya Pwani wale Waswahili tunaotokea Pwani ni kama *identity* yetu. *Identity* ya miji yetu, inapendezesha miji yetu lakini pia ni kwa wapenzi wa chakula ambacho kimeungwa na nazi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, unajua, utafiti unahitajika kufanyika kwenye zao la nazi. Minazi mingi sasa hivi ukienda Kisiju imekufa, hukuti ile minazi ya zamani sasa hivi. Ukienda Pangani, *the same story*, ukienda Lindi minazi mingi pale eneo la Ng'apa ambalo ndilo eneo linategemewa kutoa nazi nyingi, inakufa na nimekuwa nikisema mara nyingi sana. Kuna wakati nilizungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri pale ambaye sasa hivi yuko Utumishi wa Umma nilimwambia niko Jimboni nimewakuta wakulima wanalia minazi inakufa. No research tujue kwamba kitu gani kinapelekea minazi kufa ili ufanyike utafiti tuweze kutibu. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kama ujuavyo, mtu wa Pwani akila ubwabwa au wali ule bila nazi, hauendi kabisa. Tunaomba sana ufanyike utafiti wa kina ili ijulikane tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, mvua zinanyesha, kwa hiyo, ilikuwa ni wakati muafaka sasa hivi wananchi kuhakikisha wanavuna maji. Maji ya mvua yangeweza kutumika kwenye kilimo cha umwagiliaji lakini pia hata matumizi ya kawaida. Wakiulizwa swali hapa Wizara ya Maji, unakuta kila Mbunge anasimama kuonyesha kwamba kwake kuna shida ya maji. Mwaka 2019 tulipitisha Sheria ya Maji hapa. Sheria ile inataka uvunaji wa maji, mtu akivuna lita 20,000 awe analipa kodi. Ukiangalia lita 20,000 ni kidogo sana kwa matumizi.

Mheshimiwa Spika, nilifikiria Kamati ingekuja na mapendekezo, kwa sababu haya niliyaona nikiwa Mjumbe wa Kamati hii, wananchi na wadau walikuja kulalamikia kwamba sheria hii inaweza ikakwaza watu wenye malengo ya kutaka kuvuna maji ya mvua. Mvua Mwenyezi Mungu ametujalia kama mwaka huu mvua ipo ya kutosha sana, lakini shida ni hiyo kwamba sheria inataka ukishafikisha kutaka kuvuna lita 20,000 ambayo ni maji kidogo sana, uweze kulipa kodi, uitolee taarifa Wizarani na mambo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napendekeza sheria hii ingefanyiwa marekebisho. Kamati ingekuja na mapendekezo sheria hii kuifanya marekebisho kuongeza wigo na ku-encourage watu waweze kuvuna maji ya mvua ili tupunguze hili tatizo la watu kulalamikia maji, maji maji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, niliamua nichangie kwenye Sekta hii ya Kilimo. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamidu Bobali kwa kujielekeza kwenye hoja iliyo mezani kwetu. Nakushukuru sana.

Nilishakutaja Mheshimiwa Mwita Getere na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Awali ya yote nawapongeza Kamati zote mbili na Kamati shirikishi zilizokuwemo humu ndani na hasa Kamati yangu ya Ardhi Maliasili na Utalii. Kusema kweli katika miaka hii iliyoukisha, Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii imefanya kazi kubwa sana na ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa namwangalia msemaji mmoja ambaye ni Mjumbe wa Kamati, Mheshimiwa Mch. Msigwa akiwa anazungumza habari nyingi inayomhusu Waziri wa Maliasili na Utalii, nikakumbuka kwamba huko nyuma tulikuwa tunafanya *summit* kubwa sana, wakati tunafanya mambo ya utalii, tumetangaza muda mrefu sana; na tulikuwa na *summit* moja tumekwenda mpaka kule Sunderland kwenye ule uwanja wa *Stadium of Light* tukafanya matangazo ya kutosha na Sunderland wakaja hapa kwetu wakajenga Kituo cha Kindergarten hapa ambayo iko kwenye udongo mwekundu; tumefanya matangazo Wachina wakaja hapa kwenye nchi yetu karibu 1,000; matangazo ya kutosha ya Israel, wamekuja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilipomwona mwanaume mwenzangu anapiga piga yote hapa nikakumbuka ile misafara waliyokuwa wanabebana na Waziri mwenzake Nyalandu kwenda Uganda na kwenda Marekani ndiyo hiyo inayomsumbuu saa hizi hapa. Kwa sababu sasa Waziri wetu hana mkataba wa kwenda Ulaya naye, sasa amekuwa chongo kwenye mambo hayo. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu lazima tuwe na utalii wa ndani. Kuwachukua vijana wetu wa kwenda kufanya kuhamasisha utalii wa ndani, siyo kosa. Je, ikitokea katika nchi yetu watalii hao wa nje wasipokuja kwenye nchi yetu tunafanya? Tunakuwa na mapori ya aina gani?

Kwa hiyo, nafikiri kwamba vitu vingine lazima tufanye mambo ya ndani na mambo ya nje. Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi yake nzuri sana anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nizungumzie habari ya uvuvi na Waziri wa Uvuvi anisikilize vizuri. Huwa najiuliza sana, hivi makokoro yanaisha lini? Kama nchi yetu ilikuwa na mifuko ya nylon, tukapiga marufuku ikaisha, hivi makokoro ni mtaji wa nani? Ni mradi wa nani? Kwa sababu makokoro haya sasa hayaishi.

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa upande wa Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi atakaa na wavuvi sasa watengeneze *logistic* za kutosha za kuamua nyavu na milimita sita za sangara ziweje? Nyavu za furu ziweje? Nyavu za gogogo ziweje? Nyavu za nembe ziweje? Kwa hiyo, tutakaa tutengeneze *formula* ambayo itatuwezesha sasa kwenda kuvua, tukasema mwaka huu tumeepukana na haya mambo ya uvuvi haramu?

Mheshimiwa Spika, sasa uvuvi haramu umekuwa ni kama chanzo cha mapato cha watu. Wakati fulani tuna watu wa samaki, tuna Maafisa Uvuvi wako kule kwenye ziwa. Sasa inatoka hapa timu inaenda kufanya operesheni. Kama hawa wako barabarani, unajua vitu hivi mimi huwa sivielewi!

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, matrafiki wa kutoka Dodoma mpaka Arusha wako barabarani, lakini leo inatokea wanasema leo tumefanya operesheni ya kukamata mabasi. Sasa hao matrafiki walioko barabarani wamewaondoa au wamewafukuza kazi? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hao Maafisa Wavuvi walioko kwenye maeneo, leo mnaenda kufanya operesheni na wenyewe wapo, unamaliza kufanya operesheni unawaacha pale pale, kitu gani kitatoka? Tunaomba sasa tupate muafaka kwamba ni lini shughuli za makokoro zitaisha kwenye shughuli hizi za uvuvi?

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la pamba na bahati nzuri watu wa pamba wako vizuri sana. Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli ameteua vijana wazuri sana kwenye pamba. Naomba sasa watumie akili zao kuelewa haya mambo. Hivi ushirika wa sasa unatusaidia au unatugandamiza? Ushirika uliopo sasa hivi unatusaidia nini?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ushirika ule ile Kamati ya Ushirika ni Mawakala wa Makampuni, lakini ushirika wa sasa unauzia makampuni kushindana, kwa sababu ushirika wa sasa inabidi wewe kama unataka kununua pamba uende kwao. Kama ni Kituo A, kama ni Maliwanda, uende Maliwanda wewe Kampuni ya S & C, Kampuni ya Olam, Kampuni ya Kingu, Kampuni ya Bon wote mwende kwenye ushirika huo. Halafu wanawapangia muda wa kununua pamba; wewe leo utanunua mpaka hapa, wewe utanunua hapa. Ushindani wa pamba utatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa wale washirika wa zamani walikuwa na pesa. Ushirika wa sasa ulikuwa na pesa ya kununua pamba, unashindana na makampuni binafsi. Ushirika wa sasa ni mawakala.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sasa huwa najiuliza, pamba ikitoka kwa mkulima ikienda kwenye ushirika anafika pale kwenye ushirika hana hela ya kununua pamba; amekopa tayari. Huo ushirika ukichukua pamba kutoka kwenye ghala kupeleka kwenye kiwanda hawana hela. Sasa najiuliza, hivi pamba inayochukuliwa kwenye ushirika kwenda kwenye kiwanda ikianguka au ikiungua moto humo ndani analipa nani? na je tunapeleka pamba kwenye ghala halafu lile ghala likaungua analipa nani?

Mheshimiwa Spika, mimi naona, ni kweli tunataka ushirika, lakini basi tuimarishe tukubaliane ushirika wa zamani urudi, tutafute fedha tuwape ushirika wanunue pamba washindane na makampuni, vinginevyo sasa utakuwa ni wakala tu; wako pale wanakula hela na watu hawataki, wananchi hawawataki tunang'ang'ana nao tu wanakula hela. Nishukuru tu kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba angalau kipindi hiki basi tunaweza tukafanya mambo ya watu walipe kutokana na benki, inaweza kusaidia. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie habari ya TANAPA, TANAPA ni shirika letu tumewapa mzigo wa hifadhi 22 kutoka 16, lakini hifadhi zenyе faida ni tano; hata hivyo zenyе faida zaidi ni mbili tu, ni Serengeti na Kilimanjaro; sasa wanamzigo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, hili takriban ni Bunge la Nne wameomba kupunguziwa kodi. Hawaombi hela, wanaomba kupunguziwa kodi. Hivi inakuwaje leo TANAPA wakienda kunijengea mimi madarasa ya watoto shule, wanajenga Sekondari na wanalipizwa VAT? Wanalipa VAT kujenga mradi wa kijamii? Shida nini?

Mheshimiwa Spika, tumeomba hapa, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika umesema, tumesema, sasa tufanyeje ili TANAPA wapunguziwe kodi ili waweze kuijendesha? Kwahiyoo mimi naomba hili jambo lizungumzwe na liweze kufanya mafanikio kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, tuna TAWA, TAWA sasa inaonekana ni mamlaka ndogo ambayo sasa kila wakati tumekuwa tundainyanganya uchumi fulani kwa manufaa yetu sisi binafsi badala ya manufaa ya nchi kwa kweli. Kwa mfano suala la umeme wa Selous linaendelea kwa yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mapato yao wamepandisha nadhani kutoka 33.8 bilion wamepandisha mpaka 48.8 bilion; lakini sasa uendeshaji wa TAWA kwenye shughuli zao za kawaide ni bilioni 150. Sasa kama hatuwezi kuwasaidia hawa TAWA na wanalinda mapori yetu, mapori ya akiba, mapori Tengefu, maeneo oevu, kama hatuwezi kuipa fedha za kutosha watafanyaje ili wajijendeshe?

Mheshimiwa Spika, muhimu ni mishahara ya watu wa TAWA, lazima sasa Serikali sasa kama hatuna uwezo kuipa TAWA fedha za kutosha tusaidie mishahara ya watu wa TAWA ifanane na watu wa TANAPA; maana haiwezekani! Watu wanaolinda ndio walio kwenye ukingo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana ahsante naunga mkono hoja.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante, naungo mkono hoja.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Getere tunakushukuru tu kwa mchango wako mzuri muda tu ndio hautoshi. Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Dkt. Stephen Kiluswa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika taarifa za kamati ambazo ziko mbele yetu. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rarmi ya Upinzani kwa kuniamini na kunitfea kuwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Hii inaonesha ni namna gani chama chetu kinavyotoa fursa kwa wanawake kushika nyazifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwenye taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, mosi, ningependa Mheshimiwa Waziri wa Maji akija kujibu anieleze. Mradi wa maji wa Bunda umechukuwa mda mrefu sana, na tatizo kubwa lilikuwa ni ujisadi wa mkandarasi aliyejewa anaendesha mradi ule ambao sasa hivi ni takribani miaka 12 na mradi bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara mkoa wa Mara na akapata taarifa mbalimbali kuhusiana na mkandarasi huyu Nyakirang'anyi aliyepeewa kuhudumia mradi wa maji ambayo chanzo chake ni Jabeu.

Mheshimiwa Spika mkandarasi yule Waziri Mkuu aliamuru TAKUKURU imkamate kuhusiana na ujisadi unaofanya kwenye mradi wa Bunda. Kama haitoshi Mheshimiwa Rais alifanya ziara Mkoa wa Mara na kwenye Jimbo la Bunda Mjini akaelekeza mkandarasi yule akamatwe na akafunguliwa kesi ya kuhujumu uchumi.

Cha ajabu, mkandarasi yule ameongezewa mkataba tena ili kumalizia mradi Bunda; kwa ajabu. Yaani mtu amefanya madudu yote, Waziri Mkuu amesema Rais ameenda amesema bado tu Wizara mnampa tenda mwizi ambaye tayari mlisha declare wenyewe kwamba huyu mtu ni mwizi na amechelewesa huu mradi. Ilifikia kipindi account zake zote zikafungwa, Wizara kipindi cha Maghembe kikamkopessa pesa mwizi; leo tena mnampa tenda? Kwenye moja ya mkataba wake ilikuwa pia aanze kujenga vituo, hajajenga mpaka sasa hivi; mnamuongezea tena mkataba kwa ajili ya kusambaza mtandao wa maji?

Mheshimiwa Spika, haya si maneno yangu nikiongea kitu nina uhakika nacho nakuona mdogo wangu unatikisa kichwa, nina uhakika nacho.

Mheshimiwa Spika, niliongea na kiongozi mmoja mkubwa Wizarani; akasema tumeona tumuongezee mkataba ili amalize; Mara mia kuvunja mkataba wa wizi mkampa mtu mwingine; alizoiba zinatosha ili wananchi wa Bunda wapate maji safi na salama huu mradi ni wa muda mrefu na kuchelewa kusuasua kwa mradi huu na nyie pia mnapata hasara. Ningependa nipate majibu sahihi kwanini mmerudia kumpa mkataba mwizi ambaye aliwekwa ndani na nyie mnasema ni Serikali safi mnashughulika na mafisadi, huyu fisadi mmemuongezea mkataba tena.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie kidogo suala la pamba. Sisi wananchi wa Kanda ya Ziwa vitu tunavyovitegemea ni uvuvi ufugaji na kilimo cha pamba. Tangu nimeingia Bunge hili huu ni mwaka wa tisa kilio kikubwa cha wananchi wanaolima pamba ambacho Serikali ya Chama cha Mapinduzi kimeshindwa kutatua ni mbegu, bei, dawa ya kuilia wadudu na kulipa wakulima kwa muda mwafaka; imekuwa ni tatizo kubwa. Kama pamba ingewekewa utaratibu mzuri ingeleta fedha nyingi za kigeni, ingesaidia kumaliza matatizo mengine na kukuza uchumi wa taifa letu; lakini leo zao la pamba limeshuka. Sasa tunashindwa kuweka mikakati dhabiti ya kusaidia zao la pamba alifu tunakuja na maamuzi ya zima moto.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka ilivyoletwa mbegu ambayo haina ubora hatima yake Serikali ilikimbizana kulipa fidia ya mabilioni ya shilingi. Kama tungefanya utafiti wa kutosha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tukajua mbegu sahihi wakulima wangepatiwa leo tusingekuwa tunazungumza matatizo ya pamba.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha pamba kinaanza mwezi wa kumi na moja lakini hivi tunavyozungumza mpaka leo wakulima hawajalipwa. Huyu mkulima anasomesha watoto, huyu mkulima ana mahitaji mengine. Tukileta takwimu hapa za wakulima wanaodai pamba si sawa, hawa nao ni binadamu. Si mnasema ni Serikali ya wanyonge? Wanyonge ni akina nani kama si hawa wakulima wanaotafuta wanaokopa kuhakikisha hawaombi wanatafuta pesa zao kwa jasho na damu? Hivi leo tukizungumzia mko wa Simiyu peke yake wanadai takribani billion nne; hapo bado hatujazungumzia Geita hatujazungumzia Mwanza, hatujaenda Shinyanga haujagusa Mara. Lipeni, na msimu unaanza mwezi wa tano. Jamani kama ilivyo zao la zabibu tegemeo kwa Mkoa wa Dodoma, kama ilivyo korosho tegemeo kwa Mkoa wa Mtwara na sisi wananchi wa kanda ya ziwa tegemeo letu ni pamba.

Mheshimiwa Spika, akisimama Mheshimiwa Raphael Chegeni atazungumzia pamba, akisimama Mheshimiwa Richard Ndassa atazungumzia pamba na nikisimama Ester Bulaya nitazungumzia pamba, akisimama Mheshimiwa Gimbi Masaba, akisimama Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki atazungumzia pamba na Mheshimiwa Ester Matiko atazungumzia pamba. Kilio cha pamba kimekuwa kikubwa; inawezekana ninyi Mawaziri hamjui hali halisi iliyoko kule chini.

Mheshimiwa Spika, please fanyeni utafiti wa kutosha msifanye utafiti wa kukurupuka. Fanyeni utafiti wa kutosha, lipeni wakulima kwa wakati ili tuhakikishe zao letu linakua. Kila siku kumekuwa na visingizie lukuki.

Mheshimiwa Spika, hivi vyama vya msingi ni tatizo, kuna rushwa huku. Sasa hivi kumekuwa na malalamiko, na mimi nimepata malalamiko kwenye Jimbo langu Kijiji cha Chagunge. Katibu wa cha msingi amekula pesa ya mkulima takribani milioni tatu.

Mheshimiwa Spika, vilevile havifanyi kazi kwa ufanisi, kuna mazingira ya rushwa. Mtu ili alipwe naye pia lazima atowe kitu kidogo. Tusipokuwa na mifumo mizuri huku juu inaenda kuambukiza uwozo mpaka huku chini, ndiyo maana leo vyama vya msingi navyo havitimizi wajibu wake na havifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo kwenye suala la mizani kwenye vipimo. Tunajuwa inahakikiwa, tunajua; lakini leo hii mkulima anaenda kupima pamba yake, lets say ameweka kwenye shuka, kapeleka kg 15 anaambiwa hii shuka tu peke yake ina uzito wa kg. 3; ni wizi. Fuatilieni, pamoja na kwamba mmefanya uhakiki bado kuna rushwa ndogo ndogo zinamkandamiza mkulima wa pamba.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kitu kingine, nimepewa malalamiko kwa baadhi ya watu ambaao wanalipwa. Anasema, anaambiwa ameingiziwa milioni 300...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ESTER A. BULAYA: ...akienda kwenye akaunti anaziona akitoa anakuta milioni 20 wizi na utapeli ukemewe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana, nilishakutaja Mheshimiwa Stephen Kiruswa, atafuatiwa na Mheshimiwa senate George Malima Lubeleje.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili name niweze kuchangia hoja zilizopo mezani za Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii pamoja na kamati ya Kilimo Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika nitumie fursa hii kuwapongeza Kamati kwa kazi kubwa walizozifanya na Wizara husika kwa kazi kubwa wanaoifanya kupeleka mbele maendeleo ya watanzani.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe dondo chache katika sekta ya ardhi, maliasili na mifugo; na kama muda utaniruhusu nitaongelea pia suala la maji kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi; napenda kuipongeza Serikali kwa dhana nzuri muhimu sana ya kupanga kupima na kuradhimisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu; kwakweli hii dhana ni muhimu sana. Ninachelea kusema kwamba kwa ufinyu wa bajeti ambayo mapato ya ndani inatenga kila mwaka kuwapa Wizara, na kwa uhaba wa fedha za wafadhili na hata za mikopo tunayopata hatutakaa tufanikishe zoezi hili. Ningependa kuishauri Serikali kwamba twende sasa kwenye hatua ya kuiongeza, twende nje ya box kidogo. Tutafute namna nytingine ya kuongeza mapato ili tuweze kukamilisha zoezi hili kwa sababu migogoro ya ardhi haitakaa iishe kama kasi tutakayoendelea kwenda nayo ni hii ya kuhangaiya ya urasimishaji wa makazi ambayo yalishazuka kiholelea katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Badala yake twende proactively mbele na kupima ardhi yote ya Tanzania na kumilikisha; tuwahi maeneo kabla hayajavamiwa na watu ambaeo nao wanazidi kuongezeka na kila siku wanahitaji kujenga.

Mheshimiwa Spika, ingependeza kama ambavyo imeshawahi kufanywa na Bunge hili tukaongeza hata tozo zingine katika baadhi huduma za kijamii na mazao au bidhaa mbalimbali kwa ajili tu ya kuongeza mfuko wa upangaji umimaji na urasimishaji wa ardhi ya nchi yetu .

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa napenda kuishauri Serikali kwamba Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ambaeo unahitajika kwa kasi zaidi kuliko inavyokwenda sasa usipofanya kwa kuweka fedha za ziada katika Wizara hatutafika na migogoro haitapungua. Ndiyo maana migogoro iko kila siku kati ya vijiji na vijiji kata na kata wilaya na wilaya, mkoa na mkoa na hata nchi na nchi.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio naomba sana Serikali iende hatua ya ziada ya kutafuta fedha hata katika kuongeza kodi katika baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa au kuuzwa au kuletwa nje ili tuweke kodi kama ile ya TDL ambayo iko katika mazao mengine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya maliasili. Ninapenda kuipongeza kwa kweli wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa kuongezeka utalii nchini na kuimariika kwa hifadhi ya wanyamapori; na ndiyo maana hata sasa wanyama wamezidi mpaka wanakuja kurandaranda kwenye makazi ya watu na adha inazidi kuongezeka na kuwa kubwa katika mgongano unaotokea kati ya wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba, kwa sababu Wizara sasa hivi inafanya marejeo ya kanuni mbalimbali, katika marejeo inayohusika na suala la kifuta machozi pamoja na suala la kifuta jasho; pamoja na kwamba tunaamini package itaongezeka ili itie matumaini kuna kipengele muhimu ambacho hakipo; suala la majeruhi. Mtu anaweza akajeruhiwa akalipwa laki mbili na nusu lakini majeraha aliyopata anahitaji matibabu ya gharama kubwa na ambayo kile kifuta machozi hakiwezi kugharamia. Kwa mfano katika jimbo langu la Longido mtoto wa darasa la nne aliyejewa anachunga tu wakati wa likizo aliparamiwa na tembo akaaribiwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mfumo wa mzima wa sehemu zake za siri katika ya miguu. Yule mtoto angekufa, lakini Wizara ya Maliasili na Utalii ilimpeleka Hospitali ya Rufaa ya Seriani; akatibiwa takribani miezi mitatu, gharama ikapanda mpaka ikafika milioni kumi na sita. Mtoto yule angezuiiliwa pale mpaka alipe lile deni, lakini kwa sababu ya ubinadamu uliotumika na penda kuishukuru wizara ili bidi wamzamini mtoto akatoka na wizara ikatafuta kila namna tukasidiana ili yule mtoto alipiwe ile bill.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu hakuna sheria na wala haiko kwenye kanuni, ningeomba kanuni ya mafao ya kumtimu majeruhi iongezwe kwenye zili kanuni ili mtoto au mtu anapojeruhiwa lakini hajafa ile 250 tu ya kumfuta machozi haitoshi; ahudumiwe na Wizara wananchi waweze kuthamini hifadhi ya wanyamapori kwa sababu unalipa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwa upande wa sekta ya mifugo. Sekta ya mifugo kwa kweli; nimeona kwenye ripoti yao; wametia mkazo zaidi kwenye suala la kuaharakisha uwekezaji kwenye viwanda. Tukiwekeza kwenye viwanda ilhalil hatujawekeza kwenye malisho, maji, majosho, dawa za tiba na za chanjo pamoja na kuimarisha bei ya masoko ya mifugo tutakuwa hatujafanya kitu. Sawa, viwanda vinaweza vikajengwa lakini, je, kama hatujaweka mbele maslai ya ubora wa mifugo tunayofuga haijawekewa mkazo tutafika kweli? Ninaomba kwamba Serikali ijitalidi kuweka mkazo katika uboreshaji wa afya ya mifugo kwa kuwekeza kwenye maji, malisho tiba na vitu kama hivyo ili tuweze kufanikisha kuvipatia viwanda hivyo rasilimali inayostahili. Ikitokea kwamba viwanda vimekwisha na hatuna ng'ombe wenyе tija ambaо viwanda vile vinahitaji wafugaji wetu wataendelea kuwa na adha kubwa ya sehemu ya kuuza mazao yao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, na sambamba na hilo pia niombe Wizara hii ya Mifugo, zile tozo ambazo sisi Wabunge wafugaji tumelalamikia kila wakati ni kubwa. Kabla hatujapata soko la ndani hizo tozo zipunguzwe ili hawa wafugaji waendelee kuuza hata nchi ya jirani wapate hela ya kuendelea ku-support familia zao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, hivi viwanda vitakavyomalizika na vikaanza kuwa ndio watumiaji wakubwa wa bidhaa ya mifugo tunayozalisha hapa nchini ningeomba bei yenye ushindani itolewe; tusije tukaweka bei bei chini hao wawekezaji wa viwanda wakalaza bei ikawa ni kichocheo cha watu kuendelea kutamani kupekeka mifugo nje ya nchi Tanzania. Tuangalie masoko ya nje, nchi za jirani, tuweke bei ambayo ni sawia ili tuweze kutumia rasilimali ya mifugo kwa utaratibu huo na sisi tukapata faida.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya maji mimi nilikuwa nimeona kero moja kubwa sana ambayo iko katika miradi ya maji inayoanzishwa na Serikali; katika wilaya yangu kuna ile ya World bank; unakuta visima virefu vimechimbwa, watu wamewekewa miundombini stahiki na mashine kubwa za kusukuma maji ku-pump maji lakini wanaachwa wananchi wasio na ujuzi wakaendesa zile mashine; na ndani ya miaka michache generator la milioni 20 unakuta limekufa kwa sababu hawajuwi ni lini oil inabadilishwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali iwe makini kukaribia hiyo miradi ambayo imeanzishwa waendelee kuwapeleka wataalamu na wawasimamie wanakijiji kamati zile za majizisiachiwe jukumu la kuendasha mitambo ambayo hawana ujuzi nayo maana wanaingia hasara. Sasa hivi sisi katika wilaya yangu tuna visima vingi mwaka huu na mvua imearibu mabwawa yote. Watu watakaa bila maji kwa sababu mashine zimearibika na hakuna utaalamu wa kuzitengeneza na wananchi hawana uwezo wa kununua mashine kama zile zilizowekezwa na Serikali mara ya kwanza.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sambamba hili na mwisho kabisa nipende pia kusema kwamba sisi jamii ya Wana Longido ni wafugaji na asilimia 99 ya maji ya mifugo ni yanatokana na mabwawa, na mabwawa yetu yote; tulikuwa na mabwawa 25 takriban yote ama yamejaa udongo ama yamepasuka. Wizara ya Maji na Wizara ya Mifugo kwa sababu sisi tukipata maji ya mifugo binadamu watatumia hayo hayo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana...

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: ...tukipata maji ya binadamu mifugo watatumia maji hayo hayo wafanye bidii warudi Longido watusaidie kurekebisha miundombinu ya maji maana hali ni mbaya kweli kweli.

Mheshimiwa Spika ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja zote za Kamati zote.

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hizi za Kamati mbili kwanza niwapongeze wajumbe wa Kamati, wenyeviti wa Kamati hizi vilevile niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia sekta ya maji, maji ni uhai, maji ni maendeleo, maji ni uchumi. Wilaya zetu za Mpwapwa na Kongwa pamoja na Jimbo la Kibakwe kuna matatizo makubwa sana ya maji na nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji ametembelea maeneo yale kulikuwa na miradi mitatu ua minne katika Jimbo la Mpwapwa. Mradi wa Mima bado unasuasua kidogo lakini mradi wa Mzase, lyoma na Gumila Mheshimiwa Waziri wa Maji alipofika katika jimbo langu aliagiza Katibu Mkuu, makandarasi walipwe na kweli walilipwa na miradi hii inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri sana Wizara ya Maji, Makandarasi ambao mnateua, mteue makandarasi ambao wana uwezo. Pili mteue wakandarasi ambao wanaweza kutekeleza miradi bila kusubiri fedha malipo ya kazi ile ndio watekeleze mradi. Wakandarasi wa Serikali iwalipe mapema kwa sababu kuna wakati fulani miradi inachelewa tunalaumu labda wakandarasi kumbe wakandarasi hawa hawalipwi mapema. Kwa hiyo, naishauri wizara iwalipe wakandarasi hela mapema ili waweze kutekeleza miradi hii mapema.

Mheshimiwa Spika, la pili ni sekta ya mifugo, sekta ya mifugo nchi yetu ina mifugo mingi sana lakini inachangia pato la Taifa kidogo sana, sijui kama inafika asilimia 5. Bahati nzuri niliwahi kutembelea nchi ya Namibia na Botswana tulikwenda kule na Mheshimiwa Pinda alipokuwa Waziri Mkuu. Botswana wana mifugo michache sana kama milioni mbili hivi lakini mifugo yao inachangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa sana, asilimia 40 lakini mifugo yetu sisi pato ni kidogo sana. Kwa hiyo, tuwaelimishe wafugaji wafuge ufugaji bora.

Mheshimiwa Spika, kwangu pale Mpwapwa kuna kituo cha utafiti wa Mpwapwa, mifugo ya Mpwapwa. Nilishauri kwamba wakulima wa Wilaya ya Mpwapwa watumie kituo cha utafiti wa mifugo cha Mpwapwa ili kuboresha maisha yao kwa sababu wafugaji wengi wanahitaji wawe na makundi mengi ya mifugo lakini hawataki kupunguza mifugo yao ili kuboresha hiyo mifugo iweze kuongeza pato la Taifa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu sekta ya kilimo, sekta ya kilimo ndio inaleta pato kubwa sana katika nchi yetu. Katika kilimo kuna kilimo cha umwagiliaji kuna kilimo cha kawaida lakini kuna kilimo cha umwagiliaji. Utakumbuka katika jimbo lako na jimbo langu kuna miradi mingi sana ya umwagiliaji, ukiangalia bonde la Chamkoroma, Bonde la Mseta, Bonde la Tubugwe unakuja Bonde la Matomondo kuanzia Mwenzere, Mlembule, Tambi unakwenda mpaka Bonde la Mbori, Wagodegode mpaka Mabonde ya Lumuma na Malolo. Haya mabonde yangekuwa yanatumika vizuri kwa kilimo cha umwagiliaji nina uhakika hata tatizo hili la njaa lisingetokea.

Mheshimiwa Spika, skimu nyingi zimechakaa, ukitembelea miradi kwa mfano miradi katika langu na jimbo lako hii miradi tangu skimu zimekarabatiwa sasa ni miaka 5 au miaka 8 hazijafanyiwa ukarabati kabisa. Kwa hiyo, naishauri Wizara ya kilimo mkarabati hii skimu za umwagiliaji ili hawa wakulima waweeze kunufaika na kilimo hiki cha umwagiliaji. Nchi yetu ina mabonde mengi sana na yaktumika vizuri kwa kilimo cha umwagiliaji nina hakika tutaondoa tatizo hili la njaa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na haya machache tu nakushukuru sana na naunga mkono hoja zote hizi mbili na niongeze tena kwa kuwapongeza Kamati na vilevile kuwapongeza mawaziri wanaoshughulikia hizi Kamati. Ahsante sana.

SPIKA: Asante Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Rhoda Kunchela ni zamu yako dakika tano atafatiwa na Mheshimiwa Eng. Edwin Ngonyani

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi niweze kuchangia mawazo kidogo kwenye Wizara ya Kilimo, Maliasili pamoja na Maji. Nadhani hii ni karibuni mara ya kumi nimekuwa nikizungumza jambo moja katika Mkao wangu wa Katavi asilimia 90 ya wananchi wa Mkao wa Katavi wengi ni wafugaji pamoja na wakulima lakini ukisoma hotuba ya Kamati zote mbili hususan kilimo pamoja na Maliasili hizi ni Kamati ambazo zinaingiliana kwa baadhi ya mambo. Changamoto kubwa walioieleza Kamati ni pamoja na migogoro na manyanyaso yanayoendelea kwa wakulima pamoja na wafugaji katika taifa hili. Sasa kwa ujumla wake manyanyaso hayo pamoja na uonevu umekuwa ukifanyika katika mikoa ambayo ina wafugaji wengi na wakulima wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini wiki mbili zilizopita jambo la aibu Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika pamoja na Mkurugenzi wa Tanganyika walipokea pesa ya rushwa shilingi milioni 60 walimchaji mfugaji mmoja alikuwa na ngombe zaidi ya 600 wakawa wanamtoza milioni moja kwa ng'ombe mmoja.

Sasa sheria inasemaje; mambo haya tukiwa tunalalamika watu wanaona kwamba tunalalaika kila siku lakini tunachokisema katika Taifa hili katika Mkao wa Katavi naweza nikasema katika Wilaya ya Tanganyika inaongoza kwa rushwa chini ya huyu Mkurugenzi anaitwa Lumuli pamoja na Mhando, huu ni mwaka wa nne nazungumzia mambo haya.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, wizi, rushwa zimekidhiri katika Wilaya ya Katavi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, tunapokuwa tunazungumzia mambo haya...

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Rhoda kuna taarifa nilimsikia Mheshimiwa Msongozi
T A A R I F A

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, nimemsikia mchangiaji anayeendelea kuchangia akizunguza suala la Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kwamba wamepokea rushwa ya shilingi milioni 60. Kwa hiyo, nataka mchangiaji atueleze anaweza kutoa ushahidi kwa jambo hili analolizungumza?

SPIKA: Mheshimiwa Rhoda.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mchango wangu kwa sababu hata Mheshimiwa Jacqueline anayoongea haishi Mkoa wa Katavi wala haelewi kinachoendelea katika Mkoa wa Katavi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee uonevu na unyanyasaji unaofanyika na Mkuu wa Wialaya huyu huu ni mwaka wan ne na si hayo tu, Mheshimiwa Waziri alikuwepo juzi wiki tatu zilizopita anaelewa wizi wa pesa zilizopigwa na huyu Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi anaelewa. Sasa Serikali imechukua hatua gani kuwajibisha huyu Mkuu wa Wilaya ambaye kwetu kule ni mzigo watu hawamtaki kwa sababu amekuwa ni chanzo cha migogoro sio solution. Badala ya kumsaidia Mheshimiwa Rais amekuwa ni tatizo na anatamba kule yeye ndio Mfalme sasa kule yaani ndio Mungu mtu wa Wilaya ya Tanganyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, watu hawamuhitaji kutokana na kwamba amekuwa ni chanzo cha migogoro na sio solution kwenye Wilaya ya Tanganyika. Nataka Waziri akija atueleze ni sheria ipi ilitumika kuchaji ng'ombe mmoja milioni moja na sheria inasema ni shilingi 30,000 kama ni ng'ombe akiingizwa kwenye eneo la hifadhi. Sasa Mamlaka haya ya halmashauri ya Tanganyika wameyatoa wapi na wamechukuliwa hatua gani, Mheshimiwa Waziri akija atueleze wizi huu wa pesa zilizopigwa na huyu Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi, solution yake ni nini.

SPIKA: Mheshimiwa Rhoda unasema ni wamechaji milioni moja kwa ngombe mmoja?

MHE. RHODA E. KUMCHELA: Mheshimiwa Spika, ndio ngombe mmoja

SPIKA: Yesu na Maria na huyo Mkoa wa Wilaya ni nani?

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Wilaya anaitwa Muhando na Mkurugenzi anaitwa Rojazi Lomoli.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie vijiji 920 Mheshimiwa Lukuvi alikuwepo kwenye ziara ya Rais iliyofanyika mwishoni mwa mwaka jana lakini tulitangaziwa kwamba kuna vijiji 920 vilivyorasmishwa kutoka kwenye maeneo ya hifadhi wananchi wapewe kwa maana ya uhaba wa maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Spika, sasa mpaka hivi tunavyoongea si Mkoa wa Katavi peke yake mpaka na maeneo mengine baada ya kauli hizi ambazo Mheshimiwa Rais alitamka kwamba haitaji kuona wafugaji wanateseka katika Taifa lakini imekuwa ni vice versa. Wafugaji wamekuwa wakipigwa ukienda kwenye Kata ya Stalike watu wanapigwa lakini Rais alitoa kibali watu waendelee kuishi...

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Rhoda dakika tano zimeisha. Nilitaja Mheshimiwa Engineer Edwin Ngonyani utafatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na kuniwezesha leo kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nikushukuru sana kwa kunipa furs hii na kwa kweli nitajitahidi kwenda haraka nikiwa kama mmoja kati ya wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningeanza na taarifa ya jumla kwanza nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati kwa kutuletea mapendekezo saba tu na kwa kweli sekta nzima ya maji ameleta pendekezo moja sekta nzima ya mifugo ameleta pendekezo moja, kilimo pendekezo moja, umwagiliaji pendekezo moja na uvuvi mapendekezo matatu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana na Bunge lako Tukufu mapendekezo hayo tuyapitishe yawe maazimio ya Bunge letu Tukufu ili Serikali iyafanyie kazi. Nafahamu kuna pendekezo moja halijawekwa wazi ni pendekezo la kuhakikisha kwamba maazimio yaliyopitishwa mwaka jana tunaomba Serikali iendelee kuyatekeleza kama tulivyoyapitishwa mwaka jana. Mapendekezo hayo ndio yanagusa watu wengi wameyachangia hapa wanadhani kwamba hayapo katika taarifa hii ya Kilimo, Mifugo na Maji lakini kwa sababu tayari yalishafanyiwa maazimio mwaka jana ikiwa ni pamoja na pendekezo ambalo Mheshimiwa Kiruso ameongelea suala la uendelezaji wa malisho. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana hoja ya kuanza viwanda vinavyotumia mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kama malighafi, hili pendekezo tukilipitisha na Serikali ikilichukulia kwa ukina wake litatusaidia sana katika kuendeleza sekta yetu ya viwanda lakini wakati huo huo kutoa fursa kwa wakulima kupata masoko ya mazao yanayozalishwa na vilevile kuongeza thamani mazao hayo na kwa maana hiyo kuongeza ajira kuitia sekta hizo za viwanda.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika suala la umwagiliaji ni muhimu sana na tunaomba sana Serikali itilie mkazo katika kuhakikisha kwamba eneo hili la umwagiliaji linawekewa bajeti ya kutosha ili researchers wetu wanaoshughulikia na masuala ya mbegu ambazo zinagunduliwa na wataalamu wetu katika vituo mbalimbali vya utafiti viweze kuendelezwa na hivyo kupunguza kiwango kikubwa cha mbegu kinachoagizwa kutoka nje. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwa sasa tunaagiza zaidi ya asilimia 60 na kwa kweli sio sahihi kabisa kutegemea kiwango kikubwa cha mbegu kutoka nje. Ningemba sana Serikali itilie mkazo suala hili la umwagiliaji kwa sababu ni kweli changamoto kubwa kwa sasa haiwezekani kuandaa mbegu kwa kutumia mvua na wakati huo kipindi hicho hicho ndio uzalishaji wa mazao unatakiwa ufanyike.

Mheshimiwa Spika, ni kwa vyovoyote vile utakuta mbegu zinazalishwa kwa wakati mmoja na kilimo chenyewe na njia pekee ya kuondokana na hili ni kuboresha umwagiliaji ili mbegu ziweze kuzalishwa kipindi cha kiangazi kisha wakulima wazipate kipindi cha masika tuweze kupanua kilimo chetu na wakulima wetu wapate mbegu bora na waongeze tija katika uzalishaji. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ningemba kuongelea vilevile suala la force account, wapo walioongelea, mimi nina mtizamo tofauti kidogo kwa maana naungana na Kamati lakini wakati huo kuna eneo nataka niliongezee. Kitu cha kwanza niipongeze sana Wizara ya Maji na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kweli suala hili la

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutumia force account limetusaidia sana limebadilisha uwezekano wa kutekeleza miradi mingi sana ya maji kwa muda mfupi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya maji kwa maana ya kwa utaratibu ule wa zamani wa kutumia wakandarasi ilikuwa unatumia fedha nydingi sana, mradi mmoja unatumia fedha nydingi sana lakini kwa namna ambavyo sasa hivi unafanyika fedha zile zinaweza zikafanya miradi mitano hadi sita badala ya mradi mmoja na mfano huo upo katika eneo ambalo natoka Wilaya ya Namtumbo. Nashukuru sana Waziri wa Maji amesitisha mikataba miwili na mingine miwili nayo amerekebisha ili kuhakikisha force account inatumika katika kununua vifaa na wale wakandarasi wanatoa tu *labor force* peke lakini vifaa vinanunuliwa na Serikali kupitia force account na matokeo yake gharama za mradi zimeshuka sana kwa zaidi ya asilimia 40 na hivyo kuwezesha miradi mingine mingi kuweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana hilo vilevile naungana na pendekezo la Kamati na mimi nimeshiriki kutoa hilo pendekezo kwamba tuangalie suala la ajira kwa makandarasi wetu na hasa wale wanaomaliza mafunzo katika vyuo vyetu vya VETA wawze kupata kazi kwa hiyo watumike na hivyo licha ya kutumia hiyo force account ni nzuri itumike lakini wakati huo tuangalie kuingiza na uwezekano wa kuzalisha ajira kwa private sector. Kwa hiyo, nilikuwa naomba na hilo liangaliwe kama ambavyo Kamati imependekeza. (Makof)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili asante sana.

SPIKA: Ahsante sasa Waheshimiwa wanaofata wote ni dakika tano tano ili mpate nafasi. Mashimba Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Kamati hizi mbili Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Kamati ya Ardhi na Maliasili.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wenyevit na Wajumbe wa Kamati zote mbili kwa kufanya kazi yao vizuri na hatimaye kutuletea taarifa hii hapa Bungeni. Pia niwapongeze sana Mawaziri wanaohusika na sekta hizi nne kwa sababu ya kazi wanazofanya tunaona kazi wanayofanya na kwenye maeneo yetu tunaziona.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala moja tu la ushirika hasa wa mazao. Ushirika ni kitu kizuri na umekuwa kitu kizuri toka wakati wa kupigania uhuru wa nchi yetu. Imekuwa kiunganishi cha watu wetu na hata kwenye nyakati za uhur, Mwalimu Nyerere pamoja na wenzake walitumia ushirika ili kuweza kuwaunganisha Watanzania na hatimaye kudai haki yetu ya uhuru.

Mheshimiwa Spika, pia ushirika umekuwa kitu kizuri kwa sababu umeliletea Taifa hili sifa nydingi sana. Wakati wa miaka ya 1968 Ushirika ulionekana ndiyo chanzo kikubwa na kizuri kwa mapato yanayotokana na mazao. Katika Afrika sisi Tanzania tulikuwa wa kwanza na wakati huo kwa dunia nzima, kwa mambo ya Ushirika sisi tulikuwa namba tatu, baada ya Israel na Denmark. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni kuonesha tu kwamba ushirika ni jambo zuri na jambo tunaloendelea nalo mpaka leo. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu amelishupalia jambo hili na miaka miwili iliopita ushirika umefufuka kwenye maeneo yetu. Hata

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hivyo, nataka niseme mambo machache ambayo ni kikwazo katika kuendelea kukua kwa ushirika.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni uongozi katika ushirika huu. Suala hili la uongozi ni katika ngazi zote za ushirika kuanzia kile Chama cha Msingi kwenda kwenye Wilaya na Mkoa, kuna matatizo ya kiuongozi sana. Hii ni kwa sababu viongozi waliopatikana kwenye ushirika huu ni wale viongozi tuliowarithi kutoka kwenye ushirika ule ambao ulikuwa umeharibika. Wengi wao tumewachukua na kuwaleta kwenye ushirika mpya ambao tumeuanzisha kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika ya mwaka 2013. Sasa hawa watu walioko kwenye ushirika sasa hivi walikuwa na matarajio yao kinyume kabisa na matarajio ya ushirika unavyopaswa kuwa. Kwa hiyo, hawa ndio wamekuwa tatizo kubwa kwa sababu wanachojali ni maslahi yao binafsi. (Makofsi)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba sana, hebu Serikali ijaribu kuangalia muundo wa kiungozi wa ushirika wetu kuanzia ngazi ya chini mpaka mkoa. (Makofsi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimia Mashimba Ndaki, umeeleweka. (Makofsi)

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofsi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Magereli, atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, dakika tano tano.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba nianze mchango wangu kwa kuipongeza Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, lakini sana sana Mwenyekiti wetu kwa uwasilishaji alioufanya leo ambapo ameleta kitu cha pekee kabisa, ameeleza na mafanikio na shughuli zilizofanywa na Kamati. (Makofsi)

Mheshimiwa Spika, naomba nisaidie kushangaa na katika kushangaa kwangu mnisaidie na ninyi kushangaa; na tukishashangaa, Maazimio ya Kamati yetu yaweze kuchukuliwa na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nina swal la kuuliza, hivi ni kwa nini kilimo au Wizara ya Kilimo isiwe Wizara kipaumbele? Ni kwa nini bajeti ya Wizara ya Kilimo inatolewa kwa shida sana? Kwa nini mpaka leo pembejeo ni shida sana? Kwa nini mpaka leo hatuwezi hata kujitosheleza kwa mbegu tu kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo? Kila siku tunazungumza tunasema, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa, kilimo kinaajiri Watanzani wengi, lakini tunayoyafanya kwenye kilimo haya-reflect huo ukweli tunaoujadili kila siku. (Makofsi)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo inabidi tu tufike mahali tuyachukulie very serious. Bajeti ya kilimo mpaka leo, kuanzia baada ya yale niliyowaambia mnisaidie kushangaa halafu tuchukue hatua pamoja; Bajeti ya kilimo sasa itengwe ya kutosha halafu wapewe fedha yote kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Tuepushe mambo ya mazao yetu kuozea shambani, tuepushe maziwa ya akina mama kuozea huko mashambani wanakoyakamua, twende na mkakati madhubuti wa kuandaa utaratibu ambao mazao ya kilimo yatakuwa processed, moja kwa ajili ya soko la ndani lakini ikiwezekana iwe na kwa ajili ya soko la nje.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea Wizarani, kwa sasa kuna mapitio ya Sera ya Kilimo. Naomba nilete mapendekezo yangu. Kuna suala la kilimo hai, kilimo mseto na kilimo hifadhi. Hili Mheshimiwa Mama Ishengoma amelizungumzia vizuri kwa upana, dakika zangu ni tano tu. Naomba lipokelewe, liingizwe katika sera na litajwe kwenye Sera ya Kilimo kwa asilimia 96

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya wakulima wa nchi hii ni wakulima wadogo. Kilimo hai, mseto na hifadhi ni kilimo ambacho tukiki-adopt kwa hao wakulima wadogo (peasants) tutamudu kuzalisha zaidi, kutunza ardhi yetu, kuhifadhi rutuba na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la mazao ya kilimo na mboga mboga. Unaweza kuona mwenyewe; sasa hivi mazao yetu ya biashara, korosho, kahawa, chai, pamba, yote tunazidi kuserereka kuelekea negative. Basi wakati tukiangalia nini kimetukuta huko, naomba tuhamie kwenye suala la kilimo cha matunda, mboga mboga na maua. Bahati nzuri hiki ni kati ya kilimo ambacho kinaweza kulimwa pia katika ule mfumo wa kilimo hai, hifadhi na mseto, kwa sababu mazao organic yanayozalishwa katika mfumo huo yanapata soko zuri sana kwa nchi za Ulaya kwa maana yanapokuwa exported.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati tunajadili kwa nini korosho inatusumbua, kwa nini pamba imeshindwa kununuliwa msimu huu; na bahati nzuri kilimo cha matunda na mboga mboga ni watu private wanafanya; Serikali haijawekeza huko wala hakuna ambacho kimeshafanyika kwa niaba ya Serikai kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, sasa kati ya mambo ambayo ni kikwazo kikubwa sana kwenye suala la kilimo cha matunda na mboga mboga ni hizi kodi na tozo. Nina orodha ukurasa wa 11 wa Ripoti ya Kamati mnaweza kuona. Pana tozo na kodi zaidi ya 45. Nilitamani niwasomee, lakini dakika zangu ni tano. Kwakweli katika mazingira haya, maana yake tunawavunja moyo na tuna-discourage aina hii ya kilimo ambacho ni muhimu sana kwa ajili ya maisha yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la mifugo, kwa maana ya Wizara ya Mifugo. Tulipata bahati kama Kamati....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika tano zimekwishapita. Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Lucy. Mheshimiwa Maftaha Nachuma, dakika tano.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nawapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa mawasilisho mazuri, lakini pia nawapongeza baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri wanaoshughulika na hizi Kamati za Kisekta.

Mheshimiwa Spika, nitazungumza kwa haraka haraka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nitajikita sana kwenye Sekta hii ya Utalii. Kumekuwa na mpango wa kuboresha utalii Tanzania nzima na hasa ukanda ule wa Kusini; na Serikali imejikita kwenye kukopa fedha Benki ya Dunia. Hizi fedha tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu ndani ya Bunge hili, huu ni mwaka wa tatu hivi sasa, zililetwa fedha za regrow kwa ajili ya kukuza utalii maeneo ya Kusini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hizi fedha mpaka leo henzieleweki kwamba zinapelekwa wapi? Taarifa zinaeleza kwamba wanapeleka mikoa ya kule Iringa na Mkoa wa Morogoro. Wameacha mikoa ya Kusini halisi ambayo ni Mtwara na Lindi. Kwa hiyo, tunaomba Wenyeviti watakapokuja kuhitimisha hizi hoja, hili suala watueleze kinagaubaga kwamba kwa nini mkakati wa fedha za regrow ambazo ni fedha za mkopo wa Serikali na kazi yake ni kuboresha utalii Southern Circuit, tukimaanisha Mikoa ya Kusini ambayo ni Mtwara na Lindi kwa kiasi kikubwa, bado hakuna mpango wa kuboresha miundombinu ya barabara kule. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, leo barabara ya Selous kule kutoka Nachingwea kuelekea Liwale na mvua hizi, haipitiki kabisa, lakini hizi fedha zipo, Waziri anashindwa kuzileta kwa ajili ya kuboresha miundombinu ile ili watalii waweze kupita kuanzia pale Lindi Nachingwea mpaka kule Liwale. Hizo ni fedha za regrow ambazo ni mkopo wa kuboresha miundombinu ya mikoa ya kusini katika Sekta ya Utalii, tunaomba zifike Mtwara na Lindi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kuna suala hili la utalii wa mambo kale tunaona kama limesahaulika hivi. Pale Mikindani tuna majengo ya mambo kale kule Mtwara ambayo hayapo Tanzania yote hii, yapo Mikoa ya Mtwara hasa hasa Mikindani, Mtwara na Lindi. Pia kuna ule ufukwe wa bahari amba unaanzia kule Msimbati mpaka kule Kilwa Kisiwani. Tunaomba Serikali itupe mpango maalum wa kuboresha na kutangaza yale maeneo ili tuweze kuleta watalii wengi kwa ajili ya kuliingizia Taifa hili Pato.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tuna taasisi ile inaitwa TAWA ambayo iko affiliated katika Wizara. Tulikuwa tunaomba sana, wakati fulani tuliwasikia kwenye Kamati yetu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma wakaeleza changamoto zao ni nyingi sana, lakini changamoto kubwa ni kwamba ile Taasisi ya TAWA ambayo imepewa mamlaka ya kuweza kutangaza vivutio mbalimbali vya maeneo ya Pwani, kwa mfano ule Kilwa Kisiwani, yale majengo ya kale tunaomba ipewe mamlaka kamili. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, jambo la ajabu kwenye hii Taasisi ya TAWA, kuna wafanyakazi amba walipewa *training* kwa miaka mitatu hivi sasa, wale wafanyakazi amba walipaswa kuibeba ile Taasisi ili iweze kufanya kazi sawasawa na kuwa na mamlaka kamili, wale wafanyakazi wamehamishiwa Wizarani. Sasa sijui mkakati wa Serikali ukoje wa kuhakikisha ya kwamba TAWA inapewa meno ya kutosha, inakuwa ni taasisi ambayo imesimama yenye kama ilivyo Ngorongoro na TANAPA ili iweze kujitangaza na kutangaza maeneo ya kiutalii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu TAWA imepewa maeneo ya Pwani, sisi tunaamini kwamba ingekuwa na mamlaka kamili, ingeweza kusaidia kutangaza utalii maeneo yale yote ya bahari na fukwe zote na mambo kale. Ilishawahi kusemwa hapo nyuma kwamba wanyama hawa wanaenda wanakufa, mabadiliko ya hali ya nchi, hawa wanyama watapotea, utalii utakaobaki ni utalii wa mambo kale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali isidharau mambo kale. Tunahitaji miji hii ambayo duniani yamaingiza fedha nyingi sana. Kwa mfano, kuanzia pale Mikindani kwenda kule Kilwa Kisiwani na maeneo yote ya Zanzibar, Serikali iweze kuboresha, tuhakikishe kwamba inaboresha miji hii na inaitangaza ili tuweze kuingia fedha nyingi za utalii. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, tunaomba sana kwenye Sekta ile ya Uvumi, basi tumekuwa tunazungumza kwenye Bunge hili kwa muda mrefu iweze kutengwa bahari ya uvumi. Sasa imekuwa ni historia tu kila siku inazungumzwa kwamba ile bandari ya uvumi haijengwi. Wizara haitengi fedha, Waziri hatengi fedha.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumebarikiwa, Wazungu wanasema Tanzania ina virgin sea (bahari bikira), ina samaki wengi sana, kuanzia ile strip ya Kusini kule mpaka Zanzibar, hakuna bahari ya uvumi. Tunaomba Serikali mwaka huu ije na mkakati maalum kuweza kutenga bandari ya uvumi ili wavuvi wetu waweze kuvua na kuwa na masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa dakika za nyongeza. (Makofij)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Salum Rehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mafia.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kupata fursa hii japokuwa muda ni mchache. Napenda kuchangia zaidi, eneo la kwanza ni eneo la mbegu. Bado nchi yetu na Wizara hasa hatujawa serious kwenye mbegu. Nchi inapoteza fedha nydingi kwa ajili ya uagizaji mbegu.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo sasa hivi, tulitarajia na Waziri alikuja katuambia hapa tunategemea kwamba tungeweza kujitosheleza kwa mbegu kwa asilimia 20 mpaka 30, lakini hali ilivyo kwa nchi yetu tumeweza kutoa mbegu siyo zaidi ya asilimia 19. Hivyo nchi imetumia zaidi ya trilioni 1.8 kuagiza mbegu kutoka nje. Maeneo tunayo, watafiti wapo, vituo viro, tatizo hatujaamua kuwekeza katika eneo hilo. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla iangalie katika eneo ambalo tunapoteza pesa nydingi wakati uwezo wa kuzikabili hizo changamoto upo.

Mheshimiwa Spika, kingine katika eneo hilo, kuna tafiti ambazo zinahitajika ziweze kuendelea. Ile mbegu ya pamba tunayoendelea nayo mwaka huu ni wa mwisho, tunatakiwa tuwe tumetoa mbegu nydingine ambayo itachukua mbadala wake, kwa sababu ikiendelea kuzalishwa ile, huko mbele haitakuwa na mavuno yoyote, itakuwa imeshamaliza muda wake wa uzalishaji. Sasa sijui Wizara na Bodi ya Pamba ina mkakati gani katika eneo hilo. Naiomba Wizara tuangalie zaidi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la pareto. Hapa kuna changamto hasa kwenye Bodi ya Pareto. Viongozi ni tatizo kubwa na ndiyo maana Sekta ile haiendi mbele. Bado tumewaruhusu baadhi ya watu ambaao wanununa zile pareto zinakwenda kuchakatwa nje ya nchi, wakati mikataba ya kununua pareto tunataka kuiona ile crude oil inatoka hapa na kunufaisha watu wetu ndnai ya nchi wapate ajira lakini tupate raw material ambayo tunaweza kuitumia kwa uzalishaji wa vitu mbalimbali. Sasa leo mchakato wa umalizaji wa pareto unaenda kufanywa Kenya kwa sababu ipi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri hapa aje na majibu, atueleze sababu ni zipo wakati mikataba haiko hivyo? Ni kiwanda kimoja tu ambacho kinachakata hiyo crude oil na inapatikana hapa na tunauza na kuweza kupata faida na kodi zinatozwa. Kwa hiyo, tunaona tatizo ni Bodi ya Pareto na usimamizi wake bado umekuwa ni tatio kubwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa sababu ya muda, bado tunarudia tena kwenye Sekta ya Uvuvi, hatunufaiki. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuifanya kazi 0.4, kule Zanzibar imeanza kuleta matunda. Juzi tu baada ya mwezi mmoja na nusu baada ya kuruhusu ile 0.4 ambayo ni probation period, zaidi ya meli 27 zimeshasajiliwa na tunatarajia meli nydingine zaidi ya 60 zitawenza kusajiliwa, hivyo kuifanya ile Mamlaka ya Uvuvi iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi lilitokuwepo, kuna akiba kubwa ya samaki ambaao sasa hivi wanahitaji kuvuliwa. Ni eneo la buffer zone ambalo lipo baina ya Msumbiji na Mtwara. Eneo lile lina samaki wasiopungua zaidi ya milioni 50 wa tuna wazee walioko kwa miaka zaidi ya minne, mitano, wanahitaji kuvuliwa kwa percent maalum ambazo sisi kama nchi tungeingiza pesa nydingi tukaingia udau na wale ambaao watavua kwa sababu sisi hatuna vyombo vya kuvulia. Samaki wale sasa hivi wanakula samaki wadogo wanaozaliwa katika eneo lile. Tunahitaji tuweze kuiwekeza katika eneo hilo, tuwavue.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni ombi. Wenye meli kubwa wakitaka kuleta ombi hilo kwa kuvua, tuwaruhusu kwa sababu akiba tuliyokuwa nayo katika eneo letu hilo la mazalio ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

samaki kutoka Kizimkazi, Kitutio Mafia mpaka Mtwara ni zaidi ya milioni 70 ya samaki wako katika eneo lile, wanatosheleza kabisa. (Makof)

(Hapa kengele *ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rehani. Kuna wakati huwa nashangaa kule Kamati ya Mambo ya Nje unafanya nini? Naona huku ndiyo una-fit zaidi. Ahsante Mheshimiwa Rehani. (Kicheko)

Sasa Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mbunge wa Mafia.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nami nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wote wawili kwa mawasilisho mazuri. Nitakwenda kwa haraka kutokana na tatizo la muda.

Mheshimiwa Spika, nianze pale alipoishia Mheshimiwa Rehani, kuipongeza sana Serikali, Mawaziri wote wawili wa uvuvi upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara kwa kuondoa 0.4. Tumeanza kuyaona matunda. Pia nawe binafsi tunakushukuru kwa sababu mara ya mwisho tulipolzungumza hili jambo ulitia maneno yako na ninaamini Mawaziri wameyafanyia kazi na sasa tayari meli zimeshaanza kuja na tunapata mapato kama alivyosema Mheshimiwa Rehani.

Mheshimiwa Spika, nataka niendelee mbele kidogo kwamba Mawaziri wanasema wamesitisha kwa muda. Sasa ni muda muafaka sasa wakakaa wakaamua kama wanaifuta kabisa ama wanapunguza kiwango ama wanafanyaje ili hili jambo tulimaliza once and for all.

Mheshimiwa Spika, la pili, nilitaka nizungumze kidogo kuhusu suala la mkanganyiko wa matundu yale ya nyavi. Kuna sheria mbili hususan kule Mafia. Tuna sheria ya Hifadhi ya Bahari na tuna Sheria ya Uvuvi. Sheria hizi mbili zina mkanganyiko. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, alikuja Mafia ametusaidia kwenye eneo la dagaa. Tayari mgogoro kule umekwisha, lakini kwa sasa bado tuna mgogoro kwenye eneo la samaki. Sheria hizi mbili bado zinaendelea kugongana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi ili tumalize na hili tuweze kusonga mbele. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi atakubaliana nami, maeneo ya kuvua samaki wengi unatakiwa uende kidogo maeneo yenyе kina kirefu. Sasa kwa bahati mbaya Wizara inazuia matumizi ya cylinder gas ya kuweza kuzamia chini kwa ajili ya madivers kwa sababu wanasema kwamba wanaenda kuchukua majongoo bahari. Sasa watu wanapokwenda kuvua kwenye kina kirefu cha maji bila kutumia msaada wa gas cylinder tunawa-condemn to death. Tunaomba sana mliangalie hili, mlifanyie kazi ili kuruhusu wananchi hawa waweze kuvua kwa kutumia gas cylinder. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la viboko. Mheshimiwa Waziri wa Utalii naomba anisikilize. Mwaka 2019 alituambia viboko wa Mafia watakwenda kupigwa mnada. Sasa hivi wameshafika 40 na wameshaanza kuingia mijini.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utalii mje muwaondoe wale viboko Mafia kabla madhara makubwa hayajaendelea kufanyika. Mpaka sasa mtu mmoja ameshafariki, ng'ombe kadhaa wameshauawa na mazao yamekuwa yakiliwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Channel ya Utalii. Mheshimiwa Kanyasu mwaka jana hapa ulijibu swali langu kuhusiana na Channel ya Utalii kuja

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutangaza vivutio vya utalii kule Mafia vya samaki aina ya Potwe na vitu vingine ambavyo vinavutia kule Mafia lakini mpaka leo hili jambo halijatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Mafia ni sehemu ambayo ni ya kimkakati kabisa kiutalii, tungeomba sana Channel yetu ya utalii, ile ambayo inaoneshwa kwenye TBC waje kule wafanye shooting vivutio vile viweze kuonekana. Huyu samaki aina ya potwe tunamzungumza sisi tu humu ndani, watu wengi hawamjui, pengine hata Watanzania wengi nao pia hawamjui. Kupitia Channel yetu ile tunaamini kabisa mkitangaza tunaweza samaki yule akajulikana na vivutio vingine vinavyopatikana pale Mafia vikajulikana, ikatusaidia sana katika kuongeza mapato. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kilimo cha Mwani; Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi mwani Mafia unalimwa na kina mama kule baharini. Tunaomba sana, wakulima wa mwami hawana vifaa, utaalalm, hajawahi kuja mtaalam yoyote kutoka Wizara ya Uvuvi kuja kuwapa semina au maelezo yoyote kuhusiana na kilimo cha mwani kule Mafia.

Mheshimiwa Spika, amezungumza hapa Bobali kuhusu zao la nazi na kwamba zao la nazi linapendezesha sana chakula kwa watu wa Pwani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Dau dakika tano zimeisha...

MHE. MBARAKA K. DAU: ...lakini...

SPIKA: Dakika 5 zimeisha Mheshimiwa Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya kamati, nashukuru sana. (Makof)

SPIKA: Sasa Waheshimiwa tuhamie kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri, tujaribu kupata dakika saba saba. Tujitahidi dakika saba saba, watapiga ile ya dakika tano kwanza halafu watakupigia ile ya mwisho ya dakika ya saba. Tuanze na Mheshimiwa Waziri wa Maji, atafuatia na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kuchangia hoja hii. Karibu sana Naibu Waziri Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa namna ya kipekee nimpongeze sana sana Mheshimiwa wa Kamati yetu ya Mifugo pamoja na Maji Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa pamoja na wajumbe wake wamekuwa wakifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kutushauri sisi Wizara yetu ya Maji, wamekuwa msaada na wala hawakuwa kikwazo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwashakikisha Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo kwa Kamati yetu katika kuhakikisha tunaleta maendeleo makubwa sana katika sekta yetu ya maji. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kujibu hoja chache sana. Moja, kuhusu hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga kaka yangu Hamidu Bobali kuhusu suala zima la uvunaji wa maji ya mvua, kwamba lita zitakazozidi elfu 20 unatakiwa ulipie; nataka niweke sawa taarifa. Kwa mtu ambaye anavuna maji ya mvua lita zaidi ya elfu 20 hatakiwi kulipa chochote kama anatumia matumizi ya nyumbani. Hata kama ikitokea anatumia kwa matumizi mengine, ada yake ni shilingi laki moja tu lakini hii yote ni katika kuhakikisha tunalinda na kutunza vyanzo vyetu vya maji. (Makof)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, imezungumzwa hapa na dada yangu ambaye ninamheshimu sana, Mheshimiwa Ester Bulaya, kuhusu suala zima la mradi wa maji wa Bunda. Nimeshtuka kidogo akiwa kama Mnadhimu kutoa taarifa ambazo binafsi zimenishtusha sana. Nikiri kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika Bunda na akatoa agizo kutokana na athari ya baadhi ya miradi ya maji iliyokuwa ikisuasua na hata baadhi ya wataalam wetu, kwa maana ya kushirikiana kuhujumu miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, yule mkandarasi Nyakirang'anyi alikamatwa na hatua ambazo tulizichukua sisi kama Wizara; tukasema mradi ule tunaukamilisha kwa kutumia wataalam wetu wa ndani. Fedha ambazo zilitakiwa kukamilisha mradi ule zilitakiwa kiasi cha shilingi milioni 375 lakini wataalam wetu wa ndani wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Musoma wamefanya kwa force account kwa shilingi milioni 200 na mradi umekamilika mwezi Desemba mwaka jana, Mheshimiwa nakupa taarifa hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, na mimi kama Naibu Waziri wa Maji nimeshafika na Waziri amekwishafika, na nipo tayari kwenda kuongozana na wewe Bunda kukuonesha kazi nzuri ya llani ya Chama Cha Mapinduzi ilivyotekelawa katika eneo lako la Bunda. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka kusema, nataka nimjibu Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Mheshimiwa Haonga. Wakati mwingine unapojenga hoja hebu jirdhishe basi kidogo kazi zilizofanywa. Amezungumza kwamba kazi ya miradi ya maji, sisi pale katika Jimbo lake tuna mradi wa milioni 550 tumeshalipa pesa zaidi ya milioni 500. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tumeshapeleka fedha ambazo tumepata kupitia fedha za P4R zaidi ya bilioni 119 ambazo zimetengwa kwa mikoa 17 na Halmashauri 86 ikiwemo Halmashauri ya Mbozi ya Mheshimiwa Haonga zaidi ya bilioni 1.3 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, kubwa Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekeleza miradi ya maji maeneo yote bila ya ubaguzi wowote. Sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatulali, usiku na mchana katika kuhakikisha tunaisimamia na kuifuatilia miradi yetu ya maji ili wananchi waweze kupata huduma ya maji. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka niwaambie wakandarasi na wataalam wa maji vipo vitu vyta kuchezea, ukishiba unaweza kuchaze kidevu ama tumbo lako, kwa maana ya kitambi; lakini kwa yeote ambaye atakayetaka kuchezea miradi ya maji, sisi hatupo tayari tutashughulikiana ipasavyo katika kuhakikisha tunajenga nidhamu katika miradi yetu ya maji. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tangu Wizara ya Maji ianze kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, tangu 2006 mpaka sasa tumeshatekeleza miradi 2,450. Hata hivyo Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli tangu aingie 2015 mpaka Desemba mwaka jana tumeshatekeleza miradi 1,423. Miradi 792 imekamilika na miradi 600 ipo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji, na tumeshajipanga katika kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati ili azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mwanamama ndoo kichwani, kwa maana ya asilimia 85 ya upatikanaji vijiji na asilimia 95 ya maji mijini.

Mheshimiwa Spika, tuna miradi mikubwa ambayo itaongeza hali ya upatikanaji wa maji. Leo ukienda Arusha mradi wa zaidi ya bilioni 520 unatekelezwa, ukienda Orkasmet pale zaidi ya bilioni 30 mradi unatekelezwa. Ukienda Longido zaidi ya bilioni 16 ya mradi umekamilika, Tabora, Igunga, Nzega zaidi ya bilioni 600 ule ni mradi wa standard gauge/Stierglers mfano katika kuhakikisha tatizo la maji na vijiji zaidi ya 102 vitawenza kupatiwa huduma hii ya maji. (Makof)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge pia katika Miji 28 na ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, malizia Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: ...ambapo tumepewa fedha zaidi ya dola milioni 500. Nataka niwape taarifa kwamba kibali tumechapata vya Exim Bank, tunajipanga katika kuhakikisha tunatangaza tenda ile ili mkandarasi apatikane ili azma ya Mheshimiwa Rais kwa maana ya miji 28 miradi ile inatekelezwa na wananchi waweze kupata huduma ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, asante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Aweso, Naibu Waziri Maji tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge mtaona mwanga hautoshi sana ndani ya ukumbi hasa kwa sababu ya ile round pale juu ambayo taa zake takriban zote zimezima, lakini pia upande wangu wa kushoto taa nydingi zimezima. Baadhi yake zitafanyiwa kazi usiku huu; lakini kuna mtihani mkubwa sana wa kufika pale juu, sijui tutampata wapi Msukuma atakayeweza kutusaidia kuning'inia kama popo pale. Ni kwa sababu ya mvua kubwa imesababisha short kidogo baadhi ya maeneo, kwa hiyo tuvumiliane waheshimiwa Wabunge. (Kicheko)

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, karibu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, dakika saba.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii na mimi niungane na wenzangu kwanza kuzipongeza kamati zote mbili ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvubi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na ushauri wa kina ambao wametupatia katika Wizara yetu, kwa kweli tunawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kilimo ndio uti wa mgongo na tunafurahi kupata michango ya Wabunge wengi ambayo imechangiwa kwa kiwango kikubwa sana; na sisi tunasema kwamba tunapokea michango yote, tutaendelea kuifanya kazi na baadae tutaona namna tutakavyoweza kutoa majibu hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa sekta ya kilimo inachangia kwa kiwango kikubwa sana katika Pato la Taifa. Inachangia takribani asilimia 28.7 katika Pato la Taifa Ina pia inachangia asilimia 65 mpaka asilimia 75 ya ajira mbalimbali ambazo watu wameajiriwa. Vilevile inachangia kwa asilimia 66 katika malighafi za viwandani, na pia tunachangia kwa asilimia 100 ya chakula chote na lishe tunachopata katika nchi hii; lakini zaidi ya hapo kilimo kinachangia kwa asilimia 30 ya fedha zote za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na mazingira yaliyopo tuna uwezo wa kuongeza uwekezaji katika kilimo na kikaweza kutoa mchango mkubwa zaidi kuliko hizi takwimu zilivyo hivi sasa. Kwa hiyo, pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zipo lakini ni wajibu wetu sisi sote kuungana kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba tunaondoka katika kilimo cha kujikimu kwenda katika kilimo cha kibiashara. Pia tutoke hapo tulipo ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaondokana na tija ndogo na tunapata tija kubwa ili mazao mbalimbali yaweze kuzalishwa vya kutosha.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuweze kufikia hapo kuna mahitaji mengi ambayo tunayahitaji na ambayo Serikali imekuwa ikiyafanyia kazi na wajumbe wengi wamechangia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la mbegu. Ni kweli kumekuwa na takwimu ambazo zimetolewa na Wabunge mbalimbali juu ya mahitaji ya mbegu. Kama nchi mahitaji ya mbegu kwa sasa hivi ni tani 187,500; na ninaomba takwimu hizi zikae vizuri. Katika hizi tani 187,500, zinazohitajika kwenye nchi, mbegu ambazo zimepatikana kwa msimu huu mwaka huu ni tani 71,207 na kati ya hizo tani 66,033 sawa na asilimia 93 zimezalishwa ndani, hizo zimezalishwa hapahapa ndani, hazikutoka nje.

Mheshimiwa Spika, mbegu zilizotoka nje ya nchi ni tani 5,175, sawa na asilimia saba tu ya mbegu zote zilizopatikana hapa nchini; na hapa mbegu tunazozisema tunaachia mbali zile mbegu kama pingili za mihogo, miwa, chai, korosho, miche ya kahawa, yote hapa hatujayahesabu; ukihesabu na hiyo ambayo ipo zaidi ya milioni 22 maana yake uwezo wa taifa wa kuzalisha mbegu ni zaidi ya asilimia 96. Kwa hiyo, tunachotegemea nje ni kidogo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tunachosema sisi katika yale mahitaji ambayo tunayasema, kwa sababu upatikanaji ni tani 71,000 maana yake wananchi wengi bado wanaendelea kutumia mbegu za asili, ndizo zinazotumika, lakini si kwamba zinatoka nje. Lakini tunakubaliana na maoni ya wajumbe kwamba tunahitaji kuwekeza zaidi ili kuhakikisha kwamba mbegu zizalishwe wakati wa kiangazi, tuimarishe skimu zetu kusudi tuweze kupata mbegu za kutosha.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni mahitaji ya mbolea. Ni kweli kabisa mwaka huu mvua imenyesha vizuri sana katika maeneo mengi na mahitaji ya mbolea yameongezeka kwa kiwango kikubwa kwa sababu wananchi wengi wamehamasika katika kulima. Mahitaji ya mbolea ni tani 586,000 kwa mwaka lakini upatikanaji mpaka sasa hivi tunapoongea leo ni tani 454,339 ndizo zimepatikana. Katika hizo zipo mbelea aina ya DAP ambazo ni tani 71,000 na urea tani 121,000.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kumekuwa kidogo kuna upungufu wa UREA, mbolea zingine zote zipo, UREA ilipungua. Tulichokifanya ni kuhakikisha kwamba tunaagiza. Hivi ninavyoongea kuna tani 43,000 zipo bandarini na tani 222,000 zipo njiani zinakuja. Lengo ni kutaka kuhakikisha kwamba tunakuwa na mbolea ya kutosha ili ziuzwe kama nguo zinavyouzwa hapa nchini. Kwa hiyo, mbolea zitakuwepo za kutosha bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, huu upungufu uliojitokeza ni kwa sababu yule ambaye tulimpa zabuni ya ku-supply kwa mtindo ule wa ununuzi wa pamoja alichelewa kuagiza na hivyo akachelewesha kidogo ndiyo maana tukawa na upungufu wa aina moja ya mbolea, lakini zingine zote zinapatikana kwa wingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya viuatilifu ni mengi na kweli Wabunge wamechangia kwa kiwango kikubwa na sisi tunasema ni kweli kabisa tunahitaji viuatilifu vya kila namna, utafiti tutafanya na maeneo mengine yoyote tutayarekebisha.

Mheshimiwa Spika, najua kwa sababu ya muda haukuweza kutosha, tungeweza kujibu maswali yote lakini tutaweza kuwajibu Wabunge na tutaleta mbele ya Bunge lako Tukufu, ahsante sana. (Makofii)

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nakushukuru sana. Sasa nimuite Waziri wa Mifugo na Uvuvi na atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili. Mheshimiwa Waziri Luhaga Mpina.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa nafasi na vile kwa muda mfupi huu kuweza kuchangia na mimi kidogo katika taarifa ya hao Wenyeviti wawili; Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mwenyekiti wa Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti hawa wote wawili, hoja zao ni nzuri. Niwapongeze Kamati yangu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa muendelezo wao uleule wakuendelea kutusimamia vizuri sana sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kuwezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri sana hapa Bungeni lakini na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii ya muda mfupi napenda kusemea baadhi ya maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wametupongeza sana kwa jithada tulizofanya za uwekezaji wa viwanda hapa nchini lakini wakaona kwamba kama vile tunaenda kwa spidi ndogo sana katika kuboresha mifugo yenye na katika kuhakikisha kwamba mifugo hii ipo salama na inazalishwa na inakua vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumefanya mambo makubwa pia ya kuhakikisha kwamba tunapambana na magonjwa. Sasa hivi utakubaliana na mimi kwamba nchi nzima sasa hivi katika kipindi tu hiki cha nusu mwaka tayari tunakamilisha ukarabati wa majosho 449. Kama hiyo haitoshi tumepeleka dawa za kuogesha kwenye Wilaya zote kwenye majosho yote 1,725 ambayo tayari nchi nzima wanaogesha mifugo kwa ruzuku ya Serikali. (Makofiji)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi tumefanya mambo mengi kama ambavyo yamezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa mfano, kuongezeka kwa maeneo ya malisho, leo maeneo yetu yameongezeka kutoka 1,400,000 mpaka leo tumefikia maeneo yaliyotengwa hekta 2,800,000. (Makofiji)

Mheshimiwa Spika, na bado Serikali ikaenda mbali zaidi ikamega mpaka mashamba yake ya Serikali kwa ajili ya kuwagawia wafugaji na wakulima kwenye vijini 920 na imeelezwa kwenye kumega misitu na mapori ya akiba, imeelezwa kwenye kumega mashamba mpaka ya Serikali ya NARCO na mashamba mengine ya taasisi zetu. Hizi zote ni jithada za kuhakikisha kwamba wafugaji wa nchi hii wanapata maeneo mazuri ya kufugia na wanafuga vizuri. (Makofiji)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la uvuvi wa bahari kuu. Waheshimiwa Wabunge katika hili msiwe na mashaka, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga vizuri kufanya kazi hiyo na ndiyo maana Shirika la TAFICO tayari limeshafufuliwa, mpango wa biashara umeshaandaliwa wa kununua meli na kuanza shughuli za uvuvi wa bahari kuu. Na kama hiyo haitoshi bandari ya uvuvi tayari upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea na tupo kwenye hatua za mwisho na tayari tuende kwenye hatua za kujenga.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, tayari Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi Na. 1 ya Mwaka 1998 tumeifuta ili kuleta na kuwavutia watu mbalimbali waliokua wanakwazwa na sheria kuja kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya makokoro yataisha lini. Kuna changamoto, bidhaa za nyuzi hizi zinapoingia nchini zinakuwa ni halali lakini zinapokuja kutengenezwa, wavuvi wetu wanapokuja kusuka nyavu sasa wanaweza kusuka kokoro; lakini nyavu inapoingia nchini ni halali kama nyavu tu (*raw material* kwa ajili ya kutengeneza bidhaa). Kwa hiyo, hiyo ni tatizo kubwa na hili limetusababisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kukaa na wenzetu wa TBS pamoja

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watafiti wetu wa *TAFIRI* ili kutafuta namna bora ya kusimamia hili eneo. Kwa hiyo, tuna imani hivyo tutafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la hizi nyavu ni kwamba kila maeneo yana nyavu tofauti ya kuvulia kulingana na aina ya samaki waliopo kwenye eneo hilo. Samaki waliopo Bahari ya Hindi ni tofauti na samaki waliopo Ziwa Tanganyika, ni tofauti na samaki waliopo Ziwa Victoria, kwa hiyo hata nyavu zake nazo pia ni tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hapa kuna maneno mengine yalizungumzwa ya kwamba wananchi wanahitaji maji, hawahitaji ndege. Waheshimiwa Wabunge hivi hayo maji mnaenda kuyajenga bila ya kuwa na fedha? Miundombinu ya ndege inaponunuliwa nchini inawezesha uchumi kukua, mazao yetu ya samaki leo, samaki atavuliwa saa 2 Ziwa Victoria anaenda kuliwa saa 4 Zimbabwe. Samaki atavuliwa hapa Dar es Salaam saa 12 asubuhi kufikia jioni analiwa India; huu ndio uchumi wa nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa unapozungumza kwa ajili ya kujifurahisha kwamba eti wananchi wanahitaji maji hawahitaji ndege, huwezi ukaondoa mahitaji muhimu ya wananchi katika kupatikana kwa ndege. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo hii Ziwa Victoria tunavua kila siku tani 250, kwa hiyo unahitaji ndege za kubeba samaki tani 250 kila siku. Leo samaki wetu hao wanabebwa Uganda, samaki wetu hao wanabebwa Kenya, tungekuwa na ndege zetu – na ndiyo maana Waziri wa Uchukuzi nimemwambia piga, garagaza, ua lazima tununue ndege zetu za kusafirisha mazao yetu. Tani 250 kwa maji moja, hujaenda Tanganyika, hujaenda Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi, la mwisho labda ni hili Mawaziri, kwa sababu yanazungumzwa maneno hapa mengine ni vizuri kutolewa *clarification*. Mtu anasema tu hapa Mawaziri amba ni wasimamizi wa sera wanafanya mambo ya *operation*, nadhani alikuwa anazungumza kutofautisha *operational* na *oversight*. Lakini tangu lini wewe mtu wa *oversight* utafanya shughuli zako za *oversight* bila kwenda kwenye maeneo unayoyasimamia. Ni tangu lini wewe msimamizi utafanya ukiwa ndani mambo ya kisera, unasema nafanya mambo ya kisera unajifungia chumbani, utashindwa kwenda kwenye maeneo ya uvuvi, utashindwa kuonana na wavuvi, utashindwa kwenda kuwaona wafugaji, utashindwa kwenda kwenye maeneo eti wewe unatunga sera. Sera hizi utazitungia ukiwa wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri kama ukiwa huna la kuchangia unaacha tu, sio kusimama hapa na kupoteza muda wa nafasi na muda wako. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri nakuongeza dakika tano. (MakofiVigelegele)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa ongezeko hilo.

Mheshimiwa Spika nataka niweke mambo vizuri hapa; kuna suala la *oversight function*, kuna suala la *operation function*. Kama wewe ni *oversight* utawezaje kuwa *oversight* bila kukaa na hawa *operational*? Kama wewe ni *oversight* utawezaje kufanya kazi yako ya *oversight function* bila kwenda kwenye *operational sight*? Haiwezekani! Ni mambo ambayo unazungumza kama huyajui au kama umeambiwa nje unakuja nayo hapa Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka niwaambie, Serikali ya Awamu ya Tano kama mtu yeyote anatafuta eti kutupotezea uelekeo...

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa hoi kabisa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Kama mtu yeyote anatafuta kutupoteza uelekeo, kama mtu yeyote anatafuta eti kutukatisha tamaa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ilishakataa katakata kukatishwa tamaa na mtu yeyote yule. Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ilishakataa katakata kukatishwa tamaa na mtu yeyote. (Makofi/Vigelegele)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

WABUNGE FULANI: Aaaaa!

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, endelea.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukieleza hapa ni kwamba watu wajue katika taarifa hii ya Kamati kuna mambo makubwa yaliyoelezwa hapa. Nilitegemea Wabunge wakayaona hayo. Leo mapato ya uvuvi...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, naomba tusikilizane; mlipokuwa mnawapiga Mawaziri hapa wala hawakusema kitu...

WABUNGE FULANI: Ndiooo!

SPIKA: Sasa wanapojobu naomba na ninyi mtulie, ndiyo kuwa na ngozi ngumu, tulieni.

Mheshimiwa Waziri, endelea.

MBUNGE FULANI: Tulieni mpapaswe!

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeongea mambo mazuri sana ambayo leo wastani wa makusanyo ya Wizara ya Sekta ya Mifugo na Uvubi yalikuwa bilioni 21, leo yamefika bilioni 72. Fedha hizi zimeenda kwenye elimu, fedha hizi zimeenda kwenye maji, fedha hizi zimeenda kujenga miundombinu ya maji ya wananchi. Mauzo yetu ya samaki nje ya nchi yameongezeka kutoka bilioni 379 hadi bilioni 691; hiyo ni Serikali ya Dkt. Magufuli imeyafanya hayo. Tulitegemea Mbunge badala ya kwenda kwenye vitu vidogovidogo hivi angesema mambo haya makubwa yaliyofanyika ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, tumepongiza manunuzi ya samaki nje ya nchi. tulikuwa tunanunua samaki nje ya nchi kwa thamani ya bilioni 56 kwa mwaka. Leo tunafika hapa mwaka mzima manunuzi yetu ya samaki nje ya nchi ni milioni 37, fedha hizo ziko hapa kwa Watanzania, bilioni 56 zinaliwa na Watanzania leo, zinaliwa na wavuvi hawa, ni Serikali ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Spika, nataka niwathibitishie Watanzania wote na Wabunge kwamba Serikali ya Awamu ya Tano tumejipanga na tutahakikisha kwamba kero zote za Watanzania tunazishughulikia. Tutaenda site moja baada ya nyininge, tutaenda maeneo yote kuhakikisha Tanzania na matatizo ya Watanzania yanaokolewa, kuhakikisha kwamba tunafuta, kuhakikisha kwamba Watanzania ambaa wamelia muda mrefu tunafuta machozi yao, tunakwenda kupangusa machozi ya Watanzania wote walioteseka na kunyanyaswa muda mrefu, na tupo kwa ajili ya kufanya hiyo kazi. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Msigwa shati ulilovaa, hilo shati...

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, dakika saba.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, nianze kwanza kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili ambao wametoa hoja hapa Bungeni leo hii. Lakini niishie palepale alipoishia Mheshimiwa Mpina kwamba Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliteuliwa na Mwenyezi Mungu mwaka 2015 kuja kuwafuta machozi Watanzania. Na ye ye kwa mamlaka aliopewa na Mwenyezi Mungu akaunda Serikali ambayo ina mtazamo huo na ambayo inaendelea na zoezi la kuwafuta machozi Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Uhifadhi – wewe ni shahidi – Serikali ya Dkt. Magufuli imewafuta machozi wafugaji ambao walikuwa na migogoro mikubwa na maeneo ya hifadhi. Imewafuta machozi wakulima ambao walikuwa wanaishi bila amani ndani ya mipaka ya nchi yao kwa kuwa wamejikuta wapo katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, leo hii migogoro baina ya wananchi na sisi wahifadhi imepungua sana, na yote hii ni kutokana na utendaji na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mheshimiwa Rais ametutuma twende kwa niaba yake tukawafute machozi hawa wananchi. Hatuwezi kukaa ofisini tukategemea tutaweza kutatua migogoro inayowasibu wananchi bila kufika site. Iwe tutaonekana ni watendaji na sio watunga sera ama wasimamizi wa sera, potelea mbali, Cha muhimu tumewafuta machozi wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika miaka hii minne ya uongozi wa Dkt. Magufuli, mapato kwenye Sekta ya Utalii yamekua kutoka trilioni 3.8 mwaka 2015 mpaka trilioni zaidi ya 6.5 mwaka 2018. Idadi ya watalii imeongezeka kutoka milioni moja mwaka 2015 mpaka milioni moja na nusu mwaka 2018, matarajio yetu ni kwamba tutakapokuwa tunatoa takwimu za mwaka 2020 ambapo Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli na Serikali yake watakuwa wanamaliza muhula wa kwanza wa uongozi wa taifa letu, tuwe tumefikisha idadi ya watalii milioni mbili.

Mheshimiwa Spika, na mafanikio haya yamechangiwa na vitu vingi, na mtu atakayebeza kwa kiongozi wa aina yangu sipaswi kumjibu hata kidogo kwa sababu nitaanza ku-question uwezo wake, uelewa wake na uzoefu wake kwenye sekta hii, jambo ambalo kwa heshima niliyonayo na ninayopenda kumpa Mbunge mwenzangu, sipendi kulifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika miaka hii minne ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, tumeweza kudhibiti mapato yanayotokana na Sekta ya Utalii kwa kiasi kikubwa kwa kupitia kutengeneza mfumo fungamanishi wa kukusanya mapato ujulikanao kama MNRT Portal ambayo sasa inaendelea kuwekezwa kwenye taasisi zote ambazo zinakusanya mapato kwenye Sekta ya Uhifadhi na Utalii kwa ujumla wake. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeweza kuendeleza na kukuza jitihada zetu za kutangaza vivutio vya utalii ikiwemo kutumia maonesho maarufu kama Karibu Kili Fair, Karibu Kusini ambayo ilifana sana, kwao na Mheshimiwa Mch. Msigwa kule, na sasa tunaanzisha maonesho mapya ya Kanda ya Ziwa yajulikanayo kama GLITE (Great Lakes International Tourism Expo) ambayo yatakuwa yakifanyika Mwanza kwa mara ya kwanza mwaka huu mwezi wa sita. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hiyo tumekuwa tukitumia watu mashuhuri kutangaza vivutio vya utalii. Watu mashuhuri wapo ndani ya nchi na nje ya nchi, kwa malengo ya kukuza utalii wa ndani lakini pia wa nje ya nchi. Wamedhihakiwa hapa wasanii ambao tumekuwa tukiwatumia kutangaza vituo vya utalii. Sipaswi kuwajibia lakini ninapenda nieleze kwa ufupi tu concept ya kutumia *influencers* ama watu mashuhuri kwenye kutangaza katika zama hizi za sasa.

Mheshimiwa Spika, mfano msanii mmoja kama *Diamond Platinumz*, Nasibu Abdul. Ana wafiasi milioni 8.6 kwenye akaunti yake moja ya *Instagram*, anajulikana Tanzania kwa kiasi kikubwa, anajulikana Afrika Mashariki, Afrika yote na nchi mbalimbali huko duniani, na hivi ninavyozungumza hapa anafanya tour ya kutangaza muziki wake, kuuza muziki wake nchi za Ulaya, baada ya kumaliza tour nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, mtu huyu anafuatihi kwa ukaribu sana na kwa raha za vijana ambao ni chini ya miaka 35, anafuatihi kwa ukaribu kuliko hata mimi na Mheshimiwa Mch. Msigwa. Maana yake akiweka kivutio cha utalii ama experience ambayo ameipata akiwa kwenye kivutio fulani cha utalii maana yake takribani watu milioni 8.6 wana fursa ya kufikiwa na huo ujumbe, na huo ujumbe atakaouweka katika ukurasa wake utadumu kwa muda mrefu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, na kizazi ambacho tunaki-target katika zama za sasa, hususani ukiwa kiongozi visionary ni kwamba tunawatazama watoto wetu, wadogo zetu na vizazi vitakavyokuja kwa sababu sisi hatuna *tradition* ya kwenda kutalii, hatuna *tradition* ya safari na vitu kama hivyo. Sasa ili tuweze kuwafikia kizazi hicho, hatuwezi kupenyeza ujumbe wa vivutio tulivyonavyo kwenye *television*, kwenye magazeti na *all these other traditional media*, ni lazima tutumie new media ambapo ndipo watoto wetu, wadogo zetu wapo huko.

SPIKA: Malizia Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, tukubaliane tu kwamba watoto wa sasa hivi wanatumia mitandao ya kijamii kupata taarifa zaidi kuliko chombo chochote kile kingine cha habari. Kwa hiyo, kwa maana nyininge wanawafutilia hawa watu mashuhuri. Kwa hiyo, tukiwatumia hawa tuna uhakika taarifa zitafika kwa walengwa kwa haraka zaidi na kwa uhakika zaidi kuliko tukitangaza kwa kutumia njia hizi ambazo tumezizoea. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono Hoja za Kamati zote mbili. Ahsante. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi ajiandae kuja kuhitimisha hoja yake; Mheshimiwa William Lukuvi tafadhali.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nianze kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili na zaidi Kamati yangu ya Ardhi na Maliasili. Nakubali kwamba tumepokea ushauri wao waliotushauri.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme mambo mawili; la kwanza nianze na *National Housing*. Kamati imeshauri juu ya mapendekezo yao ya ukamilishaji wa miradi ile mikubwa ya *National Housing*. Nataka kuwashakikishia kwamba miradi ili itakamilika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema juzi mimi nilifanya uamuzi wa kusimamisha ukopaji wa zile fedha makusudi kwa sababu tulitaka kujiridhishe mambo fulani. La kwanza hatua ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwanza nimeunda bodi mpya yenye ueledi yenye uwezo wa kusimamia, lakini kazi ya pili ya bodi ile nimewapa ni kuhakiki ile miradi na mikataba. Tumeanza kufanya mazungumzo na contractors, tunataka tuhakiki ili kuondoa mambo fulani fulani yatakayotuwezesha kupunguza gharama za ujenzi wa ile miradi mikubwa. Lakini tatu, tunazungumza na mabenki, tunarenegotiate ili angalau tupunguziwepunguziwe hivi mariba yao yale. Na tumeanza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, tukishamaliza haya yote tunajua sasa tutapata picha ni kiasi gani cha pesa kinahitajika ili kukamilisha ile miradi. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Kamati na Waheshimiwa Wabunge, Serikali iko makini sana, lakini kama tulivyo sisi kazi yetu ni kuhakikisha kwamba pesa yetu tunaitumia kwa madhumuni yaliyo sahihi, kwa hiyo hii miradi itakamilika. Tumeanza vizuri na ule mradi wa Morocco, utakamilika kabla ya Juni, na baada ya hapo tutaenda Seven Eleven ile ya Kawe.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo miradi mingi ambayo inaendelea. Hapa Dodoma tumejenga nyumba 150 na tunaendelea kujenga nyingine 30 na mwezi ujao tutaanza kujenga apartments nyingine mpya 100; hii ni kwa fedha ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhakiki huu na kubana matumizi, Shirika la Nyumba sasa linaweza likajenga miradi mingine kwa pesa yake yenewe. Na Shirika la Nyumba sasa limeanza kuaminika kwa kutumia kampuni tanzu ya *National Housing* ya ujenzi, sasa tuna miradi 35 mikubwa ambayo tumeaminika tunajenga. (Makof)

Mheshimiwa Spika, moja ya miradi hiyo ni Hospitali ya Rufaa ya Musoma na Hospitali ya Rufaa ya Mtwara, wanaotoka huko wanajua. Hii ni kazi ambayo ilikuwa haifanywi na *National Housing*, sasa tumeamua katika Awamu ya Tano Shirika la Nyumba halitatumia contractor katika kujenga majengo yake na litashiriki katika ujenzi wa majengo mengine ya nchi. Kwa hiyo, Shirika la Nyumba sasa awamu hii inaenda vizuri zaidi kuliko awamu nyingine.

Mheshimiwa Spika, nataka msitafsiri uwezo au uendeshaji wa Shirika la Nyumba kutokana na ile miradi miwili mnayoiona pale Dar es Salaam. Ipo miradi mingi inaendelea, shirika limetulia, muundo umekamilika, bodi yenye weledi imekamilika inafanya kazi yake vizuri na yale yote ambayo yalikuwa yameshindikana sasa yatawezekana.

Mheshimiwa Spika, na zile nyumba ambazo zilikuwa zimejengwa kule mikoani tumebadilisha utaratibu sasa, watu watakuwa wanapanga zile ndogondogo zilikuwa zimejengwa muda mrefu lakini zilikuwa hazipati wanunuzi, tumeamua sasa kutengeneza utaratibu wa mpangaji mnunuzi. Kwa hiyo, mwananchi atakuwa na uwezo wa kupanga lakini hela yake mwisho wa yote atakabidhiwa nyumba. Tumeanza Kahama na sehemu nyingine, kwa hiyo zile nyumba ndogondogo kote kule tutaenda kwa utaratibu wa *tenant purchase*. Shirika la Nyumba nataka kusema linakwenda vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini nije kwa baadhi ya mafanikio mengine ambayo yamezungumzwa kwenye Sekta ya Ardh. La kwanza, Mheshimiwa Mch. Msigwa, katika miaka hii minne tumeweza kutatua migogoro zaidi ya 10,000 kwa njia ya utawala, maana yake nini? Kama wananchi hawa tusingewafikia na kutatua hii migogoro, wote wangkuwa mahakamani. Sasa wewe uniambie, wale wananchi wakiwemo wa Iringa niliowafikia juzi, miezi miwili iliyopita 500, leo wangkuwa kwenye mahakama wanatozwa hela na mawakili lakini leo wamepata nafuu kwa sababu Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Tano wamekwenda kuwasuluhisha kiutawala, wame-save gharama wananchi lakini pia wamewatua mizigo na kuleta amani na utuivu. Na hivi sasa nina mwaliko wa Iringa tena, wanachama wako 200 wananchi wameomba niende kule, na wewe unajua. (Makof)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utatuzi wa migogoro kwa Wizara ya Ardhi iko kisheria. Pia tunatumia utatuzi mwagine kutumia mabaraza ya ardhi. Lakini pia Mheshimiwa Rais ametusaidia kutatua mgogoro ambaa ulikuepo maisha, huu aliozungumza Mheshimiwa wa Maliasili. Vijiji 975 vilijikuta vimesajiliwa kwenye hifadhi za taifa, hifadhi za misitu, kwa miaka yote. Wamesajiliwa humu hati za TAMISEMI wamepewa, hati za ardhi wamepewa lakini bado kwenye GN za maliasili wanaonekana kama ni wavamizi. Na wakati huohuo baadhi ya watumishi wasio waaminifu walikuwa wanawatishatisha ili waondoke. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa kutumia usuluhishi wa namna hii wa kutatua migogoro ameamua kuumaliza kabisa mgogoro huu kwa mara ya kwanza katika nchi hii. Vijiji 920 ambaa walikuwa hawana matumaini ya kuishi katika vijiji vile sasa wamepewa matumaini mapya, watamilikishwa ile ardhi na hawataondoka katika ardhi yake. Haya ni matumaini mapya ambayo yamejengwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa hili angelijuaje maana nao huu ni usuluhishi. Sasa kama nao huu kuwapa matumaini mapya vijiji 920 vikiwepo vya Iringa, ipo mitaa minne pale Iringa Mjini ambavyo vilikuwa kwenye misitu lakini navyo mitaa ile imeambiwa ibaki pale. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwaambia kwamba utatuzi wa mgogoro umetusaidia sana katika kuleta utengamano, amani na utulivu katika nchi hii. Siyo hayo, Mabaraza ya Ardhi nayo yamesaidia katika kutatua migogoro. Kuna kesi zaidi ya 112,243 zimetolewa maamuzi kati ya kesi zilizofikishwa kwenye mabaraza 139,943. Pia tumefanikiwa katika kipindi hiki kutayarisha Hati Miliki nydingi zaidi. Katika mwaka uliopita mwaka 2019 tumeweza kutayarisha Hati Miliki 325,000 ukilinganisha na hati zilizotolewa mwaka 2015 hati 54,000. Maana yake nini? Tumewapa matumaini watu zaidi ya 300,000 kumiliki ardhi yao na hivyo sasa wameweza kukopesheka katika mabenki.

Mheshimiwa Spika, zoezi la urasimishaji limefanywa kwa huruma ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika Awamu ya Tano. Watu waliokuwa wamejenga katika maeneo mijini bila kuwa na vibali, bila kuwa na hati, bila kuwa na viwanja vilivyopangwa na kupimwa, mara zote walikuwa wametishiwa usalama wao na Manispaa na Halmashauri za Miji kwamba waondoke, lakini Mheshimiwa Dtk. John Pombe Magufuli amesema hawa ni Watanzania walijenga tukiwaona, waraslimishiwe wapewe hati zao katika makazi yao mijini. (Makof)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante, malizia Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, zoezi hilo limefanikiwa sana tumetoa hati zaidi ya 500,000. Kwa hiyo, nakushukuru sana. Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Kamati ile ya Maliasili na Ardhi kwamba tutaendelea kushirikiana na yale mapendekezo mengine yote tumeyachukua, tutafanya kazi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama kuna wanachi wenye kero waleteni tu, sisi kazi ya Serikali ni kusikiliza kero za wananchi, hatutachoka. Tutafanya, hii ni kazi yetu ya kuwashudumia wananchi kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.(Makof)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa William Lukuvi tunakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kemilembe Lwota aitimishe hoja yake. Jitahidi utumie dakika 15.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuhitimisha hoja ya Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kamati yetu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wanane. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote; Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Mheshimiwa Jitu Soni, amezungumzia suala la miundombinu mibovu katika hifadhi zetu za Taifa. Hili suala ni kweli, nasi kama Kamati ya Maliasili tumelizungumzia kwenye Kamati yetu na tukatoa mapendekezo kwa Serikali ifanye utaratibu wa haraka kushughulikia miundombinu yote ya hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu Wizara ya Maliasili ina mchango mkubwa sana wa pato la Taifa katika nchi yetu. Kwa hiyo, kuboresha miundombinu hii kutawezesha watalii wetu wa nje na ndani kufika kwenye hifadhi zetu kiurahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jitu Soni pia alizungumzia miradi ya ujirani mwema ya TANAPA. Mawazo yake ni mazuri na nina imani Wizara imechukua maoni yake na itayafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa pili alikuwa Mheshimiwa Mch. Msigwa ambaye alizungumzia masuala ya utalii kuhusu Wizara kutofanya jukumu la kutangaza watalii kutoka nje kwa sehemu kubwa linalofanywa na makampuni ya utalii. Nianze kwa kuonyesha kwanza masikitiko makubwa kwamba Mheshimiwa Msigwa ndio Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii na jitihada zote zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii hazoni.

Mheshimiwa Spika, kazi inayofanywa na Wizara ni kubwa, watalii wameongezeka Mheshimiwa Waziri ametuambia kutoka milioni moja mwaka 2015, mpaka milioni 1.5 mwaka 2020 ambayo tupo. Suala lingine ambalo Mheshimiwa Msigwa alizungumzia ni kuhusu wasanii wetu wa ndani. Napenda nimwambie Mheshimiwa Mch. Msigwa, utalii ni two way traffic; tunahitaji watalii wa nje na vilevile tunahitaji sana watalii wa ndani. Tanzania ina watu zaidi ya milioni 50 na mpaka sasa tunavyozungumza ni watalii 600,000 tu wa ndani ambaa ni Watanzania kwa takwimu za mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni jukumu letu sote kama Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi wa wananchi wa Tanzania ambaa tumo humu ndani kulisemea na kufanya kampeni nchi yetu. Wote tuendelee kusema na tuwashawishi Watanzania wenzetu waende kutembelea hifadhi zetu kwa sababu pia tunahitaji sana watalii wa ndani ambaa wanatokana na sisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mch. Msigwa vilevile amezungumzia masuala ya wasanii wetu wa ndani na akatoea mfano wa Steve Nyerere. Mheshimiwa Waziri amelizungumzia hili vizuri, lakini kwa kuongezea tu, huyu Steve Nyerere ana segment ya watu ambaa wanamfuata na ni muhimu pia kwa hao watu. Kwa hiyo, ni vizuri tuiswabeze wasanii wetu wa ndani kwa sababu wanakubalika ndani na vilevile na nje ya nchi yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Getere amezungumzia kuhusu utalii wa ndani, nadhani nimeshalizungumzia hilo. Pia ameongelea suala la TANAPA ambalo tumeshalileta kwenye

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bunge lake Tukufu. Ni katika miaka minne yote ambayo nimekuwa kwenye hiyo Kamati, tumelizungumzia mara kadhaa, tumeomba TANAPA wapunguziwe tozo kwa sababu hifadhi zimeongezeka kutoka hifadhi 15 zilizokuwepo mpaka 22 sasa hivi tunavyozungumza na hifadhi tano tu ndizo ambazo zinaweza kuijendesha na hifadhi mbili ya Serengeti na Kilimanjaro ndizo ambazo zinachangia kuendesha hifadhi nyiningine ambazo haziwezi kuijendesha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mzigo walionao ni mkubwa. Ni vyema kabisa Bunge lako Tukufu tukaishauri Serikali kutafuta namna bora ambayo itaiwezesha TANAPA kuweza kukidhi mahitaji waliyonayo. Kwa mfano, mdogo tu ambao tunaweza kuutoa, watu hawa wa TANAPA wanafanya SCR (*Social and Cooperate Responsibilities*) lakini katika kazi ambazo wanazifanya za kijamii kwa mfano wakijenga shule au wakifanya shughuli yoyote ya kijamii bado wanatozwa kodi kwenye kazi ambazo wamezifanya; na kazi hiyo wanazozifanya ni kubwa na ni nyangi. Kwa hiyo, kwa kuwapunguzia tu hata hiyo, tutakuwa tumpunguza mzigo ambao utawawezesha kwenda kufanya mambo mengine na kwenye hifadhi nyiningine kuziboresha zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwininge anayefuata ni Dkt. Kiruswa, amepongeza Wizara na Serikali kwa kazi inayofanya. Mheshimiwa Kiruswa pia amezungumzia suala upimaji wa ardhi ambayo napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza, kazi ya kupima na kupanga ardhi ya nchi hii imepewa mamlaka hiyo. Siku zote *traditionally* imekuwa kazi ya TAMISEMI, lakini ukweli ni kwamba mpaka leo ardhi ambayo imepimwa ya nchi hii ni chini ya asilimia 20 ambayo kwa kweli siyo kitu kizuri. Ndiyo maana tumekuwa na migogoro mingi ya ardhi, wafugaji na wakulima. Kwa sababu ardhi kubwa ya nchi hii haijapimwa na kupangwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha nyangi sana na kuwapa Wizara ya Ardhi ambayo kuna miradi mikubwa miwili ambayo itakwenda kupima, kupanga maeneo yote ya Tanzania. Ardhi yote ya Tanzania itapimwa na kupangwa. Hili siyo tu kwamba litaongeza mapato kwa sababu ya kulipia hati ambazo wananchi watakuwa wamepata, lakini vilevile itapunguza migogoro mingi sana ya ardhi ambayo inaendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maendeleo hayana chama, wote tunafahamu. Naomba kuchukua fursa hii kukuomba kushauri Wabunge wote tulimo humu ndani ya Bunge hili Tukufu, tuchukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kumpigia makofi mengi sana san asana kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kupima na kupanga maeneo yote ya ardhi nchini mwetu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwininge alikuwa Mheshimiwa Rhoda ambaye amezungumzia suala la viji 920 ambalo Mheshimiwa Waziri amelitolea maelezo vizuri kabisa, nadhani amelielewa, nasi kama Kamati tunaunga mkono, lakini ripoti hiyo haijaja rasmi kwenye Kamati yetu na itakapokuja tutaiwasilisha Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maftaha amezungumzia suala la TAWA. Sisi kama Kamati kweli tunamuunga mkono na tumeliongelea kwenye ripoti yetu, TAWA tangu imeanzhishwa bado haijapa sheria na haijajitegemea. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo inashindwa kufanya kama mamlaka kwa sababu hawana maamuzi ya kuweza kufanya kama mamlaka kamili. Kwa hiyo, tunaisihi Serikali, tunaiomba Wizara ifanye huu mchakato kwa haraka ili TAWA iweze kupata sheria yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dau amezungumzia suala la viboko wa Mafia; watu wamefariki, hili suala siyo kwa Mheshimiwa Dau peke yake, limejitokeza kwa Waheshimiwa Wabunge wengi, Mheshimiwa Gekul ameshalizungumzia hilo suala Bungeni hapa, Mheshimiwa Mulugo ameshatuambia wazazi wake wote wawili walifariki kwa sababu ya viboko huko Ziwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tanganyika. Kwa hiyo, hili suala ni muhimu, nami na Kamati yetu tunaomba sana hili suala la viboko lifanyiwe utaratibu wa haraka ili tuweze kutatua changamoto hii ambayo inaleteleza vifo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipitishe maazimio tulivoleta mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa mawasilisho mazuri sana. Mheshimiwa Mwenyekiti umeonesha uwezo mkubwa tunakushukuru sana pamoja na Wajumbe wa Kamati yako.

Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba nielekee kwenye kuwahoji.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Utekelezaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za Kamati hiyo kwa mwaka 2019 hadi Januari, 2020 pamoja na Maoni na Mapendeleko yake yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Naona kama wote wameafiki. Kwa kweli nawapongeza sana Wanakamati wa Kamati hii, mmefanya kazi kubwa sana katika mwaka 2019, nami ni shahidi jinsi ambavyo mmejitoa, mmesafiri kwenda maeneo ya mbali kabisa. Kama Kamati, mmekwenda kujionea kabisa kwenye site kule nini kinafanyika, japo baadhi yetu wamewalaumu Mawaziri kwa kufanya hivyo hivyo. Yaani Kamati zangu mmeenda mpaka kwenyewe kabisa kule, hamkubakia na sera hapa hapa tu Bungeni hapana. (Makofi)

Kwa hiyo, ni utaratibu mzuri, mwendelee nao, nasi kama Ofisi ya Bunge tutaendelea kuwa-support kwa kila hali kuhakikisha kwamba mwaka 2020 kazi yenu inaboreka zaidi.

Nakupongeza Mwenyekiti, nawapongeza Wajumbe na Mawaziri wote ambao wako katika Kamati hii ya Ardhi, Maliasili na Utalii, mwendelee na kazi hii njema mnayoifanya. Ahsante sana.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mgimwa, uje uhitimishe hoja yako. Pia jitahidi kama dakika 15. (Makofi)

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, nakushukutu tena kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Maziri wa Kilimo Mheshimiwa Japhet Hasunga pamoja na Manaibu Mawaziri wake; Mheshimiwa Mgumba na Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Waziri wa Mifugo na Uvvi Mheshimiwa Luhaga Mpina na Naibu wake, Mheshimiwa Abdallah Ulega. Naomba nichukue fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mbarawa Makame, pamoja na Naibu wake Jumaa Aweso

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa ushirikiano wanaotupatia kama Kamati na kazi nzuri wanazofanya katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kutekeleza baadhi ya maazimio ya Bunge lililopita. Naomba nichukue fursa hii tena kuiomba Serikali iendelee kutekeleza maazimio ya Bunge lililopita yale ambayo bado hawajayafanya kazi. Nawapongeza wote waliochangia katika ripoti yetu. Katika wachangiaji 21, 20 wamechangia katika hii Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, nawapongezeni sana.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo hoja ambayo imechangiwa na Wabunge wengi ni suala la bajeti ndogo. Kila Mbunge alipokuwa anasimama hapa, ukiyasikiliza maelezo yake kwa kina alikuwa anazungumzia udogo wa bajeti; na siyo udogo wa bajeti tu; na kiwango cha pesa kinachokwenda katika utekelezaji wa hiyo bajeti.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tuliliona hili, ndiyo maana katika mionganini mwa maombi yetu tumekuomba Wizara hii ya Kilimo iingie kwenye Wizara za vipaumbele kwa sababu ndiyo Wizara ambayo inaaqiri Watanzania walio wengo na ndiyo Wizara inayotoa malighafi ya kutosha. Asilimia 80 ya malighafi hapa nchini yanapatikana katika Wizara hii ya Kilimo. Kwa hiyo, tunkuomba sana hii Wizara ya Kilimo iingie kwenye Wizara za vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Tanzania tuliingia kwenye Azimio Malabo au Maputo Declaration. Azimio hili linasema Serikali inatakiwa itengeta asilimia 10 ya bajeti kuu kwa ajili ya Sekta ya Kilimo. Tunaiomba tena Serikali iliangularie jambo hili kwa sababu hata 4% katika bajeti kuu ambayo inakwenda kwenye maeneo ya kilimo haiendi. Eneo hili ni very sensitive na tunahitaji kuona viwanda vyetu vinafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, kama tunataka twende kwenye uchumi wa viwanda, hatuna sababu yakutokuboresha katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lilichangia na baadhi ya Wajumbe wengi ni suala la horticulture; kilimo cha mboga mboga pamoja na kilimo cha matunda. Kilimo cha mboga mboga na matunda kitatusaidia kupata fedha nyingi za kigeni, lakini kuna tatizo katika eneo hili. Kuna takribani kodi zaidi ya 45 ambazo zinawakwaza kwa njia moja wakulima katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ifike wakati Serikali ilitambue jambo hili kusudi tuendelee kupata mapato ya kutosha tuangularie mchakato huu ambao uko kwenye blueprint, ifanyike mapema iwezekanavyo kusudi tuweze kuondokana na hii adha wanayoipata wakulima wetu. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amejitahidi kuzungumzia suala la mbegu, lakini katika suala la mbegu tatizo kubwa lipo, bado kuna tatizo la bajeti.

Mheshimiwa Spika, ili tupate mbegu bora na za uhakika, lazima tujielekeze katika kuwekeza kwenye eneo la utafiti. Hata hivyo, tuna shida kwenye eneo hili la utafiti. Mara nyingi tunazungumza kwamba Serikali imetenga asilimia moja kwenye bajeti kuu kwa ajili ya eneo hili la utafiti, lakini ni shilingi ngapi linakwenda kwenda kwenye eneo hili la utafiti? Kwa hiyo, ifike wakati Serikali ijiekeleze kwenye eneo hili kuongeza kwenye bajeti eneo la utafiki kusudi tuweze kupata mbegu za uhakika na nyingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tuliliomba Wizara ya Kilimo ifanye marekebisho ya Sera na Sheria ya Kilimo na iletwe Bungeni mapema ili kuondoa ukakasi uliopo. Mabadiliko haya yatawasaidia wakulima. Kwa mfano, mkulima wa mahindi wa Mufindi anapoanza kulima mahindi yake hakuna sehemu yoyote Serikali ina-interfere. Anaingia shambani, analima, anapanda, anaweka mbolea, anavuna. Anapoanza kuvuna tu, akitaka kuanza kuuza Serikali

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inaingia kati, inaanza kusema kwamba sasa hivi mahindi yasiuzwe. Kwa hiyo, ifike wakati tuwekewe Sera na Sheria iliyokuwa bora ambao itaondoa ukakasi uliokuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo wamechangia wachangiaji wengi ni eneo la mifugo. Hili ni eneo muhimu na kama tulivyozungumza kwenye ripoti yetu kwamba Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na mifugo mingi katika bara la Afrika, lakini je, kuwa wa pili katika Bara ya Afrika na kuwa na mifugo mingi inaleta tija? Hilo ndilo suala la kujiliza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya vizuri kupidia Wizara yetu ya mifugo kwa kupidisha chanjo nyingi kwa mifugo yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri amelitekeleza zoezi hili vizuri, lakini bado kuna shida kwenye eneo hili. Kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa kina kusudi tupate ng'ombe walio bora wenye quality bora kusudi tuweze kupata soko zuri katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi sisi kama Watanzania tuna soko la uhakika Dubai na Oman, lakini hatuna soko la uhakika nchi za SADC na Ulaya. Kwa nini hatuna soko la uhakika? Ni kwa sababu quality ya ng'ombe wetu hajifikia hadhi ya nyama ambayo inaweza kuuzwa kwenye Soko la Dunia. Sisi kama Kamati tunaendelea kuishauri Serikali iangalie kwa kina kwenye eneo hili kusudi tupate ng'ombe waliokuwa bora na tuweze kupata soko la uhakika katika nchi za Ulaya na SADC.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi ni muhimu sana kwa mustakabali wa uchumi wa nchi yetu. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wavuvi wetu, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa uvuvi tena, alianza mchakato wa kuhakikisha tunafanya mabadiliko ya Sheria ya Uvuvi. Mchakato huu umechukua muda mrefu. Tunaomba mchakato huu uje Bungeni kwa sababu tunaamini kabisa mchakato huu ndio mwarobaini ya malalamiko ya wavuvi katika nchi yetu. Kwahiylo, mionganoni mwa maazimio yetu, tunaomba Serikali iharakishe kuleta mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Uvuvi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ni eneo la maji. Katika wachangiaji wetu akiwemo Mheshimiwa Jitu Soni, amezungumzia kodi ya mitambo ya kuchimba visima iangaliwe. Ni kweli kuna haja ya kuangalia kwa sabbau Watanzania wana matatizo mengi ya maji. Kwa hiyo, Serikali iangalie zile kodi ambazo siyo za lazima kwenye eneo hili zipunguzwe kusudi watu wengi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, kuna shida nyingine, kuna watu wengi katika nchi hii wamejitolea kuisaidia nchi yetu katika Sekta ya Maji, lakini kuna tatizo. Wanapoanza kufanya kazi za kusaidia katika Sekta ya Maji kuna shida, wanapoagiza vifaa kutoka nje, Serikali inaendelea kuwatoza kodi nyingi ikiwemo VAT. Ifike wakati wale wote ambao wanasaidia nchi yetu kupata maji, Serikali isamehe kodi za VAT pamoja na kodi mbalimbali kusudi wale wafadhili wetu waweze kujielekeza zaidi katika maeneo makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la mwisho ambalo nataka kuchangia hapa ni eneo la force account. Wizara ya Maji imeamua kabisa kujielekeza katika kuhakikisha miradi yake inatatuliwa kwa utaratibu wa force account. Force account inapunguza gharama, inaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi na inapunguza ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida hizi tatu tulizoiona hapo juu, lazima tuweke angalizo. Tunaweza kuwa tuna faida hizi za msingi hapa tatu, lakini je, ubora wa miradi uko sawa? Kwa hiyo, tuijangalie, tunapokwenda kwenye force account tuhakikishe na miradi yetu inakuwa bora.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, la pili, tunawaondolea ajira Watanzania wengi wenyewe makampuni ya maji. Kwa hiyo, kwenye eneo hili lazima tuhakikishe Serikali inafanya kazi yake kuhakikisha na watu wengi ambao wamesajili makampuni ya kutekeleza miradi ya maji wanapata fursa ya kufanya hiyo. Kwa sababu kwa kuziondoa hizi kampuni za maji kunakosesha kodi kwenye Serikali na kunaondolea ajira vijana wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho wataalam wa kutosha kwa kutekeleza hiyo miradi ya force account hatuna. Wengi wamesimama kulizungumzia suala la force account, lakini kwa nini Wizara ya Maji imeamua kujielekeza kwenye force account kuna shida sehemu.

Mheshimiwa Spika, BOQ za miradi ya maji zinaandalishi na wataalam wa Wizara ya Maji. Ifike sehemu Serikali iangalie wataalam wake wanavyoandaa hizo BOQ wanaandaa kwa uhalisia? Kama hawaandai kwa uhalisia Serikali iwachukulie hatua waandaji wote BOQ ambao wanafanya ulaghai katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipitishe Maazimio tuliyoleta pamoja na marekebisho ya takwimu yaliyoletwa na Serikali kupitia Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofii)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mgimwa, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwamba sasa Bunge lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli za Kamati hiyo kwa mwaka 2019 pamoja na maoni na mapendekezo yake na marekebisho yaliyoletwa.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019 mpaka Januari, 2020 Ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati hii muhimu sana ya Kilimo, Mifugo na Maji, ambayo ya kweli ndiyo inagusa hasa watu vijijini ambao ndiyo sehemu kubwa sana ya idadi ya watu wetu katika nchi yetu, mmewasemea mmewatembelea, mmetoa ushauri, mmetoa maoni.

Pia nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Ardhi, wa Mifugo, Uvuvi na wa Maji kwa kazi kubwa sana ambayo mnaendelea kuifanya nchi nzima. Kazi yenu tumeiona. Kama nilivyosema, kwa sababu Wizara zenu zinagusa wananchi walio wengi kwa kweli mmekuwa na mzigo mzito sana wa kuzunguka nchi nzima. Hongereni sana, tunawatia moyo mwendelee na kazi 2020.

Basi baada ya maneno hayo, kwa kweli shughuli zilizopangwa kwa ajili ya siku ya leo zote tumezikamilisha. Nina tangazo moja tu, kama kuna mtu amepotelewa na miwani yake, tuna miwani hapa, itakuwa na Makatibu Mezani, naomba muichukue kabisa. Mheshimiwa yeoyote ambaye amepotelewa na miwani yake leo humu humu ndani ya ukumbi iko hapa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Basi sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge. Tusimame niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu Kamili asubuhi.

*(Saa 1.26 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 4 Februari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*